**11 MEI, 2023**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

### Kikao cha Ishirini na Tatu – Tarehe 11 Mei, 2023

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* - KATIBU WA BUNGE:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**SPIKA:** Hati za kuwasilishwa Mezani, Waziri wa Afya, kwa niaba yake Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya Mheshimiwa Dkt. Mollel.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:**

Randama ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**SPIKA:** Ahsante sana.

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* - KATIBU WA BUNGE:**

## MASWALI KWA WAZIRI MKUU

**SPIKA:** Maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nimuite Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa. *(Makofi)*

Ahsante sana, Mheshimiwa George Ranwell Mwenisongole, Mbunge wa Mbozi.

**MHE. GEORGE. R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kumuuliza swali Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Sera ya Ushirika ya Vyama vya Msingi ililetwa kwa nia njema ya kumsaidia mkulima wa Kahawa lakini kwa wakulima wa kahawa ya *Arabica* nchini sera hii imekuwa kama kaburi kwao. Kwa sababu kwenye hivi vyama vya msingi makato ni mengi, wizi na viongozi wengi wa vyama vya ushirika ni wezi na wanawaibia wakulima na imekuwa kama inamdidimiza mkulima.

Je, Serikali haioni ipo haja sasa ya ku-*review* hii sera ili kuwaruhusu wanunuzi binafsi nao wapate nafasi kumruhusu mkulima auze kokote anakotaka? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kujibu swali la Mheshimiwa Mwenisongole, Mbunge wa Mbozi, niungane na Watanzania wote kuipongeza klabu yetu ya *Dar young Africans. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hakika *Dar Young Africans* inaendelea kupeperusha vema bendera ya Tanzania na niwapongeze sana kwa matokeo ya jana. Tunawaombea sana kwa mchezo wa marudio kule Afrika Kusini mshinde kwa magoli mengi. Watanzania tuna hamu ya kuona Tanzania ikiingia kwenye mashindano haya kwenye ngazi ya fainali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia niipongeze Klabu ya Simba kwa hatua waliyofikia, tunaamini wamejifunza na wameona kutoka klabu jirani na hatua waliyofikia. Kwa hiyo, msimu ujao tunaamini vilabu vyetu viwili au zaidi vitafanya vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nirudi kwenye swali la msingi linalohusu ushirika. Ni kweli kwamba ushirika una malengo mazuri sana kwa wakulima, si tu kwa wakulima bali kwenye vikundi vilivyoamua kukaa pamoja. Ushirika kwa mazao yetu nchini unatazamiwa na unatarajiwa kuwakusanya wakulima, mazao hayo pamoja ili kuwaongezea nguvu ya kupata maelekezo bora ya namna ya kulilima zao lenyewe lakini pia namna ya uhifadhi, elimu ya jumla ya zao hili lakini pia kuwapa nguvu ya pamoja ya kutafuta masoko.

Mheshimiwa Spika, tunakiri kwamba tunazo changamoto kwenye ushirika kutokana na baadhi ya viongozi waliopewa dhamana ya kuongoza ushirika kufanya mambo tofauti na misingi ya ushirika ulivyo. Kwa bahati nzuri siku tatu zilizopita Mheshimiwa Hussein Bashe, Waziri wa Kilimo, alitumia muda mrefu sana kueleza faida na umuhimu wa ushirika na kwamba ushirika hauepukiki katika kuleta maendeleo ya mkulima na mazao haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, moja kati ya mambo makubwa ambayo yameleta udhaifu kwenye ushirika ni pale viongozi wanapoona kwamba hiyo ni fursa ya kupata kipato kupitia uongozi wao kwenye ushirika. Hiyo ni kasoro na tutaendelea

kuisimamia. Tumeshuhudia viongozi wasiokuwa waadilifu kuweka makato mengi sana kwenye ushirika na kupunguza mapato ya mkulima.

Mheshimiwa Spika, tumeyaona hayo kwenye zao la korosho ambako kulikuwa na makato zaidi ya 25 tumeyapunguza na yakabaki matano na inawezekana na ndio yanayoendelea. Kwenye zao la kahawa lenyewe kulikuwa na makato 47 tumeyapuinguza tumefika makato matano mpaka sita yale ya msingi tu na kumwezesha mkulima kupata fedha nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushirika huu pamoja na changamoto hizo ambazo Serikali tunaendelea kuzifuatilia na kuzitatua imeleta pia mafanikio ya kupanda kwa bei ya mazao kwa mfano zao lenyewe la kahawa. Nitoe mfano wa mkoani Kagera ambako zao hili wakulima wake wengi walikuwa wanaamua kulipeleka nchini Uganda kwa gharama kubwa tu kwa sababu tu ya kero walizoziona. Baada ya Serikali kuingilia kati na kuzitatua changamoto hizi leo wanauza kutoka shilingi 1,200 ya awali tumeenda mpaka shilingi 1,800 mpaka shilingi 2,000 kwa sasa na kupitia usimamizi wa ushirika.

Mheshimiwa Spika, hii ina maana ya kwamba ushirika unaweza kuongeza nguvu ya wakuilima kupata soko zuri badala ya kuruhusu mnunuzi mmoja mmoja kwenda kwa mkulima nyumbani kwake na kumshawishi kununua kwa bei ambayo anaona yeye inafaa, wakati mwingine anauza kwa bei ndogo sana kuliko hata ile iliyokuwa inauzwa. Hata hivyo, tunaendelea kuangalia mifumo mizuri zaidi ya kuuza mazao yetu chini ya ushirika. Ushirika unaweza ukatoa kibali kwa watu waliolima kahawa nyingi kama soko linakuwa lina mwelekeo mzuri tunaweza kuruhusu.

Mheshimiwa Spika, nataka niwaahidi na nimwahidi Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge ambao pia

tunalima mazao yale makubwa yenye ushirika, kwamba tunaendelea kufanya mapitio, tunaendelea kusimamia kikamilifu ushirika ili ulete manufaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha majibu ya swali hilo.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, Mbunge wa Nkenge.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Spika, nishukuru kwa nafasi.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, tumeona Serikali imeonesha nia njema ya kuboresha utoaji wa mikopo ya asilimia 10 ambayo inatokana na halmashauri kwa kufanya maboresho ambayo yatafanya sasa mikopo hii itolewe kwa tija.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, mikopo hii inatolewa katika makundi ya wananwake, vijana na makundi ya watu wenye ulemavu. Mheshimiwa Waziri Mkuu, Vijana inapofika miaka 35, vijana wa kike wana–*qualify* kuendelea na mikopo hiyo kwa sababu wanakuwa ni wananwake lakini vijana wa kiume mikopo hiyo husitishwa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, katika maboresho haya mazuri yanayofanyika sasa hivi, Serikali haioni sasa kuna haja ya kuboresha eneo hilo kuingiza kundi la wanaume ambao kimsingi ni wapambanaji wa kiuchumi ili sasa makundi hayo yote manne, wanaume, wanawake, vijana na watu wenye ulemavu waweze kupata mikopo hii waweze kuinua uchumi wao? Mheshimiwa Waziri mkuu nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kyombo, Mbunge wa Nkenge kule Misenyi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tunayo mifuko ya mikopo ikiwemo na huu wa asilimia 10 uliopo chini ya halmashauri. Mifuko hii imetoa fursa ya wale wanaohusika wanaoweza kuingia kwenye masharti ya mfuko huo kupata mikopo. Mkopo wa asilimia 10 unaosimamiwa na halmashauri kupitia mapato ya ndani umeainisha na kuwalenga zaidi wanawake, vijana na walemavu. Sawa, wanawake, vijana na walemavu haijatamka wanaume lakini kwenye *category* ya vijana tuna wanaume pale lakini ni vijana. Hata hivyo, haikuwabagua wanaume kwa sababu sio mfuko pekee unatoa mikopo hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, tuna mifuko mingi ambayo pia inatoa mikopo kwa wote. Hata hivyo Serikali inafanya jitihada za kutoa fursa kwa yeyote yule awe mwanamke, mwanaume, kujana lakini pia wenye mahitaji maalum kupitia taasisi za fedha.

Mheshimiwa Spika, tuna NMB, CRDB, NBC, AZANIA na mabenki mengine yote ikiwemo Benki ya Kilimo ina fursa ya kwenda kukopa. Kwa hiyo, tunapoona eneo hili huna nafasi nalo nenda kwenye chanzo kingine. Nataka nifike Misenyi nione unaposema unaona vijana wanapewa wanawake tu na wavulana hawapewi sasa nataka tuone ni nini kinachotekelezwa kule Misenyi kwa sababu sisi tunaposema vijana ni wale wa kike na wa kiume wote wakapate mikopo. Kwa hiyo, naona fursa hii tunayo.

Mheshimiwa Spika, kwanza nataka niagize kwenye halmashauri, nirudie agizo langu la kwamba mapato ya kuanzia Aprili, Mei na Juni robo ya mwisho wa mwaka wa fedha, mapato haya yasikopeshwe kwanza tunataka kuyawekea utaratibu mzuri ambao pia unaondoa dosari

kama hizo ambazo zinaonekana na zimejitokeza kwenye halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, tutatoa kauli tukiwa katika kipindi hiki hiki cha Bunge kwa mapato haya ya mwezi nne, wa tano na wa Sita ili tupate mfu,mo mzuri zaidi. Kama kuna ushauri tunaupokea, je, fedha hizo tutumie utaratibu upi katika kukopesha na ziende kwa maeneo yapi yanayoweza kufikiwa kwa haraka zaidi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba tunaendelea kupanua wigo wa maeneo ya kupata mitaji kwa makundi yetu mbalimbali wanaume kwa wanawake, wazee, vijana ili waweze kusimamia miradi yao na eneo hilo liwe kama sehemu ya kupata mitaji. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ritta Enespher Kabati, Mbunge wa Viti maalum.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Mheshimiwa Waziri Mkuu, Tanzania imekuwa nchi ya kwanza Afrika Mashariki kutumia gesi asilia. Kwa sasa takwimu zinaonesha zaidi ya magari 2000 yameanza kutumia gesi hiyo.

Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kusambaza huduma hii nchi nzima ili wananchi waweze kufaidika na gesi yetu? *(Makofi)*

**SPIKA**: Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ritta Kabati, Mbunge Mkoa wa Iringa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tunayo gesi asilia nchini na ni kweli tumeanza kuitumia kwenye maeneo mbalimbali. Kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge amesema tunatumia kwenye magari lakini gesi hii tunaipeleka viwandani na tunao mpango wa kupeleka gesi hii majumbani.

Mheshimiwa Spika, wizara yetu ya Nisjhati imeweka utaratibu mzuri wa kupanua wigo wa matumizi ya gesi hii. Sasa hivi tunakamilisha ujenzi wa kituo cha kukusanyia gesi hii kutoka kule Mtwara - Songosongo pale Jijini Dar es Salaam ili sasa tuweke utaratibu mzuri wa kusambaza gesi hiyo iende kwa matumizi hayo tuliyoyasema.

Mheshimiwa Spika, pia tumeshirikisha sekta binafsi baada ya kuona uwezo wetu Serikali peke yetu hatutamudu kuifikisha gesi hii kwa wananchi. Pamoja na uwezo tulio nao tukiunganisha nguvu na sekta binafsi tunaamini tutawafikia kwenye matumizi haya. Iwe ni kupeleka viwandani, majumbani hata kwenye matumizi mengineyo ikiwemo na hayo magari.

Mheshimiwa Spika, tayari zabuni zimekwisha tangazwa na watu wengi wameomba. Sasa hivi wako wachache ambao wameruhusiwa kutekeleza mfumo huo na wengine mchakato unaendelea na bado tumefungua fursa kwa sekta binafsi kushiriki katika mchakato wa usambazaji wa gesi.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu tumeigawa kwenye *zone* ambazo tutalaza mabomba kuelekea huko. Tutakwenda na bomba la kwenda Kaskazini kwa mikoa ya Kaskazini, tutakuwa na bomba linalopita Kanda ya Kati mpaka Magharibi ili kufikia mikoa ya hapa kati na tutaweka bomba kule kule Kusini ambako inatoka gesi hii kwa ajili ya mikoa ya Kusini. Lengo ni kuifikia kwa ukaribu na kwa haraka, mikoa, wilaya na kama uwezo utakuwa mzuri na sekta binafsi ikiingia ikiwekeza zaidi tunataka tufike vijijini ili wananchi walioko vijijini nao wanufaike na hii gesi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo basi, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imejipanga vizuri kwenye eneo hili na ninaamini kupitia bajeti hii Wizara ya Nishati itakapokuja hapa itatoa ufafanuzi zaidi kwenye eneo hili. Pia nimwagize Mheshimiwa Waziri, sasa moja kati ya maelezo ambayo tutahitaji kwenye Bunge hili iwe ni namna ambavyo gesi itawafikia watanzania kwenye maeneo yao. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ramadhan Suleiman Ramadhan, Mbunge wa Chakechake.

**MHE. RAMADHAN SULEIMAN RAMADHAN:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, siku za hivi karibuni kumekuwa na taarifa ya baadhi ya balozi zimetangaza kwamba zitafunga ofisi zake hapa Tanzania ikiwemo Balozi ya Denmark na tumepata wasiwasi taarifa hizi zimefika mbali zaidi kwamba hakuna mahusiano mazuri baina ya Tanzania na balozi hizo. Ni ipi kauli ya Serikali juu ya jambo hili?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ramadhan Suleiman Ramadhan, Mbunge wa Chakechake, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Tanzania inayo mahusiano na nchi mbalimbali za kibalozi na tumefungua ofisi kwenye nchi hizo. Lakini na nchi rafiki nazo zimekuja kufungua balozi hapa Tanzania na hiyo Denmark ni miongoni mwa nchi ambazo zina ubalozi hapa na sisi pia kwenye nchi zao.

Mheshimiwa Spika, nataka niwahakikishie kwamba Tanzania ina mahusiano mazuri sana na Denmark ya

kidiplomasia, tumejikita kwenye siasa lakini pia kiuchumi, tunafanya biashara, tuna wawekezaji pia wako hapa nchini na Watanzania wachache waliowekeza nchini Denmark wanaendelea na shughuli zao. Balozi wa Denmark aliyepo nchini Tanzania ameendelea kufanya kazi yake na hana matatizo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa bahati nzuri sana wiki mbili zilizopita tumekuwa tukifanya mawasiliano na Waziri Mkuu wa Denmark juu ya maboresho ya mahusiano haya. Ni kweli Dernmark imebadilisha sera zao, sera za nchi na nchi, kwamba wanakusudia kupunguza baadhi ya ofisi kwenye Bara la Afrika kwa lengo la kufikia malengo ya sera yao. Sera yao wanasema wanajikita zaidi kwenye nchi ambazo hazina usalama, nchi ambazo zina tatizo la kiusalama; Tanzania ni nchi salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya pia tulipata nafasi ya kuzungumza na Mheshimiwa Balozi wa Denmark hapa nchini, alieleza haya na sisi tuliendelea kuonesha faida inayopatikana kwa nchi zote mbili kwa mahusiano haya na wanakusudia kufanya hivyo mwaka 2024, bado wako kwenye mchakato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi kupitia Wizara ya Mambo ya Nje, kupitia viongozi wakuu yako mazungumzo yanaendelea kubadilisha mwelekeo huo ili waendelee kubaki na pawe na ofisi nchini Tanzania na sisi tuwe na ofisi Denmark ili tuendelee kuimarisha mahusiano yetu kwa ukaribu zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunataka tuone shughuli zetu zote ambazo ziko kwenye makubaliano yetu zinaendelea kama zilivyo. Kwa kuwa mazungumzo yanaendelea basi tuna matumaini kwamba Denmark watatusikiliza Tanzania na watabaki nchini na sisi tuendelee kushirikiana nao na tuendelee kunufaika na yale yote yanayopatikana kupitia shirika lao la maendeleo linaitwa *DANIDA*.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, naomba mpokee hilo na kwamba tuhakikshe kwamba mazungumzo yanaendelea ili kufikia hatua nzuri, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Emmanuel Peter Chereheni, Mbunge wa Ushetu.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kumekuwa na malalamiko makubwa sana hapa nchini kwa ndugu zetu wafugaji waliotaifishiwa na kuuziwa ng'ombe wao katika hifadhi zetu, na wakaenda Mahakamani wameshinda kesi na Mahakama ikaamuru Serikali iwarejeshee mifugo yao hawa wananchi, sasa Serikali imekaa kimya. Nini kauli ya Serikali juu ya suala hili?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Cherehani Mbunge wa Ushetu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, natambua kuwepo kwa migogoro mingi kati ya wafugaji na wakulima, wafugaji na maeneo ya hifadhi. Wiki moja iliyopita siku ya Alhamisi nilikuja hapa mbele yako kutoa ufafanuzi wa kero hii ambayo inagusa maeneo yote kwa wafugaji, wakulima lakini pia maeneo yetu ya hifadhi, nilitolea kauli hapa, hili ni eneo moja kati ya maeneo ambayo nilitolea kauli. Tunatambua na tunajua kwamba tuna kesi nyingi ambazo wafugaji wameweza kupeleka Serikali Mahakamani au hifadhi imepeleka wafugaji Mahakamani. Kwa kuwa jambo hili ni la kisheria sana na lina sheria zake, pale ambapo imeamriwa ni lazima tutekeleze kwa sababu hakuna ambaye anaweza kupinga amri ya Mahakama.

Mheshimiwa Spika, kama imetokea kuna mahali hukumu imetoka, Mahakama imeamua, halafu hakuna aliyetekeleza jambo hili tunaweza kupata taarifa ni wapi huko ili

tuwaambie Serikali watekeleze mara moja kwa sababu ni hukumu na hatuwezi kupinga Mahakama. Lakini pia nitoe wito pale ambapo kuna migogoro ya aina hii Mahakama imetoa maamuzi yake uko utaratibu, kama eneo moja hilo iwe wafugaji au hifadhi hawajaridhika ni kukata rufaa badala ya kupinga moja kwa moja kutotekeleza amri hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kwa hiyo nitoe wito kwenye maeneo yote ambayo yana amri hii lazima tuheshimu mamlaka ya Mahakama na tutekeleze maamuzi ya Mahakama. Kwa kufanya hivyo tutajenga mshikamano zaidi kwenye mihimili yetu hii mitatu ambayo pia inafanyaka kazi kwa kuheshimiana na tunaenda vizuri. Kasoro kama hizo, tukipata mahali kuna tatizo hilo basi Mheshimiwa Mbunge atujulishe ili tuchukue hatu ili tuweze kuhakikisha kwamba kila mmoja anapata haki yake kupitia chombo kinachosimamia haki, ambayo ni Mahakama.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Aysharose Ndoghori Mattembe, Mbunge wa viti maalum

**MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuumuliza swali Waziri Mkuu. Kila ifikapo tarehe 15 Mei ni Siku ya Maadhimisho ya Familia Duniani. Kwa sasa jamii inapita katika wakati mgumu sana kutokana na mmonyoko wa maadili na ukiukwaji wa haki za wanawake na watoto.

Je, ni nini mkakati wa Serikali wa kuitumia siku hii kama sehemu ya kuielimisha jamii na kuhamasisha umuhimu wa malezi bora pamoja na maadili ili kukabiliana na changamoto hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Asharose Mattembe, Mbunge wa Mkoa wa Singida kama ifuatanyo: -

Mheshimiwa Spika, tunalo tatizo na changamoto ya ukiukwaji wa maadili kwenye maeneo mengi kwa watoto wadogo, wanawake wakati mwingine hata wanaume nao wanaonewa; hayao yote ni mmomonyoko wa maadili na Serikali tuko mstari wa mbele kukemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, dunia iliamua kuwa na siku moja maalumu ya kuelimisha umma juu ya kila mmoja kuhakikisha kwamba tunapiga vita mmomonyoko wa maadili lakini pia ukatili wa kijinsia na watoto vilevile, na sisi Tanzania tumejiunga kwenye siku hiyo. Kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge anataka kujua Serikali tumejipangaje? Na sisi pia tunasheherekea siku hiyo, siku hiyo pia tunakutana, siku hiyo pia tunatoa elimu kwa umma ya namna ya kila mmoja kushiriki katika kuhakikisha kwamba nchi hii mila zetu, desturi zetu utamaduni wetu lakini maadili ya nchi hii yanazingatiwa ili kupata kizazi ambacho kitakuwa endelevu katika sekta mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kwamba tumejipangaje siku hii; tunajua tarehe 15 ni siku tatu nne zijazo, nitoe agizo kwa wakuu wa mikoa na wakuu wa wilaya chini ya usimamizi wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia pamoja na TAMISEMI kila mkoa upange mpango thabiti wa kuwaleta pamoja wananchi kwenye siku hiyo ili haya ninayoyasema yaweze kutekelezwa. Kwanza tutoe elimu, tutoe makaripio lakini pia tuonyeshe dira ya nchi ya umuhimu wa kukinga mmomonyoko wa maadili hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa kufanya hivyo sasa huu ndio mkakati ambao tunaweza kuutumia. Lakini mkakati huo hauishii tarehe 15 tu, hili suala la kukemea kukiukwa kwa maadili na mmomonyoko ni suala endelevu kwa hiyo wakuu

wa mikoa nawaagiza tena, wakuu wa wilaya nawaagiza tena. Tunataka ishuke mpaka kule chini maafisa tarafa, watendaji wa kata, vijiji mpaka vitongojini. Ni muhimu sana Taifa hili tulilinde kwa kuwa na maadili mema, tuendeleze utamaduni wetu na mila na desturi zetu ili kujenga kizazi kipya ambacho kitakuwa endelevu kwa nchi hii na wataweza kufanya kazi yao vizuri.

Mheshimiwa Spika, huo ndio mkakati wa Serikali wa namna ya kuitumia vizuri tarehe 15 mwezi wa tano siku hii ya kupinga mmomonyoko wa maadili.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala Mbunge wa CHADEMA viti maalum.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na mimi kwa kunipatia nafasi ili niweze kumuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu swali.

Mheshimiwa Spika, kupitia sera ya Serikali kupitia Wizara ya Habari na Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kutoka kwenye mfumo wa analogia kwenda kwenye mfumo wa kidigitali, kwa kutekeleza sera hiyo Serikali imeamua kwa kuanza kwenye mfumo wa malipo kutaka wananchi kuanza kulipa kwa njia ya kielektroniki lakini mfumo huu umekuwa na changamoto kubwa sana ya makato makubwa lakini pia na mawasiliano pia mtandao kutokuwa sawa. Sasa swali langu;

Je, ni nini mkakati wa Serikali moja kupunguza makato lakini pili kuhakikisha inaboresha mfumo wake ili mfumo uweze kufanya kazi kwa uthabiti ili kuondokana na kadhia kubwa ambayo Watanzania wanaipata kwa namna ambavyo jinsi mtandao huu unavyofanya kazi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kunti Mbunge Mkoa wa Dodoma kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, uko ukweli kwamba Tanzania kutokana na maendeleo ya tehema na sisi tumeanza kutekeleza mifumo mbalimbali kwa ajili ya kurahisisha utendaji kazi ndani ya Serikali, ikiwemo na ukusanyaji wa mapato kwa mfumo wa kielektroniki.

Mheshimiwa Spika, Tananzia ni moja kati ya nchi ambazo zinaanza siku za hivi karibuni kutekeleza mifumo mbalimbali kielektroniki. Tunapitia katika nyakati kadhaa za mafanikio lakini pia changamoto tunapoelekea kujiimarisha. Ukusanyaji wa mapato yetu kielektroniki ni mfumo ambao unaendelea vizuri sasa pamoja na hizo changamoto. Sasa, ili kukabiliana na changamoto hizi yako maelekezo thabiti yaliyofikiwa na serikali yetu kupitia Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Spika, moja ameanzisha Wizara maalumu inayoshughulikia Habari Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa lengo la kufanya mapitio ya kina kwenye mifumo hii na kuimarisha tehama hapa nchini, na kusimamia kampuni zote za taasisi na sekta binafsi ambazo zinajishughulisha na mawasiliano ili kuimarisha mifumo hii ya mawasiliano. Kwa hiyo kuna tozo kuwa kubwa lakini pia kuna mtandao kutofanya kazi vizuri suala la tozo hili ni wale walioamua tozo hiyo kuwepo. Haya tunayafanyia kazi, na tumewasikia Waheshimiwa Wabunge mara kadhaa na wananchi pia kuitaka Serikali ipitie makato mbalimbali au tozo mbalimbali ambazo zinazotozwa kwenye maeneo mbalimbali, hilo linafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, suala la mtandano hili Mheshimiwa Waziri wa Habari Mawasiliano na Teknolojia ya Habari atakuja mbele yetu Waheshimiwa Wabunge kuja kuwasilisha mpango

wa bajeti, mpango wa kazi ambao tutaufanya mwaka ujao na kuomba ridhaa ya fedha. Moja kati ya mambo ambayo nitamwagiza hapa ni kuja kueleza nini wizara inafanya katika kuimarisha mifumo ya mawasiliano na hasa hii mitandao kuwa imara bila kukatika. Kwa sababu hata pia upande wa Serikali tunapata hasara sana lakini baadhi ya watu ambao wanapata vitendea kazi vya kielektroniki kwa kuzima na kusingizia kwamba mtandao haupo na kujipatia mapato, pia Serikali tunapata hasara.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunataka tuimarishe eneo hili ili tuwe na mfumo mzuri wa mtandao kupitia taasisi zetu zinazofanya kazi ya kusambaza mitandao lakini pia Serikali inaimarisha tozo mbalimbali ili kuleta unafuu kwa Watanzani.

Mheshimiwa Spika, malengo yetu tunapokwenda kwenya maendeleo ya tehama tuwe na tehama ambayo inaweza kumhakikishia mtanzania kuitumia katika shughuli zake binafsi na hiyo ndio mwelekeo wetu.

Mheshimiwa Spika, hayo ndio maelezo ya eneo hili ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** ahsante sana Mheshimiwa Mhandisi Ezra Chiwelesa

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi pia na mimi nimuulize Mheshimiwa Waziri Mkuu swali. Mheshimiwa Waziri Mkuu ni sera ya nchi yetu kwamba watu wanapotimiza umri wa miaka 18 wana-*qualify* kupata Vitambulisho vya Taifa. Tumeona hata kwenye Sensa iliyopita idadi ya Watanzania imeongezeka.

Mheshimiwa Spika, tunajua kwamba kuna watu kipindi kile wanaaandikisha kwa mara ya kwanza wame-*qualify* na umri umeongezeka na hawajaandikishwa. Pia baadhi ya

maeneo ya pembezoni mwa nchi hii wananchi walio wengi hawakupata fursa ya kuandikishwa kwenye ile *round* ya kwanza. Kwa hiyo wengi wamekaa bila vitambulisho ilhali vitambulisho ni *requirement* kubwa ambayo inatumika katika kila eneo sasa hivi ambalo wananchi wamekuwa wanahusushwa.

Je, hamuoni kwamba ipo haja ya Serikali kuanza mchakato huu upya kama tulivyofanya kipindi kile cha mwanzo ili Watanzania wengi waliofikia fursa hii iweze kuwapata na hatimaye wapate fursa kama Watanzania wanzao walio na vitambulisho wanavyoendelea kunufaika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Chiwelesa Mbunge wa Biharamulo kama ifatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu inaendelea na zoezi la utoaji wa vitambulisho kupitia taasisi yetu ya *NIDA*. Sote tunafahamu, kwamba tulipoanza kutoa vitambulisho hivi tulipitia hatua kadhaa, na hatua hizi zimekuwa na mafanikio lakini pia changamoto. Awali tulikuwa na idadi ndogo sana ya watumishi kuwafikia wananchi kwa ajili ya kutoa vitambulisho kwenye maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, mkakati wa Serikali ni kumwezesha Mtanzania kupata vitambulisho mpaka akiwa kijijini kwake. Sasa tumeongeza idadi ya watumishi na nashukuru Mheshimiwa Mbunge ameipongeza Serikali kwa mafanikio kuwa idadi ya wanaopata vitambulisho imeongezeka Lakini bado kuna maeneo kadhaa.

Mheshimiwa Spika, mimi nimefanya ziara biharamulo na Mkoa wa Kagera kwa ujumla nimepita pia Kigoma lakini pia kule Mkoani Arusha maeneo ya Longido kumekuwa na

changamoto ya watu wetu kadhaa kutopata vitambulisho kwa haraka. Nirudie tena. hapa niliwahi kupata swali hili na nikalijibu; nirudie tena kueleza kwamba inawezekana kabisa wale ambao bado hawajafikiwa na hasa wa mikoa ya pembezoni ni kuwepo kwa chngamoto ya mwingiliano na mataifa ya jirani.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu kitambulisho hiki ni cha Taifa, tunapozungumzia kitambulisho cha Taifa tunazungumzia Usalama wa Taifa letu. Tusingependa kitambulisho hiki kila mmoja awe nacho kwa sababu kitambulisho hiki ni kwa ajili ya Watanzania. Sasa pale ambako tunapakana na nchi jirani umakini unaongezeka ikiwemo na idadi ya *staff* ambao wanaweza kufanya kazi hiyo; na mkakati wetu kukamilisha kwa haraka sana.

Mheshimiwa Spika, Sasa hivi tumeimarisha tumepata mashine mpya. Nilipata nafasi ya kwenda nchini Korea na Mtendaji Mkuu wa *NIDA* kuzungumza na taasisi ambazo zina-*supply machines* na tulishapata mashine za kutosha vitambulisho vinatolewa. Kwa hiyo tutawafikia Watanzania katika kipindi kifupi kwa au kuwapa namba kwanza tukichapa vitambulisho au kuwafikia na vitambulisho vyenyewe moja kwa moja, kwa sababu pia Serikali tumerahisisha Watanzania ambao bado wanachelewa kupata vitambulisho basi wapewe namba na hiyo namba itumike kwenye mahitaji yao popote pale.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wote ambao kwenye maeneo yao kuna tatizo hili la upatikanaji wa vitambulisho kwa haraka sana kwa wananchi kwamba Serikali tumejipanga vizuri taasisi yetu ya *NIDA* imejipanga vizuri na sasa kasi inaongezeka kwa sababu tumeongeza watumishi ambao wanawafikia wananchi kwenye vijiji ambao tumewaweka kwenye wilaya zetu zote. Pale ambapo kutakuwa na tatizo kubwa sana tunawaruhusu wakati huu

tukiwa hapa Bungeni mje mtupe taarifa ya maendeleo ya utoaji wa vitambulisho kwenye maeneo yenu. Niwahakikishie tena kwamba kitambulisho hiki kitamfikia kila Mtanzania na si vinginevyo; na tushirikiane katika kuhakikisha kwamba kitambulisho hiki wanokipata ni Watanzania tu kwa sababu suala la kitambulisho nirudie tena ni Usalama wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba risala ya Serikali kuhakikisha kwamba inatatua migogoro kati ya wananchi na maeneo yenye hifadhi za Serikali. sasa ningependa kujua nini mkakati wa Serikali kukomesha migogoro hii katika maeneo haya niliyoyataja?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Waitara Mbunge wa Tarime, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waitara analizungumza hili akijua kwamba tumelifanyia kazi sana pia kwenye eneo lake ambako kuna mgogoro wa wananchi na hifadhi; na tulliunda timu ya mawaziri walienda kwenye eneo lake. Kwa hiyo, nataka nimhakikishie, kwamba mkakati wa Serikali wa kukomesha haya ni kushirikisha wananchi kwenye maeneo haya yote ambayo yamejitokeza na migogoro hii ili kuwa na mapitio ya pamoja ya mipaka ilipo kila mmoja ajue mpaka upo wapi. Serikali tumeagiza mamlaka hizi za hifahdi kuweka vigingi kama alama inayoonesha pande zote mbili kwamba hapa ndio ukomo wa watu kuingia kwenye upande mwingine; na vigingi hivi navyo tumesema viwe virefu siyo vile vidogodogo kirefu wapake rangi nyeupe kionekane kwa mbali ili kila mmoja apate kuelewa. Sasa jukumu hili

tunapolifanya kwa kushirikiana pamoja tunaamini migogoro itapungua kwa sababu kila mmoja atakuwa anajua.

Mheshimiwa Spika, siku tatu/nne zilizopita hili limejitokeza sana kule Tarime ambako kata kadhaa na vijiji kadhaa kulikuwa na mgongano wa kutoeleweka kwa mipaka yake, na hili pia tumeona hata juzi siku mbili zilizopita kwa kutoelewana viongozi wa Serikali za vijiji walijiuzulu. Nafurahi kusikia pia jana viongozi wa Chama cha Mapinduzi Wilaya ya Tarime wameenda kuwatembelea wananchi wamewaelimisha. Nawashukuru sana viongozi wale kwamba wamerudi kwenye nafasi zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka niwahakikishie wananchi wale ambao wako kwenye migogoro si Tarime lakini maeneo mengine yote, Serikali tunajipanga kufanya mapitio ya maeneo yote ili kuhakikisha kwamba hii migogoro haijirudii, lakini kila mmoja anakuwa na uelewa kwa kushirikisha na viongozi wale ambao wamerudi moja kati ya taarifa ambazo tumezipata ni kwamba wanahitaji kupata taarifa zaidi. Kwa ile Timu ya Mawaziri iliyoenda inakamilisha taarifa yake wataileta kwangu, tutaipitia kwa pamoja, tutashirikisha kwanza ndani ya Serikali, tutakwenda sasa Mkoa Mara, Wilayani Tarime mpaka kwenye vile vijiji. Tutakuwa na mikutano kwenye vile vijiji vya kuendelea kuelimisha zaidi kwa ukaribu na kuwashirikisha ili kila mmoja awe anajua. Sisi ndani ya Serikali tunaamini kwamba vijiji vyote, wananchi wote wanaoishi pembezoni mwa mipaka hii ya hifadhi watakuwa walinzi nambari moja wa kulinda hifadhi zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tutawajibika kwenda kutoa elimu maeneo yote. Tunajua hata hapa Kondoa kuna Pori la Mkungunero lina mgogoro, Babati, eneo la Tarangire lina mgogoro. Tunaambiwa Bunda pale katikati, katika ya Daraja na Mji wa Bunda pale kuna eneo lina mgororo, Serengeti nako pia kuna mgogoro. Haya maeneo yote tutayapitia eneo moja baada ya moja, tutakutana na wananchi,

tutawaelemisha. Tunataka Watanzania tuone umuhimu wa hifadhi, lakini na sisi wahifadhi tuone umuhimu wa raia wanaokaa pembezoni mwa hifadhi. Tukiwa na dhana hii itatusaidia sasa kutunza rasilimali zetu popote zilipo kwa pamoja zaidi, wananchi pamoja na miundombinu tuliyonayo ndani ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa swali hili na huo ndio ufafanuzi wangu. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Maswali.

Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Mheshimiwa John Marko Sallu, Mbunge wa Handeni Vijijini sasa aulize swali lake.

Na. 292

**Hitaji la Kituo cha Afya Kata ya Segera – Handeni Vijijini**

**MHE. JOHN M. SALLU** aliuliza:-

Je, ni lini Kituo cha Afya katika Kata ya Segera, Tarafa ya Mkumbulu kitajengwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ukiwa unajibu maswali kiti chako ni hicho hapo ili niwe najua nani anayesimama.

Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA YA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa John Marko Sallu, Mbunge wa Handeni Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali ilitenga fedha shilingi bilioni 117 kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya vya kimkakati katika kata 234 kote nchini. Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Handeni ilipewa shilingi milioni 500 ya ujenzi wa Kituo cha Afya Sindeni.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya kwenye Kata za kimkakati nchini ikiwa ni pamoja na ujenzi wa Kituo cha Afya Segera katika Tarafa ya Mkumbulu.

**SPIKA:** Mheshimiwa John Marko Sallu, swali la nyongeza.

**MHE. JOHN M. SALLU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri, lakini kule kwenye Tarafa ya Kwamsisi ni tarafa iliyoko pembezoni sana. Sasa ni lini Serikali itaona umuhimu wa kujenga Kituo cha Afya katika Kata ya Kwa Msisi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; Handeni Vijijini tuna upungufu mkubwa sana wa watumishi, takribani tuna upungufu wa zaidi ya asilimia 60. Sasa je, ni mkakati gani wa Serikali katika kupambana na upungufu huo wa watumishi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA YA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, kwenye swali lake la kwanza la Tarafa ya Kwamsisi ni lini itapata kituo cha afya; nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge katika mwaka wa fedha 2024/2025, tarafa hii na Kata ya Kwa Msisi itatengewa fedha kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya.

Mheshimiwa Spika, nikienda katika swali lake la pili la upungufu wa watumishi, kama ambavyo wote ni mashahidi katika Bunge lako hili tukufu, Serikali inaendelea kuajiri na hivi sasa kuna ajira zaidi ya 21,000 ambazo zimetangazwa na Serikali itaendelea kuajiri vile vile kadri ya uwezo wake wa kibajeti na katika hawa watumishi 21,000 ambao wanaajiriwa hivi karibuni vile vile Handeni Vijijini watapata watumishi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 293

**Hitaji la walimu wa kike – Chemba**

**MHE. KUNTI Y. MAJALA** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kupeleka walimu wa kike katika shule za sekondari na msingi – Chemba?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA YA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikitoa ajira ili kukabiliana na upungufu wa walimu shuleni unaotokana na walimu kustaafu, kuacha kazi, kufukuzwa, kufariki na ongezeko la idadi ya wanafunzi wanaoandikishwa. Kwa mwaka 2021/2022 Serikali imeajiri jumla ya walimu 26,598 wakiwemo 16,640 wa shule za msingi na 9,958 wa shule za sekondari.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ajira zilizotangazwa 2021/2022, Halmashauri ya Wilaya ya Chemba ilipata Walimu 46 wa kiume na Walimu 49 wa kike kwa shule za msingi na sekondari.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, TAMISEMI imetoa maelekezo kwa Makatibu Tawala wa Mikoa yote Tanzania Bara kufanya msawazo wa Walimu kutoka shule zenye ziada na kuwapeleka katika shule zenye upungufu zaidi kwa kuzingatia jinsia ili kuwa na uwiano wa Walimu wa kike na kiume kwenye shule zetu mbalimbali.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala, swali la nyongeza.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ili niweze kumuuliza Mheshimiwa Waziri, maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Serikali, lakini ni ukweli usiofichika kwamba mazingira ya walimu wetu kwa maeneo ya vijijini ni tofauti kabisa na maeneo ya mjini. Sasa kumekuwa na upungufu mkubwa wa walimu wa kike kutokana na mazingira hususan kwenye halmashauri ama majimbo ama wilaya za vijijini.

Swali langu la kwanza; je, ni lini Serikali itaanza kulipa posho kwa ajili ya mazingira magumu kwa walimu wetu Tanzania, hususan wa kike? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; kutokana na upungufu mkubwa wa walimu, Wilaya ya Chemba tuna shule zaidi ya sita ambazo wanafunzi wameshindwa kuendelea na masomo, hatuna walimu. Shule hizo ni Shule ya Magarasta Sanzawa, Mialo Kwa Mtoro, Hanaa Gwandi, Magandi Soya, Mkandinde Soya pamoja na Lugoba Kata ya Kimaha.

Je, ni lini Serikali itapeleka walimu hawa ili watoto wetu kwenye shule hizi sita waanze masomo ili na wao waweze kutumiza haki yao ya kikatiba? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA YA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, nikijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge; swali lake kwanza la mazingira, Serikali hakuna *incentive* maalum ya mazingira na hivi sasa Serikali inaandaa mwongozo kwa ajili ya posho ya masaa ya ziada. *Incentive* kubwa ambayo inatolewa na Serikali kwa sasa ni kuhakikisha kwamba inaweka mazingira bora kwa kujenga nyumba, kutengeneza miundombinu ya barabara, kuvuta umeme kwenye vijiji vyote vya nchi yetu hii ambayo nayo inatengeneza mazingira bora kwa watumishi wetu kwenye maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, nikijibu swali lake la pili, Mheshimiwa Mbunge la maeneo haya ambayo ni Sanzawa, Gwandi, Soya ni lini yapata watumishi. Kama nilivyosema hapo awali Serikali imetangaza ajira zaidi ya 21,000 ambapo katika ajira hizi za Walimu na maeneo haya yaliyotajwa nayo yatapata. Nimueleze tu Mheshimiwa Mbunge kwamba katika ajira za mwaka uliopita, Halmashauri ya Wilaya ya Chemba ndio ilipata Walimu wengi zaidi wa kike katika Mkoa huu wa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Minza Simon Mjika, swali la nyongeza.

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Mkoa wa Simiyu una upungufu sana wa walimu kwa upande wa sekondari na shule ya msingi. Walimu wa kike ni wachache sana na shule zingine hazina kabisa walimu wa kike.

Je, Serikali ina mpango kutuletea walimu wa kike katika Mkoa wa Simiyu? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA YA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, tayari Ofisi ya Rais, TAMISEMI ilishatoa maelekezo kwa Makatibu Tawala wote wa mikoa ya Tanzania Bara. Kuhakikisha wanafanya msawazo katika shule zilizo ndani ya mikoa yao na kupeleka walimu wa kike na wakiume katika maeneo ambayo hayana.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii ya Bunge lako tukufu kwa Niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kumwelekeza *RAS* wa Mkoa wa Simiyu kuhakikisha anafanya msawazo na kupeleka walimu katika shule ambazo hazina Walimu wa kike wa kutosha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara inayofuata, niwakumbushe maswali ya nyongeza yawe mafupi na yaende moja kwa moja kwenye swali.

Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 294

**Ujenzi wa barabara ya Mzumbe hadi Mgeta**

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Mzumbe hadi Mgeta?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mhandisi Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* inaendelea kujenga kwa kiwango cha lami Barabara ya Mzumbe kuanzia Eneo la Sangasanga – Langali – Luale hadi Kikeo, yenye urefu wa kilometa 59.16 ambapo jumla ya kilometa 13.5 za lami zimejengwa na zimekamilika kwenye maeneo korofi yenye maporomoko na milima mikali. Aidha, Serikali inatafuta fedha kwa ajili ya kuifanyia upembuzi yakinifu na usanifu wa kina barabara hii kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri, hata hivyo nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; ni lini barabara ya Gairo hadi Milima ya Nongwe ambayo ni agizo la viongozi wa kitaifa, itajengwa kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; barabara ya Ifakara – Mbingu – Chika – Mlimba ni mbovu sana; je, ni lini itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Gairo kwenda Nongwe ni barabara ya mkoa ambayo haijafanyiwa upembuzi yakinifu wala usanifu wa kina. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hii *TANROADS* kupitia Mkoa wa Morogoro wameomba iwekwe kwenye upembuzi yakinifu na usanifu wa kina. Kwa maana ya kufanya maandalizi ya kujenga kwa kiwango cha lami kwa mwaka huu wa fedha tunaouendea.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara aliyoitaja ya Ifakara - Mlimba - Kibena. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali ya Awamu ya Sita tayari ilishatangaza barabara hii kuanza kuijenga kwa kiwango cha lami, ambapo imegawanya katika *lot* mbili kuanzia Ifakara hadi Mbingu na Mbingu hadi Chita. Kwa hiyo, tayari iko kwenye hatua za manunuzi na tunategemea kabla ya mwisho wa mwaka huu wa fedha barabara hii itakuwa pengine imeshaanza kujengwa, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Salim Alaudin Hasham, Mbunge wa Ulanga, sasa aulize swali lake, kwa niaba yake Mheshimiwa Abubakari Asenga.

Na. 295

**Ujenzi wa barabara ya Ifakara hadi Mahenge**

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA K.n.y. MHE. SALIM A. HASHAM** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga kwa kwango cha lami barabara ya kutoka Ifakara hadi Mahenge?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Salim Alaudin Hasham, Mbunge wa Ulanga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Ifakara Kibaoni hadi Mahenge Mjini yenye urefu wa kilometa 55.4 ni sehemu ya Barabara ya Ifakara – Mahenge– Malinyi – Kilosa kwa Mpepo – Londo hadi Lumecha yenye urefu wa kilometa 435 ambayo Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* tayari imetangaza zabuni kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami kwa utaratibu wa *EPC+F*. Uchambuzi na tathmini ya zabuni za kumpata Mkandarasi na Mwekezaji atakayetekeleza mradi huu zinaendelea na zinatarajiwa kukamilika kabla ya mwisho wa Juni, 2023, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Abubakari Asenga, swali la nyongeza.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nashukuru sana Serikali kwa kuanza mchakato wa barabara hizi za kufungua Mkoa wa Morogoro. Sasa kipande cha Ifakara - Lupilo kimetangazwa.

Sasa swali langu la kwanza, je, ni lini kipande cha Lupilo – Mahenge – Liwale kitaanza ujenzi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa kipande hiki cha Ifakara – Lupilo kitapita *by pass* ya Ifakara Mjini ambako wananchi wa Kata ya Mbasa na Katindiuka wamesubiri kwa muda mrefu sana, zaidi ya miaka minne kulipwa fidia na Serikali yao.

Je, ni lini Serikali itawalipa fidia wananchi hawa pamoja na hasara ya kusubiri zaidi ya miaka minne? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kipande cha Barabara ya Lupilo – Mahenge - Liwale kina sehemu mbili. Kwanza kuanzia Lupilo hadi Mahenge ni barabara kuu ambayo itakuwa ni sehemu ya ujenzi kwenye barabara hii kubwa ambayo nimeitaja kwa mpango wa *EPC*, lakini kuanzia Mahenge kwenda Ilonga hadi Liwale tumesema mwaka huu tumeingiza kwenye mpango wa kuanza kuifanyia upembuzi yakinifu na usanifu, maana hiyo barabara haipo lakini Serikali kwa sababu ya maombi ya muda mrefu kuunganisha Mkoa wa Morogoro na Lindi tumeshaweka kwenye mpango wa kuanza kuifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *by pass* ya Ifakara; hii *by pass* ya Ifakara ni sehemu ya huo mpango mkubwa na kitakachofanyika sasa ni pamoja na kuhuisha zile tathmini zilizofanyika kwa wananchi ambao wataathirika na mradi huu kwa ajili ya kuwalipa fidia. Kwa hiyo watakuwa ni sehemu ya huo mradi mkubwa ambao tunaenda kuutekeleza, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hassan Selemani Mtenga, Mbunge wa Mtwara Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 296

**Ujenzi wa Daraja la Kilambo – Mtwara Vijijini**

**MHE. HASSAN S. MTENGA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Daraja la Kilambo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hasan Seleman Mtenga, Mbunge wa Mtwara Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Daraja la Kilambo linalopendekezwa kujenga litaunganisha Nchi ya Tanzania na Msumbiji katika Barabara ya Mangamba – Madimba – Tangazo – Kilambo yenye kilometa 36.8 Mkoani Mtwara. Kwa kuwa ujenzi wa daraja hili utahusisha Nchi mbili za Tanzania na Msumbiji, Serikali tayari imeanza mazungumzo ya awali na Nchi ya Msumbiji ili ziweze kukubaliana kuhusu ujenzi wa daraja hilo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hassan Seleman Mtenga, swali la nyongeza.

**MHE. HASSAN S. MTENGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza nimshukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini swali la kwanza; ni lini upembuzi yakinifu na usanifu wa kina utafanyika kwenye daraja hilo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa Serikali ya Mozambique iko tayari kutoa ushirikiano wa ujenzi wa daraja hilo, ni lini mazungumzo haya yatakuwa yanaendelea kwa kina? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kutambua umuhimu wa barabara hii kwa upande wa Tanzania, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba sisi upande wa Tanzania tuko tayari kuijenga hiyo barabara na katika mwaka huu wa fedha ambao tunakwenda kuleta bajeti, tumeweka fedha kwa ajili ya kuanza kufanya maandalizi ya kufanya usanifu na kufanya upembuzi na usanifu wa kina, lakini kama nilivyosema kazi hiyo itaanza tu pale ambapo tutakuwa tumekamilisha na wenzetu wa Msumbiji kwa sababu ni daraja la pamoja, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Deodatius Philip Mwanyika, Mbunge wa Njombe Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 297

**Mpango wa kufufua Kiwanda cha Maziwa – Njombe**

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA** aliuliza:-

Je, nini mpango wa Serikali kufufua Kiwanda cha Maziwa Njombe?

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, nakushukuru, kwa niaba ya Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Deodatus Phillip Mwanyika, Mbunge wa Njombe Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua changamoto za kiwanda cha maziwa *Njombe Milk Factory Company Limited* na Serikali kupitia uongozi wa mkoa imekwishaanza kuchukua hatua za kukikwamua kiwanda hicho. Hatua za awali zilizochukuliwa ni pamoja na kuwakutanisha wanahisa wa kiwanda na uongozi wa Mkoa wa Njombe.

Aidha, ninapenda kumuahidi Mheshimiwa Mbunge kuwa, kwa kushirikiana na uongozi wa Mkoa wa Njombe, Serikali itahakikisha kiwanda hicho kinaweza kufufuliwa kwa haraka ili sekta ya viwanda vya maziwa izidi kukua na kuleta manufaa kwa wafugaji na wanahisa, ninakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Deodatus Phillip Mwanyika, swali la nyongeza.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, pamoja na majibu ambayo ni mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, tatizo la kiwanda siyo tu wanahisa, tatizo la kiwanda ni deni la Benki yetu ya Kilimo.

Swali la kwanza, je, Waziri haoni haja sasa ya kuhakikisha kwamba anaratibu majadiliano akishirikisha Wizara ya Mifugo ambayo ndiyo inasimamia sekta hiyo kwa haraka sana? *(Makofi)*

Swali la pili, anawahakikishiaje Wananjombe na wafugaji wa Njombe kwamba majadiliano hayo sasa yatafanyika kwa haraka katika kipindi hiki cha Bunge au mara tu baada ya kuisha Bunge hili? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, kama nilivyosema nia ya Serikali ni kuona kiwanda hiki kinafanya kazi na kwa taarifa tu kwa sababu ya umuhimu wake Wizara wenye dhamana ya kuhakikisha maendeleo ya viwanda nchini yanafanikiwa na kuwa na tija, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tutaratibu majadiliano ya wanahisa kwa maana ya *NJOLIFA,* Njombe Wilaya, Njombe Mji, *Roman Catholic* ambao nao wanahisa na wengine. Muhimu zaidi kama nilivyosema moja ya sababu iliyopelekea kukwama kiwanda hiki ni mtaji ambao sasa kupitia Benki ya Kilimo *(TADB)* ilitoa zaidi ya shilingi bilioni 1.6. Sasa tutaandaa kikao, tutawaita kabla ya kuisha Bunge hili ili wanahisa wote na wenzetu wa *TADB* tuje tukae hapa, tuone namna gani tunakwamua mkwamo wa kiwanda hiki ili kiendelee kuzalisha kwa tija lakini pia kupata manufaa kwa nchi katika sekta ya viwanda.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Madini, Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 298

**Hitaji la wapima miamba ya madini mikoa ya Rukwa na Songwe**

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka wapimaji wa miamba ya madini katika Mikoa ya Rukwa na Songwe?

**NAIBU WAZIRI WA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Madini, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania *(GST)* imekwishafanya utafiti wa miamba katika Mikoa ya Rukwa na Songwe na kuchora ramani za miamba katika kipimo cha skeli ya 1:100,000 ambazo hutumika kuonesha uhusiano wa miamba na madini. Ramani hizi za miamba zinapatikana *GST* na ndizo kwa sasa hutumika kuvutia uwekezaji katika sekta ya madini kwa maeneo hayo. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata swali la nyongeza.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza kabisa nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali lakini pamoja na hivyo nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, kwa kuwa Serikali tayari ina taarifa za miamba yenye madini katika Mkoa wa Rukwa na Songwe. Je, ni lini sasa itatoa taarifa na kusambaza kwa wananchi ili wananchi hawa waweze kuomba leseni kwa ajili ya uchimbaji? *(Makofi)*

Swali la pili, ni nini sasa mpango wa Serikali kwa kuwapa mitaji wachimbaji wadogo wakiwemo wanawake? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, taarifa za kijiolojia za maeneo yenye madini nchini hutolewa na *GST* kupitia chapisho la kitabu cha madini yapatikanayo Tanzania ambacho toleo la mwisho lilitolewa mwaka 2019. Kutokana na tafiti zilizoendelea kuna aina nyingi za madini zimeendelea kugundulika na hivyo toleo la tano limekamilika, tuko kwenye hatua za kuandaa uzinduzi wa kitabu kipya cha madini hayo na siku ya uzinduzi wa hicho kitabu tutawaalika Wabunge wote na wadau mbalimbali wa madini waweze kupata nakala ya vitabu hivyo ili taarifa hizi ziweze kuwafikia walengwa katika maeneo ya Wilaya zote za nchi yetu.

Swali lake la pili kuhusu mpango wa kuwapatia wachimbaji wadogo mitaji ulikwishawekwa kupitia maelewano na mabenki ya ndani, kwamba watoe mikopo kwa wachimbaji wadogo waliokidhi vigezo na tayari mabenki ya ndani yameshatoa zaidi ya shilingi bilioni 145 kwa wachimbaji wadogo wenye leseni, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hussein Nassor Amar swali la nyongeza.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa kuwa Wilaya ya Nyang'hwale wachimbaji wadogo wadogo wameendelea kuvumbua maeneo mbalimbali kama vile Isonda, Igalula, Isekeli, Shibalanga, Ifugandi, Rubando, Lihulu, Bululu pamoja na Mahagi.

Je, Wizara ina mpango gani wa kupeleka mitambo ya kufanya utafiti ili uchimbaji ule uwe wa kuendelea?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kupeleka mitambo ya kuwasaidia wachimbaji wadogo, Wizara kupitia taasisi yake ya *STAMICO* imeagiza mitambo mitano ambayo tayari ilishaagizwa na mingine

mitano pia imeshaagizwa kwa ajili ya kuwa na zana mahsusi kwa ajili ya kusaidia uchimbaji wa wachimbaji wadogo waweze kufanyiwa upimaji wa maeneo yao wajue aina ya madini na kiasi kinachopatikana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 299

**Hitaji la umeme Kata ya Mletele – Songea**

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kupeleka umeme katika Kata ya Mletele Wilayani Songea?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kata ya Mletele katika Manispaa ya Songea ina jumla ya mitaa sita ambayo ni Mletele, Makemba, Liumbu, Nonganonga, Mdundiko na Mji Mwema. Mitaa mitano ya Mletele, Makemba, Liumbu, Nonganonga na Mdundiko tayari ina umeme. Mtaa wa Mji Mwema tu ndiyo bado haujafikiwa na umeme.

Mheshimiwa Spika, mtaa huu tayari umefanyiwa tathmini na utapata umeme kwa kuweka miundombinu

itakayogharimu shilingi 115,767,782.60 katika mwaka wa fedha 2023/2024. Nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, swali la nyongeza.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri sana ya Serikali, pamoja na hivyo bado naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, Sera ya Taifa inaeleza kwamba maeneo ya pembezoni mwa Miji na Manispaa yatakwenda kuwekewa umeme kwa gharama ya shilingi 27,000 na siyo shilingi 300,000 kama ilivyo sasa.

Je, ni kwanini Serikali inakwenda kinyume na sera yake yenyewe? *(Makofi)*

Swali la pili, je, ni lini Serikali itapeleka umeme kwenye Kata zenye mazingira ya vijijini ambazo ni Rilambo, Shibira, Dilimalitembo, Mletele, Shule ya Tanga, Mwengemshindo, Mbati na Wenje? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, kwenye swali la kwanza la kuhusu bei ya shilingi 27,000 kwenye sera, naomba kuliarifu Bunge lako kwamba bei zinazotumika kuunganisha umeme kwa wateja wa *TANESCO* zinapangwa na kusimamiwa na Mamalaka ya Udhibiti ya *EWURA*. Kwa hiyo, kinachofanywa ni kuangalia maeneo maalum na kuyapangia bei yake. Maeneo ya vijijini ni shilingi 27,000 maeneo ya mijini ni shilingi 321,000 na kuendelea.

Mheshimiwa Spika, ilijaribiwa kufanyiwa shilingi 27,000 kila sehemu lakini kwa uhalisia ilionekana ni ngumu, lakini zoezi la

kuendelea kubaini ni kiasi gani kitumike kuunganisha eneo gani kinaendelea kama ambavyo tumekuwa tukitoa taarifa na jambo hilo litakapokamilika basi bei nzuri za kila eneo zitatangazwa ili ziweze kutumika.

Mheshimiwa Spika, katika swali la pili. Kuhusu umeme kupelekwa katika maeneo ya vijijini lakini yaliyoko mijini tunafanya hivyo, kwenye baadhi ya maeneo tayari kuna awamu ya kwanza ilishafanyika kwa Mikoa kadhaa, awamu ya pili imefanyika na sasa inaendelea awamu ya tatu. Nimhakikishie Mheshimiwa Msongozi kwamba katika maeneo aliyoyataja nayo yamo katika *plan* za Serikali na upatikanaji wa fedha utakavyokuwa tayari maeneo hayo pia yatapelekewa umeme katika maeneo ya mijini yenye uso wa vijijini kwa kadri ya upatikanaji wa fedha katika siku chache zijazo. Nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, swali la nyongeza.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niulize swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kutokana na tatizo kubwa la umeme tulilonalo Wilayani Urambo, ni lini kituo kinachojengwa Kata ya Vumilia eneo la Uhuru litakamilika kama utatuzi wa tatizo hilo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, Kituo cha Uhuru kilichopo Urambo ni mojawapo ya vituo 14 vinavyojengwa katika mradi wetu wa Gridi Imara na kabala ya mwaka huu kuisha kituo hicho kitakuwa kimekamilika kwa sababu tayari mashineumba *(transformer)* zimeshakaguliwa kiwandani na sasa zimefungwa kwa ajili ya kuja kuwekwa

katika kiwanda hicho kwa sababu jengo tayari lilishakamilika na *lane* inaendelea kujengwa.

Mheshimiwa Spika, hivyo, kabla ya mwaka huu kuisha kitakuwa kimekamilika ili kuweza kuhudumia wananchi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda swali la nyongeza.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mkoa wa Kigoma unaunganishwa katika Gridi ya Taifa, mpaka sasa Wilaya za Kigoma na Uvinza bado hazijaunganishwa. Je, ni lini Serikali itakamilisha kazi ya kuunganisha Wilaya hizi ili kukamilisha Mkoa wa Kigoma? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Kigoma umeunganishwa kwa Gridi ya Taifa kwa *line* ndogo inayotoka katika kituo chetu cha kupoza Umeme cha Nyakanazi na *line* hiyo ya msongo wa kilovolti 33 iliishia maeneo ya Kibondo, lakini tayari mradi mkubwa wa kilovolti 400 unaojengwa kutoka Nyakanazi kwenda Kidahwe Mjini Kigoma wa kilometa 280 unaendelea, kabla ya mwaka 2025 utakuwa umekamilika na hivyo Mkoa wote wa Kigoma utapata huduma ya umeme wa Gridi ya Taifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Yahaya Omary Massare, Mbunge wa Manyoni Magharibi sasa aulize swali lake.

Na. 300

**Kukarabati njia kuu ya kusafirisha umeme Singida**

**MHE. YAHAYA O. MASSARE** aliuliza:-

Je, ni lini ukarabati utafanywa katika njia ya umeme kutoka kituo kikubwa kuelekea Ikungi, Manyoni, Itigi, Mitundu hadi Mwamagembe?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Yahaya Omary Massare, Mbunge wa Manyoni Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Singida umeunganishwa na Gridi ya Taifa kutoka katika kituo cha kupoza umeme kilichopo Mkoani Dodoma kupitia njia ya kusafirisha umeme za msongo wa kilovolti 220 na 400 hadi kituo cha kupoza umeme cha Singida. Kwa kutumia msongo huo mkubwa, Serikali kulingana na upatikanaji wa fedha imepanga kujenga kituo kikubwa cha kupoza umeme Wilayani Manyoni ili kuondoa changamoto za umeme kusafiri umbali mrefu.

Mheshimiwa Spika, matengenezo ya njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa kilovolti 33 kutoka kituo kikubwa cha kupoza umeme cha Singida kuelekea Manyoni, Itigi, Mitundu hadi Mwamagembe tayari yanaendelea na katika mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali imetenga kiasi cha shilingi 471,000,000.00 kwa ajili ya matengenezo ya njia hiyo. Vilevile mkandarasi wa njia ya reli ya *SGR* atakapomaliza ujenzi eneo la Kintinku, *TANESCO* itaunganisha njia ya umeme kutoka Wilaya ya Bahi kwenda Manyoni, hivyo kuimarisha upatikanaji wa umeme katika maeneo hayo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Yahaya Omary Massare swali la nyongeza.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana ninayo maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Manyoni inapata umeme kutoka Singida na kutoka Singida – Ikungi – Manyoni lakini Itigi – Mitundu hadi Mwamagembe, kutoka kituo kikubwa kinachopoza umeme ni karibu kilometa 400. Serikali ilikuwa na mpango wa kujenga vituo vya kupoozea umeme *substation* katika Mkoa wa Singida ikiweo Iramba na hiki cha Manyoni ambacho amekitaja kwenye majibu na cha Mitundu.

Je, ni lini sasa wanaenda kujenga vituo hivi katika Mkoa wa Singida? *(Makofi)*

Swali la pili, nguzo za zege sasa hivi tunaziona katika maeneo mengi zikiwekwa, njia hii ndefu ya kutoka Singida kama nilivyoitaja na umbali wake kutoka Manyoni lakini kutoka Itigi kwenda Mitundu mpaka Mwamagembe kilometa ni nyingi. Ni lini wataweza kuweka sasa nguzo za zege kwa sababu maeneo haya kuna maeneo chepe chepe, maeneo ya misitu lakini maeneo yenye *acid* yanakula sana nguzo hizi za miti.

Je, ni lini sasa Serikali itaanza kufanya hilo zoezi ili kufanya maisha yawe mazuri, umeme ni maisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, mojawapo ya sababu ya umeme kukatika katika maeneo mengi ni kusafiri kwa umbali mrefu. Serikali kupitia *TANESCO* ilifanya upembuzi yakinifu na kubaini mahitaji ya vituo vya kupooza umeme takribani 88 katika Halmashauri zetu zote, imetafuta fedha kupitia mradi wetu wa Gridi Imara na tukapata karibia

shilingi trilioni nne na shilingi bilioni mia mbili ambazo zitakuja kwa awamu nne. Awamu ya kwanza tumepata shilingi bilioni 500 na tutajenga vituo 15 katika Wilaya mbalimbali. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge Massare pamoja na Waheshimiwa wengine kwamba itakapofika miaka mitano, sita ijayo baada ya mradi wa Gridi Imara kukamilika, kila wilaya tunatarajia iwe na kituo cha kupoaza umeme ili umeme usisafiri umbali mrefu na kuweza kukatika katika humo njiani.

Mheshimiwa Spika, sasa vituo alivyovitaja vya Iramba, Mkalama na maeneo mengine vitajengwa pia katika awamu hizo kulingana na wale ambao wana hali ngumu zaidi kufuatia wenye hali nzuri kidogo.

Mheshimiwa Spika, kwenye eneo la nguzo za zege ni kweli Serikali inafanya jitihada za kuhakikisha inabadilisha nguzo za miti kuweka za zege katika maeneo chepe chepe, yenye wadudu waharibifu na maeneo ya mapori ambapo hatuwezi kuingia mara kwa mara kufanya marekebisho. Maeneo aliyoyasema ni ya kipaumbele na tutaenda kuyatazama ili tuyaweke kwenye mpango wa kuyabadilishia kutoka nguzo za mbao kuweka za zege ili umeme upatikane kwa wakati wote katika maeneo hayo na maeneo mengine pia. Ninakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Boniphace Nyangindu Butondo Mbunge wa Kishapu, sasa aulize swali lake.

Na. 301

**Mpango wa kuwa na Mahakama katika kila Kata**

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO** aliuliza:-

Je, nini mpango wa Serikali wa kuhakikisha kila Kata inakuwa na Mahakama hasa maeneo ya Vijijini?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria napenda sasa kujibu swali la Mheshimiwa Boniphace Nyangindu Butondo, Mbunge wa Kishapu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inayo azma na dhamira ya kusogeza huduma za haki karibu na wananchi, hususan kwa kujenga na kukarabati majengo ya Mahakama. Katika kutekeleza azma hii, tunao mpango wa ujenzi na ukarabati wa majengo ya Mahakama, katika ngazi zote, kuanzia Mahakama za Mwanzo hadi Mahakama za Rufani.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mahakama za mwanzo, dhamira ya Serikali ni kuhakikisha kuwa walau kila Tarafa inakuwa na Mahakama ya Mwanzo na baadaye tuweze kwenda hadi ngazi ya Kata kadri upatikanaji wa fedha utakavyoruhusu. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Boniphace Nyangindu Butondo swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na ninapongeza kwa majibu mazuri ya Serikali lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, ninaomba nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuunda hii Tume ya Hakijinai lakini moja kati ya mambo ya msingi ambayo Hakijinai itakwenda kuyafuatilia na kuyaona ni kuhakikisha kwamba huduma za kimahakama kwa maana ya huduma za kisheria kwa wananchi zinasogezwa.

Swali la kwanza, Kata ya Mwakipoya, Masanga, Lagana, Bunambiyu na Mwasuge ni Kata ambazo ziko pembezoni na ziko mbali na maeneo ya huduma ya kisheria. Sasa ni nini mpango wa Serikali walau wa kusogeza huduma hizi kujenga katika Kata hizi muhimu hizi Nne? *(Makofi)*

Swali la pili, huduma hizi za kisheria ni za muhimu sana na Halmashauri ama Wilaya ya Kishapu haina Mahakama ya Wilaya. Ni lini Serikali inakwenda kujenga Mahakama ya Wilaya katika Wilaya ya Kishapu? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Butondo, Mbunge wa Kishapu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza Mheshimiwa Mbunge amependa kufahamu mpango wa Serikali katika kujenga Mahakama katika kata ambazo amezitaja. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Butondo kwamba tumeshaanza kama Serikali, na mwaka huu wa fedha tumetenga Shilingi bilioni 57 kwa ajili ya kujenga Mahakama 60 za mwanzo nchini. Kwa hiyo, kata zake alizozitaja Mhehsimiwa Butondo zitafikiwa.

Mheshimiwa Spika, swali lake pili ametaka kufahamu kama tuna mpango wa kujenga Mahakama katika Wilaya ya Kishapu. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge pia,

katika mwaka huu wa fedha, bajeti hii ambayo tulileta katika Bunge hili, kati ya Mahakama 24 za Wilaya ambazo tunazijenga kwa zaidi ya shilingi bilioni 31 na Mahakama ya Kishapu ipo, kwa hiyo itajengwa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali kutoka kwenu na majibu kutoka upande wa Serikali.

Nilete tangazo nililonalo la wageni walioko hapa Bungeni asubuhi hii. Kwanza ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge.

Tunao wageni saba wa Mheshimiwa George Simbachawene, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ambao ni viongozi wa CCM kutoka Kata ya Mtera kutoka Wilaya ya Mpwapwa, Mkoa wa Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wa Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda ambao kwanza ni familia yake wakiongozwa na mke wake, Ndugu Happiness Kileo, karibuni sana. Happiness Kileo ndio yupi?

*(Hapa Ndugu Happiness Kileo - mke wa Mhe. Kilumbe S. Ng'enda alisimama)*

**SPIKA:** Haya, ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo pia wageni wengine wa Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda ambao ni viongozi wa CCM kutoka Kigoma Mjini wakiongozwa na Mwenyekiti wa Chama na Katibu wa chama, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yupo mgeni wa Mheshimiwa Jafari Chege ambaye ni Meneja wa *RUWASA* kutoka Wilaya ya Rorya, Mkoa wa Mara; na wageni wa wawili wa Mheshimiwa Rashid Shangazi kutoka *Azam Media;* karibuni sana, karibuni sana. *(Makofi)*

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Vedastus Mathayo ambaye ni Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Mwisenge; na pia wapo wageni 40 wa Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu ambao ni wanafunzi na wakufunzi kutoka Chuo cha *The Arusha East African Training Institute,* ahsanteni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mnaozungumza, bado nimesimama.

Wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Saashisha Mafuwe kutoka Jijini Arusha; wageni nane wa Mheshimiwa Mwita Kembaki kutoka Tarime; na wageni wawili wa Mheshimiwa Dkt. John Pallangyo kutoka *Star TV,* karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo pia wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, nao ni wanafunzi 80 na walimu 10 kutoka Shule ya Msingi *Heaven of Peace* ya Jijini Arusha; na wanafunzi 39 kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hao ndio wageni tulionao Bungeni. Matangazo mengine yatawajia kadri yanavyokuja hapa mbele.

Katibu.

**MHE. FRANCIS L. MTEGA:** Mheshimiwa Spika, Hoja ya Dharura.

**NDG. MONICA MWAGA - KATIBU MEZANI:** Hoja za Serikali kwamba Bunge sasa likubali…

**SPIKA:** Katibu, subiri kidogo. Mheshimiwa Francis Mtega, Mbunge wa Mbarali.

**MHE. FRANCIS L. MTEGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Kwa mujibu wa Kanuni ya 54 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo Februari, 2023 naomba kutoa hoja kwamba Bunge lisimamishe mjadala ili liweze kujadili jambo halisi la dharura na lenye manufaa kwa umma.

Mheshimiwa Spika, Jimboni kwangu Mbarali kuna mgogoro wa Tangazo la Serikali Namba 28 ambalo lilijumuisha vijiji 33 kwenye hifadhi bila kushirikisha wananchi, lakini Serikali ilifanya mchakato na kuviondoa vijiji 27 na vikabaki vichache tu kwenye hifadhi na baadhi ya vitongoji.

Mheshimiwa Spika, tulipewa maelezo na maelekezo mahususi kwamba mchakato unaendelea ndani ya Serikali kwamba wanaainisha mipaka mipya, wanafanya uthamini wa mali za wananchi na baadaye watalipa fidia na kuwahamisha rasmi.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa vile maeneo yale yaliyobaki ndani ya hifadhi ni muhimu sana kwa uchumi wa Mbarali, na ndiyo tegemeo kubwa la kilimo cha mpunga, hivyo tuliiomba Serikali yetu sikivu kwamba turuhusiwe tuendelee kulima maeneo yale na matumizi mengine hadi hapo mchakato ndani ya Serikali utakapokamilika na kupewa tangazo jipya baada ya mipaka mipya kuainishwa.

Mheshimiwa Spika, cha kushangaza hivi karibuni tarehe 6 Mei 2023 imefika helikopta Kijiji cha Mwanavala na watumishi wa *TANAPA* wamevamia wananchi, wameanza kuwapiga, kuwashambulia na kupora mifugo, ng'ombe 250. *(Makofi)*

Sasa yule mfugaji aliye-*surrender* na kuachia mifugo yake, ameathirika kisaikolojia anataka kujinyonga. Wananchi

wana kazi kubwa ya kumshikilia muda wote ili asitekeleze azma hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna kijana mwingine ambaye yeye alikomaa kutetea mifugo yake isiporwe, aliambulia kipigo cha hali ya juu sana mpaka alilazwa, na nina picha kwenye simu hapa, zikiwa *displayed* kwenye *screen* hapo, nina hakika Waheshimiwa wote mtatokwa na machozi. Walikuwepo akina mama, wamevuliwa nguo zote, wamebaki utupu, wamechukua panga, wanaweka kwenye moto wanababua mwili wote. Waliendelea kupigwa na kuteswa.

Mheshimiwa Spika, wale wananchi wanamshukuru rubani wa ile helikopta kwamba ndio yeye aliona huruma akaanza kuwaamulia na kuwaambia waache wasiwaue. Baadaye kwa hasira wakapiga risasi na kuua mbuzi wawili na mbwa watatu pale pale.

Sasa vitendo hivi kama Serikali haitachukua hatua za haraka, kwa kweli…*(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nipeni nafasi ya kumsikia. Mkipiga makofi, simsikii.

**MHE. FRANCIS L. MTEGA:** Mheshimiwa Spika, vitendo hivi vinaleta taharuki kubwa sana. Viongozi wangu wa Chama cha Mapinduzi kule wameumia sana, Waheshimiwa Madiwani wanaumiza vichwa, hawana cha kuwaambia wananchi na vilevile jambo hili limechonganisha wananchi na Serikali yao, wanashindwa kuiamini. Kwa hiyo, hali ni mbaya sana.

Majina ya waliojeruhiwa, mmoja anaitwa…

**SPIKA:** Mheshimiwa, malizia hoja yako. Unataka Bunge lifanye nini?

**MHE. FRANCIS L. MTEGA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja ya kuahirisha mjadala unaoendelea sasa ili kujadili jambo hilo la dharura ambalo linaendelea jimboni kwangu.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja itaungwa mkono nikishajiridhisha kama ni ya dharura au hapana, ndiyo utaratibu wa kanuni zetu.

Waheshimiwa Wabunge, amesimama hapa Mheshimiwa Francis Mtega, Mbunge wa Mbarali akitumia Kanuni ya 54 akitoa maelezo ambayo sote tumeyasikia yanayoeleza kwamba kuna jambo la dharura ambalo angependa Bunge liahirishe shughuli zake lijadili jambo hilo.

Sasa ametoa maelezo kwa kirefu, nadhani sote tumemsikia, sina haja ya kuyarejea. Kwa sehemu jambo ambalo amelizungumzia hapa, nafikiri wakati Waziri Mkuu akijibu maswali yaliyokuwa yameelekezwa kwake, ameeleza kuhusu utatuzi wa migogoro kwenye maeneo ambayo wananchi wanapakana na hifadhi.

Sasa ametaja baadhi ya maeneo hayo, nami siwezi kusema kama nilimsikia katika hayo maeneo kama Mbarali imetajwa au hapana, lakini ni dhahiri kwamba changamoto iliyoko Mbarali ni sehemu ya yale aliyokuwa anayasema Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba yapo maeneo ambayo yana migogoro kati ya hifadhi na wananchi.

Mheshimiwa Spika, sasa taarifa alizozitoa Mheshimiwa Mtega ninadhani ndiyo maana Waheshimiwa Wabunge wengi baada ya yeye kusema anaomba Bunge lijadili na kutoa hoja, mmesimama wengi kuashiria kwamba taarifa alizozitoa zinahitaji hatua za ziada ambayo... *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana.

Waheshimiwa Wabunge, inahitaji hatua za ziada kuliko zile za kawaida ambazo huwa zinachukuliwa, hata hivyo, kabla sijampa nafasi kwa mujibu wa kanuni zetu sasa, kwa sababu kwamba jambo ni la dharura; ni kwa sababu kuna changamoto kubwa ambayo yeye ameieleza kwa maelezo ambayo sina haja ya kuyarejea; kwamba inahitaji hatua za ziada; ndiyo, linahitaji hatua za ziada.

Hata hivyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu hapa wakati akijibu swali, kwa sababu alijibu kwa ule ujumla, na sasa yupo, hebu nimpe nafasi kidogo halafu nitatazama kama hilo jambo nilitoe kwenu tujadili ama tutakuwa tumemwelewa.

Mheshimiwa Waziri Mkuu nikupe nafasi uzungumzie hiyo hoja ambayo ameisema Mheshimiwa Mbunge wa Mbarali. *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, Serikali imemsikia Mbunge wa Mbarali akizungumzia changamoto ambayo Serikali ilishatoa maelekezo tulipofanya ziara kwenye eneo hilo.

Kwanza nimsihi asisitishe shughuli za Bunge, lakini pia nawaomba Waheshimiwa Wabunge mliounga mkono, tusifanye hivyo kwanza. Nawaomba hili kwa sababu najua jambo hili ni nyeti na linaonesha kwamba lina changamoto, na hiyo ndiyo sababu ambayo ilinifanya mimi Alhamisi iliyopita kuja hapa na kutoa kauli maalum juu ya eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo pia kupitia swali la Mheshimiwa Mwikwabe Waitara pamoja na Mheshimiwa Cherehani, nimelitolea ufafanuzi na nimeweka *commitment,* ahadi ya kwenda kutatua tatizo hilo. Naiagiza Wizara ya Maliasili sasa popote walipo Waziri, Katibu Mkuu na Mtendaji Mkuu wa

*TANAPA* waende Mkoani Mbeya kukutana na Mkuu wa Mkoa kwa kuwa…*(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu samahani kidogo.

Waheshimiwa Wabunge, naomba tumsikilize kwa sababu nadhani maelezo yangu mmeyasikia wakati nikimpa nafasi. Mtupe nafasi tumsikilize, halafu tutapiga makofi mwishoni, inanisaidia mimi kufanya maamuzi juu ya jambo hili.

Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, tulipokuwa Wilayani Mbarali na kutoa maelekezo ya vijiji vyote ambavyo vilikuwa na mgogoro wa *GN 28* ambako kulikuwa na vijiji zaidi ya 32, baada ya mapitio, kuona yale maeneo kama je, yana tija kwa wakulima au yana tija kwa hifadhi, tuliridhika kwamba vijiji 27 havina tija kwa hifadhi, na tukaruhusu vijiji hivyo viachwe wananchi waendelee kwa kilimo.

Mheshimiwa Spika, vijiji vingine vitano, hivyo vilikuwa kwenye eneo oevu, na tulikubaliana kwa pamoja, Wawakilishi wa Wilaya, uongozi wa Mkoa na *TANAPA* kwamba vijiji hivyo viachwe kwa muda huu, kwa sababu tayari walishaanza maandalizi ya kilimo, waendelee na kilimo mpaka mazao yatakapoiva, huku Serikali ikifanya tathmini. Itakapokamilisha tathmini sasa wataambiwa waondoke waende kwenye maeneo ambayo pia yameelekezwa na watakuwa wameshalipwa fidia yao.

Mheshimiwa Spika, hawa ambao Mheshimiwa Mbunge ameeleza kwamba sasa wanaondolewa bila kufuata maagizo yale, kuna maagizo pale kwamba wananchi wale wabaki maeneo yale, walime mpaka mazao yatakapoiva watafanyiwa tathmini, pande zote zimeridhika za tathmini, ndipo ndipo watapewa nafasi ya kuondoka.

Mheshimiwa Spika, lakini vijiji vitatu ililazimika viondoke kwa sababu viko kwenye eneo ambalo kabisa kabisa linatoa maji. Maelekezo haya tuliyatoa, tulikutana na wananchi, tumezungumza nao kwenye mkutano wa hadhara, wananchi walifurahi. Najua wale walioambiwa waondoke moja kwa moja hawakuridhika, lakini ni vijiji vitatu; lakini vijiji 27 viliruhusiwa kubaki kwenye maeneo yao kwa ajili ya hili na Maliasili wanajua.

Mheshimiwa Spika, sasa ilimradi Mheshimiwa Mbunge ameeleza kinachoendelea, kwanza nimuahidi kwamba Serikali tunachukua hatua mara moja ya kwenda kwa kumwagiza Waziri na timu yake ya Wizara pamoja na Mtendaji Mkuu wa *TANAPA* waende pale; na hawakupaswa kufanya hilo bila kum-*consult* Mkuu wa Wilaya ambaye anajua agizo, Mkuu wa Mkoa ambaye anajua agizo, na kwa maana hiyo, tutafuatilia maeneo yote hayo ili tuweze kuchukua hatua muhimu ili kukabiliana na hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niwasihi Waheshimiwa Wabunge kupitia Mbunge wa Mbarali kwamba tunaomba muwe watulivu wakati Serikali inachukua hatua hiyo. Hata hivyo, tayari nilishawaita Wizara, Bodi ya *TANAPA* na watendaji wa *TANAPA,* kesho saa mbili usiku kuja Ofisi kwangu kutoa maelezo ya maeneo haya yenye migogoro na hatua inayoendelea ili tuanze kufanya ziara kwa pamoja; kukutana na mamlaka za mikoa na wilaya kwenye maeneo yote yenye migogoro, pia kwenda zaidi mpaka vijijini ikiwemo na eneo la Tarime ambalo jana Wenyeviti wameridhia kurudi madarakani kwa sababu Serikali imeonesha nia ya kukaa chini na kuzungumza kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, haya tutayafanya kila mahali ambako kuna mgogoro.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, samahani; hili agizo la Mawaziri kwenda Mbarali, wanakwenda lini?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, Wizara ipo na inasikia hili. Ninaposema sasa hivi, maana yake watafute vyombo, waende. Kesho jioni saa mbili tutakutana ofisini. Nitapokea taarifa ya Tarime, nitapata taarifa ya Mbarali na tutaendelea na kikao cha kujadili na maeneo mengine.

Kwa hiyo, Wizara popote walipo, waondoke waende Mbarali, wakutane na Mkuu wa Mkoa, waende Mbarali, na wana vyombo vya usafiri, watafika leo na kesho siku nzima, saa mbili usiku tutakutana ofisini kwangu, kesho. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sote tumemsikia Mheshimiwa Waziri Mkuu na maagizo ambayo ameyatoa. Kwa hiyo, tunatarajia kwamba hawa watu wataenda huko leo, muda wowote, lakini Waziri Mkuu ataipata taarifa kesho usiku ya hicho kinachoendelea huko Mbarali.

Waheshimiwa Wabunge, sasa kwa sababu tuna changamoto nyingi zinajitokeza kwenye hii Wizara ya Maliasili na Utalii na hii migogoro, ni vizuri tukifika mahali tuwe tunalimaliza moja, tunaelekea lingine na lingine. Sasa imeagizwa Wizara ielekee Mbarali, tunatarajia itakapokuja itakuwa imetatua mgogoro wa Mbarali.

Waheshimiwa Wabunge, nadhani tuvute subira. Maelezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu yako dhahiri kwamba Mawaziri wameagizwa waelekee wapi? Mbarali, na kesho usiku yeye atapata taarifa. Sasa kama kutatokea tena changamoto, Mheshimiwa Mbunge bado yupo hapa, *Inshallah* Mwenyezi Mungu amweke, tutazipata hizo taarifa.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, tunakushukuru sana kwa maelekezo uliyoyatoa, na tunaamini tutapata mrejesho kwa wakati unaostahili. *(Makofi)*

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Matiko.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nimesimama kwa mujibu wa Kanuni ya 76 kwa jambo lililotokea na nashukuru kwa maelekezo na maagizo ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, utakumbuka takribani kama wiki tatu hivi kwenye Bunge lako tukufu alikuja Mheshimiwa Waziri Mkuu hapa akatoa *statement* ambayo kwa kweli ilikuwa ni *ridge statement* ambayo ingekuwa inatekelezwa tungekuwa tunafika mbali.

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo aliyotoa Mbunge wa Mbarali ina maana baada ya ile *statement* Waziri Mkuu ambayo ilikuwa na maelekezo makali zaidi bado tunaona watendaji wanaendelea kukiuka, maana yake kilichotokea Mbarali ni baada ya yale maelekezo ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nilikuwa nataka mwongozo wako pamoja ya kwamba Waziri Mkuu ametoa hapa *statement* ambayo inaonyesha ukali na maelekezo makali zaidi na maelekezo ya mwanzo ambayo ndiyo yalikuwa *valid* zaidi inaonekana hawa ambao wanapelekwa bado awatatui hilo tatizo ambalo linaelekezwa. Kwa sababu kama ni maelekezo yameishatolewa *several times* hao wanakaidi kwa makusudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nilikuwa naomba mwongozo wako, pamoja ya kwamba tunavumilia mpaka hiyo kesho. Wanaoteseka Tanzania siyo Mbarali tu ni Tanzania kote na ile *statement* aliyotoa Waziri Mkuu ni ya Tanzania kote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa naomba muongozo wako, Bunge li–*take charge* iweze kuundwa *something else* kwa sababu tunaona Serikali wanaelekezana bado wanakiuka. Bunge lako tukufu ambalo Serikali imeshakuja hapa inatoa maelezo mara kadhaa lakini yanajirudia rudia iiundwe Tume ya Bunge ifatilie hivi vitu viweze kuwa wazi *and for all* ili Watanzania wasiteseke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakuomba sana, kwa sababu Mwanamke kuvuliwa nguo na kuanza kupigwa na panga la moto *it is unbecoming* kabisa *it is not human at all. (Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Matiko, Kanuni ya 76 unaifahamu jambo gani unalotaka kujua kwa kutumia mwongozo ambalo haliruhusiwi ama lina ruhusiwa ni lipi?

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, la Waziri Mkuu kutoa maelekezo *yet* hayatekelezeki ni Bunge lako tukufu hili, sasa ndiyo maana nikasema hiki kinachotokea anakuja anatoa maelekezo kwenye Bunge tukufu lakini watendaji huko Serikalini hawatekelezi, *that is what happen. (Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, amesimama Mheshimiwa Esther Matiko akiomba mwongozo wa Spika kwa maelekezo ambayo ameyatoa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa Wizara ya Maliasili na Utalii. Amejielekeza kwenye kanuni ya 76 akisema Mheshimiwa Waziri Mkuu alitoa hapa maelekezo siku ya Alhamisi iliyopita ama ni ile nyingine kuhusu jambo hili ambalo limejitokeza tena na Mbunge analizungumzia.

Sasa kwa sababu amesimama Mheshimiwa Esther Matiko baada ya kuwa nimetoa maelezo ya nini cha kufanyika kuhusu jambo ambalo alikuwa ameliomba Mheshimiwa Francis Mtega, inatupeleka kwenye Kanuni ya 5; na Kanuni ya 5 ni kwamba nikishatoa maelezo yanakuwa

hayo ndiyo yaliyosimama. Kwa hiyo, huwezi kuwa unayaombea muongozo maelekezo ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu ameyatoa na mimi nimeeleza uamuzi wangu juu ya maelekezo aliyoyatoa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Sasa kwa sababu nimeishafanya maamuzi juu ya jambo hilo haliwezi tena kurejea kwangu ili nifanye maamuzi.

Waheshimiwa Wabunge, nadhani mmenisikia hapa ndiyo maana nilimuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu wanaenda huko lini? Tuipe Serikali muda wa hizi siku mbili, kwani kesho usiku Ishaallah jamani si tutakuepo? Jambo limeagizwa leo na tumeambiwa kesho usiku Mheshimiwa Waziri Mkuu atapata mrejesho na baada ya kupata mrejresho kesho ni Ijumaa wiki ijayo tutakuepo hapa.

Sasa msiwe na wasi wasi wala msiwe mnawaza kwamba kuna jambo pengine Waziri Mkuu analisema halafu hakuna mtu anafuatilia ni utaratibu wa kawaida kwa sababu maelekezo kama mlivyosema yalikuwa ni makali na yalikuwa ni mengi. Sasa Serikali inavyoyafanyia kazi haiyumkiniki kwamba ndani ya saa 24 maelekezo aliyoyatoa Waziri Mkuu yote yale yatafanyiwa kazi.

Kwa hiyo, maana yake yanafanyiwa kazi kwa utaratibu ambao Serikali imejiwekea lakini linapokuja jambo mahususi kama hili kwetu ndiyo hatua kama hizi tunaweza kuchukua. Tuwape muda wafanye kazi ndani ya hizi siku ambazo Mheshimiwa Waziri Mkuu amezisema halafu tutapata mrejesho na msiwe na wasiwasi kuhusu nia ya Bunge ya kusaidia Serikali kutatua mgogoro huu.

Bajeti ya Maliasili na Utalii iko mbele kwa hiyo msiwe na wasiwasi wala msige sana makofi leo kwamba tume iundwe, ifanye nini? Hapana tunazo namna nyingi za kuiwajibisha Serikali, tunazo namna nyingi za kuishauri Serikali na hata wao wanapotupa haya majibu ni kwasababu wanafahamu kabisa kwamba Bunge tunaweza kufanya jambo gani. Kwa

hiyo, tuwape nafasi walishughulikie hili tutapata mrejesho. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. MONICA MWAGA – KATIBU MEZANI**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano. Ninayo majina hapa mbele ya Wabunge ambao wameomba kuchangia tutaanza na Mheshimiwa Deus Sangu atafitiwa na Mheshimiwa George Natany Malima na Mheshimiwa Profesa Patrick Alois Ndakidemi ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. DEUS C. SANGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa fursa hii ya kuchangia katika Wizara hii muhimu Bajeti ya Wizara ya Maji.

Kwanza kabisa nimpongeze sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo amekuwa akiitupia jicho Wizara hii ya Maji, kwa kuipatia bajeti kila mwaka wa bajeti na imekuwa ikiongezeka kwa kweli nampongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, pili nikupongeze wewe Waziri, Naibu Waziri wako na timu nzima ya menejimenti katika Wizara hii ya Maji kazi yenu mnayofanya ni kubwa na mmeonyesha uwezo

kama vijana mnatoa chachu kubwa na jinsi mnavyoisimamia hii wizara nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia niwapongeze watendaji wenu ndani ya Mkoa wa Rukwa nikianza na meneja wa *RUWASA* Mkoa ndugu yangu Boaz na *DM* wangu Maganga pamoja na ndugu yangu Mkurugenzi wa *SUWASA* ndugu yangu Nzowa. Wanafanya kazi nzuri na tunawaamini sana mna vijana wazuri ndani ya Mkoa ya Mkoa wa Rukwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hii kabla sijaenda kwenye hoja nianze moja moja hapa kwenye jambo la watumishi, watumishi ndani ya hasa *RUWASA*. Waheshimiwa Wabunge wengi wamesema kwenye Wizara yako hasa upande wa *RUWASA* ma–*DM* wengi na mahali pengine ma–*RM* wanakaimu zaidi ya miaka miwili, mitatu. Sasa *brother* kazi yako nikubwa na una wa–*entrust* watendaji hawa kwa mabilioni ya pesa kwenda kusimamia miradi ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kuwakaimisha kwa muda mrefu hii ni jambo ambalo nakuomba waziri kaondoe hii dosari tunajua mmewafanyia *probations* ya kutosha zaidi ya miaka miwili, mitatu sasa kawa–*confirm* wawe *proper* wafanye kazi ya kusimamia Wizara yako na itaongeza ufanisi.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili; niliuliza swali ndani ya Bunge juu ya Miji midogo ya Laela na Mmpui hasa ukosefu wa maji hii miji inaisha tu kipindi cha masika baada ya hapo kunakuwa na shida kubwa ya maji. Hili jambo mmeji–*commit* kuanza kuchimba visima, lakini nikusisitizie kwa mji mdogo wa Laela *solution* narudia tena ni kutumia maji ya Mto Momba. Mmejipanga itahudumia karibia taarifa nzima ya Laela na ambayo hiyo mmejipanga kuanza upembuzi yakinifu.

Mheshimiwa Spika, naomba ulitupie jicho la pekee na ndugu yangu nakuamini nilikuletea wazo la kuchukua maji Kwela na sasa hivi ukaleta bilioni tano najua jambo la

kumaliza tatizo la maji Mmpui na Laela liko ndani ya uwezo wako ndugu yangu Aweso ujawahi niangusha katika jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili; niongelee jambo la wakandarasi. Umejitahidi sana na Wizara hii mnapata fedha nyingi, lakini kuna shida kubwa ya wakandarasi hasa wazawa. Kumekuwa na *tendency* moja ya wakandarasi kuwa na tamaa, wanaomba *tender* mikoa mbalimbali na wanakuwa na *tender* nyingi ikifika hatua *execution* wanashindwa ku–*perform* kwenye mikataba.

Mheshimiwa Spika, takupa mfano katika Jimbo langu la Kwela kuna mradi mmoja wa Ngomeni na kijiji kinaitwa Mpembano, mkandarasi alipewa kufanya zabuni yenye thamani ya shilingi milioni 940. Cha ajabu huyu bwana alikuja kuripoti *site* tukampa *advanced payment* ya milioni 100 badaye aka-*abandon site* akapotea.

Mheshimiwa Spiia, nawashukuru sana watendaji wako wa Mkoa wakiongozwa na Boaz walili–*cover* ile *advanced payments bond* ya shilingi milioni 100. Lakini tayari ilitakiwa atupe mradi ule Desemba, 2022 naambiwa mko kwenye *process* ya ku–*terminate* mmechukua muda mrefu wananchi wa Ngomeni na wa Mpembano Kata ya Lusaka wanasubiri kupata maji.

Mheshimiwa Spika, mkandarasi huyu ametuchelesha zaidi ya mwaka na ninaomba uende stepu mbili zaidi mbele msiishie tu ku–*terminate contract* lazima watufanyie watulipe *liquidated damage* hizi ambazo wamesababisha kwa kutucheleweshа.

Mheshimiwa Spika, pili, muwafanyie *debarment* mwende *PPRA* muwafungie. Hatutaki kuwa na wakandarasi ambao wanakuja kutuchezea wanaomba kazi kumbe hawana uwezo. Lakini pia nina miradi mingine inayoendelea

kuna mradi unaitwa *Mkunda Group* pale ndani ya jimbo langu huo unapeleka maji Kata ya Kaengesa Kijiji cha Kaengesa A na B na kwenda Kianda. Mkandarasi huyu ilitakiwa amalize kazi yake mwezi Aprili, lakini mpaka sasa hivi ajajenga lile tenki na kuna kazi kubwa ya ku–*supply* mabomba.

Mheshimiwa Spika, ningeomba shughuli hii ya mabomba mfanye nyie wenyewe *RUWASA* kwa kutumia *force account* huyu hawezi kufanya hii kazi la sivyo utakuja kukuta huo mradi nao unaleta shida. Hali kadhalika mradi wa Iremba mkandarasi ni hivyo hivyo bilioni 1.9 tumempa hiyo kazi, lakini shughuli yake pale ameshindwa ilitakiwa naye akabidhi mwezi wa tatu hajakamilisha na inaoneka, chukueni basi ile *part* iliyobaki mfanye kwa *force account*.

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika na mradi mwingine wa Lura Chitete huo ni mradi ambao pia ni muhimu sana ambao mkandarasi wake. Nina wakandarasi hao watatu niliokupa. Kwa mfano yule mkandarasi Kobeki wa Kwela anafanya kazi nzuri ni mtanzania mzalendo wakandarasi kama wale ndiyo tunawahitaji, umeampa kazi ndani ya muda mfupi amefikisha asilimia 75 na atatukadhi mradi mkubwa wa bilioni tano.

Mheshimiwa Spika, nikuombe Mheshimiwa Waziri katika jambo hili kaufatilie kwa umakini uwafanye *review* siyo wakandarasi tu ndani ya Jimbo la Kwela wakandarasi nchi nzima kawafanyieni *performance appraisal* muone je hawa tunawapa msiwarundikie kazi nyingi mtakuta mnawapa kazi nyingi wengine hawana uwezo wanafurahia tu ku–*apply* kazi mnawapa.

Mheshimiwa Spika, vilevile jambo lingine la muhimu ni juu ya vitendea kazi halmashauri yangu kwa maana ya Jimbo la Kwela tuna jiografia ambayo ni ngumu na inachangamoto ya miundombinu. Niombe sasa gari lile mlilotupatia limechoka *brothe,* fanya utaratibu mtafutieni *DM* ambaye

anafanya kazi nzuri aweze kutekeleza majumu yake vizuri na hatimaye asimamie miradi ya mabilioni ya pesa mnayo peleka ndani ya Jimbo la Kwela.

Mheshimiwa Spika, pia niongelee suala lingine muhimu la Ziwa ya Tanganyika kwa maana ya hii *project*. Ulifanya *commitment* kubwa hapa jana na ukachukua na ku–*quote* maneno ya Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Kwamba nia unayo na umejipanga na kujidhatiti, tunaomba sasa sisi tunatega sikio unapo *wind up* hotuba yako ya bajeti utuambie mpango kazi na mkakati ni upi juu ya kutoa maji *Lake* Tanganyika kwa Mikoa ya Rukwa, Katavi na Kigoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kweli tulikuwa na mijadala kwa Wabunge wa ukanda juu ya wewe kukushikia shilingi tunakusubiri kwenye ku *wind up commitment* gani unakuja nayo juu ya mradi huu wa kutoa maji Ziwa Tanganyika? Sisi hatuna shida tupe tu picha ambayo na ramani nzuri inayotekelezeka ili tujue mpango kazi aliyotupa Waziri ndani ya Bunge ni mpango kazi unaotekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa George Natany Malima, atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Patrick Alois Ndakidemi na Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani ajiandae.

**MHE. GEORGE N. MALIMA:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi kuchangia Hotuba hii ya Waziri wa Maji. Kwanza naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Rais, kwa jinsi ambavyo sisi watu wa Mpwampwa ametugusa kwa upande wa maendeleo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tunalo bwawa kubwa linajengwa pale Msagali lenye thamani zaidi ya shilingi bilioni 27 lakini tunayo madarasa zaidi ya 80 tumejenga katika kipindi hiki lakini pia barabara upande wa *TARURA* tumefungua barabara karibu zote za vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni pia tumepewa fedha kwa ajili ya kujenga mabweni katika shule yetu ya Sekondari ya Mpwawa *high school* ili iweze kuchukua wanafunzi wengi. Kwa hiyo, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa sababu ni mara ya kwanza Mpwapwa kupata miradi mingi hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nimshukuru sana Waziri Maji ndugu yangu Aweso. Aweso anasifa moja ni msikuvu sana, Mpwapwa tuna miradi mingi ya maji, tuna mradi wa Kisokwe – Biro – Mazae lakini tuna mradi wa Mpwapwa Mjini ambao utahudumia Ving'hawe mpaka Mang'angu lakini tuna mradi mwingine ambao unatekelezwa pale katika Kata yetu ya Lupeta ambayo utaudumia vijiiji viwili Lupeta Namakutupa. Tuna mradi katika shule yetu ya Sekondari ya Berege unaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *concern* yangu kubwa nikwamba miradi hii haitekelezeki, haikamiliki dhamira njema ya Serikali ni kumtua ndoo kichwani mama wa kitanzania lakini jambo hili linaenda linachukua muda mrefu sana. Katika miradi hii niliyoitaja katika Wilaya ya Mpwapwa ina miaka zaidi ya miwili sasa. Mheshimiwa Waziri utakubaliana na mimi kwamba kuna siku moja nilikupeleka katika Shule ya Sekondari ya Berege ukaona shida ya watoto wale, watoto wako wengi zaidi ya 1,000 hawana maji ya kunywa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukatoa maelekezo kwamba, kisima kichimbwe mara moja na kwamba kilichimbwa mara moja lakini baada ya pale watoto wale wamekuwa wakishuhudia

mtambo ule. Hakuna pampu imewekwa, na shida ya maji inaendelea katika Shule ya Sekondari ya Berege. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba sana Mheshimiwa Waziri utoe maelekezo ya haraka kama ulivyotoa mara ya kwanza kuchimba, utoe maelekezo kisima kile kiwekwe pampu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, iko miradi ya kuchimba visima virefu katika jimbo langu la Mpwapwa iko katika vijiji vya namba thelathini Kata ya Mlembule kule, Nana, Ngaramiro, Katechitemo kuna Igojirani kuna mradi wa kusambaza maji unaendelea. Mheshimiwa Waziri miradi hii kila mwaka naiona kwenye bajeti inakuja bajeti inapita vijiji hivi maji hayachimbwi, na nilikuwa nategeamea kwamba miradi ya kuchimba visima ni miradi yenye gharama ndogo sana, lakini watu wanateseka sana kwa sababu ya miradi midogo kama ile. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nikuwa nakuomba sana Mheshimiwa unapo *wind up* hotuba yako ningependa kusikia miradi hii ya Mpwapwa itatekelezwa lini? Naamini Mheshimiwa Rais angetaka kuona kweli wakinamama wakitanzania wametuliwa ndoo kichwani. Lakini naona kama tunasubiri mpaka wachoke sana ndiyo tutue hizo ndoo kichwani. Kwanini mpaka wachoke? Dhamira hii nadhani hii *slogan* ingekamilika haraka ili tutafute nyingine, tumekuwa kila mwaka tunazungumzia kumtua ndoo kichwani mama wa kitanzania lakini matokeo yake bado utekelezaji haupo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa nashauri tuwaongezee bajeti. Najua labda tatizo ni fedha ndiyo maana miradi hii aikamiliki tuongeze bajeti ili miradi hii ikamilike Waheshimiwa Wabunge siasa ya kwenye majimbo yetu ni maji piga uwa ni maji, maji lazima yapatikane. Sasa kama maji hayapatikani watu wanashuhudia mkandarasi

yupo anazunguka tu hakamilishi mradi siasa ya kule kwenye majimbo inakaa vibaya. Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana Mheshimiwa Waziri uliangalie sana jambo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulizunguzia ni utaratibu wa kutoa bili za maji, kumekuwa na malalamiko sana kwa wananchi kwamba wanabambikiwa bili maana yake nini? Maana yake bili inayokwenda, inayomkuta mraji wa maji inakuwa kubwa kuliko maji ambayo ameyatumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nadhani hii inatokana na ukweli kwamba wafanyakazi wa mamlaka zetu wengi hawafiki kwenye maeneo ambako wananchi wanatumia maji. Badala ya kusoma zile mita wanafanya hesabu za makadirio sasa katika kukadiria kuna *impact* mbili moja ni hasi kwamba Taasisi yetu ya Maji itapata hasara kwa sababu unaweza uka-*under bill* ukamuwekea bili ndogo kuliko maji anayotumia. Lakini nyingine ni kwamba mnunuaji unaweza ukamzishia bili akatakiwa kulima hela nyingi kuliko kiasi cha maji anachotumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa nashauri kwanini msi–*shift* kutoka kwenye *current billing system* mwende kama wanavyofanya watu wa *TANESCO*. Tufanye *pre-paid system* ili mtu akinunua *unit* ya maji anatumia ikiisha maji yanakatika, hili aweze kupata hiyo huduma tena lazima anunue kama tunavyonunua umeme na tunavyonunua simu hii itawasaidia kuondoa hizi lawama na kelele kwa ajili ya watumiaji wa maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kuchangia kuna hizi taasisi za watumiaji wa maji wanaita *COWSOS, ideally it was good* lakini utekelezaji wake nimeona kama umekuwa na matatizo makubwa ni changamoto kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, mfumo ni kwamba kunakuwa na kamati za maji kwenye vijiji lakini wale watendaji ambao wanafanya kazi *technical* wanaletwa na uongozi wa Wilaya wa Maji *RUWASA*. Sasa wakishwa letwa pale kinachotokea ni kwamba wale watendaji wanapo ajiriwa pale kamati ile ya wanakijiji inampa mkataba, lakini utakapompa maelekezo anapofanya vibaya hawezi kuwasilikiliza hawa anasikiliza wale waliyomleta.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kumekuwa na vurugu miradi haiendelei, matumizi mabaya ya fedha lakini wale wameletwa na mtu wa wilaya. Kwa hiyo, hawawezi kusikiliza Kamati, Kamati haiwezi kutoa ushauri kwa huyo mtu. Baadae kamati ya kijiji ambayo ndiyo wenye maji wanageuka kuwa watumwa wa mtendaji wa maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sana jambo hili Mheshimiwa Waziri walipitie upya ili waone kama kuna namna nyingine ya kubadilisha.

Mheshimiwa Spika, wameharibu mambo mengi, mahali pengine niliona Mtendaji Mhasibu wa maji ana–*paralyze* mpaka *system* ya kijiji. Wakitaka kuitisha mkutano waulize mapato na matumizi ya mradi wa maji, anahonga wenyeviti wa vitongoji ili wasiitishe mkutano asije akaulizwa hayo maswali. Kwa hiyo unakuta hata Serikali ya Kijiji haiwezi kufanya *functions* zake kwa sababu anawa–*paralyze* kwa visenti *(cent)* vilevile vya mradi wao…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa.

**MHE. GEORGE N. MALIMA:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ningeomba sana Mheshimiwa Waziri anaposimama basi

atueleze kwa nini miradi haikamiliki, na ikiwezekana aniambie Mpwapwa miradi itakamilika lini?

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge niwakumbushe ukiwa unachangia jitahidi kutazama huku mbele ukishaona nimewasha hiki ujue muda wako umekwisha umalizie sentensi.

Mheshimiwa Profesa Patrick Alois Ndakidemi, atafuatiwa na Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani. Mheshimiwa Jacqueline Kainja Andrea ajiandae.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa; na nianze moja kwa moja kwa kumpongeza sana Waziri wetu wa Maji Mheshimiwa *Engineer* Jumaa Aweso, Mheshimiwa *Engineer* Mahundi, Katibu Mkuu Kemikimba na nisiwasahau wale watendaji wetu kule mkoani *Engineer* Munishi, Kija Limbe, Mussa Msangi wa Wilaya, na kwa namna ya pekee *Engineer* Mussa wa Mfuko wa Maji. Ninawashukuru sana kwa jinsi ambavyo mnatusaidia kule Moshi Vijijini.

Mheshimiwa Spika, pongezi zangu za pili kwa Rais wetu. Mama ana nia thabiti ya kuwatua akina mama wenzake ndoo kichwani. Nasema hivyo kwa sababu tunaona bajeti ya Wizara ya maji imeongezeka kutoka shilingi bilioni 705 kwenda shilingi bilioni 756 kwenye bajeti inayokuja. Na ile ya maendeleo imeongezeka kutoka bilioni 657 mpaka 695. Hizi zote ni Juhudi za Mama, juhudi nzuri, moyo mzuri, nia njema ya kuwasaidia akina mama.

Mheshimiwa Spika, katika miradi ambayo Wizara ya Maji itatekeleza, nitachangia zaidi kwenye mradi ya maji vijijini. Nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa sababu wametenga pesa ya kutosha kabisa. Asilimia 72 ya fedha

zote za maenedeleo ambazo ni shilingi bilioni mia tano na, zinakwenda kujenga miradi 1,546 vijijini, kuhudumia zaidi ya wananchi milioni 13. Hili ni jambo zuri kusema ukweli. Sasa baada ya kusema hayo, katika bajeti hii, ukienda kwenye ukurasa wa 262, kule moshi vijijini Mheshimiwa Waziri na timu yake wametukumbuka vizuri. Tunakwenda kujengewa chanzo cha maji na kuweka mitandao ya bomba kwenye mradi wa Kilema-Okaoni ambapo wametenga shilingi bilioni 204, tunashukuru. Mnakwenda kupanua mradi wa Tema, Shishamaro na Uru Shimbe ambako mmetenga shilingi milioni 699. Mnakwenda kuboresha mfumo wa mradi wa maji katika chanzo cha Urunduma ambao utapeleka maji katika Kata za Okaoni na Kibosho Kati, mmetenga shilingi milioni 300, tunashukuru; na mmetenga shilingi 69,000,000 kwa ajili ya kufanya usanifu na kugundua vyanzo vipya vya maji katika maeneo ya Tema, Shishamaro na Uru Shimbwe, tunashukuru kwa hili.

Mheshimiwa Spika, sasa, ili tufikie ile azma na sisi watu wa Moshi Vijijini tuwe na asilimia 85 naiomba Wizara inisikilize na inisaidie kwenye mambo yafuatayo. Katika kata ya Uru Kusini kuna wakazi 31,000, na kuna miradi mitatu ya maji ambayo ni mradi wa Mang’ana, Kisimeni na Mbora. Kwenye kata hii zipo taasisi nyingi za Serikali ikiwemo Chuo Kikuu cha Kikatoliki cha Mwenge. Katika miradi hii niliyoitaja maji ni kidogo na mabomba mara nyingi yako tupu. Tunamuomba Mheshimiwa Waziri na timu yake watuletee mradi wa kuongeza maji kwenye hii miradi mitatu ili hii kata ambayo ina watu wengi sana kule kwenye jimbo langu wapate maji ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, kata ya pili ni Kata ya Arusha Chini ambako ina wakazi kama 13,900 hivi, na kwenye kata hii Vijiji vya Mikocheni na Chemchem hakuna maji, badala yake wanahudumiwa na mradi wa Kirua Kahe ambapo watu wanapeleka maji kwa punda, kwa trekta kusaidia hivi vijiji. Ni kweli hawa watu wa Chemchem na Mikocheni wana shida.

Kutokana na uhaba huu kuna mito inapita pale karibu, tunamuomba Waziri ikiwezekana mtujengee miradi hata kutoa kule mtoni tuje tutibu yale maji tuwape watu wa hii kata wapate maji kama Watanzania wengine.

Mheshimiwa Spika, kata ya *Old Moshi* Magharibi kuna mradi mkubwa wa Tellamande ambao namshukuru Waziri mkuu alikuja akaufungua. Maji ni mengi na yanapasua mabomba. Lakini eneo la *Old Moshi* Magharibi katika vijiji vya Mandaka Munono na vitongoji vya Sanindo hakuna maji. Tunaomba tu *MUWSA* wapeleke maji kwa kutumia chanzo hiki hiki au *RUWASA* watusaidie kutumia chanzo hiki ili hawa watu na wao wapate maji ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, katika kata ya Uru Kaskazini ambako kuna watu elfu kumi mia nane naa kuna chanzo kizuri cha maji ambacho kinatoa maji Uru Kaskazini kuyapeleka Uru Kusini na Kata ya Pasua kwenye Manispaa ya Moshi Mjini. Lakini wale watu wa Uru Kusini Vijijni vya Njari na Msumi hawajaunganishwa kwenye huu mfumo wa maji na maji yanataoka kwao. Nikuombe chonde chonde Mheshimiwa Waziri tuangalie hawa watu kwa sababu maji yanatoka kwao, watakuwa walinzi wazuri wa hii miradi, na wao waunganishwe katika huu maradi.

Mheshimiwa Spika, Kata ya Kimochi, ina watu 16,000. Tunaishukuru Serikali ilitupa milioni 500 na *MUWASA* bado wametupa ili kuboresha mfumo wa maji katika maeneo haya. Lakini bado vijiji vya Sango, Shiha na Kisaseni havijapata maji. Tunaomba Mheshimiwa Waziri utusaidie katika hili.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa ni Kata ya Mabogini ambayo ina watu kama 56,000, na ndiyo kata kubwa kabisa na yenye watu wengi kuliko zote katika Mkoa wa Kilimanjaro. Niombe sana, nashukuru Serikali mlitupa shiling milioni 500 tukawajengea miradi ya maji, maana kuna vijiji vilikuwa

havijapata maji tangu tupate uhuru. Niombe, kwenye Viijiji vya Mabogini kwenye Kitongoji cha Sanya *Line* D, Vijiji vya Muungano, Vitongoji vya Mwamko, Umoja, Uru, Relini, Kijiji cha Chekereni, Kitongoji cha Chekereni, Kijiji cha Maendeleo, Kitongoji cha Uarushani na Kijiji cha Mtakuja kitongoji cha Upareni, Kijiji cha Mserekia, Kitongoji cha Remiti, wanahitaji maji.

Mheshimiwa Spika, namuomba sana Mheshimiwa Waziri ni kijana mchapakazi Pamoja na timu yako. Mimi ukinitendea haya utakuwa umewatendea watu wa Jimbo la Moshi Vijijini haki, na tutaendelea kuwaombea daima.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache naomba kuunga mkono hoja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani, atafuatiwa na Mheshimiwa Jacqueline Kainja Adrea, Mheshimiwa Dkt. John Danielson Pallangyo ajiandae.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana wewe kwa kazi nzuri unazozifanya na kutusaidia sisi Wabunge wako lakini pia nimshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri ambazo anazifanya kwenye Wizara ya Maji. Nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri na Naibu wake Pamoja na Makatibu Wakuu mmekuwa wasikivu sana. Kwa kweli tuwapongeze kwa dhati kabisa kutoka kwenye mioyo yetu.

Mheshimiwa Spika, lakini pia tumpongeze sana *Engineer* Clement Kavigelo anafanya kazi nzuri; ndiye anaye-*design* miradi mikubwa ya maji hapa nchini, anafanya kazi nzuri sana. Kuna siku moja Wabunge walisema kwamba Chifu wa *TARURA* anastahili tuzo na huyu kijana anastahili tuzo, anafanya kazi kubwa, nina Imani kila Mbunge amemgusa.

Mheshimiwa Spika, mimi nijikite pia kwenye miradi yangu. Nishukuru sana, Mheshimiwa Waziri amenipatia fedha kwenye Kata yangu ya Chona Kijiji cha Itumbili milioni 500, mradi wa maji unaendelea vizuri. lakini pia umenipa fedha 1,200,000,000 Kata ya Sabasabini, mradi wa maji unaendelea vizuri na wananchi wanakunywa maji.

Ombi langu, niendele kukuomba Mheshimiwa Waziri, kuna vijiji ambavyo vinazunguka maradi wa maji ambavyo vinahitaji kupatiwa maji. Kwa mfano Kijiji cha Bungungu kiko jirani na tenki la maji lakini hakina maji. Kuna Kijiji cha Lusonzo nacho kipo jirani na tenki la maji lakini hakina maji. Niendelee kukuomba Mheshimiwa Waziri kwamba wananchi hawa tuwasaidie. Hawa ni walinzi wa miradi yetu, tu sipowasaidia maji madhara yake nina imani Mheshimiwa Waziri wewe mwenyewe ni shahidi, yanaweza ikawa makubwa sana.

Mheshimiwa Spika, vilevile kuna Kata yangu ya Igwamanoni na kwenyewe kuna mradi wa milioni 450 umenipatia maji, wananchi wa Igwamanoni Pamoja na Ilamba wanakunywa. Lakini kuna vijiji vyake ambavyo havipati maji kabisa, viko pale. Kijiji changu cha Kipangu na Nyakashagala, Kitongo pamoja na Luhaga bado havijapatiwa maji. Sasa faida ya mradi huu wa maji bado haujawafikia wananchi kwenye kata kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Spika, lakini kubwa sana, Mheshimiwa Waziri wewe mweyewe ni shahidi, hali ya Ushetu ni mbaya sana. Zaidi ya kata 11 mmepeleka magari ya kuchimba; nimpongeze sana Menaja wa *RUWUSA* Mkoa wa Shinyanga ndugu yangu Julieth, amepeleka magari yeye mwenyewe ni shahidi; lakini kinachokutana pale hakuna maji. Kata ya Ulowa ambayo ina wakazi zaidi ya 35,000 hakuna maji. Kuna Kata za Ubagwe, K Ulewe, Uyogo, Bukomela, Kinamapula, Mapamba, Ushetu pamoja na Chona ambako pia anatoka Mwenyekiti wangu wa Mkoa wa Chama Cha Mapinduzi, hakuna maji. Mheshimiwa Waziri hata kile kisima cha *pump*

angalau tungelikuwa angalau na visima vya *pump* navyo hakuna kwa sababu maji hakuna kabisa. Kwa hiyo ningekuomba Mheshimiwa Waziri unapokuja kuhitimisha naomba nijue hatma ya wananchi wangu wa Jimbo la Ushetu.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze, juzi alinitumia wataalamu wake wa *RUWASA* pamoja na *KASHIWASA* wameenda ku-*design* mradi wa Ziwa Victoria ambapo umechelewa kwa muda mrefu kwa wananchi wa Ushetu. Ulitakiwa uwe umeshafika muda mrefu, niombe Mheshimiwa Waziri aandike historia kwa wananchi wa Ushetu; ni kilomita 20 tu kutoka Kahama Mjini. Pia kuna Kata ya Igunda pamoja na kata ya Ukune, hizo ni kilomita saba kwa wananchi wanaokunywa maji ya Ziwa Victoria wao hawana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ni kipindi ambacho kama Mbunge napata wakati mgumu sana, na Mheshimiwa Waziri ni Mbunge mwenzangu anajua hali. Majimbo sita ya Mkoa wa Shinyanga, Jimbo la Ushetu tu peke yake ambalo halina mradi wa Ziwa Victoria, kata 11 hata visima vya *pump* hakuna, vinateseka, vinahangaika. Mradi wa maji wa Nyamilangano kidogo kidogo uliozinduliwa na Mwenge mwaka jana, ambao ulitumia Zaidi ya milioni kama 700, kidogo inasaidia, ambao tunaomba na wenyewe upanuliwe sasa kwenye vijiji vinavyozuunguka Halmashauri ya Kata ya Nyamilangano, Makao Makuu ya Halmashauri ili kule ambako mji unaendelea kupanuka tuweze kupata.

Mheshimiwa Spika, lakini jingine Mheshimiwa Waziri niendelee kukusihi tu kwamba shida ya maji katika Jimbo la Ushetu ni maji ya mradi wa Ziwa Victoria. Najua umeweka upembuzi pale vijana wako wamefanya kazi;akini naogopa kushika shilingi kwa kazi nzuri unazozifanya naona aibu lakini naomba tu unapohitimisha nipate jambo la kufanya kwa wananchi wa Ushetu.

Mheshimiwa Spika, kingine…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungunzaji*

**SPIKA:** Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa. Ahsante sana. Mheshimiwa Jacqueline Kainja Andrea, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. John Danielson Pallangyo, Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris ajiandae.

**MHE. JACQUELINE K. ANDREA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kuchangia katika Wizara hii ya Maji. Kwanza kabisa niweze kuipongeza Wizara kwa kazi nzuri inazofanya. Nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa namna ambavyo anahakikisha Wizara hii ya Maji anaipatia nguvu na kuiangalia kwa jicho la pili zaidi. Vilevile Waziri wetu Jumaa Aweso, Mheshimiwa Waziri hongera sana kwa kazi pamoja na dada yangu Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kazi nzuri unazozifanya. Mmekuwa ni viongozi mahiri na wenye usikivu zaidi.

Mheshimiwa Spika, Pamoja na sifa hizo nzuri lakini vile vile watendaji wa *RUWASA* napenda kuwapongeza watendaji wa *RUWASA* walioko mkoa wa Tabora hususan injinia wetu *Eng.* Kapufi, hongera sana kwake kazi zinafanyika na zioneonekana.

Mheshimiwa Spika, pamoja na sifa hizo bado Mkoa wetu wa Tabora una changamoto ya maji. Mnamo mwaka 2021 Februari, Hayati John Pombe Joseph Magufuli alikuja mkoani kwetu kuzindua mardi wa maji ya Ziwa Victoria, na akasema Mei 21, maji yatakwenda katika Wilaya tatu ambazo hazijaenda.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wetu una Wilaya saba. Kati ya Wilaya saba nne zimefikiwa na maji ya mradi wa Ziwa Victoria ni pongezi sana kwenu hiyo ni hatua nzuri, lakini Wilaya hizi

ambazo ni tatu hazijafikiwa na mradi huu wa maji zilionekana Mei 21 maji yataweza Kwenda katika Wilaya hiyo; lakini mpaka hivi sasa maji hayajaenda. Na wakasema, kuna bilioni 25 ambazo zimebaki kwenye mradi wa maji ya Ziwa Victoria kutoka Nzega na Igunga ndizo zitakazopeleka maji katika miji hii mitatu ya Urambo, Kaliua na Sikonge.

Mheshimiwa Spika, mradi huo ni miaka miwili sasa hakuna chochote kinachoendela. Wananchi wanasikiliza hotuba zinazosomwa, na ndicho wanachokiweka kichwani. Hawajui kama maofisini watu wamekaa na Mkandarasi michakato inaendelea wao hicho kitu hawajui. Wanachokitaka ni kumuona mkandarasi yuko *site* anafanya kazi wako watu na makoleo na nondo sio hizi mambo za maofisini wao hawajui.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Mheshimiwa Waziri unapokuja kuhitimisha hotuba yako hapo tunaomba utueleze wananchi wa Urambo, Sikonge na Kaliua ni lini? ni tarehe ngapi? ni mwezi gani? na mwaka gani? mkandarasi huyo ambaye ameshapatikana anasubiriwa yeye aingie *site* ataanza kufanya kazi ili wananchi hawa wa miji hii mitatu waweze kunehemeka na maji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni kwa muda mrefu sana tangu mimi nazaliwa wilaya ya Urambo tunahangaika na maji, tunaita maji ya mlindiko, tunalindika maji mpaka sasa hivi ninvyorudi nyumbani bado naendelea na heka heka ya maji ya mlindiko. Hatujui kufungua koki, wananchi wa Urambo, Kaliua na Sikonge. Tunaomba Mheshimiwa Waziri ukija hapa utueleze. Usipotueleza leo hiyo siku unayohitimisha mimi nitashikilia shilingi yako. Kwa sababu wananchi wanahitaji kujua hatma yao ya shida ya maji ili tuweze Kwenda na sera ya Mheshimiwa Rais ya kumtua mwanamke ndoo kichwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile sambamba na haya maji ya mradi wa ziwa Victoria, kaka yangu Jumaa Aweso. Maji haya ya mradi wa Ziwa Victoria hayawezi kuhakikisha kufika katika Mkoa mzima wa Tabora. Mkoa wenye kata 206, tukisubiri hayo maji ya Ziwa Victoria ndiyo yafike kote huko tutafika mpaka miaka 200 ya uhuru watu bdo hawajafikiwa na mradi wa ziwa Victoria. 2021 nilisimama hapa kuchangia katika bajeti yako, nikaomba kwamba maji tuwe na mabwawa ya kuvuna maji ya mvua. Nikushukuru mmeshatenga maeneo katika miji hii mitatu ambayo bado inahangaika sana na maji kwa mfano Ichemba wako kwenye hatua za manunuzi tunaomba hizo hatua ziharakishwe.

Mheshimiwa Spika, unaweza kukuta manunuzi tu yanachukua miaka miwili. Haya maji watu watafikiwa lini? Maji yanatuhama Tabora tuna mvua nyingi, sasa tunajikuta tunaingia kwenye adha ya kuharibu miundombinu ya barabara, tunalia na *TARURA* madaraja yameharibika. Watu wako visiwani, inapofika kiangazi maji watu wanalia hawana maji. Sasa hiki ni nini? Kwa nini tusiharakishe hii michakato ambayo mmefanya.

Mheshimiwa Spika, tunashukuru milioni 75 amabzo mmeweka kwa ajili ya Ichemba, lakini vilevile Kizengi mmeweka milioni 300 kwa ajili ya mabwawa haya ya kuvuna maji. Nikuombe hizi michakato ziendelee kwa haraka hizi ndizo zinazoturudisha nyuma kwenye kufikia asilimia 85 ya upatikanaji wa maji vijijini na asilimia 95 ya upatikanaji wa maji mjini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tukifanya haya kwa uhakika na kwa uharaka Zaidi, haya mambo yataenda pesa zipo, nini kinachocheleweshа? Mkandarasi haendi *site* kwa wakati, mnamvuta vuta kwa ajili ya nini? Kama hafai atolewe aje mtu mwingine.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba niunge mkono hoja, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa John Danielson Pallangyo, atafuatiwa na Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris, Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo ajiandae.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na mimi kwa kunipa nafasi nichangie kwenye bajeti hii ya Wizara ya Maji, Wizara ambayo ni muhimu sana kwa Watanzania kwa kuwa maji ni uhai.

Mheshimiwa Spika, niungane na wenzangu kwanza kutoa shukrani zangu na pongezi kwa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambaye kwa kweli anatufanyia Watanzania kazi nzuri sana na amedhamiria kwa dhati kabisa kuinua ubora wa maisha ya Watanzania, siyo kwenye sekta ya maji tu, lakini sekta zote. Na wewe pia Mheshimiwa Spika nakupongeza sana kwa kazi nzuri unaendesha hili Bunge kwa umahiri mkubwa. Sasa niende kwa Waziri, Waziri tunakupongeza, Waziri, Naibu Waziri na timu nzima pale Wizarani ni Pamoja na watendaji Wakuu kwenye Mkoa mnafanya kazi nzuri sana, kuhakikisha kwamba azma ya Mheshimiwa Rais ya kumtua mama ndoo kichwani inatimia; ile ndoto inatimia.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada zenu na sisi kule Arumeru Mashariki tumeopata neema, kuna miradi mingi ambayo inaendelea. Miradi ambayo inandelea sasa hivi ina takribani bilioni 12. Mradi wa Patandi unaendelea vizuri, mradi wa Nkure umemalizika wananchi wanakunywa maji na wanaoga mara tatu sasa kwa siku. Mradi wa Imbaseni Maji ya Chai ambao una bilioni sita, pamoja na Kikatiti unaendelea vizuri. Mradi wakule Uwiro bilioni nne, uko kwenye taratibu za manunuzi na taratibu zinaendelea vizuri. Kwa kweli nakupongeza na nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo niweke angalizo, tumeshuhudia changamoto za mabadiliko ya tabianchi, wakati ukame ulipotokea maji yalikosekana kabisa kule Meru. Hata Mheshimiwa Waziri wa Habari alikuwa pale *Kili Golf* alishangaa kuona kwamba, hakuna maji Meru na mlima uko jirani pale unatoa maji mengi.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni kwamba, kwa kuwa maji yale yanakwenda kwa *gravity,* kuwe na matenki makubwa kwenye vyanzo vya kuhifadhi yale maji yasipotee hovyo, lakini pia matanki ya ku-*reserve* yawe mengi kwenye *main line* kwa ajili ya kuhakikisha kwamba, *pressure* inakuwa sawasawa mpaka kule mwisho kwenye vijiji vya mwisho. Mheshimiwa Waziri, kipekee kabisa nikushukuru, tarehe 27 Februari, 2022 alikuja Arumeru Mashariki, tukafanya kikao pale kwa *DC,* nikampelekea kilio cha Korongo la Mpeduwima ambalo lilikuwa limepotea kwamba, linahitaji kufufukuliwa.

Mheshimiwa Spika, Waziri hakuchelewa akatuma wataalam wa Bonde la Mto Pangani tukaenda kufanya *survey* na badaye ile kazi ilifanyika na alikuja kuzindua. Kwa kweli, lile korongo sasa hivi limerudi kwenye hali yake. Takribani kilometa 18 lile korongo linaonekana, mvua za mwaka huu hazijaleta matatizo. Namshukuru sana ndugu yangu Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kawaida ukishasafiri safari ya kwanza inaita safari ya pili. Baada ya yale maji sasa kwamba, yamepelekwa kule mwisho, yamekwenda kuishia Kata ya Majengo, sasa Kata ya Majengo ndio inateseka, maji yanakwenda kutuama kule yanawanyima wananchi kuishi kwa furaha na amani. Nimwombe Waziri sasa aweke kwenye mipango yake, tuje tujenge bwawa pale Kata ya Majengo yale maji yakusanywe pale yaunganike na mifereji ambayo itajengwa kwa kuanzia kule Kimweli Malula kwa ajili ya kuvuna maji ya mvua na mafuriko ambayo yanatokea. Hata juzi kuna mafuriko yalitokea mpaka yakasomba gari. Yale

maji yakusanywe yapelekwe kwenye bwawa ambalo litajengwa pale Majengo, hayo maji yatumike kwa ajili ya mifugo na kwa ajili ya *irrigation. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii. Nilikuwa nataka kuongeza lingine, lakini kwa haya machache, kwa leo nasema ahsante, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris atafuatiwa na Mheshimiwa Florence Lawrance Kyombo na Mheshimiwa Ester Amos Bulaya ajiandae.

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ambayo iko mbele yetu katika Wizara ya Maji, Wizara ambayo ni muhimu katika ustawi wa maisha ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, niendelee kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya katika kuhakikisha kwamba, huduma ya maji inaendelea kuboreka nchini, lakini nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa ambayo anaifanya. Sisi Wabunge tumekuwa mashuhuda nadhani kwamba, kila Mbunge anaponyanyuka anampongeza Mheshimiwa Aweso na wasaidizi wake na watendaji wote katika Wizara yake, nami nifanye hivyo.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii, cha kwanza nieleze Bunge lako tukufu kwamba, chanzo cha maji katika Mto Ruvu ambao ndio juzi katika semina tulielezwa pale na Mheshimiwa Waziri kwamba, asilimia 76 ya uchumi wa viwanda katika Mkoa wa Dar es Salaam na Pwani unategemea Bonde la Mto Ruvu. Mto Ruvu unaanzia katika Mto unaoitwa Mbezi unaanzia katika Kata ya Kibogwa, lakini vilevile kuna Mto Mfizigo ambao unatoka kwenye Kata ya Kibungo Juu, kuna Mto Mvuha unatoka Kata ya Bungu, kuna Mto Dutumi unatoka Kata ya Kolelo, lakini kuna Mto Mngazi

unatoka Singisa na kuna Mto Mgeta Kafa unaotokea huko huko Singisa. Mtiririko wa maji hayo ndio unaofanya kwamba, ustawi wa Mto Ruvu ukamilike na wenzetu wa Dar es Salaam waendelee kupata maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina simanzi kidogo, sisi ambao ndio tunatunza vyanzo vya maji, lakini sisi tunashindwa kupata maji. Sisi tunaotunza vyanzo hivyo vya maji, sisi ndio hatupati maji, tunaendelea kupata miradi midogo midogo ya milioni mia tatu, mia nne, mia tano, mia sita, lakini unakuja kuangalia wenzetu ambao wanafaidika kwa sisi ambao tumewatunzia wanatengewa miradi mikubwa. Mheshimiwa Waziri nakumbuka alikuja jimboni nilimweleza, tuna mradi unaoitwa *Kibana Group Water Project* ambao ulikuwa unahitaji bilioni 7.8, aliniahidi kwa kujua umuhimu kwamba, sisi ndio tunaomtunzia maji, aliniahidi kwamba, kama tutashindwa kufanya kwa wakati mmoja, basi atanifanyia walau kwa awamu mbili, angenipa bilioni nne baadaye angenipa bilioni tatu mradi huo ukamilike.

Mheshimiwa Spika, katika kitu cha kushangaza na kuumiza sana kwa wananchi wa Morogoro Kusini, Halmashauri ya Morogoro, ndani ya bajeti tukaonekana kwamba, mradi huo haufanyiki. Nilienda ofisini kwake na watendaji wangu akaniahidi kwamba, tutaufanya na akasema twende tukaweke fedha, walau *token,* ili mradi ukamilike. Imewekwa milioni 200, nimwombe Mheshimiwa Waziri, tafadhali sana sana tunauhitaji Mradi wa Kibana ili wananchi waweze kupata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mradi huu ukikamilika unahitaji fedha ndogo, kama tunaweza kupeleka Dar es Salaam mabilioni kwa *billions of money,* juzi kwenye semina unaangalia kuna mahali kuna watu wanapata bilioni 90, kwa nini sisi watu wa Morogoro Kusini? Kwa nini sisi watu wa Halmashauri ya Morogoro tusipate mradi wetu huo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sitaki kusema kwamba, nitakamata shilingi, lakini naamini Waziri ni mtu mwenye hekima, ana busara. Tumekaa na watendaji wake, lile jambo ambalo ameliahidi wakati ana-*wind up* naomba aje athibitishe ndani ya Bunge kwamba, tutapata maji au hatupati kupitia mradi wetu wa Kibana ili wananchi wangu wa kata nne, vijiji 12 wakapate huduma hiyo ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kingine kuna Mradi wa *E-Water,* kuna wadau wamekubali kuweka bilioni 1.5 ili Vijiji vya Mirengwerengwe, Kijiji cha Mngazi na Dakawa waweze kupata huduma ya maji. Watu hawa wanachotaka ni *commitment* ya Serikali na kutupa kibali, ili watumbukize fedha hiyo, wananchi wapate maji na mradi huu ni mradi ambao utakuwa unarudisha fedha. Katika makubaliano na vijiji hivi ninavyovitaja na wananchi tumekubaliana kwamba, ndoo itauzwa kwa shilingi 100. Nimwombe Mheshimiwa Waziri, watupe hicho kibali, hawa wadau wakatumbukize fedha za maendeleo, wananchi wapate huduma hiyo, lakini kama wanadhani kwamba, kwa mujibu wa Sera inapingana, basi tunaomba watupatie hiyo bilioni 1.5, wananchi wangu hawa wakapate maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine nizungumzie Bwawa la Kidunda. Niipongeze Serikali kwa ujenzi wa Bwawa la Kidunda kwa sababu, ujenzi wa Bwawa la Kidunda ndio itakuwa suluhisho la uhakika wa upatikanaji wa maji safi na salama Dar es Salaam.

Naomba nitoe angalizo kwa Wizara, tunaenda kutumbukiza fedha nyingi kwenye mradi huu, ni vizuri tukaangalia uhifadhi wa mazingira. Mkoa wa Morogoro una bahati ya malisho, una bahati ya maji. Matokeo yake kipindi cha kiangazi wafugaji wanavamia vyanzo hivi nilivyovitaja vya Mto Ruvu na kuweza kukausha maji katika Mto Ruvu.

Mheshimiwa Spika, sasa nimwombe Waziri kupitia *DAWASA,* kupitia Bonde, tukaangalie jinsi gani tunaisaidia Halmashauri ya Morogoro Vijijini na Ofisi ya *DC* katika kutunza vyanzo hivi vya maji. Haiwezekani tunatoa hela sisi kama Halmashauri za *own source* kwa ajili ya kutunza maji ambayo yanakwenda kupata uhifadhi Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, vilevile kuna Mradi wa Umwagiliaji wa Kongwa Turo. Mwaka jana, mwaka juzi, ulifungwa wakati *water right users* wanalipia, lakini unafungwa kwa ajili watu wa Dar es Salaam wapate maji. Kwa hivyo, nimwombe Waziri nahitaji watu wangu wapate nao kutumia maji hayo ambayo wanayatunza, lakini vilevile tunaomba uhifadhi wa mazingira ufanyike ili kuweza kulitunza hilo Bwawa la Kidunda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine, watu wa *DAWASA,* mwaka jana wakati tunachangia bajeti, kuna mambo ambayo ni ya msingi kwa wananchi wangu wa Kata ya Serembala, bado hawajapata toka tumekubaliana wakati tunakubali kuhama ili kupisha ujenzi wa bwawa. Kuna makaburi yao hawajalipwa, kuna Kituo cha Polisi hakijajengwa, kuna maji hayajakwenda; nimwombe Mheshimiwa Waziri wakati ana-*wind a*waambie watu wa *DAWASA,* tunataka tumalizane kwa pamoja. Nilimwona Mtendaji wa *DAWASA* akaniambia kwamba, anasubiri tutakwenda.

Mheshimiwa Spika, tarehe 15 tunakabidhi Mwenge, kama Mkoa wa Morogoro. Mheshimiwa *DC* wangu yuko tayari, mimi Mbunge na mdogo wangu Mheshimiwa Tale tuko tayari, tunataka twende tukamalizane, ili kusudi mradi huo uanze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile nimwombe Mheshimiwa Waziri, jana hapa mdogo wangu Mheshimiwa Tale alisema, sisi tunatengeneza hilo bwawa kwa wenzetu wa Pwani na Dar-es-Salaam wafaidike. Tunataka na sisi bwawa hili

litusaidie kwa vijiji jirani, lakini maji ikiwezekana yafike Mvuha kwenye Makao Makuu ya Halmashauri yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, atafuatiwa na Mheshimiwa Ester Amos BUlaya. Mheshimiwa Rehema Juma Migila ajiandae.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi ya kuchangia katika Wizara yetu ya Maji. Niungane na Wabunge wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi nzuri ambayo inafanyika ndani ya Wilaya ya Misenyi, Jimbo la Nkenge na hasa kwa huduma ya maji ambayo tukiangalia historia ya miaka miwili iliyopita na sasa, tuko sehemu nzuri sana kwa miradi iliyotekelezwa.

Mheshimiwa Spika, niwapongeze sana Waziri Mheshimiwa Aweso, Naibu Waziri Mheshimiwa Maryprisca Mahundi, kwa kazi nzuri wanayoifanya, lakini nyuma yao wapo watu ambao wanawapa *support*. Kwa nafasi ya pekee pia, nimpongeze dada yangu Katibu Mkuu, Nadhifa Kemikimba, lakini na Ndugu yetu Bwana Cyprian Luhemeja, ambao na wenyewe wanashiriki kwa kiasi kikubwa kuhakikisha kwamba, wanasogea.

Mheshimiwa Spika, Wizara inafanya kazi nzuri, lakini na katika mikoa yetu wapo watendaji ndani ya Wizara hii ambao wanafanya kazi vizuri. Nichukue fursa hii pia kumpongeza *Regional Manager* wa Mkoa wa Kagera, ndugu yangu Warioba Sanya. Pia na Meneja wangu wa Wilaya ya Misenyi, bwana Andrew Kiembe, pamoja na timu zao zote kwa sababu, wanafanya kazi kwa ushirika. Mheshimiwa Waziri kama anavyojua anao watoto wengi, lakini anao wa *BUWASA*. Ninaye ndugu yangu pale John Silati naye,

Mtendaji Mkuu wa *BUWASA* pamoja na wasaidizi wake wanafanya kazi nzuri, wanamwakilisha vizuri Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijachangia nimpongeze Mheshimiwa Waziri, kulikuwa kuna mfumo ambao kidogo ulikuwa unachelewesha utendaji kazi wa manunuzi wa kikanda, sasa hivi ameupiga chini, ameuweka ngazi ya Mkoa. Nimpongeze sana kwa sababu ni hatua kubwa ambayo inarahisisha kazi kwa wasaidizi wake na kazi ikaenda kwa *speed* kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasimama hapa nikiwa nina furaha kubwa kwa niaba ya wananchi wa Misenyi. Kazi imefanyika kubwa, kata 20 zote leo tunapoongea nyingine tumemaliza suala la maji katika kata nzima, lakini sehemu nyingine tuko katika mkakati wa kupeleka maji pale. Tukiangalia Kata ya Gera maji yameenda katika vijiji vyote wananchi wanapata maji safi na salama. Ukiangalia Kata ya Ishozi mradi mkubwa wa maji uko pale, sasa hivi maji yanawekwa kwenye tenki ili ku-*test* mifumo, ili kuona maji sehemu ambapo yanaenda vizuri na sehemu ya kurekebisha.

Mheshimiwa Spika, pia tukiangalia Kata ya Buyangu, Serikali imetuletea fedha, mradi umekamilika, wananchi wa Rutunga, wananchi wa Rwamachi wanapata maji na eneo la Buyangu lililobaki tunaona tunapata maji kutoka mradi mkubwa wa Kata ya Kitobo ambapo vijiji vitano vyote vya Kata ya Kitobo, lakini na huku Vijiji vya Kishoju, Rushasha na Kikono watapata maji kutoka kwenye mradi huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaona Kata ya Nsunga mradi umekamilika na Kijiji cha pembeni cha Ngando sasa hivi kisima kinachimbwa ili kiweze kupelekewa maji. Nimwombe Mheshimiwa Waziri ambacho, wakandarasi wetu pale katika maeneo hayo miradi hii wakati mwingine malipo yanachelewa. Jana ametuambia mahususi kwamba, pochi

la mama limefunguka, tuombe basi wakandarasi hawa wapate fedha zao kulingana na maombi yao na kazi waliyofanya ili sasa waweze kukamilisha hizo kazi kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunao Mradi mkubwa wa Kyaka - Bunazi. Mheshimiwa Waziri mradi huu ni mkubwa sana na amefanya juhudi yeye pamoja na Wizara yake kuhakikisha kwamba unakamilika na ulikamilika. Mheshimiwa Rais amekuja ameuzindua mwaka jana, lakini kuna kazi kubwa ambayo wameifanya kwa kutumia akili ya kuhakikisha wanavusha maji kutoka upande wa Kyaka kwenda upande wa Kasambya kupitia katikati ya Mto Kagera. Ilisumbua sana kitaaluma kupitisha chini ya daraja, ikaonekana sio kweli, lakini wamezama ndani ya maji, maji yakavuka, lakini mwuombe Mheshimiwa Waziri thamani ya kuvusha maji yale kule mbele kwa wananchi bado haijaonekana vizuri kwa sababu, bado kuna maeneo ambayo wananchi hawajapata maji.

Mheshimiwa Spika, tukiangalia katika Kijiji cha Gablanga maji hayajafika, lakini ukiangalia Kakindo maji hayapo. Ukiangalia Mabuye sehemu imepata maji, lakini sehemu nyingine maji bado hayajafika, lakini pia ukiangalia Nyabiyanga maji yamepita baadhi ya maeneo. Tungependa kwamba, Mheshimiwa Waziri akipeleka maji katika Kijiji fulani, vitongoji vyake vyote amemaliza na hiyo kazi inakuwa imeisha.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Kyaka tunaona katika Vitongoji vya Nyakashaga, Doga, lakini pia na Bungabo bado maji hayajafika. Kwa hiyo, nimwombe Waziri kwa kazi kubwa iliyofanyika katika eneo hilo, basi aweze kukamilisha mradi huo ili uweze kuwa mradi wenye thamani kwa wananchi ambao wako katika Makao Makuu ya Wilaya ya Misenyi.

Mheshimiwa Spika, niipongeze Serikali, wakati naingia hapa kilio changu kilikuwa ni kuhakikisha kwamba, tunapata maji kutoka Ziwa Victoria na Mheshimiwa Waziri ninaposema Ziwa Victoria sisi kwetu ni hatua kumi kwenda ziwani, sio kama hizi kilometa nyingine ambazo zinaombwa kwa sababu, Ziwa Victoria liko hapo kandokando ya kata zetu. Sasa kilio changu ni Kata ya Kashenye, Mradi kutoka Ziwa Victoria sasa hivi ni mwaka wa pili, lakini nimshukuru Mheshimiwa Waziri, nimewasiliana na wataalam wangu kwamba, sasa hivi Mradi mkubwa wa Maji kutoka Ziwa Victoria kwenda katika Kata ya Kashenye katika Vijiji vyote vya Kashenye, Bukwali na Bushago, sasa hivi unaanza na taratibu za manunuzi zimeshafanyika.

Mheshimiwa Spika, mradi huu hauishii Kashenye unaenda mpaka Kata ya Kanyigo yote ili watu wapate maji safi na salama ya uhakika, unaenda Kata ya Bwanja. Nimwombe Mheshimiwa Waziri kuna kata jirani za pale ambazo zina shida ya upatikanaji wa vyanzo vya maji, kwa mfano, nikisema Kata ya Bugandika; nimwombe mradi huo ukishakuja kwa *phase* hizo jinsi walivyojipanga kibajeti, basi hata hizo kata ambazo ziko jirani zina shida ya kupata vyanzo tuziangalie ili mradi huo sasa uweze ku-*extend* mpaka Kata ya Bugandika ili wananchi waweze kupata maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naangalia maeneo mengine ambayo sasa katika bajeti ya 2023/2024 tumeweka kwenye bajeti, Kata ya Bugorora hakuna maji, lakini tunaona Kata ya Minziro. Niombe Mheshimiwa Waziri fedha hizo kinapofika kipindi cha bajeti basi tupate fedha hizo ili wananchi hawa wa kata hizo na wenyewe wasijione wapweke kwa sababu, katika kata nyingine kama nilivyosema miradi ya maji kwa kweli, ni mizuri, ni ya uhakika na mingine inaendelea. Ni pongezi sana kwa Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna kata nyingine ambazo zinahitaji maboresho, bado tunatafuta vyanzo vya maji. Kata ya Ruzinga bado mpaka sasa hivi suala la maji halijawa la uhakika, lakini tunaona Kata ya Ishunju, Mabali na Kirimilile na eneo la Mutukula, niombe sana. Tumeomba fedha milioni 450 Mheshimiwa Waziri ni kidogo kwa Kata ya Mutukula kupeleka maji katika vitongoji vyake ambavyo ni vitatu, ambavyo havina maji.

Mheshimiwa Spika, kwa kusema maneno hayo, nikushukuru kwa nafasi. Naamini sasa bajeti ya Misenyi itakamilika ili wananchi waweze kupata maji. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ester Amos Bulaya, atafuatiwa na Mheshimiwa Rehema Juma Migila na Mheshimiwa Aboubakar Asenga ajiandae.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kiukweli, kiroho safi, hata kama wengine hatupongezi hovyo hovyo, Mheshimiwa Aweso anafanya kazi na Naibu wake. Ni *term* yake ya kwanza humu Bungeni, lakini akikaa kwenye *podium* utadhani ni mzoefu zaidi. Pia nimpongeze Katibu Mkuu, nimpongeze na kaka yangu kijana wa Bunda, Naibu Katibu Mkuu, anatuwakilisha vyema wananchi wa Mkoa wa Mara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Aweso sifa yake pekee ni unyenyekevu, hajavaa cheo. Mungu ambariki safari yake ya kumtua mwanamke ndoo kichwani itimie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kuchangia na nashukuru Waziri wa Fedha yupo hapa anisikilize. Hivi kwa nini Serikali na taasisi zao hawataki kulipa madeni ya maji wakati wanatumia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa aliwakumbusha Wabunge walipe madeni ya nyumba, leo tunawakumbusha wao wasitumie maji bure, walipe pesa za maji, ili mamlaka za maji kwenye maeneo yao hizi shida ndogondogo waweze kuzifanya. Hivi mbona hatuoni wakienda sheli nyie kukopa mafuta kwenda kufanya ziara? Au kwa sababu, Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri na watendaji wake hawawezi kusimama hapa kuwadai madeni? Yaani wanatakiwa wadaiwe na wafanyakazi, wadaiwe, hata kulipa maji wanayotumia kwenye taasisi zao? Aah, *I see? (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naanza hapa kwa kutoa mfano, Tanga, Mamlaka ya Maji Tanga inadai taasisi za Serikali bilioni 2 na milioni 477, wanatumia tu. Kwa nini hawaendi *shell* kukopa? Kwa nini huku wanatumia maji hawalipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naendelea, Masasi inadai taasisi za Serikali milioni 307 na hii mpaka ilitokea aibu, mamlaka ikataka kwenda kukata maji Hospitali ya Wilaya, walipe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naendelea, haya, taasisi mbalimbali *DAWASA,* inadai bilioni 9.0 hee! Miaka mingapi hii hawajalipa bili ya maji? Wananchi wanalipa bili ya maji, *private sector* wanalipa bili ya maji, kwa nini wao hawalipi bili ya maji? Walipe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naendelea, Newala wanadai milioni 33.7, Mamlaka ya Maji Tabora milioni 126, Sumbawanga milioni 122, Kigoma milioni 534, Mtwara bilioni 1.3, Nzega milioni 22. Hapa namtetea Mheshimiwa Bashe. Naendelea, Korogwe milioni 21; Mamlaka ya Ludewa milioni 17. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi mnataka hizi mamlaka zijiendesheje? Kwa nini mnamchelewesha Waziri wa Maji Mheshimiwa Aweso safari ya kumtua mwanamke ndoo kichwani? Hivi wananchi hawa wanafanya biashara kwa

kipato kidogokidogo wanalipa bili ya maji, ninyi hamtaki kulipa bili ya maji. Wanachi wasipolipa wanakatiwa, Mheshimiwa Aweso, kwa nini usikate? Waende siku moja ofisini wakose hata maji ya kuosha vikombe vya kunywea chai. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Unipe taarifa ya Yanga kushinda, mengine siyataki. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ester Bulaya, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Waziri wa Fedha na Mipango.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge anayechangia, nimeona tangu mwanzo amesema na Waziri wa Fedha yuko hapo na kila anapochangia namuona ananiangalia.

Mheshimiwa Spika, ninataka nimpe taarifa kwamba nasi Wizara ya Fedha tunahimiza taasisi zote zinazotumia huduma zilipe. Zikishalipa wasitengeneze madeni mengine. Huu ndiyo msimamo wa Mheshimiwa Rais na ndicho ambacho tumekuwa tukisisitiza sisi tunaosimamia mafungu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ninataka nimuunge mkono Mheshimiwa Mbunge na kwa kweli nitoe rai taasisi zinapotumia huduma wanatakiwa walipe na wasitengeneze madeni, hiyo ndiyo itakayochachua uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilitaka nimpe taarifa tu maana yake nimeona ananiangalia kwelikweli. Ninaomba kutoa taarifa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ester Bulaya, badala ya kumuangalia Mheshimiwa Waziri kwa sababu unaongea na Spika mwangalie Spika ili usimtishe Mheshimiwa Waziri. Unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, mimi kwanza siipokei, lakini hapa nakuangalia wewe ambaye na wewe hutaki madeni.

Mheshimiwa Spika, hivi anaongea tu hela wamepeleka sasa, hao anaotaka walipe? Hela za bajeti tukipitisha hapa anapeleka zote kule? Lipeni madeni. Leo hapa tutataka mtuambie mtaanza kutenga shilingi ngapi ili mlipe madeni.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Kunti jana alisema, machache tu ni shilingi bilioni 33 sasa unganisha nilizozisema mimi. Mnatumia maji bure tu. Siku moja Mheshimiwa Aweso nakwambia Kata washindwe hata kuosha vikombe vya kunywea kahawa ofisini, uone kama hawatalipa madeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa mwanangu nisikilize mama yako nina ombi na andika kabisa. Nashukuru Mradi wa Maji wa Bunda wa kutoka Nyabehu umefika Mjini, umeanza kusambazwa baadhi ya maeneo. Nawe uliukuta ukiwa na asilimia 40, mimi na wewe tumefikisha asilimia 99 kufika pale Mjini, ninachotaka Kata zote 14 za Halmashauri ya Mji wa Bunda Mjini zipate maji. Tunahitaji shilingi bilioni saba tuweze kuhakikisha tumeweka miundombinu ya maji katika Kata zote 14. Hivi leo maji yanayozalishwa zaidi ya asilimia 45 hayatumiki kwa sababu gani; hakuna miundombinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Aweso, sasa nisikilize, kuna ujenzi pale wa tenki ambalo litakuwa na ujazo wa milioni tano, hapa zinahitajika bilioni tatu. Naomba huu mradi ukamilike, wananchi wa Bunda waweze kupata maji safi na salama. Kwa mfano, kueneza mtandao wa maji Kata ya

Guta, ili kata nzima iweze kupata maji zinahitajika milioni 876. Kata ya Wariku, milioni 786, Sazila milioni 564, kwenda Kiwasi milioni 687. Sasa huku ukitaka kwenda Nyamatoke – Bukole milioni 987, sasa na kusogea huku Bunda *DC* milioni 456. Tunahitaji tusiwe na mradi tu ambao umefanya maji yaje mjini, tunahitaji maji kwenye Kata zote 14. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, waliopo humu tangu 2010 wanajua huyu ni mtoto wangu niliyemlea, sasa amekua anataka kutembea kwenye Kata zote 14 wananchi wa Halmashauri ya Mji wa Bunda wapate maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Aweso jambo lingine, Mamlaka ya Mji wa Bunda bado changa, hampeleki ruzuku. Unajua shida yake? Wanaongeza bili inakuwa kubwa kwa wananchi na wanalipa kwa sababu wanahitaji maji. Tuwapunguzie mzigo, tupeleke ruzuku waweze kujiendesha. Halafu ule mradi sasa usiwe laana, uwe una neema na bili ya maji iwe *standard.* Nimesema wananchi hapa wanalipa bili za maji, ambao hawataki kulipa ni huko Serikalini tu, tunaomba bili iwe *fair,* wananchi wameupokea mradi, mkikamilisha Kata 14 watalipa bili kwa wakati na hizo fedha wataweza ku-*maintain* maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, bomba kuu linalotoka katika ule mradi linamwaga maji, linavuja, kuna upotevu mkubwa wa maji, ukitoka huku Bunda *Store* mpaka kule Nyamakokoto maji yanamwagika sana. Tunaomba muangalie, hii inachangia upotevu mkubwa wa maji. Nendeni mkaangalie tatizo ni nini kwenye lile bomba. Naomba sana, ambalo pia linakwenda mpaka kule Kaswaka, naomba muangalie sana.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, jambo lingine…

**SPIKA:** Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Ahaa, ndiyo nilikuwa nashuka mambo ya Bunda. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Pole sana. Ahsante sana. Mheshimiwa Rehema Juma Migilla, atafuatiwa na Mheshimiwa Abubakari Asenga, Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka ajiandae.

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kukushukuru kwa nafasi ili niweze nami kuchangia Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa zawadi ya uhai na afya. Pia niwashukuru Mawaziri wote wawili, Kaka yangu mzee wa ukinizingua nakuzingua, na dada yangu pale Mheshimiwa Maryprisca, mnafanya kazi nzuri, bila kuwasahau viongozi wetu, hasa wa *RUWASA, Engineer* wangu makini sana Kapufi, *Engineer* wangu wa Wilaya, *Engineer* Mapambano na kwa ushirikiano mkubwa kabisa wa Mkuu wetu wa Wilaya, Kaka yangu Rashid Chuachua.

Mheshimiwa Spika, baada ya shukrani hizo nataka nianze kuchangia Wizara hii kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Halmashauri yetu ya Kaliua yenye Kata 28, vijiji 99 na idadi ya watu 700,000 mpaka leo upatikanaji wa maji ni asilimia 45, *very shameful.* Miaka 62 ya uhuru sasa, karne ya 21 bado tuna asilimia 45 tu ya usambaaji wa maji, hii hali haikubaliki! Mheshimiwa Aweso, nikuulize, hivi ninyi Wizara yenu haina ile sera ya Wizara ya Afya kwamba mgonjwa aliye mahututi ndiye anapewa huduma haraka? Kama Kaliua tuna asilimia 45 hamtuongezei miradi mnapeleka maeneo mengine, Kaka yangu safari hii ukinizingua tunakuzingua Wanakaliua. Tunaomba miradi ya maji iende Kaliua na maji yapatikane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo ninapenda nichangie leo ni kuhusu mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria. Kwanza tuanze kushukuru kwamba katika mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria wa miji 28 na Kaliua tumo, ambao utakwenda ku-*save* Kaliua na Jimbo la Ulyankulu.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuwekwa kwenye huu mradi, tukiwa Tabora pale kwenye Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi kulikuwa kuna nyomi ya hatari, Rais wetu Hayati Dkt. John Pombe Magufuli, aliongea kwamba wakati anazindua mradi wa maji wa Tabora, Igunga na Nzega kuna fedha ilibaki shilingi bilioni 25, na akasema zile fedha zitakwenda kusambaza maji Kaliua, Urambo na Sikonge, lakini mpaka leo zile hela hatujui zimeyeyukia wapi. Kaka yangu, Mheshimiwa Aweso, leo nimesema nakuzingua kwa kushika shilingi yako, nataka nipate majibu, hizi shilingi bilioni 25 ambazo tulitengewa zimekwenda wapi, hatuoni mradi umeanza, hatuoni ma-*caterpillar* huko au wakandarasi. Kaka yangu tunaomba utupe maelezo ya kutoka hizi fedha zimekwenda wapi, kwa sababu watu bado wanapata shida ya maji, tunaendelea ku-*share* maji na wanyama, karne ya 21 hii ni aibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndoa nyingi zinakufa huko vijijini kwetu kwa sababu ya watu kwenda kutafuta maji, bado wananchi wangu hasa akina mama kule watu wanasema siyo pisi kali kwa sababu hata kusuka nywele hawasuki vizuri. Atasuka nywele aende kufuata maji mbali? Naomba Kaka yangu Mheshimiwa Aweso, leo kitaumana hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kutoa shukrani, nimeona Bwawa langu la Ichemba tumelitengea shilingi milioni 750 kwa ajili ya kuanza utekelezaji. Sasa hivi hatutaki mbambamba, yale masuala ya ukinizingua nakuzingua au ubwabwa unaonekana kwenye sahani hatutaki, tunataka kwamba tumetenga hizi fedha tuone wakandarasi wamekwenda *site* kule na hawa wakandarasi wawe ni

wakandarasi wasio makanjanja, tumeteseka kwa kutosha Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni katika gharama za uunganishaji wa maji na bei ya maji. Mheshimiwa Waziri, maji tunayotumia ni ya *RUWASA,* hatuna chanzo kingine. Kama inavyofahamika utafiti umeonesha Wilaya za Kaliua na Urambo vyanzo vya maji haviko karibu. Kwa hiyo, chanzo kikubwa cha maji ni kutumia *sources* nyingine. Urambo na Kaliua maji yaliyo karibu ni kutoka kwenye Mto Ugalla au Mto Malagarasi, lakini mpaka leo hatuoni mchakato wowote wa kuchukua maji kutoka Mto Ugalla au Mto Malagarasi.

Mheshimiwa Spika, sasa tunauliza hivi kuna agenda gani juu ya maji ya Ziwa Victoria? *Why* maji kutoka Ziwa Victoria? *Why* hatuoni mpango wa kutoa maji Ziwa Tanganyika au Mto Ugalla ambapo ndiyo karibu na kwetu Kaliua na Ulyankulu? *Why* hatuoni kuna mpango wa kuyatoa maji kutoka Malagarasi kuyaleta Kaliua lakini tunataka tuyatoe Ziwa Victoria? Kuna utafiti gani ambao mmefanya mkaona maji yanayofaa kwa matumizi ya binadamu ni ya Ziwa Victoria na siyo ya Ugalla wala siyo majiya mto Malagarasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hali hii kwa sababu mnayatoa mbali mnasababisha hata gharama za uunganishaji kuwa kubwa lakini bado hata hakuna bei elekezi, leo mtu anatamani aunganishe maji lakini kwa sababu hakuna bei elekezi maji yanachacha. Tunashukuru kuna miradi ya maji pale lakini yale maji yanachacha, watu wanaunganishiwa kwa bei kubwa lakini bado hata ndoo shilingi 50. Shilingi 50 kwa mwanakijiji jamani ni kubwa sana. Leo hana uwezo wa shilingi 50 kwenda kununua maji, matokeo yake wanasafiri umbali mrefu kwenda kuchukua maji kwenye vile visima walivyovizoea. Hebu tu-*regulate* hii bei ya maji ili wananchi wengi waweze kuunganishwa na kuendana na kasi ya Mama Samia ya kutua ndoo kichwani.

Mheshimiwa Spika, tumekalia tu kusema *RUWASA,* maji bombani, maji bombani hayatoki. Hatujawahi kufungua maji. Niombe sana huu mpango wa kuunganisha itoke bei elekezi ili hawa wananchi wetu waweze kupata maji, waweze kuingiza majumbani kwao kama inavyotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye suala hilohilo la maji, tunaona kwamba bado kuna migogoro mingi sana na ushirikishwaji kwenye miradi ya maji watu wetu hawashirikishwi. Hali hii inasababisha miradi iweze kukwama au isifanyike kwa wakati. Unakuta hata Wabunge tupo huku mambo kule yanaendelea. Matokeo yake wale wananchi wanazua migogoro, hawalipwi fidia zao, tunaomba sasa tunapopeleka hii miradi tuhakikishe kuna suala la ushirikishwaji wa wananchi kwenye hii miradi, waione kwamba ni ya kwao sasa ili hata uvunjifu wa mikataba au uharibifu mwngine usiweze kutokea. Kwa hiyo, ninaomba sana wananchi washirikishwe, kama ni fidia walipwe kwa wakati wasiwe na kinyongo. Mwananchi akiwa na kinyongo ukipeleka mradi usiku kwa usiku atauhujumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kaka yangu Mheshimiwa Aweso, naamini wewe ni kijana na ninaamini utendaji wako wa kazi na Watendaji wako mnafanya kazi vizuri sana na nina-*appreciate,* lakini leo suala la kusema ubwabwa wa kushiba unaonekana kwenye sahani Kaka yangu leo nitakamata shilingi yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, siungi mkono hoja mpaka maelezo yangu na mahitaji yetu ya Wanaulyankulu na Kaliua yatakapokamilika. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Abubakari Asenga, atafuatiwa na Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka, Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta ajiandae.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi nami niweze kuchangia katika Wizara yetu ya Maji.

Mheshimiwa Spika, wakati naanza kuchangia na mimi niwapongeze timu ya Wananchi kwa ushindi mkubwa sana na jambo zuri ambalo wamelifanya, hizi ni baraka zinazotokana na Waziri wetu kuhudhuria mechi hii, pamoja na mfadhili wetu *GSM*, Mwenyezi Mungu awabariki kutupa raha hiyo kiasi hicho. Hapo nje ya Bunge nimekutana na Naibu Waziri wa Michezo, Mheshimiwa Mwana FA, ananiambia amehamia rasmi timu ya Wananchi na ametangaza kwenye *page* yake kwamba amehamia timu ya Yanga. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, naanza kwa kuchangia Wizara yetu ya Maji kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kama mnakumbuka tulikuwa tuna suala la miji 28 na Wabunge wote ambao tunahusika na miradi ya maji katika miji 28 tulikuwa kila mara tukimsumbua Mheshimiwa Waziri kuhusu miradi hii na tulipopata nafasi ya kukaa na Mheshimiwa Rais katika kikao, Waheshimiwa Wabunge walipomuuliza Mheshimiwa Rais alisema subirini tutalifanyia kazi jambo hili na baada ya miezi sita tumeona matokeo yametoea. Nami katika Halmashauri ya Mji wa Ifakara mradi wangu wa maji wa Kiburubutu Mkandarasi amefika kwa bajeti ya shilingi bilioni 42 na sasa hivi wanapima udongo pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, nawashukuru sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, wote mmefika Jimboni kwangu mmepanda milimani kule mmeona hali halisi, nawapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watumishi wote wa Wizara hii ya Maji pamoja na *Engineer* wetu wa *RUWASA* Wilaya ya Kilombero, *Eng.* Mlelwa. Kwa kweli mradi ule wa Kiburubutu ni muhimu sana katika Halmashauri ya Mji

wa Ifakata ambako utasambaza maji katika Kata Tisa za Tarafa ya Ifakara, ni mradi muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri ni aibu sana Mji maarufu kama Ifakara wenye wajanja wengi, unapita barabarani unakutana na mabomba ya mdundiko. Ifakara *water base* yetu ipo juu ndiyo maana tunapata mafuriko kila mara. Kwa hiyo, mwananchi akichimba tu mita tatu chini anapata maji. Watu wanakunywa maji ambayo hayajapimwa, hayana viwango. Kwa hiyo, huu mradi unasubiriwa kwa kiasi kikubwa sana na kwa hamu kubwa sana ukamilike.

Mheshimiwa Spika, kuna wananchi ambao wanapanda kwenda Kiburubutu kule kuangalia kweli Mkandarasi yupo na kweli jambo hili litatokea? Maana yake ni mradi ambao umetangazwa tangu wakati wa Mwalimu Nyerere. Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Dkt. Samia Suluhu Hassan wameleta fedha na kwa mara ya kwanza tunaona Mkandarasi. Wizara na Mheshimiwa Waziri tunakuomba, umefika Ifakara umeona presha ile ya watu ilivyo kubwa wakisubiri mradi huo. Tunakuomba sana utusaidie mradi huu uweze kukimbizwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na kweli tuna imani na ile Kampuni ya *LNT* kwa sababu imekuwa ikiwaita viongozi wa Wilaya na viongozi wa wananchi, mimi mwenyewe Mbunge kila mara wanani-*update* kinachoendelea, kinachofanyika, kwa hiyo na mimi nikipita kwenye mikutano ya wananchi ninasemea. Jimbo letu la Kilombero, Halmashauri yetu ya Mji wa Ifakara unaweza ukafanya mambo yote, lakini kwa kweli Mradi huu wa Kiburubutu ndiyo namba moja kuliko vitu vyote. Kwa hiyo, ukikaa na watumishi wako wa Wizara huko muangalie muwe mnagusia jambo hili, ni kila kitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, tunaomba wakati tunaendelea na mradi huu wa maji wa Kiburubutu, gari la

Wizara lilipita kwenda kuchimba visima Jimbo jirani la Mlimba kwa ndugu yangu Mheshimiwa Kunambi na likapita pale Ifakara, tuliomba kwamba kuna visima ambavyo tulichimba tunaomba tupatiwe pesa ili visima hivi vianze kufanyiwa kazi. Vijiji cha Kanyenja, Mikoreko, Iyanga na Mtaa wa Jangwani pale Ifakara.

Mheshimiwa Spika, kwa vile mradi huu wa Kiburubutu utatumia miaka miwili mpaka mitatu, kwa haraka basi tupatiwe fedha katika maeneo haya yenye visima hivi, miradi ya maji ya matenki iwekwe pale kama ulivyotusaidia Sagamaganga na Ungongole wananchi waendelee kutumia maji haya katika miaka hii miwili au mitatu wakati wakisubiri huu mradi wa miji 28.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu, Kata zangu kumi kutokea Zinginari, Kiberege, Kisawasawa, Mwaya, Mang'ula A, Mang'ula B, Sanje, Mkula mpaka Kidatu, wananchi hawa wako kandokando ya Milima ya Udzungwa na Hifadhi ya Udzungwa, Hifadhi ile ya Udzungwa inaporomosha maji kwenda kwenye mashamba ya miwa, huko nyuma wananchi walitengeneza miundombinu yao wenyewe, walichangishana wakapeleka matenki kule juu wakajenga wakatega maji kwenye maporomoko yale ya udongo na maji yakawa yanateremka wanatumia majumbani kwao.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi imekuja *system* ya mita, hatukatai kwamba lazima tuchangie maji. imefungwa *system* ya mita kwamba tunatakiwa kuchangia. Wananchi wanauliza swali kwamba miundombinu hii tulijenga sisi, tunaweza kuzungumza na Serikali, na *RUWASA* tukakubaliana tupate bei hata ya chini sana ya kuchangia bili za maji, kwa sababu wanaenda kutoza sehemu ambako *RUWASA* haikuweka fedha. *RUWASA* wanasema kwamba huko mbeleni ikitokea miundombinu imeharibika watakarabati, lakini tayari wanatumia maji miaka yote. Kwa hiyo, tunaomba sana suala la bili kwa wananchi wetu ambayo miundombinu

ilikuwa ya kwao, ipitiwe upya, hasa elimu kabla ya kutoza ifanyiwe kazi, vinginevyo hali itakuwa ngumu sana.

Mheshimiwa Spika, mwisho ni suala la mafuriko. Tumeona Ifakara juzi tumepata mafuriko na kila mwaka karibu tunapata mafuriko. Nami nilisema suala la mafuriko katika Halmashauri ya Mji wa Ifakara ni suala mtambuka. Wizara ya Kilimo, Wizara ya Maji na Wizara ya Nishati mnaweza mkakaa mkajadili kuhusu yale mafuriko. Mamilioni ya lita za maji kila mwaka yanapotea kwenda kwenye mashamba ya watu na makazi ya watu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri amefika mpaka kwenye kile kichaka cha Mto Kilombero ambacho kilikuwa kimezibwa. Namshukuru sana *Engineer* Bonde Emmanuel anafanya kazi nzuri, wamefukua pale, maji yanapita. Tuliomba Wizara ya Nishati, tunaomba Wizara ya Kilimo, na ninyi mfukue ule mto. Kwanza utaongeza maji. *Fifty percent* sasa hivi inachangia kwenye mto Kilombero ambao Mto kilombero, ambao unachangia *sixty five percent* kwenye Bwawa la Nyerere. Kwa hiyo, tutapelaka maji kujaza Bwawa la Nyerere; pili, kwenye kilimo watapata maji yale ambayo yanapotea kwenye mabwawa ya kilimo; tatu, maji yale yanaweza yakafanyiwa utaratibu mzuri, ninyi Wizara ya Maji mkayatumia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunasisitiza sana Mheshimiwa Waziri, mafuriko ya Ifakara haiwezi kuwa historia ya mazoea. Siyo kweli. Hata wazee wetu zamani walikuwa wanaboresha tuta na mafuriko yanapungua. Sasa msizoee yale mafuriko, naomba mkae kama Wizara tatu kwa pamoja na mkisaidiana katika jambo hilo, mfikirie, na Ifakara inaweza kuondokana na mafuriko.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nawashukuru sana, naishia hapa. Mheshimiwa Wazri nakushukuru sana. Naomba

Kiburubutu, naomba suala la bili za maji na mafuriko mnisaidie. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka, atafuatiwa na Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, na Mheshimiwa Dkt. Christina Christopher Mnzava, ajiandae.

**MHE. MASACHE N. KASAKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kupata nafasi nami niweze kuchangia kwenye Wizara hii muhimu sana ya maji ambayo tunasema maji ni uhai. Nasi watu wa Chunya tunaitegemea sana Wizara hii kuhakikisha kwamba mji wetu unakuwa na maji ya kutosha. Tuna imani kubwa sana na Mheshimiwa Waziri pamoja na wasaidizi wake wote wa Wizarani, wakiongozwa na Naibu Waziri. Pia tumpongeze Mheshimiwa Rais, Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kuhakikisha kwamba anatoa fedha ya kutosha ili waweze kufanya kazi yao vizuri sana. Tunawapongeza sana.

Mheshimiwa Spika, kwenye Wilaya yetu ya Chunya, katika Mkoa wa Mbeya sisi ndio tunapata wastani wa maji ya chini sana. Sisi tunapata maji kwa wastani wa asilimia 40, ambayo ni kiasi kidogo sana ukilinganisha na mikoa mingine na ndani ya Mkoa wetu wa Mbeya. Kwa hiyo, hili jambo ambalo linafanyika hapa lazima tuliseme ili kuhakikisha kwamba maji yanapatikana ndani ya Wilaya ya Chunya. Tuwapongeze kwa kweli kwenye upande wa *RUWASA,* wanafanya kazi yao vizuri sana. Kuna miradi Chunya inaendelea ambapo pesa zinaletwa pale, na miradi mingine imeweza kufanyiwa kazi. Kwa hiyo, tunapongeza kwa kazi bora inayofanywa. Tunampongeza *Engineer Hans* pamoja na *Engineer Ismail* kwa ushirikiano wao, juhudi zao zinaonekana na wananchi wanaona kazi ambayo inafanyika.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi hiyo ambayo inaendelea kufanyika, tunashukuru pia Serikali kwa kutuletea mtambo wa kuchimba maji kwenye Mkoa wetu wa Mbeya,

na gari hili limeweza kufanya kazi kwenye Wilaya ya Chunya. Tayari katika vijiji 14, vijiji vinne vimeshafanyiwa kazi. Kijiji cha Itumbi wameshachimba maji, kikiwemo na Kijiji cha Matondo, Kijiji cha Igundu na Kijiji cha Shoga. Tunapozungumza sasa hivi, tayari fedha zote zilishalipwa, zaidi ya takribani Shilingi milioni 250, lakini wale watu wa mamlaka ya kuchimba maji, *DCCIA* hawapo eneo la *site*. Kwa hiyo, nakuomba sana Mheshimiwa Waziri uwasisitize, pesa wameshalipwa, warudi *site* ili waweze kuchimba vijiji kumi ambavyo vimebaki.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri kama anakumbuka wakati anasaini mradi wa maji wa Kiwira alituahidi kutuletea Shilingi milioni 250 kwa ajili ya mradi wa maji wa Itumbi. Kisima kimeshakamilika tayari, na tayari *Engineer* wa Maji Wilaya alishakuandikia barua ya kukukumbusha, naomba nami nikukumbushe kwa niaba ya wananchi wa Chunya na wananchi wa Itumbi utuletee hizi pesa ili mradi huo uweze kukamilika.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi nzuri ambayo inaendelea, naishukuru tena Wizara, imetuletea pesa kwa ajili ya mradi wa maji wa *extension* ya Makongorosi zaidi ya Shilingi milioni 200, kazi inaendelea, na mradi wa Matwiga pia wametuletea pesa ya kumalizia. Naomba kupitia Wizara yako, wasisitize mradi huu wa Matwiga uweze kukamilka kwa wakati. Fedha ipo, na mradi huu kutokana na kuwa ni wa muda mrefu sana, naomba sana uwasisitize mradi huu uweze kwisha ili vile vijiji vya mwanzo viwili; Kijiji cha Matwiga pamoja na Kijiji cha Isangawana, viweze kutumia maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumze kuhusu mradi wa maji wa miji 28. Sisi watu wa Chunya ni moja kati ya wanufaika wa mradi wa maji huu katika miji 28, na mradi huu wa maji, tuna imani ukikamilika utakuwa mkombozi mkubwa sana kwa wananchi wa Chunya hasa Chunya Mjini.

Mheshimiwa Spika, Sera ya Maji ya mwaka 2022 inasema kwamba, ushirikishaji wa wadau ambao ni wanufaika wa maji, lazima uzingatiwe. Kwenye Wilaya yetu ya Chunya, ukiwaza kuwashirikisha wadau, utamshirikisha Mbunge, Mkuu wa Wilaya, Mwenyekiti wa Halmashauri, Mkurugenzi, Mabaraza ya Madiwani pamoja na wananchi kwa ujumla. Kwa huu mradi wa maji ambao unaenda kwenye miji 28, tunasikitika sana kwamba ushirikishaji wake ni mdogo sana kwa sisi wadau wa Wilaya yetu ya Chunya. Katika mradi huu wa maji, sisi tuna maoni yetu namna ambavyo tunataka kushirikishwa.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Chunya ni moja kati ya Wilaya kame, na uchimbaji wa Visima umeweza kuchimbwa kwa muda mrefu na matunda yake yameonekana ni madogo sana. Mwaka 2017/2018 ulijetwa mradi wa maji wa Nyatura. Kilichimbwa kisima cha maji na lilijengwa tenki la lita karibu 500,000, lakini mpaka leo tunapozungumza, maji hayapo kwenye ule mradi. Kwa hiyo, tuna *experience* ya kutosha kuhakikisha kwamba miradi ya maji kwa kutumia visima kwa Wilaya ya Chunya sasa hivi haifai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi watu wa Chunya tulishauri na tukapendekeza kwamba ili kutatua changamoto ya maji ndani ya Wilaya ya Chunya, tuweze kutumia maji ya Mto Bwaziva na Wizara ilifanya kazi hiyo. Mheshimiwa Naibu Waziri ni shahidi, ametembelea mara kadhaa kile chanzo cha maji na mwaka huu pia aliweza kutembelea pamoja na wataalam wake wa maji kuonesha kwamba kile chanzo cha maji kitaweza kutufaa kwa muda mrefu zaidi.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya maji ya Chunya kwa sasa hivi ni takribani lita milioni mbili na nusu, na kile chanzo kina maji zaidi ya lita milioni saba na nusu kwa siku. Kwa hiyo, ni chanzo cha uhakika kwa miaka mingi zaidi. Masikitiko yetu, kupitia Mradi wa Maji wa Miji 28, wataalam wa Wizara

wanataka wautekeleze mradi huu kupitia visima, kitu ambacho tayari huko nyuma kimeshaonesha kimefeli.

Mheshimiwa Spika, watu wa Chunya wamenituma tuwaambie Wizara, sisi watu wa Chunya hatuko tayari kuona mradi huu unatekelezwa kwa takribani zaidi ya Shilingi bilioni 11 kuchimba visima vya maji ambavyo tuna uhakika kwamba havitakuwa na tija kwa muda mrefu. Nawaomba sana Wataalam wako, wiki iliyopita nilikuja Wizarani nikaonana nawe, nikaonana na Katibu Mkuu, tunashukuru wameweza kulifanyia kazi, amewatuma kule wataalam, wameshaenda kule, naomba mlifanyie kazi.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Chunya wamesema hawako tayari kuona kwamba mradi huu unatekelezwa kwa visima hivi vinavyoenda kuchimbwa kwa sababu wanajua hautaweza kuwanufaisha. Wataalam wa maji wanaishi Dar es Salaam, wanaishi Dodoma, sisi kule ndio wahanga wakubwa wa maji. Watatekeleza wanavyoona wao, lakini wakiondoka sisi ndio tutakaopata shida.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba sana, sisi watu wa Chunya ndio tunaojua adha. Mheshimiwa Waziri ana usemi wake mmoja unaosema kwamba, anayelala na mgonjwa, ndiye anayejua mihemo yake. Sisi ambao tuko Chunya, ndio tunaojua hii adha. Hao wataalam ambao wako Dodoma na Dar es Salaam, hii adha hawaijui. Naomba sana Mheshimiwa Waziri, unapokuja ku-*wind up* hapa utupe jibu la swali hili ili wananchi wa Chunya kule nao waweze kuwa tayari kupokea mradi huu.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge nimeletewa hapa ujumbe na Mheshimiwa Cherehani, lakini najaribu kutazama kwenye kiti chake simwoni. Atakaporejea, aah, yupo upande mwingine.

Mheshimiwa Cherehani umeleta ujumbe kwamba ulichangia dakika tano badala ya nane; na nimejiridhisha ni kweli ulichangia dakika tano. Kwa hiyo, ilikuwa ni kengele ya kwanza, na siyo ya pili. Sasa nitakupa nafasi ukishajiandaa kidogo ili umalizie mchango wako ambao ulikuwa hujachangia, ahsante sana. *(Makofi)*

Ahsante sana. Utakaporejea kwenye kiti chako, utaniandikia ukiwa tayari, ili nikupe dakika zako tatu umalizie.

Waheshimiwa Wabunge nilishamtaja Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Christina Christopher Mnzava, Mheshimiwa Bilakwate, ajiandae.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami nichangie hoja iliyoko Mezani inayohusu maji.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi hii. Pia nawashukuru wananchi wa Urambo kwa kuendelea kufanya kazi pamoja nami. Vile vile kipekee nitoe shukrani kwa upande wa Waziri, Mheshimiwa Jumaa Aweso na msaidizi wake wa karibu, Naibu Waziri Mheshimiwa *Engineer* Mahundi na Katibu Mkuu, *Engineer* Kemikimba; na Naibu Katibu Mkuu, *Engineer Luhemeja;* na wakati huo *Engineer* Kapufi wa Mkoa wa Tabora na *Engineer* wa kwetu Urambo ambaye tunafanya naye kazi sana katika sekta ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Kwa kweli anatujali, hasa kwenye suala la maji, tangu ameingia kazini

akiwa Rais, fedha nyingi na juhudi kubwa zake yeye binafsi na kupitia pia Wizara yake tumeziona, kwa kutupatia fedha shilingi 5,085,000,000 kwa eneo hili ikiwemo shilingi milioni 220 kwa ajili ya bwawa litakalojengwa Kalemela Urambo.

Mheshimiwa Spika, ninapokuwa kwenye mikutano yangu ya hadhara huwa naendelea kuwakumbusha wananchi wa Urambo kwamba najua changamoto za Urambo, na ya kwanza kabisa ni maji. Mengine huko yanafuata, upatikanaji wa mbolea kwa wakati, umeme na kadhalika, lakini ya kwanza huwa ni changamoto ya maji.

Mheshimiwa Spika, changamoto ya maji imekuja kutokana na aina ya miamba tuliyonayo. Pamoja na jitihada nyingi za Serikali za kuchimba visima, kwa kweli ilifikia wakati hata fedha, Shilingi milioni 500 zilirudi Wizarani baada ya Mkandarasi kushindwa kuzitumia kutokana na ugumu wa upatikanaji wa maji Wilayani Urambo. Hata hivyo, naishukuru Serikali hii, na hasa alipopata Wizara hii Mheshimiwa Jumaa Aweso, ametambua kwamba kweli Urambo kuna matatizo ya maji. Nakushukuru sana Waziri. Ndiyo maana akatuingiza kwenye miji 28. Mwenyezi Mungu akubariki sana baba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa Mheshimiwa Waziri nakuheshimu, nakupenda, mwanangu, tangu tulikwenda Chamwino tukashuhudia kusaini, maji yale bado. Nakuomba leo kwa heshima na taadhima, utakapokwenda pale mbele, hebu tamka kwa uwazi kabisa mwanangu Mheshimiwa Jumaa Aweso. Lini maji yanafika Urambo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulikwenda kushuhudia maji yalipofika Tabora, ni kilomita 90 tu, halafu kwenda Kaliua kule ni kilomita 30 tu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri utamke leo wananchi wa Urambo wapate imani na Serikali yao, wajue sasa ukombozi wa maji umefika. Hilo tu ndilo nakuomba mimi, na siendelei kukuhutubia zaidi, kwa sababu

ninachokitegemea ni hicho, kwamba leo Mheshimiwa Waziri Jumaa Aweso atatamka lini maji yanafika Urambo? Nakuomba pia, siku wanaanza ile kazi, nawe uwepo, au ukishindwa kabisa, mtume Mheshimiwa *Engineer* Mahundi ili tuzindue, na wananchi wawe na imani na Serikali yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa kuwa nategemea leo atatamka pale mbele kwamba lini maji yanafika Urambo, kazi inaanza lini? Sina haja ya kuendelea.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Christina Christopher Mnzava, atafuatiwa na Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate, na Mheshimiwa Jonas Van Zeeland, ajiandae.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema kwa kuendelea kutupa uhai na afya njema, na leo amenipa kibali cha kusimama mbele ya Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Spika, naishukuru sana Serikali ya Awamu ya Sita ya mama yetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo inafanyika katika Wizara hii ya Maji. Nawashukuru sana Waziri na Naibu Waziri pamoja na Watendaji wote. Kwa kweli mnafanya kazi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mradi wa Ziwa Victoria ulianza katika Mkoa wa Shinyanga, ukijumuisha Mkoa wa Shinyanga Mjini pamoja na Manispaa ya Kahama. Kwa kweli sisi wakazi wa Shinyanga ambao tulizaliwa miaka ya 1970 tukakulia pale Shinyanga, tunajua adha ambayo tulikuwa tunaipata. Ilikuwa

kabla hujaenda shule, ni lazima uhakikishe umechota maji, na unayachota saa nane usiku, ndiyo unaweza ukayapata yakitoka kwenye Bwawa la Lilwa; lakini sasa hivi maji katika Mkoa wa Shinyanga hasa Shinyanga Mjini na Kahama ni historia. Tunaishukuru sana Serikali yetu kwa juhudi kubwa ambazo imezifanya.

Mheshimiwa Spika, Shinyanga ina majimbo sita. Jimbo la Ushetu lipo katika Wilaya ya Kahama, lakini ni Jimbo pekee ambalo maji ya Ziwa Victoria hayajafika. Ukitoka Kahama kwenda Tabora ni kilomita nyingi, lakini kutoka Kahama Mjini kwenda Ushetu, Kijiji cha mwisho cha Manispaa ya Kahama kwenda Ushetu ni kilomita tano; kutoka Nyandekwa kwenda Ukune ni kilomita tano; kutoka Nyandekwa kwenda Igunda ni kilomita saba; lakini watu wao hawana maji. Mheshimiwa Aweso mmefanya kazi kubwa sana, na tunashukuru katika bajeti hii mmeweza kusema kwamba mmetenga Shilingi bilioni 47 kwa ajili ya maji ya Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu. Tunaomba tutakapopitisha bajeti hii, masuala ya upembuzi yakinifu, usanifu, yafanyike kwa haraka ili wananchi wa Ushetu nao waweze kuepukana na hii adha ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia maji yamefika Tabora. Kutoka Ushetu kwenda Kaliua, ni kilometa kama 40. Kule Tabora wenzetu wanapata maji, huku Ushetu hawapati maji. Wale wananchi wanakuwa wanyonge, wanaanza kuwaza vibaya kwamba kwa nini sisi tumetengwa? Mheshimiwa Waziri kwa sababu kwenye bajeti hii mmetenga fedha shilingi bilioni 47 kwa ajili ya Halmashauri ya Ushetu, tunaomba basi mweze kutekeleza suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunashukuru sana kwa Halmashauri ya Msalala, maji ya Ziwa Victoria katika baadhi ya Kata yapo, hasa katika ule mradi wa upanuzi wa maji ya Kagongwa – Isaka. Tunashukuru sana, matenki matatu yenye ujazo mkubwa wa lita 470,000, yameshajengwa, na utekelezaji umefikia asilimia 80. Kuna vijiji ambavyo vinafaidika kama

Jana, Mwalugulu na Itogwamholo, tunaomba basi, katika Halmashauri ya Msalala, kata ambazo hazijafikiwa na haya maji, waweze kupata maji. Ukiangalia Ikinda kule, maji hayajafika; ukiangalia Lunguya, maji hayajafika. Tunaomba kuwe na usawa ili kila mtu aweze kufaidi haya maji ya Ziwa Victoria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata katika Jimbo la Kishapu, Wilaya yetu ya Kishapu kuna miradi ambayo inaendelea. Kuna utekelezaji wa mradi ambao unatokea Kishapu – Mwataga, Mkandarasi tayari yuko kazini. Tunaomba huyo Mkandarasi aanze kazi mara moja. *Speed* aliyonayo Mheshimiwa Waziri, tunaomba na kwa watendaji *speed* hiyo hiyo iendelee.

Mheshimiwa Spika, pia tumepata mradi wa Shilingi bilioni 6.5 wa Igaga - Mwamashele - Ngofia – Lagana, na Mkandarasi yuko *site*. Tuseme nini sisi watu wa Shinyanga? Kwa kweli tunashukuru. Kwa sababu upungufu ni kidogo kuliko mafanikio na maendeleo ambayo tumeyapata kwenye sekta hii ya maji. Tunaomba basi sehemu ambapo kuna upungufu, Serikali iongeze msukumo. Watu wa *SHUWASA, DUWASA* na *RUWASA,* wanafanya kazi kubwa sana, wanatusikiliza Wawakilishi wa Wananchi, wanafanya mambo makubwa sana, na Waheshimiwa Waheshimiwa wa Majimbo wanapambana sana kuhakikisha kwamba wananchi wao wanapata maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie na Jimbo la Solwa, Wilaya ya Shinyanga. Kwa kweli katika Wilaya hii, nafikiri kama kuna Wilaya ambazo zimependelewa, na Mheshimiwa Mbunge ame-*fight* sana kuhakikisha kwamba wananchi wake wanapata maji, basi ni katika Jimbo la Solwa. Kwa kweli kuna miradi mikubwa ambayo inaendelea; mradi wa Tinde – Shelui, zaidi ya vijiji 34 vinapata maji, vikiwemo 22 vya Jimbo la Solwa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri, tunaomba basi utekelezaji wa sehemu ambazo maji hayajafika hasa katika miradi ambayo inaendelea na fedha zimekwisha tengwa basi maji yaweze kufika kwa wakati na wananchi wa Mkoa wa Shinyanga hususani Jimbo la Solwa, waendelee kupata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba nitoe ushauri, Serikali yetu imetenga fedha nyingi kwa ajili ya miradi ya maji, wakandarasi wako *site*, wengine wanakaribia kumaliza kazi zao, wengine wamekwisha maliza. Tunaomba muwalipe fedha kwa wakati kusiwe na ucheleweshaji wa aina yoyote. Kwa sababu unapomchelewesha mkandarasi kuna masuala mazima ya kupigwa faini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Christina, kengele ya pili imeshagonga ahsante sana.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ninaunga mkono hoja kwa asilimia 100. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate, atafuatiwa na Mheshimiwa Jonas Van Zeeland, Mheshimiwa Profesa Skukrani Elisha Manya, ajiandae.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi ya kuchangia. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu ambae amenijalia afya na nguvu za kuendelea kuwatumikia mabosi wangu wananchi wa Jimbo la Kyerwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, kuona ile ndoto yake ya kuwatua wakinamama ndoo kichwani inatimia. Pia nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Aweso, Mdogo wangu pamoja na

Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu, kwa kazi kubwa mnayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa najaribu wakati mwingine unapopata nafasi watu hawa wanaofanya kazi vizuri unaenda mbele ya Mungu kuwaombea. Wakati ninaomba kwa ajili ya Mheshimiwa Aweso pamoja na timu yake nikawa najaribu kumuuliza Mungu, hawa watu yaani ukija kuwangalia nia yao, kusudio lao ni moja yaani wamejipanga vizuri. Ukienda kwa Mheshimiwa Aweso, ni mnyenyekevu mpole, ukienda kwa Naibu Waziri hivyo hivyo, ukienda kwa Katibu Mkuu, hivyo hivyo, ukienda kwa Ndugu yangu Bwire, hivyo hivyo lakini hatujaishia hapo hata hawa watumishi mliowaweka mikoani ndugu yangu Warioba anafanya kazi nzuri pamoja na Tungaraze wanafanya kazi vizuri sana ndio maana mnaona haya mafanikio makubwa tunayoyasema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati mwingine tunapokuwa tunasifia, tunasifia kwa sababu vitu vimefanyika. Ninataka nieleze kwa upande wa Kyerwa. Miradi inayoendelea upande wa Kyerwa baada ya kukaa na Mheshimiwa Aweso na Katibu Mkuu pamoja na wasaidizi wake nikawaomba sana na ninakumbuka maneno uliyoniambia Mheshimiwa Aweso, ukaniambia hutakuwa kikwazo kutupatia maji wananchi wa Jimbo la Kyerwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukienda kwenye kata ya Murongo, kuna mradi wa milioni 589 mradi huu umekamilika, ukienda kwenye Kata ya Mabira, tuna mradi wa bilioni 768 mradi huu tenda imetangazwa na wiki ijayo mkandarasi anakabidhiwa Mradi. Ukienda kwenye Mradi wa Kata ya Nkwenda, Iteera mpka Rwabwere, Mradi wa bilioni 4 na milioni 600, mradi huu unaendelea vizuri na uko kwenye asilimia 75. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukienda kwenye kata ya Kimuli, mradi wa bilioni 2 milioni 116 unaendelea vizuri. Ukienda

kwenye Kata ya Kaisho, Isingiro na Rutunguru, mradi wa bilioni 1 na milioni 900 mradi unaendelea vizuri, tukienda kwenye Kata ya Rwabwere, mradi wa milioni 738 umekamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Aweso, ninakushukuru sana maana nilikusumbua sana lakini ukasema hautakuwa kikwazo ni hakika maneno yako nimeanza kuyaona. Mungu akubariki na ninasema kama mtumishi wa Mungu kama Mungu wangu aishivyo hatakuacha wala kukupungukia wewe pamoja na timu yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru, pamoja na kupongeza hawa watu namna walivyojipanga, ukiangalia hata wakandarasi wanaowaleta ni wakandarasi ambao wako makini. Mkandarasi mliyempa mradi kule Kyerwa anaitwa *JAMTA*, mkandarasi huyu ameanza kufanya kazi hata kabla hajaanza kulipwa. Ukiangalia miradi yote inayoendelea yuko karibu asilimia 80 lakini angalia alipolipwa ni kwenye kama asilimia 40 au asilimia 50. Wakandarasi wa namna hii tuwalinde na tuendelee kuwaunga mkono na kuwapa miradi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri, tumekaa tena na wewe, Katibu Mkuu lakini pia Waziri wa Fedha. Tunao mradi ambao unakwenda kuhudumia Kata ya Kyerwa, Kata ya Nyaruzumbura, Kata ya Nyakatuntu, Kata ya Kitwe, Kata ya Bugara, Kata ya Kikukuru, Kata ya Kitwechenkura. Mradi huu unahitaji fedha nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimekuomba na tumekaa sana na Mheshimiwa Waziri wa Fedha, mmenihakikishia mradi huu unakwenda kuanza na nimeuona kwenye bajeti mmeuweka. Niombe sana kama ambavyo umekuwa msaada, umekuwa mtu wa karibu kwa wana Kyerwa wewe pamoja na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na wasaidizi wako. Nikuombe mradi huu tunapomaliza bajeti uweze kuanza ili wananchi wa

Kata hizi ambazo nimezitaja na wao waweze kupata maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu Kyerwa mnaweza mkaona ni miradi mingi. Kyerwa tulikuwa mbali sana hatukuwa na miradi, miradi mingi ambayo walikuwa wanapigia mahesabu ile miradi ya zamani. Kwa hiyo, niombe sana Mheshimiwa Waziri, miradi hii iweze kukamilika ili wananchi wangu, mabosi wangu wa Jimbo la Kyerwa na wao waweze kupatiwa maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ambacho nilikuwa nataka nishauri Serikali, ukija kuangalia Mkoa wa Dodoma ni Mkoa ambao tunatumia maji ya kuchimba. Lakini maji haya ni maji ya chumvi, ni maji kiasi gani tunayoyapoteza? Maeneo mengi Mkoa wa Dodoma mafutiko ni mengi. Mheshimiwa Aweso, sisi tunakuamini pamoja na timu yako, hebu angalia ni namna gani tunaweza tukavuna maji yanayopotea ili wananchi wa Mkoa wa Dodoma waweze kupata maji, yanaitwa maji safi, maji laini? Yale maji ambayo sio maji chumvi. Mheshimiwa Waziri, kwa hiyo, niombe sana hili uliangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine wameeleza hapa Wabunge, Wizara ya Maji madeni ni mengi mnayodai. Kwa nini msije na mfumo wa mtu kulipia kama tunavyolipia umeme akalipia maji ili kuondoa hii adha ambayo mnaipata ya madeni kuwa mengi? Lazima tuje na ubunifu, mwananchi anakwenda analipia akishamaliza kulipia ndio anapata huduma ya maji. Vinginevyo, Mheshimiwa Aweso, hawa watu wataendelea kukukwamisha pamoja na Waziri wa Fedha. Tunataka tupate pesa hii ili pesa hii iende kuwasaidia wananchi wengine maeneo mengine ambayo bado hawajapata maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, nikushukuru tena na nikutakie kila la heri. Lakini ndugu zangu niwaombe, pamoja

na hawa watendaji kufanya kazi nzuri hebu tumkumbuke Rais wetu ambae kwa kweli anafanya maajabu katika nchi hii. Tumuombee kwa Mungu ili Mungu aendelee kumlinda, aendelee kumpa afya njema ili aendelee kuwatumikia watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Jonas Van Zeeland, atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Shukran Elisha Manya, Mheshimiwa Emmanuel Cherehani, ajiandae kumalizia muda wake.

**MHE. JONAS V. ZEELAND:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nianze kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa zawadi ya uzima. Pili, nimshukuru sana ndugu yangu Mheshimiwa Aweso pamoja na Naibu wake, kwa kazi nzuri wanazozifanya kwenye Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Spika, sisi Mvomero, tuna miradi ambayo inaendelea ya zaidi ya shilingi bilioni 12. Nichukue nafasi hii pia kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mvomero, kumshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Rais, kwa kutupa fedha nyingi za Miradi ya Maji. Haijawahi kutokea kupata miradi mingi ya maji kwa pamoja kama ambavyo tumepata sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri, yako mambo machache ambayo tutaomba utusaidie kwenye hii miradi ambayo wakandarasi wapo *site* wanaendelea na kazi. Mfano kule Kibogoji na Pandambili, mlitupatia milioni 530 na mradi ule umekamilika. Lakini kuna tatizo baadhi ya vituo havitoi maji na mradi huu hauna hata miezi mitatu, minne.

Mheshimiwa Spika, tuna Kijiji kimoja pale Dibuluma kipo katika Kata ya Kibati hakina maji kabisa. Tunaomba mtusaidie

ili ili tuweze kuunganisha vijiji vyote vya kata ya Kibati viweze kupata maji. Tuna vijiji vya Ndole kule Kinda, Matale pale Mvomero mmetupatia milioni 978, tatizo pale bado kitongoji kimoja ambacho kipo kwenye mkataba wa mkandarasi, kitongoji kile hakijapata maji na mkandarasi hataki kuweka maji kwenye kile kitongoji. Nimekwisha zungumza sana na *engineer* wetu wa Mkoa na *engineer* wa wilaya lakini bado tatizo hili halijaisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri, kwa mara ya kwanza Tarafa ya Mgeta ambayo ina vyanzo vyenye uhakika vya maji, haikuwahi kupata miradi mingi kama ambavyo umetupatia safari hii. Mwaka 2021 nilismama hapa nikakuomba miradi mingi sana nashukuru sana mmetupa ile miradi. Tuna miradi kule Chenzema, Luale, Kibuko, Londo, Masalawe na Kibagala, mkandarasi anaendelea kazi ya shilingi bilioni 2.2 mkandarasi yuko kwa asilimia 60. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna changamoto hapa Mheshimiwa Waziri, mkandarasi huyu anapo *rise certificate* kwenu mnachelewa sana kumlipa. Kazi hii itachukua muda mrefu kama atacheleweshewa malipo yake. Naomba anapoleta *certificate* alipwe kwa wakati ili kazi iendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kuna mradi kule Lusungi – Mwalazi wa shilingi bilioni 2.3 mradi huu unakwenda kwenye vitongoji vya Nyabeni A na Nyabeni. Niliomba mwaka 2021 tunashukuru mmetupatia hizi fedha mkandarasi yuko kwa asilimia 25 na yeye anasuasua, ukimuuliza nini anasema malipo hajapata.

Mheshimiwa Spika, tuna mradi mkubwa na Mheshimiwa Waziri ulikuja Mvomero, wananchi wamefurahi sana ujio wako uliokuja kule Mvomero. Kazi kubwa ambayo tunaifanya ya kutoa maji kule Bunduki - Maguruwe yanapita Homboza – Mlali halafu yanakwenda Kipela, Kinyenzi, Mkuyuni, Lukuyu,

Mgeta. Vijiji vingi vitapata maji kutokana na huu mradi isipokuwa kuna vijiji viwili ambavyo viko kwenye kata ya Mlali, Kijiji cha Vitonga na Lugono hamjaweka kwenye huu mradi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri, nikuombe sana ule mradi haiwezekani watu wa Kipela wapate maji, watu wa Mkuyuni wapate maji lakini watu wa Vitonga na Lugono wasipate maji wakati maji yatakuwa yamefika karibu kabisa na maeneo yao. Mheshimiwa Waziri, niombe sana tufanye marekebisho kidogo, mkandarasi aongezewe fedha aweze kufikisha maji kwenye hivi vijiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, Mheshimiwa Waziri, Tuliani tuna mradi mkubwa wa maji wa shilingi bilioni 3 na milioni 600, mkandarasi yupo *site*. Lakini nina wasi wasi na huyu mkandarasi atakuwa ni msanii mjanja mjanja. Kwa sababu mpaka sasa hivi amefanya kazi chini ya asilimia 10. Mradi wa bilioni 3.6 atamaliza mwaka gani? Kwa hiyo, niombe sana Mheshimiwa Waziri, Wizara yako imchunguze huyu mkandarasi nina wasi wasi nae.

Mheshimiwa Spika, pia kwenye Mradi wa *TUILIWASA* ambao huyu mkandarasi wa bilioni 3.6 anakwenda kusambaza maji kwenye Tarafa nzima ya Tuliani. Tatizo la ule Mradi wa *TULIWASA* bili ambazo wananchi wanalipa, wanaletewa bili mwisho wa mwezi baada ya kutumia ni kubwa sana. Huu mradi haya maji ni ya mseleleko sio maji ya kuvuta na umeme. Hayana gharama kubwa sana kuyapata haya maji.

Mheshimiwa Spika, kwa mwezi wanapewa bili kubwa kiasi kwamba wanashindwa kulipa, wengine sasa hivi wanaanza kutumia visiwa. Watu wa *TULIWASA* wanaanza kuwakamata watu ambao wanataka kuwasaidia wananchi kuwachimbia visima. Sasa kama wao wanashindwa kuja na bei ambayo mwananchi wa kawaida ataweza kulipa mwisho wa mwezi, wawaache hawa wananchi wakitaka kutumia

visima watumie visima. Kama wanataka washushe *unit* moja ya maji iende mpaka 840 ili wananchi waweze kulipa mwisho wa mwezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia tuna mradi mkubwa pale Dakawa wa bilioni 2.3. Mkandarasi amesaini mkataba huu mwezi wa pili anasuasua tu hatujui tatizo ni nini? Leo nimezungumza na Injiania wa Mkoa amenihakikishia wiki ijayo ataanza kazi wako kwenye makabidhiano. Sasa miezi miwili fedha za Mheshimiwa Rais zimeletwa ziko pale mkandarasi haeleweki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunashukuru sana mmetupatia fedha za kuchimba vizima tisa kwa milioni 378, tumechimba kule Msongozi. Kata ya Msongozi ina tatizo kubwa sana la maji. Pia pale Magali, Melela, lugono, Makuyu kule Mvomero, Milama, Manza na Sokoine.

Mheshimiwa Spika, kipekee nikushukuru sana Mheshimiwa Waziri, nilikuomba utusaidie kutupatia fedha kwa ajili ya kutatua tatizo la Maji pale Sokoine. Wananchi wa Sokoine walikwa wanakunywa maji na Wanyama. Ziko *clip* ambazo nilikutumia Mheshimiwa Waziri na nilikuomba utusaidie, ukatupatia mitambo imechimba visima virefu na sasa hivi wanaendelea na ujenzi, wanajenga chumba kikubwa kwa ajili ya kuhifadhi mashine lakini wanajenga pia na *tank* kwa ajili ya kuhifadhia maji waanze kusambaza kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, niombe sana msukumo wako kwa sababu wananchi wa Sokoine wameteseka kwa muda mrefu kwenye adha ya maji. Niombe msukumo wako kwa huyu ambae anasimamia pale mradi, ahakikishe kwamba mradi huu ikiwezekana mwezi wa saba kama ulivyotuahidi ulivyokuja Mvomero ili wananchi waanze kupata maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda Mvomero tuna shida ya gari. Mheshimiwa Waziri, hatuna gari, injinia wetu ana gari bovu halijapata kutokea. Tunaomba utupe gari ili injia aweze kukimbia kimbia. Kwa sababu ya jiografia yetu nafikiri unaijua vizuri…

**SPIKA:** Mheshimiwa Jonas, kengele ya pili imeshagonga.

**MHE. JONAS V. ZEELAND:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Profesa Shukrani Elisha Manya, atafuatiwa na Mheshimiwa Emmanuel Cherehani, Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya ajiandae.

**MHE. PROF. SHUKRANI E. MANYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ya Waziri wa Maji, ambayo anataka Bunge limuidhinishie bilioni 756.21 kwa ajili ya kuendelea kuwapelekea huduma ya maji watanzania. Nakushukuru sana.

Mheshimiwa Spika, moja ya sekta ambazo zimeiheshimisha Serikali ya Awamu ya Sita ni sekta ya maji. Hii ni kwa sababu ya miradi mingi ambayo imekwenda moja kwa moja kwa wananchi na haya hayawezekani isipokuwa kwa utendaji mzuri wa watendaji wa Wizara, Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote. Kwa msingi huo kwa kweli pongezi wanzozipokea wanastahili. Kwa mtindo wanaokwenda wanaitekeleza kabisa azma ya Mheshimiwa Rais, kuwatua wanawake ndoo kichwani na tunawaombea baraka zote za Mwenyezi Mungu juu ya hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitangulie kuunga hoja mkono kwamba Wabunge wote tuweze kukubali bajeti hii ya bilioni 756.21 iweze kwenda kuwasaidia wizara kutekeleza majukumu yao katika mwaka fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, ninazo hoja tatu za kuchangia katika hotuba ya Waziri asubuhi ya leo.

Mheshimiwa Spika, moja ni ambayo imezoeleka kwa lugha rahisi ya *local content* lakini kiswahili chake ni uwezeshaji watanzania kushiriki ujenzi wa miradi mikubwa ya maji. Katika hoja hii mara nyingi sana tunazo hoja mbili muhimu kwa nini watanzania au kampuni za kitanzania huwa hazipewi kandarasi katika ujenzi wa miradi mikubwa ya maji.

Mheshimiwa Spika, moja ni uwezo wa kitaalamu; pili, ni mtaji. Lakini kama nitakavyoongea haya mambo mawili yametucheleweshа na kwa misingi hiyo fedha nyngi imeendelea kupelekwa kwa kampuni za nje kumbe tunaweza. Kwa sababu gani ninasema hivi? Ukweli si kwmba hawana uwezo. Je, wamepewa nafasi kuonesha uwezo wao? Kamati yetu ya Maji na Mazingira ilitembelea mradi wa Dareda – Sigino – Singu – Bagala ambao pia unaleta maji katika Mji wa Babati. Tulichokiona Mradi huu ulisanifiwa na wazawa, wale wa *BAWASA,* wataalam wazawa lakini mradi huu pia umejengwa na wazawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mradi huu pia ukaokoa bilioni 15 ukatumia bilioni 12.7 badala ya bilioni 27 na unatekelezeka kwa ubora uleule. Hoja hapa ni kwamba kumbe wataalam wetu wanaweza. Tujifunze kupenda cha kwetu, kwa sababu mara nyingi sana tukikaa hapa tuna dhana ya kwamba watanzania hawawezi kumbe watanzania wanaweza kama watapewa nafasi, kama watawezeshwa hilo limedhihirika wazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nampongeza Mheshimiwa Waziri, pomoja na menejimenti yake kwa kuwaamini watalamu hawa ambao wameweza kutekeleza mradi kwa uwezo mkubwa sawasawa na miradi mingine ambayo tumeitembelea. Na kwa jinsi hiyo liwe ni funzo ndani ya Serikali yetu, kwamba wazawa wapewe nafasi na pia

wapewe mitaji. Na wakati mwingine, kama tumeona uwezo wao ni mzuri wahamasishwe kufungua kampuni zao ili waweze kuchukua kandarasi kubwa badala ya kusubiri mtu astaafu miaka sitini halafu ndipo atumie utaalamu wake kwa kufungua kampuni. Wahamasishwe kufanya hivyo ili huko mbele katika miradi mikubwa hii inayoendelea kujengwa hapa nchini tupate kampuni za Kitanzania ambazo zitashindana ndani pamoja na nje ya nchi. Kwa hiyo hilo ni jambo zuri la kujifunza kutoka Ofisi ya Babati jinsi ambavyo wanatekeleza mradi wao wenyewe.

Mheshimiwa Spika, hoja yangu nyingine inatokana na ziara hiyohiyo ya Kamati tulipotembelea katika maeneo ya Nzega. Kumekuwa na uzoefu wa wananchi ambao wanaamua kuanzisha makazi mbali kidogo na wenzano; wanakaa kwenye mashamba huenda ya babu zao. Sasa mradi unatekelezwa halafu wao wako mbali kidogo, kwa hiyo Serikali inatumia gharama kubwa kuwapelekea watu wachache mradi wakati ni kwa sababu wao waliamua kujitenga; na nadhani hili pia ndio limeleteleza hizi shule shikizi kwa sababu watu wachache wapo mahali walikoamua kwenda lakini Serikali inalazimika kuwapelekea huduma.

Mheshimiwa Spika, hoja hapa ni kwamba nadhani kuna sababu ya sisi kupanga makazi na namna ya kurahisisha Serikali kutotumia gharama kubwa kwa ajili ya kuwapelekea watu huduma, la sivyo watu wata *detach,* wataenda mbali halafu wanahitaji huduma. Hivyo nilitamani kwamba Serikali iangalie, kwamba tuweze kupanga makazi kwa ajili ya kurahisisha kuwapelekea watu huduma bila kutumia gharama kubwa.

Mheshimiwa Spika, hoja ambayo pia Wabunge wengine wameiongelea, mafanikio haya tunayoyashuhudia katika Sekta ya Maji yametokana mara nyingi kwa kutumia vyanzo ambavyo ukiacha mradi wa Ziwa Victoria yanayoweza kuathirika na athari za mabadiliko ya tabia ya nchi na katika

ukurasa wa 81 wa hotuba ya Waziri amedokeza juu ya mpango kabambe wa kitaifa wa uendelezaji wa maji ameuita *National Water Master Plan* upo katika mpangokazi wake wa kutekeleza katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri anayo bajeti moja tu ya mwakani kuelekea 2025. Ningemsihi Mheshimiwa Waziri, katika mpango wake huu hebu ile tunayoiongelea kama gridi ya taifa ya maji hebu iweke, itakupa *mileage,* itakupa cha kuzungumza baada ya wewe kumaliza uwaziri wako.

Mheshimiwa Spika, ni kwa sababu gani nasema hivi, hii itatusaidia pia kuanza kutumia maji kutoka katika vyanzo ambavyo havikauki. Yaani Misri wanatumia maji ya chanzo kikubwa kutoka Ziwa Victoria, wanakunywa wanamwagilia wanapata faida lakini sisi tunavyanzo vikubwa vya maji lakini hatuja vitumia vizuri. Kwa hiyo katika ule mpango kabambe wake ninamsihi sana Mheshimiwa Waziri; kwamba haina maana watu kama wa Kisiwa cha Ukerewe ambao wao wanazungukwa na maji lakini leo hii bado upatikanaji wa maji ni asilimia 57, siyo sawa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri watu wa Katavi, Rukwa watu wa Mbeya watu wa Kigoma wanazungukwa na ziwa ambalo lina kina kirefu sana lakini bado hawatumii maji ya kutosha. Mheshimiwa Waziri mcheza kwao hutunzwa, kwenye *National Water Master Plan* wayaingize haya na atakwa amefanya vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana nakuksukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Emmanuel Chereheni ili amalizie muda wake tunakuomba radhi sana sasa unazo dakika tatu umalizie, ahsante sana.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI**: Mheshimiwa Spika, ahsante nakushukuru sana kwa kweli wewe ni msikivu na unasikiliza sana Wabunge wako.

Mheshimiwa Spika, nilitajka tu nimalizie mchango wangu kwa Mheshimiwa Waziri. Kwanza niendelee kuiomba Wizara ya Maji iangalie visima ambavyo wanachimba nchi nzima waviwekee miundombinu kwa ajili ya kuwafikia wananchi. Kwa mfano ukiangalia kuna Kata ya Masaka ambako ndio kwa mwenyekiti wangu wa kamati, kule kuna visima vizuri kabisa lakini miundombinu haipo.

Mheshimiwa Spika, kuna suala jingine la Mbauti. Miradi mingi ya maji ambayo wanaijenga Wizara ya Maji wanawasahau wafugaji, ningeendelea kuwaomba; ndiyo maana kuna kitu, kama inawezekana hawajagundua Wizara ya Maji, kuna migogoro inakuwa inaibuka kule kwenye miradi mikubwa ya maji. Wafugaji wanazunguka kutafuta maji lakini kwenye kijiji chao kuna miradi mikubwa ya maji.

Mheshimiwa Spika, sasa ningeomba Wizara ya Maji na Wizara ya Mifugo wakae wakubaliane kwenye mradi mkuu wa maji ulipojengwa kuwepo na kitu kinaitwa Mbauti kwa ajili ya kunyweshea wafugaji. Waunganishwe kwenye eneo la mradi wawekewe kama ushirika hivi wawe pamoja halafu wafungiwe na mita yao. Wafugaji hawana shida badala ya kuendelea kuhangaika kuhamahama, wanaondoka kwenye miradi mikubwa ya maji badala yake inaweza kuwasaidia wasiendee kuzunguka kuzurua. Hii kelele wakati mwingine ya wafugaji na wakulima tunaweza tukaipunguza kupitia Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Spika, ningeomba Mheshimiwa Waziri aliangalie hili. Tumeliona hata kipindi cha ziara tulipokuwa kwenye kamati, limekuwa ni kero, wafugaji wanalalamika na madhara yake wanaharibu miundombinu ya maji ambayo ni hatari sana.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri aweke mbauti pale wafungue mita, wajikusanye wao wasajiriwe; tena ifike mbali Mheshimiwa Waziri na Waziri wa Mifugo wawasajiri wale wakulima kama wanavyofanya Wizara zingine. Wale wafugaji wakiwasajiri pale wana uhakika kabisa kwamba watafanya kazi vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni uvunaji wa maji ya mvua; ningeomba tuwe na *center* ya uvunaji wa maji ya mvua kwa sababu maeneo mengi maji ya mvua yanapotea. Wakifanya hivyo kelele nyingi za ndugu zetu wakulima tutaziondoa kwa sababu maji yanapotea yanaenda kwenye mto wananchi wanapata shida.

Mheshimiwa Spika, mimi nikushukuru sana naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya atafuatiwana Mheshimiwa Ahmed Ally Salum muda ukitosha tutaendelea na Mheshimiwa Jeremiah Mremi Amsabi.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi niweze kutoa mchango wangu katika hoja ya maji. Lakini kabla ya kutoa mchago wangu, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kuchangia bajeti, naomba nitoe shukrani za pekee kwa Serikali yetu ya chama cha mapinduzi chini ya Mama yetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa fedha nyingi zilizoletwa katika Jimbo la Meatu kwa ajili ya kutekeleza miradi. Naomba niseme kwamba chini ya uongozi wa Mama Samia amwekwenda kuandika historia katika Jimbo la Meatu kwa miradi ambayo haikutekelezwa na haikuwahi kufikiriwa kwamba itatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, nishukuru, tumepata mgao wa shilingi milioni 348.5 kwa ajili ya kujenga shule mpya ya msingi

Mwanuzi "B" katika Jimbo la Meatu, nakushukuru Mheshimiwa Angela Kairuki. Lakini nashukuru pia jana tumepokea shilingi milioni 229 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa *VETA* ya Wilaya ya Meatu. Nawashukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Naibu wake. Vijana wanaenda kufurahi, vijana wanaenda kutimiza ndoto zao. Niwaombe tu masomo yatakayopelekwa yaendane na fursa zinazopatikana katika Wilaya ya Meatu. Nishukuru kwa mawaziri wote kwa ushirikiano wao wanaonipa mimi wakati natekeleza majukumu yangu.

Mheshimiwa Spika, sasa nijielekeze katika hoja. Niishukuru Serikali mwaka juzi tulipata fedha kwa ajili ya mradi wa dharura wa kuongeza maji katika Mji wa Mwanuzi, mradi wa kutoa maji Mwagwira, kwa kuongeza maji pale mjini Mwanuzi hali ni nzuri tunaendelea vizuri tofauti na miaka mitatu ilivyokuwa wananchi walikuwa wakitumia Bwawa la Mwanainya, kwa hiyo walikuwa wanatumia matope matupu. Lakini mradi huu kulingana na ukame unaoendelea bado baadaye utaanza kuonesha changamoto. *Solution* kubwa ni kupata mradi wa maji ya kutoka Ziwa Victoria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, 2016 Ofisi ya Makamu wa Rais iliibua mradi wa maji wa kukabiliana na athari ya mabadiliko ya tabianchi chini ya Waziri January Makamba, lakini leo ni miaka saba bado mradi huo haujaweza kutekelezwa; na badala yake Serikali imekuwa ikitupiga danadana kila mwaka, na hata maana halisi ya kukabiliana na athari ya mabadiliko ya tabianchi inaondoka.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana katika hotuba yake Mheshimiwa Waziri alisema kwamba mfadhiri yuko tayari kutoa fedha lakini, mpaka leo hakuna dalili yoyote; kwa sababu mwaka jana walisema anatafuta mkandarasi wa ujenzi lakini mpaka leo ni zaidi ya mwaka mmoja yule mkandarasi hajatafutwa. Mimi niliomba, kama mfadhiri ameshindwa basi akabidhi mradi huu Serikalini ili utekelezwe na fedha za Serikali kwa sababu Mheshimiwa Rais

ameongeza fedha katika mfuko wa maji kupitia shilingi 100 ya kila lita ya mafuta.

Mheshimiwa Spika, mpaka leo hakuna dalili yoyote. Inawezekana kuna masharti magumu; naomba Waziri unapohitimisha uliweke wazi sisi wananchi tuelewe. Mwaka jana pia ulisema kwamba mradi huu katika awamu ya kwanza utatekelezwa mpaka Wilaya ya Meatu, bomba litafika, lakini nimezipata taarifa mradi huu wa awamu ya kwanza ya Meatu haitakuwemo.

Mheshimiwa Spika, mimi mwaka jana nilienda kifua mbele nikaitisha mkutano mkubwa, nikawaambia wananchi Meatu inaingia katika awamu ya kwanza. Leo hii Mheshimiwa Waziri tukimaliza bajeti twende ukawajibu wewe kwa nini mradi haufiki katika awamu ya kwanza. Wewe mwenyewe umekiri kuna hali ya ukame mkubwa katika Jimbo la Meatu lakini tumekuwa tukipata fedha za kusuasua katika bajeti. Kwa mfano, mwaka jana kati ya bilioni 3.1 jimbo la meatu limepata mradi mmoja wa makao shilingi milioni 600 sawa na asilimia mbili. Mwaka huu katika bilioni 5.7 tulikuwa tumepangiwa bilioni 1.4 sawa na asilimia 20 lakini nimepambana ndani ya wiki angalau tumepata asilimia 50 katika bajeti hii tunayoendelea kuitekeleza.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tutawezesha kutekeleza mradi Mbushi Kata ya Burashi, Mwangudo, Mwakipopo, Mwanjoro.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa na maombi yafuatayo kwa Mheshimiwa Waziri. Tunaomba gari jipya la maji. Jiografia ya Meatu unaijua. Lakini ninaleta kwako, ninaomba uniruhusu nilete maombi maalum kuweza ku-*rescue* hali ya maji katika Jimbo la Meatu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri mwenyewe anaijua, na tumekuwa tukipata asilimia ndogo ya bajeti. Kwa

hiyo naomba nilete maombi maalumu kwa ajili ya kulisaidia Jimbo la Meatu. Lakini ninaomba sasa katika eneo la Lukale Kata ya Bukundi ambako kuna Lake Eyasi eneo lile ni la chumvi maji yale yakipelekwa kwenye *sample* huwa hayakubaliwi kwa ajili ya matumizi ya binadamu

Mheshimiwa Spika, niombe; katika bajeti ya Serikali Kuu naomba bwawa moja kwa ajili ya Kijiji cha Muhabagimu ambacho kitasaidia Likale na vijiji vya jirani ili wananchi waondokane na adha ya maji ya chumvi ambayo hayaruhusiwi kwa matumizi ya binadamu. Lilijengwa bwawa la Mwanjoro limepasuka kabla ya kutumia, naomba likwarabatiwe na Wizara kwa sababu mkoa na wilaya hawalitambui, lilijengwa na Wizara. Naomba Wizara waje walikarabati ili liweze kusambaza maji.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ukame katika Jimbo la Meatu nilitaka kutoa ushauri ufuatao;

Mheshimiwa Spika, tunapotekeleza miradi ya barabara, kwa kuwa Serikali ni moja, niombe kila baada ya kilomita kumi moramu ya kujenda barabara itoke kandokando ya barabara ili tuweze kuruhusu ile mifereji iingie katika yale mashimo yaliyojengwa. Maji yale yatasaidia mifugo, na kwa baadaye yataweza kusaidia kuchimba kisima kirefu baada ya muda mrefu ili tutafute *solution* ya kukabiliana na ukame ulipo katika Jimbo la Meatu. Kwa mfano kutoka Mwanuzi kwenda Mwabuzo tuchimbe pale Mwangikuru ambako hawana chanzo chochote cha maji.

Mheshimiwa Spika, niombe pia katika Bwawa la Mwanyaina basi awatume wataalau wake wakajaribu ku-*test* kama watapata maji kiweze kuchimbwa kisima kirefu kwa pembeni kusaidia upungufu wa maji. Niombe, kupitia mitambo iliyoletwa, kama alivyosema, kwamba inakuja Meatu, lakini gharama ya uendeshaji wa mitambo hii mikubwa ni asilimia 100 ni sawa na bei ya mkandarasi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mitambo hii ni ya Serikali halafu ni mipya kwa nini bei isiwe nusu? Badala ya kujenga visima vinne tutajenga vinane. Na kwa kuwa meneja wa visima ni nchi nzima ni *pool,* fedha zote zinaingia mle badala yake msisubiri mitambo ichakae muanze kununua mitambo michache michachemichache ili inapoharibika ile ya zamani iwepo mingine ya kuweza ku-*replace* kutokana na mfuko huu wa *revolving.*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Ahmed Ally Salum.

**MHE. AHMED A. SALUM:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Mimi binafsi naunga hoja mkono kwenye Wizara hii ya Maji. kama kuna siku ambayo mimi binafsi Mbunge wa Jimbo la Solwa sina changamoto nyingi kwenye Jimbo la Solwa kwenye suala zima la maji kama awamu hii awamu ya sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ni kubwa na ninajua kabisa Mama yetu Rais wetu mpendwa kubwa anaifanya sana; anaitendea haki Jamhuri yetu ya Muungano wa Tanzania. Ninajua sana chini ya Wizara ya Maji chini ya Waziri Mheshimiwa Aweso, Naibu wake na timu nzima ya Wizara ya Maji mnaitendea haki Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Solwa mwaka 2005 tulikuwa tuna vijiji 16 tu vyenye maji ya Ziwa Victoria. Lakini tulikwenda awamu baada ya awamu uvumilivu na ustahimilivu chini ya Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi miradi ambayo inatekelezwa sasa hivi katika Jimbo la Solwa ni mingi.

Mheshimiwa Spika, Ukianza na mradi wa Masengwa *package* vijiji vinane awamu ya pili wenye gharama ya bilioni 4.7 wakandarasi wako kazini wanafanya kazi. Mradi huu una

awamu tatu. Mpaka tunamaliza awamu tatu tutakuwa tuna vijiji 12. Katika Masengwa *Package* tuna Kijiji cha Ishnabulandi, Bubale, Idodoma, Isela, Ibingo, Mharanga, Mwamara na Nalibanza katika kata ya Mhamara. Tumeshajenga tenki Ishnabulandi na sasa hivi inajengwa tenki Mwamara kwenye kata ya Mwamara.

Mheshimiwa Spika, Ndugu zanguni katika Jimbo la la Solwa tuna vijiji vingine sita ambao unagharimu zaidi ya bilioni tatu Jimbo la Solwa tu hilo Mwandutu, Mwabageu, Maemiru, Mwasenge, Mwongozo, na Mwenge vijiji sita tayari wanakunywa maji ya Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Spika, katika *Tinde package* kuna vijiji 22 hata Makamu wa Rais alipokuja kuzindua ule mradi pale tinde walikuja pamoja na Mheshimiwa Waziri sasa hivi mabomba yanalazwa kwenda kwenye Kijiji cha Jomu kwenye Kata ya Tinde. Kata ya Tinde nadhani Waheshimiwa Wabunge wengi mnaifahamu, ni *junction* kubwa sana ambayo kila mtu lazima aipite kwa maana ya kwamba kama anakwenda nchi jirani.

Mheshimiwa Spika, vijiji 22 lakini katika Kijiji cha Jomu sasa hivi mabomba yanalazwa. Kwa hiyo mwezi wa sita wataanza kunywa maji ya Ziwa Victoria. Mradi huu una-*cost* bilioni sita. Kata za Mwamara, Didia, Tinde, Osanga pamoja na Nsalala katika Tinde *package* hii ambayo sasa hivi nafikiri na nina Imani kabisa Wizara wanafanya mchakato wa kuleta fedha ili tukamilishe. Hoja yangu na ombi langu kwa Mheshimiwa Waziri, tunapoomba fedha kwa ajili ya kukamilishaji kwa ajili ya *Tinde package* nikuombe sana ije kwa wakati ili miradi hii yote ikamilike kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mwalukwa kuna miradi pia sasa hivi inatekelezwa katika vijiji vitatu, kwa kushirikiana na *life water, t*unawashukuru sana. Tunaendelea, na mradi utaisha baada ya miezi mitatu minne na wenyewe watakunywa maji ya Ziwa

Victoria, lakini pia Kilimawe bilioni 304. Kilimawe kijiji kiko ndani sana lakini tunapeleka maji kwa kuwashirikiana na *life water, RUWASA* wanasimamia pale. Pia Mwashagi katika zile fedha za *COVID* tumepeleka maji. Vilevile kwenye Kata ya Mwakitorio, nafikiri hata Mheshimiwa Waziri amekuwa akiitolea mfano sana kwenye mikutano yake yote; ule mradi ulitusumbua sana. Sasa hivi kwenye Mwakitorio wenyewe kijiji hicho wanakunywa maji.

Mheshimiwa Spika, vilevile Mheshimiwa Waziri alitoa maelekezo ya kujenga tenki, tenki limeisha, linachukua lita laiki tano, ambalo litahudumia vijiji vitatu, ambavyo ni Mwakitorio, Nyarigongo, na Nyang'ombe. Hivi ninavyoongea kwa faida ya wananchi wa Nyerigongo na Nyang'ombe niwaambie tu mabomba yameshashushwa pale Ofisi ya *RUWASA,* wiki hii hii na wiki ijayo tutapeleka mabomba kulaza ili wananchi wa Kijiji cha Nyerigongo na Nyang'ombe wapate maji ya Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tunaomba fedha kwa ajili ya usanifu wa vijiji 22 vingine. Nimuombe sana Mheshimiwa Waziri, vijiji 22 vingine vya Kata za Ryabukande, Iryamidati, Ilola, Bukene, Usule pamoja na Puni, tulikuomba fedha hizi utuletee ili tukamilishe vijiji 22. Tunajipanga kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Ndani ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi asilimia 85 kupeleka maji vijijini, yaani tuwe tumekamilisha kufikia 2025. Miradi hii yote ikikamilika sasa sisi kwenye Jimbo la Solwa tutafika asilimia 87 kufika 2025, na tutakuwa na vijiji 105 ndani ya vijiji 126.

Mheshimiwa Spika, ni miujiza. Yaani wakati mimi nasoma shule nilikuwa nikitoka Kijiji cha Mhangu ninakwenda, kuna wakati kama kuna ukame, mnachukua gari kwenda kuchukua maji kilomita 30 ambako Serikali ilichimba bwawa moja kubwa sana kwenye Kata ya Nindo pale Selamagazi. Unatoka kule unaenda kuchukua maji wengine walikuwa wanakwenda kwenye Malambo kule.

Mheshimiwa Spika, ukikumbuka enzi hizo wakati nasoma mpaka sasa hivi nimekuwa Mbunge wa Jimbo la Solwa, kwa kushirikiana na chama changu utekelezaji wa ilani chini ya awamu ya sita leo tumefanya maajabu na miujiza mikubwa mno katika Wizara hii ya Maji

Mheshimiwa Spika, mimi niseme tu ndugu zanguni tumpe Mama moyo mkubwa sana katika awamu ambayo mimi nimefanya kazi kwenye Jimbo la Solwa hakuna fedha nyingi zimekuja kama awamu hii ya sita yenye miradi yote ikiwemo miradi ya maji. Vilevile nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Aweso, Aweso chapa kazi wewe mdogo wangu uko vizuri sana. Sina tu cha kusema. Sisi tukuiingia Mskikitini kuswali tunakuombea dua. Zaidi ya kuombea dua ufanye kazi yako vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine niombe tu *Engineer* wangu Meneja Eng. Nkopi, anakaimu, hebu ichukue hii tumthibitishe, mthibitisheni huyu. Mimi nimefanya kazi na ma-*engineer* wengi sana hakuna *engineer* ambaye unafanya naye kazi unamuelewa anasimamia…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Haya, kengele ya pili imeshagonga.

**MHE. AHMED A. SALUM:** Mheshimiwa Spika, naomba tu athibitishwe na alatewe gari ili kazi tufanye vizuri na nawashukuru sana katibu mkuu meneja wa maji vijijini, wote kwa pamoja Mungu awabariki sana nawashukuru sana ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa ahsante sana umeshasikika. Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa sehemu ya kwanza ya uchangiaji, tutaendelea na Wabunge wengine tutakaporejea alasiri.

Mheshimiwa Aysharose Ndogholi Mattembe, Mheshimiwa Zaytun Seif Swai, Mheshimiwa Jeremiah Mrimi Amsabi, Mheshimiwa Daniel Awack Tlemai tutaendelea nao na wengine tutaendelea kuwataja kadri muda utakavyokuwa una kwenda.

Sasa baada ya kumpa Mheshimiwa Cherehani muda wa kumalizia alipokuwa amepewa dakika tano badala ya nane nimeletewa hapa maelezo na Wabunge wengine hawakupewa muda wao kwa ukamilifu.

Sasa kwa sababu hawa hawakuchangia leo kidogo itakuwa changamoto kuwarejeshea muda wao; lakini Makatibu Mezani hakikisheni hilo mnalifanyia kazi ili Wabunge muda wanaotajiwa wachangie muda huo sawasawa.

Pia niwaombe Waheshimiwa Wabunge, kwa ujumla tu, kwa sababu Wizara nyingi ziko huko mbele na hapa nilikuwa napitia orodha ya Wabunge wote, Wapo Wabunge ambao mpaka sasa kwa ajili ya kuandika vikaratasi hapa mbele mmeshakamilisha Wizara tano kwenye kuchangia. Sasa hapa ataamka mtu, kwa sababu miundombinu bado, na najua huko mko wengi na huku tayari kuna wengine tayari mmeshachangia mara tano. Huko mbele kuna ardhi, huko mbele kuna maliasili nanyi mmeshachangia mara tano. Sasa kipaumbele, upande huu wa upinzani viongozi wenu wawape wale ambao hawajachangia kabisa. Vivyo hivyo upande wa Chama cha Mapinduzi, makatibu wahakikishe wale ambao hawajachangia kabisa wanapewa kipaumbele kabla ya wale ambao wameshafika tano. Wale ambao wameshachangia mara tano tayari wapewe nafasi kwenye Wizara ambayo wengine wote hawajaomba

Hiyo tuelewane vizuri kwa sababu Waheshimiwa Wabunge wote tuna lingana hadhi zetu humu ndani na kwa hivyo kila Mheshimiwa Mbunge apewe nafasi ya kuwasemea wananchi waliyomtuma humu ndani. Sasa hilo nafikiri

litakuwa limeeleweka wale waliochangia mara tano wasihangaike kumsumbua katibu wala hapa mbele, hilo limeeleweka vizuri.

Baada ya kusema hayo kuna mgeni wa Mheshimiwa Aweso na huyu ni bwana Abdallah M. Kufunzi ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya Mfuko wa Taifa wa Maji. Karibu sana *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge pia kuna tangazo lingine la wageni. Wapo wanafunzi 80 na walimu sita kutoka Shule ya Msingi Mtawala ya Mkoa wa Morogoro wamekuja Bungeni kwa ajili ya kujifunza. Karibuni sana *(Makofi)*

Lipo tangazo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Anjelina Mabula, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge kwamba hapa kuna huduma zinaendelea kutolewa katika mabanda ambayo yapo katika viwanja vya Bunge. Kwa hiyo mbunge yoyote ambaye anachangamoto yoyote inayohusu ardhi aende hapo akapate ufafanuzi; na mabanda hayo yapo hapa Bungeni kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge tutumie fursa hiyo.

Baada ya kusema hayo waheshimiwa Wabunge nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi alasiri.

*(Saa 7.06 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 10.00 Alasiri)*

*(Saa 10.00 Alasiri Bunge Lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. MONICA MWAGA – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na majadiliano, tutaanza na Mheshimiwa Aysharose Ndogholi Mattembe, atafuatiwa na Mheshimiwa Zaytun Seif Swai, Mheshimiwa Jeremiah Mrimi Amsabai ajiandae.

**MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hoja iliyoko mezani. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenijalia uzima na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu. Nikupongeze wewe kwa kazi nzuri unayoifanya kwa kuliongoza vyema Bunge letu.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii pia kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Juma Aweso, Naibu wake Mheshimiwa Maryprisca na watendaji wote wa Wizara ya Maji kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuhakikisha maji yanapatikana katika maeneo yote. Nawapongeza sana, lakini pia nimpongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi nzuri anayoifanya ya kumtua mama ndoo kichwani na kuhakikisha maji yanapatikana katika Mkoa wangu wa Singida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Singida, nampongeza sana na namshukuru sana. Maji ni uhai, pamoja na pongezi hizo, Mkoa wangu wa Singida bado una changamoto kubwa sana ya upatikanaji wa maji safi na salama. Natambua jitihada kubwa za Serikali za kuhakikisha

maeneo yote yanapata maji hususan ya vijijini lakini mkoa wangu bado una changamoto kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naishukuru sana Serikali kwa Wilaya yangu ya Manyoni kupata maji katika Vijiji vya *Rift Valley*, Kintinku, Lusilile, Makasuku, Sasilo na uchimbaji wa maji visima 10 lakini upo mradi ambao tumekuwa tukiupigia sana kelele, Mradi wa Maji Kintinku, Lusilile. Namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kutupatia fedha kiasi cha bilioni tano. Niiombe sana Serikali, basi fedha hizi zitoke kwa wakati ili sasa mradi huu uweze kukamilika, kwa kuwa umekuwa ni wa muda mrefu toka Awamu ya Nne, mradi huu hadi sasa haujakamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naishukuru pia Serikali kwa kupata miradi katika Wilaya yangu ya Mkalama ambapo ni Kijiji cha Singa, Tumuli, Mdilike, Matongo pamoja na uchimbaji wa visima 10, lakini yapo maeneo ambayo bado hayana maji kabisa katika Wilaya ya Mkalama. Maeneo haya ni Vijiji vya Mwangeza, Kisiluhida pamoja na Singa. Yana changamoto kubwa sana ya upatikanaji wa maji, niiombe Serikali iviangalie kwa jicho la kipekee vijiji hivi ili navyo viweze kuapata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru pia Serikali kuweka Mradi wa Maji Vijiji 28 na katika Mkoa wangu wa Singida tumeweza kupata Kiomboi, Manyoni pamoja na Singida Manispaa, lakini bado ipo miji ambayo inakuwa kwa kasi kama vile Ilongero, Ikungi, Mitundu na Nduguti. Niombe sana basi miji hii nayo iweze kupatiwa fedha kwa ajili ya upanuzi wa miradi ili wananchi wa maeneo hayo waweze kupata maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya yangu ya Singida Vijijini, tumepata Mradi wa Semfuru, Ndugira, Ikiwu na Kinyamwenda, lakini kipo kijiji kimoja ambapo kupata chanzo cha maji ni changamoto kubwa sana. Kwa hiyo, niombe

sana kijiji hiki cha Mangida nacho kiangalie kwa jicho la pekee. Yapo maeneo ya karibu ambayo yana ambapo maji hayo yanaweza kuvutwa hadi kupelekwa katika kijiji hicho cha Mangida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wangu wa Singida kuna changamoto kubwa ya watumishi na niombe pia Serikali iangalie na tuweze kupata watumishi wa kutosha katika Mkoa wangu wa Singida ili utekelezaji wa miradi ya maji uweze kufanyika kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, niwapongeze sana watendaji wa *RUWASA* katika Mkoa wangu wa Singida ambao wamekuwa wakifanya kazi nzuri sana ya kuhakikisha maji yanapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache, naunga mkono hoja na nakushukuru sana kwa nafasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Zaytun Seif Swai atafuatiwa na Mheshimiwa Jeremiah Mrimi Amsabai, Mheshimiwa Daniel Tlemai Awack ajiandae.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa niweze kuchangia machache kwenye Wizara hii pamoja na kutoa ushauri wangu ili kuweza kuboresha huduma hizi za maji safi na maji taka. Naomba nianze kwanza kumshukuru Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Mama Samia Suluhu Hassan, kwa kuweza kutekeleza miradi mingi ya maji na kuipa kipaumbele sekta hii muhimu kwa wananchi wetu. Vile vile nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa maono yake na moyo wake dhabiti alioonesha kwa ajili ya kumtua mama ndoo kichwani. Niwapongeze Wizara hapa, maono haya wao ndio wanayatekeleza kwa kiasi kikubwa, niwapongeze sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pongezi hizi ziende sambamba kwenye Serikali ya Mkoa wa Arusha ikiongozwa na Ndugu John Mongela pamoja na viongozi wote wa Chama cha Mapinduzi wa Mkoa wa Arusha, wamekuwa wanaipa miradi hii kipaumbele na wamekuwa wakiifuatilia kwa karibu sana kuhakikisha inatekelezwa kwa kiasi kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nishukuru sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi, juzi tu hapa Mkoa wangu wa Arusha tumepokea mtambo mkubwa wa kuchimba visima virefu. Kwa ajili ya kuweza kutatua matatizo ya maji hususan kwenye maeneo ambayo yana shida ya vyanzo vya maji kama Wilaya ya Longido, Monduli, Ngorongoro, Karatu na sehemu zingine ambazo zina shida ya changamoto za maji. Shukrani zangu hizi ziende sambamba pia tumekamilisha Miradi 10 ya Maji Vijijini hadi kufikia mwezi Februari. Katika Wilaya ya Monduli kuna Mradi mkubwa wa Maji wa Meserani Bwawani umekamilika mwezi Februari, lakini katika Wilaya ya Arumeru pia kuna miradi takribani nane imekamilika Februari, 2023. Katika Wilaya ya Karatu pia kwenye miradi hii ya maji vijijini, Mradi mmoja wa Gidbasso umekamilika. Vile vile Serikali yetu haijaishia hapo, kuna miradi miwili ya maji katika Wilaya ya Ngorongoro ambayo inatarajia kukamilika mwezi Juni, 2023. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nianze na hali ya upatikanaji wa maji pamoja na takwimu hapa za upatikanaji wa maji alizotupa Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba yake. Waziri amesema hapa, hali ya upatikanaji wa maji vijijini imeimarika kutoka asilimia 70.1 hadi kufikia asilimia 77, lakini mijini imeimarika kutoka asilimia 84 hadi kufikia asilimia 88. Kama alivyosema Mheshimiwa Waziri huu hapa ni wastani tu na takwimu hizi zimekaa kiujumla mno. Namwomba Mheshimiwa Waziri kama ataweza kutupatia mchanganuo wa takwimu hizi ili tupate kiwilaya ili tujue hali halisi ya upatikanaji wa maji kwenye majimbo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema hivi kwa sababu kuna maeneo mengine ya Mkoani Arusha, ina asilimia sifuri kabisa ya upatikanaji wa maji. Naomba nimweleze tena Mheshimiwa Waziri hapa, anayejua hali ya mgonjwa ni yule anayemuuguza na mimi kama Mwakilishi wa Mkoa wa Arusha, ndiyo nakaa wananchi wangu na najua hali halisi ya upatikanaji wa maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nafahamu vizuri wewe ni mama na una huruma sana, ukienda kwenye baadhi ya vijiji katika Mkoa wa Arusha, kwa mfano Longido, ukienda Noondoto, Kisilya, Mundarara, Wosiwosi, utalia kwa jinsi akinamama wanavyopata shida kutafuta maji. Wanatembea zaidi ya kilometa 30 kwenda kutafuta maji. Sio maji salama tena, kutafuta maji ambayo wakishayapata wana–*share* na mifugo. Maji hayo wanachangia na punda, wanachangia na ng'ombe na aina nyingine ya mifugo. Binafsi nimetembelea maeneo haya na nimeona hali halisi ya maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, ukienda Monduli Lepurko, Naalarami hali ni hiyo hiyo. Kwa hiyo naomba sana Waziri pamoja na Wizara, basi waweke kipaumbele sehemu zile ambazo zina asilimia chache ya upatikanaji wa maji, basi na wao pia asilimia ziongezeke ili twende nao sambamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo napenda kuchangia mchana wa leo ni kuhusiana na uvunaji wa maji. Kamati imeshauri vizuri sana. Serikali lazima iongeze juhudi katika kuweka miundombinu ya uvunaji wa maji, lakini iwaelimishe wananchi pia kuhamasisha wananchi wetu kwenye suala zima la uvunaji wa maji. Kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri hapa amesema vizuri kwamba katika mvua zilizonyesha hivi karibuni Kanda ya Kaskazini imeongoza kwenye wastani hadi kufikia milimita 1,350. Mvua hizi zimeleta madhara makubwa sana kwa wananchi wa Mkoa wa Arusha. Zimeharibu miundombinu na vile vile zimeleta

mafuriko makubwa na hivyo kupelekea vifo kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nitumie fursa hii pia kuwapa pole wananchi wangu wa Mkoa wa Arusha walioathirika wote na kadhia hii, lakini Mheshimiwa Waziri ataona hapa tungekuwa na miundombinu mizuri ya uvunaji maji, haya yote yasingetokea. Naomba sana niungane na maoni ya Kamati, Serikali iongeze juhudi kuweka miundombinu hii ya uvunaji wa maji ili maji haya yaweze kuwasaidia wananchi wetu pia kipindi cha kiangazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee suala lingine la usambazaji wa maji; katika Mkoa wa Arusha kuna mradi maarufu na mradi mkubwa sana wa bilioni 520. Waziri ametuambia mradi huu umekamilika kwa takribani asilimia 92 hadi sasa, lakini kuna baadhi ya maeneo mradi huu unapita maji hayajasambazwa, Kamati pia imeshauri jambo hili. Mradi huu unapita Wilaya ya Arumeru lakini ukienda Nduruma maji hamna. Kwenye Jiji la Arusha mradi huu upo, lakini kuna sehemu kama Terrat maji hamna. Kwa hiyo, naomba nimalizie, niombe Wizara iweke kipaumbele maeneo yote ya miji na vijijini, sehemu ambayo mradi unapita basi waweze kuwapa kipaumbele wananchi wa pale kwa kuwapa maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Jeremiah Mrimi Amsabi, atafuatiwa na Mheshimiwa Daniel Tlemai Awack na Mheshimiwa Emmanuel Lekishoni Shangai ajiandae.

**MHE. JEREMIAH M. AMSABI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Awali ya yote nimshukuru sana sana Rais Dkt. Samia kwa kazi kubwa ambayo ametufanyia pale Serengeti. Kwa muda mrefu kabisa barabara zetu zilikuwa ni changamoto,

lakini Rais ametoa fedha nyingi, iko barabara sasa inajengwa kutoka Tarime mpaka Serengeti, lakini ipo nyingine kutoka kule Bunda mpaka katika Mji wetu wa Serengeti. Tunamshukuru Rais bado katika miradi mingi katika afya, katika elimu na kadhalika, lakini katika miradi ya maji tumeona akifanya mapinduzi makubwa sana. Katika miaka yake miwili iko miradi mingi ambayo inaendelea kutekelezwa, iko Miradi ya Kibanchabancha, Nyiberekera, Rigicha, Gesarya, Motukeri, Nyamitita, Kenyana na Nyamakobiti, iko mingine mingi kwa sababu ya muda siwezi kuitaja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa nishukuru kwa jitihada hizi za Rais za kutafuta fedha, miradi ambayo nimeipendekeza, nimewasilisha pia imeweza kuingizwa katika bajeti ya mwaka 2023/2024. Upo Mradi wa Nyamisingisi, Nyamihuru, Gantamome, Bwitengi, Nyichoka, Iharara, Kuitete, Iseresere, Mesaga, Masinki, Ketembere, Misarara, Nyansurura, Tamkeri na Manyata, lakini pia viko visima 20 ambavyo vinachimbwa katika sehemu tofauti. Pia nimpongeze sana Mheshimiwa Aweso, Naibu wake na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi kubwa ya usimamizi na utekelezaji wa shughuli hii kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa muda huu mfupi niseme changamoto chache ambazo tunaziona na tunashauri zifanyiwe kazi katika Mradi wetu mkubwa wa Maji katika Mji wa Mugumu pale Makao Makuu ya Wilaya ya Serengeti. Tunamshukuru Rais kipekee, mradi huu ulikuwa umeshindikana katika miji yote 28, lakini Rais kipekee kabisa amepata fedha. Sasa bilioni 11.5 zinazokuja pale Mugumu kwa utekelezaji wa mradi huu naishauri sana Wizara iangalie namna ya kuupitia tena ule mradi. Ule mradi unakutana na changamoto ya *scope*, una-*cover* maeneo machache. Wakati mradi huu unakuwa *designed* miaka iliyopita huko wali-*focus population* ndogo.

Mheshimiwa Spika, Mji wetu wa Mugumu ulikuwa na watu takribani 30,000 na hata mji ulikuwa hujapanuka kiasi ambacho umepanuka sasa hivi. Sasa Mji wetu wa Mugumu una wakazi 59,348, ukiona ni karibu mara mbili ya ongezeko la watu ambao walikuwepo. Kwa hiyo, tunaomba, kwa mfano *specific* ukienda Kata ya Matare maji yanafika kwenye Eneo la Senza pale. Ukienda maeneo ya mbele Igina mpaka Shule ya Sekondari Kambarage, kuna zahanati imejengwa kule maji katika mradi huu hayatafika. Kwa hiyo, ombi letu na ushauri kwa Mheshimiwa Waziri, mradi huu sasa uongezewe ile *scope* uweze kukutana na watu wengi kulingana na *population* ya watu ambao imeongezeka katika mji wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, changamoto ya pili ni chanzo cha maji; katika chanzo cha maji cha mradi huu wa bilioni 11 iko changamoto kubwa. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri nilimwandikia barua, nimezungumza naye mara kadhaa na Waziri ameonekana kuwa msikivu. Waziri Aweso namfahamu ni mtu msikivu, ni mtu wa mabadiliko, ni mtu anayeweza kubadilisha vitu na akavifanya kuwa bora zaidi. Mradi huu najua kwa uwezo wako, kwa umahiri wako angekuwa ni yeye ndiyo ameu–*design* kwa wakati huu angeufanya kuwa wa tofauti, lakini nimwombe sana Mheshimiwa Aweso, bado hatujachelewa. Alituma wataalam baada ya ombi langu wakaja, wakafanya tathmini, kwa maana ya chanzo kile sasa ambacho ni kidogo. Wakati bwawa hili linajengwa lilikuwa na uwezo wa kuwa na maji lita milioni 23, sasa hivi limeweza kupungua mpaka lita milioni 14. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati linajengwa lilikuwa ni kwa ajili ya mji ule mdogo ambao ulikuwa bado kijiji, *population* yake ilikuwa ni *around* watu 7,000 tu. Sasa *population* imekuwa kiasi hiki, lakini pia mahitaji yamebadilika kwa maana ya namna ambavyo ule mji sasa unaendelea kubadilika na nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, timu ile ilijielekeza sana kumshauri kuhusu kuchukua maji kwenye chanzo cha maji ya

Mugango, Kiabakari, Butiama na wakamwambia kwamba haiwezekani. Ni kweli kwa sababu tayari Mradi wa Mugango – Kiabakari - Butiama ulikuwa umeshafika mbali, lakini bado hawakuwa na *option* nyingine.

Mheshimiwa Spika, tunamwomba Mheshimiwa Waziri, watu wa Serengeti tunaona shida hii inaweza ikawa kubwa baadaye na upo ushauri wa wataalam wengi, Profesa James Scott wa *University of Yale* kule Marekani. Huyu ni Profesa wa *Political Economy* katika kitabu chake cha *Weapons of the Weak,* anasema *long term solutions is the function of proper planning.* Kwa hiyo, sisi katika hali yetu hii, uchumi wetu huu bado tunapambana hivi, tunapaswa kuwa na mpango ambayo ni sahihi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana sasa tunamwomba sana Mheshimiwa Waziri Aweso aangalie, ilipangwa miradi mingi ya muda mfupi kutafuta *solution* ya muda mfupi mpaka leo tumepoteza fedha nyingi kwa ajili ya Taifa hili. Pale Serengeti ipo miradi ya *HESAWA* ilijengwa mingi sana, *almost* kila kijiji leo ukienda vijiji vingi vinaonekana havina maji, kwa sababu vile visima vilikuwa ni *temporary solution.* Iko pia miradi mingine ya mabwawa mengi katika sehemu mbalimbali za nchi ambazo yote mpaka leo inaonekana siyo kitu, miradi ile imeisha na tumefikiri tena miradi mingine.

Mheshimiwa Spika, unapofikiria *long term solution* lazima uangalie *scope* kwa upana kabisa, *population* ya watu inaongezekaje, mahitaji na vyanzo vyenyewe. Ukiona kama chanzo cha Bwawa la Manchira wakati ule kilikuwa kina vijito takribani nane vilivyokuwa vinaingiza maji. Kutokana na *population pressure,* wakati ule Serengeti ilikuwa na watu takribani 180,000, sasa kwa sensa ya 2022 tuna watu 340,349, watu wameongezeka sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya *pressure* hii, vyanzo vingi vya maji vilivyokuwa vinapeleka katika bwawa hili

vimeharibika. Kutokana pia na mabadiliko ya tabianchi hatupati mvua za kutosha. Kwa hiyo, ni dhahiri chanzo hiki cha maji ya Bwawa la Manchira hakiwezi kuwa cha kudumu ni cha muda mfupi. Kwa hiyo, hatutaki tena baada ya muda mfupi tuliingize Taifa katika shida ya kutafuta namna tena ya kujenga miradi mingine.

Mheshimiwa Spika, leo tumeshuhudia mahali pengi miradi ilijengwa baadae tena wanaacha yale mabomba wanaweka mengine, wanaweka mabomba makubwa. Huu ni uharibifu wa fedha ya Taifa hili. Kwa hiyo, tunamuomba ndiyo maana tumekuja na ushauri mkubwa kabisa kwa Mheshimiwa Waziri lazima tuwe na *integrated water systems* kwenye nchi. Kama kwenye nchi nzima ni shughuli kubwa basi walau iwe katika *regional.* Lazima tuwe na mpango ambao ni unganishi na shirikishi wa kupata maji katika Mkoa.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano Mkoa wa Mara, Mkoa wa Mara leo tungeweza tukawa na vyanzo vikubwa vitatu tu, vikubwa sana. Watu wengi hapa kila wakati wameshauri nchi hii ni vizuri tukawa na mipango ya miaka 50, miaka 60 kwa maana gani? Tunapofikiri kuwa na maji, tusi-*focus* kuwa na maji ndani ya miaka mitano au 10, tufikirie miaka 50 kwa maana hiyo tunaweza tukajenga mradi mkubwa wa maji kule Mugango ambao unge-*fucus population* ya watu zaidi ya milioni 10 kwa wakati unaokuja. Sasa leo tutaweka milioni moja, milioni mbili baada ya muda watu wameongezeka, maji yale hayatoshi tena tunaanza upya, tunatafuta fedha upya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Mheshimiwa Waziri tunakuomba sana Mji wa Mugumu utakapokuja katika *ground bricking ceremony* ya mradi huu mkubwa wa maji, tunaomba uje na taarifa ambayo wananchi wa Serengeti wanaitamani. Tunatamani kusikia tunao mradi mkubwa wa maji sasa unaanzia kule Rorya - Tarime na unakuja mpaka mji wa Nyamongo. Kutoka Nyamongo mpaka Mugumu ni

takribani kilometa 57, ni rahisi sana kuleta maji katika Mji wa Serengeti.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo rai yetu ni kwamba ule mradi tunauhitaji…

**SPIKA:** Mheshimiwa kengele ya pili imeshagonga.

**MHE. JEREMIAH M. AMSABI:** Mheshimiwa Spika, tunamuomba sasa Mheshimiwa Aweso aweze kufikiria mradi ule uendelee lakini ujengwe katika *scope* ya kuchukua maji Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Daniel Tlemai Awack atafuatiwa na Mheshimiwa Emmanuel Lekishon Shangai, Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi ajiandae.

**MHE. DANIEL A. TLEMAI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia katika Wizara hii ya Maji. Namshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutupatia fedha nyingi Jimbo la Karatu kupitia TAMISEMI mwezi huu wa Mei tumepokea zaidi ya shilingi bilioni mbili ya kuendelea kujenga madarasa, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Karatu tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais na pia namshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI kwa kutupatia Jimbo la Karatu fedha za kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Maji na Watendaji wa Wizara ya Maji na leo nachangia nikiwa na furaha kwamba kuna majukumu makubwa sana kwenye hii Wizara imefanyika katika Jimbo la Karatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, miaka miwili iliyopita nilikuwa nachangia bei kubwa ya maji katika Jimbo la Karatu, ilikuwa maji kwa Jimbo la Karatu upatikanaji wake kwa *unit* ni shilingi 3,500, sasa upatikanaji kwa *unit* katika Jimbo la Karatu inapatikana kwa shilingi 1,300, kwa maana hiyo namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kutoka shilingi 3,500 na leo wananchi wa Jimbo la Karatu katika Mji wa Karatu wanapata maji kwa shilingi 1,300 kwa *unit. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kuunganisha. Karatu kulikuwa na Bodi mbili, kulikuwa na Bodi ya *KAFIWASU* ambayo ilikuwa inauza maji kwa shilingi 3,500. Kulikuwa na Bodi ya *KARUWASA* ambayo wanauza maji kwa shilingi 1,750 baada ya kuungana sasa maji yanapatikana kwa shilingi 1,300. Tunakushukuru sana na ninaamini kwamba ni sera ya Wizara kuunganishwa ili wananchi wale wasiendelee kuwa na mwingiliano katika hizi bodi mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri pia nakushukuru baada ya kuunganisha wafanyakazi wale wote wa *KAFIWASU* na wale wa *KARUWASA* wakaunganishwa hakuna aliyekosa kazi wote sahizi wanaendelea kufanya kazi. Pia ulipendekeza aliyekuwa *Manager* wa *KAFIWASU* sasa kuwa Mkurugenzi wa Maji katika Mji wa Karatu na anafanya kazi nzuri sana katika Mji wa Karatu na wananchi wanapata maji. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile jana Mheshimiwa Paresso amechangia akisema kwamba wananachi wa Karatu wanalalamika. Nikuhakikishie nimetoka Jumapili Jimbo la Karatu, wananchi wa Karatu hawalalamiki. Wananchi wa Karatu walipata shida kutoka mwaka 2002 kununua maji kwa shilingi 3,500 lakini niweke kumbukumbu sawa, siyo kwamba Karatu baada ya 2002 ndiyo kwamba mradi wa maji ulianza. Mradi ulikuwepo kabla ya 2002 na ulirithi miradi ya Serikali ambayo ni matenki na ma-*lane* na wakaendelea kuhudumia

kwa bei ghali ya shilingi 3,500. Kwa hiyo, nikuambie Mheshimiwa Waziri hakuna Wananchi wa Karatu wanaolalamika, mimi ndiyo Mbunge wa Jimbo la Karatu, wananchi wamefurahia kuunganishwa kwa ile vyombo, kwa sababu hitaji letu ni maji, sisi hatuna shida na majina ya *KAFIWASU* na *KARUWASA*, shida ya wananchi wa Karatu ni wapate maji ili maendeleo yawepo katika Jimbo la Karatu, hatuna shida na *KAFIWASU* na *KARUWASA*, lengo letu kubwa ni mwananchi apate huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo nikushukuru sana kwa hilo ila nina lalamiko la Wanakaratu, uliwaahidi utawapatia shilingi bilioni 4.5. Hili ndilo lalamiko la Wanankaratu isipopatikana shilingi bilioni 4.5, na nikushukuru kwa sasa mmetoa shilingi milioni 865 kati shilingi bilioni 4.5. Tunachoomba Wanakaratu sasa hizo fedha zingine zilizobaki katika shilingi bilioni 4.5 zipatikane ili wananchi wa Jimbo la Karatu waendelee kupata neema ya maji katika Mji wa Karatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukipata shilingi bilioni 4.5 upatikanaji wa maji katika Mji wa Karatu utakuwa zaidi ya asilimia 100 katika Mji wa Karatu. Kwa maana hiyo nikuombe Mheshimiwa Waziri tuweze kupatiwa shilingi bilioni 4.5 katika Mji wa Karatu maji yatapatikana kwa zaidi ya asilimia 100. Hii shilingi milioni 865 mliyotoa, inaweza kupeleka maji kutoka asilimia 70 mpaka asilimia 78, tukipata hizo fedha zingine zilizobaki ina maana tunakwenda kumaliza tatizo la maji katika Mji wa Karatu. Nikuombe sana hii shilingi bilioni 4.5 ambayo umeahidi Wananchi wa Jimbo la Karatu na tulikuwepo Wabunge wote wawili, tulikuwepo Baraza la Madiwani, walikuwepo Wenyeviti wote wa Mitaa katika Mji wa Karatu. Ulituahidi utatupatia shilingi bilioni 4.5. Ombi langu kwako tuweze kupta hiyo shilingi bilioni 4.5 ili wananchi wa Karatu waweze kupata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri kuna maeneo mengine hela chache chache zimebaki siyo hela nyingi sana ili mradi ukamilike. Kwa mfano, katika Mji wa Karatu kuna mradi ambao unatekelezwa eneo la Bwawani Mangaki ambao Serikali imeleta shilingi milioni 375 na mradi ule ulikua unahitaji shilingi milioni 640. Tulikuwa tunaomba hiyo hela nyingine kidogo iliyobaki mtupatie kama Wizara, lakini lingine ni shilingi milioni 640 eneo la Kata ya Mang'ola. Tunaomba mtupatie hizo fedha shilingi milioni 640.

Mheshimiwa Spika, lingine ni mradi ambao unatekelezwa katika eneo la Laja ambao unagharimu, umebaki shilingi milioni 136. Tukipata hiyo shilingi milioni 136 inamaana suala la maji katika eneo la Laja linaisha kabisa, vilevile kuna eneo la Chemchem, Mkandarasi pale anahitaji shilingi milioni 192 ili aweze kumaliza majukumu yale ya maji katika eneo la Chemchem. Tukipata hii shilingi milioni 192 kazi pale Chemchem itakuwa imeisha eneo la Kata ya Rotia.

Mheshimiwa Spika, vilevile tukipata fedha shilingi milioni 64 kumalizia mradi ambao unatekelezwa katika eneo la Mang'ola Juu Kijiji cha Mang'ola Juu Kata ya Daa. Vilevile niseme Mheshimiwa Waziri tunakushukuru sana, wananchi wa Jimbo la Karatu tunakuomba utupatie hizo fedha na mimi naamini ukitupatia hizi fedha nilizotaja hapa ni kwamba katika eneo la Mjini maji yanakwenda asilimia 100, maji katika eneo la vijijini inakwenda asilimia zaidi ya 75. Nikuombe tupatie hizi fedha ili wananachi wa Jimbo la Karatu waendelee kupata neema ya maji ambayo imekosekana kwa muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri mimi nikuombe katika Jimbo la Karatu maeneo ya vijijini hitaji letu sisi maji yanapatikana, huwezi kuchimba zaidi mita 100. Kwa hiyo, tunachoomba ni kwamba sasa utaratibu ule wa gari zile za Mkoa ambayo sasa imeletwa kwa Mkoa wetu wa Arusha Mheshimiwa Zaytun amechangia hapa kwamba tayari tuna

gari, ombi letu ni kwamba sasa katika eneo la Karatu uweze kutupatia visima vichache katika maeneo ya vijijini ili wananchi wetu waendelee kupata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri nakushukuru sana na nikutoe hofu wananchi wa Jimbo la Karatu wanakusubiri kwa hamu kubwa sana ili wakushukuru, kwa niaba yao nimkuja kuleta shukrani kwako kwa watu walinyonywa miaka 20 iliyopita kwa shilingi 3,500 na leo tunaendelea kula neema ya shilingi 1,300 kwa *unit. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye *DP* maji leo zinapatikana kwa shilingi 1,000 kwa *unit.* Nikushukuru sana Mungu akutangulie uendelee kutuletea mambo mengine mengi katika Jimbo la Karatu sana, nikushukuru sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Emmanuel Lekishon Shangai atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, Mheshimiwa Amandus Julius Chinguile ajianae.

**MHE. EMMANUEL L. SHANGAI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia bajeti ya Wizara ya Maji. Nitangulize kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuwatumikia Watanzania kwa upendo mkubwa pamoja pia na kumpongeza Waziri wa Maji, Naibu Waziri wake, Katibu Mkuu na Wasaidizi wote pamoja na watumishi wa *RUWASA* Wilaya ya Ngorongoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi binafsi nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri. Nimemfuata sana kuhusiana na suala la mradi wa maji wa vijiji nane, mradi wa Mageri. Mradi huo umeanza toka mwaka 2016, mradi huu ungetakiwa kuwasaidia zaidi ya wananchi 80,000 lakini mpaka leo bado una suasua. Nashukuru kwamba nilikuona toka wiki iliyopita umeweza kutusaidia tumepata zaidi ya shilingi milioni 500 kwa ajili ya mradi huo.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru pia kwenye mradi wa Lopolu umetupatia shilingi milioni 100 ambayo itaenda kumaliza tatizo la maji kwenye Kijiji cha Lopolu pamoja Oldonyouwas, nashukuru kwa hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye Wilaya yetu ya Ngorongoro tuna miradi zaidi ya 14 ambayo inaendelea, miradi hiyo yote inahitaji zaidi ya shilingi bilioni 10 ili iweze kuwahudumia wananchi, lakini mpaka sasa kwenye bajeti ya mwaka jana tumepta fedha 40% tu kwa miradi yote inayoendelea. Kwa hali hiyo ni kwamba hatuwezi kwenda kutatua shida ya maji tunakuwa na miradi mingi inayoendelea lakini fedha hazitoki. Mimi nikusihi Mheshimiwa Waziri tunaomba tunapotenga fedha hasa katika maeneo ambayo yana shida ya maji kama Wilaya ya Ngorongoro tujitahidi kuwapa kipaumbele, tuwaletee fedha kwa wakati ili wananchi wanufaike na juhudi za Serikali yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna suala lingine, kwa mfano leo kati ya miradi inayoendelea kwenye Wilaya ya Ngorongoro kuna mradi wa maji Digodigo. Inahitaji shilingi milioni 42 na imefika 90%, tukipata hizo fedha mradi huu utaisha. Tuna mradi wa maji wa Oldonyosambu Masusu. Mradi huu umeanza toka mwaka 2018 lakini mpaka leo mradi huo umefikia 85%, mkandarasi hajalipwa, fedha zinadaiwa shilingi milioni 270 kwenye mradi huo.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni uchimbaji wa visima viwili katika Vijiji vya Loswas na Soitsambu. Inahitajika shilingi milioni 112 na mradi umefikia 100% lakini fedha hazijafika. Wananchi wanahitaji kutumia yale maji lakini bado fedha hazijalipwa, maana yake kuna vitu bado vinahitajika kwa ajili ya kumalizia. Kwa hiyo, nikuombe Mheshimiwa Waziri utupe kipaumbele kwenye miradi hii ili wananchi waweze kupata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mradi mwingine ni mradi wa ukarabati Oldonyosambu, Kisangiro, Olaika imefikia 95% lakini fedha shilingi milioni 117 bado hamjapeleka. Nikuombe wewe binafsi Mheshimiwa Waziri unafanya kazi nzuri lakini tukichelewesha fedha maana yake wananchi hawatapata maji. Nikuombe mpeleke fedha huko.

Mheshimiwa Spika, mradi wa Olemishiri nashukuru kwamba hilo umeshatatua tumepata shilingi milioni 100 kwa ajili ya kumalizia mradi ule lakin mradi wa Mbuke awamu ya kwanza na awamu ya pili bado wanadai shilingi milioni 550 hamjapeleka mpaka leo. Wananchi wale wanafuata maji zaidi ya kilometa 40. Tunatakiwa kuwasaidia mradi wa Mbuke *phase one and two*. Kwa sababu baada ya wataalamu kuanza kufanyia marekebisho kwa sababu ni *existing project* sasa hivi wananchi hawapati maji. Niwapongeze wataalamu kwa sababu juzi wamefunga *solar* lakini bado haiwafikii wananchi imefika Shule ya Msingi Arash lakini haifiki kule ambako kuna wananchi kwenye *DP* zile tisa zingine.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri suala lingine ambalo nataka tuone ni kwamba kwenye Wilaya ya Ngorongoro kuna zile Kata ambazo zimefuatana na eneo la Pori Tengefu. Wananchi wale walikuwa wanategemea maji kutoka yale maeneo yaliyotengwa lakini sasa hivi hawana maji. Ukienda Kata ya Ololosokwan wananchi wanategemea kwenda kuchukua maji kule kwenye eneo la Pori Tengefu lakini hakuna na kule pia hakuna vyanzo vingine vya maji. Mlichimba visima lakini mpaka leo tunasikia tu *procurement* ya *pump* bado zinafanyika ngazi ya Wizara. Tunaomba mfanyie kazi hilo kwa sababu wananchi hawapati maji na ndiyo maana bado unasikia kwamba bado kuna vurugu kati ya wananchi na wahifadhi kwa sababu hawapati maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine kwenye Kata za Arash pamoja na Piaya inaonekana kwamba kuna uhaba wa

vyanzo vya maji. Kwa hiyo, tunahitaji visima zaidi. Suala lingine ni suala la Kata ya Piaya. Mheshimiwa Waziri nikuombe ombi *special* kabisa. Kwenye Kata hiyo ya Piaya wananchi wanakunywa maji ya chumvi ambayo ina *fluoride* ambayo ukiwakuta watoto wadogo wanadhurika. Kwa hiyo, nikuombe ututafutie mtambo wa kusafisha maji kwenye Kata ya Piaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni suala la bei ya maji na hii nitaondoka na mshahara wako leo usipotuambia. Ukija kuhitimisha hapa, mwaka jana nilichangia kwenye Mji wa Waso na Loliondo bei ya maji ni kubwa sana ambayo wananchi wanashindwa kumudu. Nikuombe tena utakapokuja kuhitimisha utuambie kwamba kwa sababu ulishawatuma wataalam wa *EWURA* kuja kushughulikia jambo hilo tujue kwamba limefika wapi ili wananchi wapate ahueni. Wananchi wengine wameamua badala sasa ya kuchota maji kwenye bomba kama anavyodhamiria Mheshimiwa Rasi, kuna wakina mama wamerudi mtoni kwa sababu hawawezi kumudu bei ya maji kwenye Mji wa Waso na Loliondo. Kwa hiyo nikuombe sana uweze kushughulikia hilo.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni suala la vitendeakazi. Unajua jiografia ya Wilaya ya Ngorongoro Mheshimiwa Waziri kwa sababu wewe umefika. Ukitoka Makao Makuu uende mpaka Pinyinyi kwenye mradi uliopo ambao unatekelezwa ambao pia bado inahitaji fedha na gari lenyewe iliyopo kwenye Wilaya yetu ambayo *RUWASA* wanayo ni gari bovu. Wanaweza wakakaa zaidi ya wiki mbili hawawezi kwenda kwenye mradi kwa sababu ya tatizo la gari. Kwa hiyo, nikuombe Mheshimiwa Waziri kama nilivyowasilisha mwaka jana nikuombe tena uweze kutusaidia kupata gari kwa ajili ya wataalam wa *RUWASA* ili wananchi wa Wilaya ya Ngorongoro wanufaike na matunda ya Serikali ya Awamu ya Sita. Kwa hiyo, nikuombe sana hayo uweze kufanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo mimi nishauri, naomba nishauri urasimu mkubwa uliopo kwenye Wizara yako. Tujaribu kuangalia namna ya kuweza kutatua tatizo hilo kwenye utekelezaji wa miradi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nashukuru sana. Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi atafuatiwa na Mheshimiwa Amandus Julius Chinguile, Mheshimiwa Boniphace Nyangindu Butondo ajiandae.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi hii. Nianze kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai na kunifanya nisimame leo mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya na hasa kwenye sekta hii ya maji. Mambo makubwa sana yamefanyika, uwekezaji mkubwa sana umefanyika na changamoto nyingi tulizokuwanazo kwenye sekta ya maji sasa zimepungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitawapongeza Wizara ya Maji. Mheshimiwa Waziri, Naibu na timu yote ya watendaji, kwa kweli mnafanya kazi kubwa sana. Mimi ni shuhuda kupitia Jimbo langu la Ukerewe, mmefanya kazi kubwa. Pamoja na kwamba kuna changamoto bado, lakini tulipokuwa, na hapa tulipo, kuna kila sababu ya kuwapongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Tanzania kama Taifa, tuna vyanzo vingi vya maji. Sisi Ukerewe tunazungukwa na Ziwa Victoria. Katika ukubwa wa eneo la Wilaya ya Ukerewe, *squire kilometer* kama 6,400 ni asilimia 10 tu iliyo nchi kavu. Asilimia 90 yote ni maji. Sasa kwa kusema hivyo, wakati mwingine

inaleta shida unapomwambia mtu kwamba Ukerewe tuna shida ya majisafi na salama.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza Wizara, mmefanya kazi kubwa. Mwaka 2022 mmetupa pesa nyingi kwa ajili ya miradi ya maendeleo, tumepiga hatua. Miradi hii ikikamilika, kimsingi tutabakiza eneo dogo sana. Hivi sasa tuna chini ya asilimia 70 ya maeneo ambayo yanapata majisafi na salama, lakini miradi yetu ikikamilika, tutakuwa tumeenda mpaka zaidi ya asilimia 90, ni jambo la kupongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Wizara kwa ujumla, kwa mwaka huu wa fedha mmetutengea zaidi ya Shilingi bilioni tano kwa ajili ya vijiji vyetu vitano vya maji; Kijiji cha Chabilungo, Kamea, Mkuno, Halwego na Bugorora, jambo ambalo litafanya *coverage* ya watu watakaokuwa wanapata majisafi na salama, kama miradi hii itakamilika, kuongezeka.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, tuna shida kubwa moja ambayo niliona ni muhimu niiseme hapa ili Mheshimiwa Waziri uone namna gani utaweza kutusaidia. Mwaka 2021 tulikuwa na tatizo kubwa sana kupitia mradi wetu wa maji vijijini, maarufu kama Mradi wa Kazilankanda, ambao unahudumia zaidi ya vijiji 10. Mradi ule unapata umeme kutoka *TANESCO* lakini bahati mbaya wana-*treat* mradi huu ambao unatoa huduma kwa wananchi kama mradi wa kibiashara, jambo ambalo limekuwa linafanya kila mwezi kunakuwa na *service charge* kwenye bili zaidi ya Shilingi milioni tatu.

Mheshimiwa Spika, haingii akilini kwamba inakuja bili ya Shilingi milioni tano, lakini *service charge* pekee ni zaidi ya Shilingi milioni tatu. Jambo hili lilitufanya tuweze kukaanao na kushauriana. Wakatushauri tutafute *pump* nyingine ambazo zitaendana na kiwango kile cha matumizi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri nawashukuru, mlinisaidia sana tukaweza kuagiza *pump,* tukazifunga. Wakatuomba tulipe deni, tumelipa, lakini bado wanakuwa wagumu sana kubadili mita yao, jambo linalopelekea bili iwe kubwa, na inakuwa ni mzigo kwa wananchi. Wanaingia gharama kubwa sana kulipa deni lile. Mwisho wa siku katika mwezi, wananchi wanapata maji wiki moja, wiki tatu hawapati maji.

Mheshimiwa Spika, sasa naiomba Wizara, sioni sababu ni kwa nini *TANESCO,* Taasisi iliyo chini ya Serikali, *RUWASA* Taasisi iliyo chini ya Serikali, mnashindwa kukaa na ku-*solve* tatizo kama hili, mwisho wa siku wanaoteseka ni wananchi.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Ukerewe wanaopata maji kupitia mradi huu wa maji vijijini, Mradi wa Kazilankanda wanapata mateso makubwa sana. Leo kwa mfano ninavyozungumza hapa, wananchi wanaopata maji kupitia mradi huu, wana zaidi ya wiki tatu hawajapata maji, kwa sababu tu ya kukosa muafaka kati ya Wizara ya Maji na Wizara ya Nishati, juu ya nini kifanyike kwenye suala la umeme ili wananchi wapate huduma wanayostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru wakati Mheshimiwa Naibu Waziri, amekuja Ukerewe alisaidia angalau ku-*solve* tatizo hili. Baada ya hapo, atakumbuka tulikubaliana kwamba sasa baada ya ku-*clear* deni, *TANESCO* wabadili mita, lakini bado jambo hilo halikufanyika. Kwa hiyo, naiomba Serikali ilichukulie jambo hili kwa uzito. Haiwezekani tunazungukwa na maji halafu bado wananchi wa Ukerewe waendelee kuathirika na maradhi yanayotokana na matumizi ya maji yasiyo safi na salama. Ni jambo lisilokubalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sana Mheshimiwa Waziri alichukulie jambo hili kwa uzito wa pekee. Nawashukuru, tulileta maombi tusaidiwe angalau kuongeza mtandao wa usambazaji wa maji kwenye eneo la mjini. Kwenye bajeti hii

tumekubaliwa, wametupa angalau shilingi milioni 300. Ni jambo jema, lakini bado nitaendelea kuomba, kwa lile ombi la karibu shilingi 1,200,000,000 waendelee kutusaidia.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza Mameneja wa Maji wa eneo la wilaya na mkoa, wanafanya kazi kubwa sana. Mtusaidie kutupa pesa hizi tuongeze mtandao. Wana uwezo wa kujisimamia na kukusanya mapato yatakayowafanya waweze kuongeza mtandao kwa gharama zao, lakini kinachokosekana ni ule mtaji tu wa kuongeza mtandao. Watusaidie kwenye eneo hili, ili mamlaka ya maji pale iweze kujiendesha. Sina mashaka nao. Zaidi ya hilo, nawapongeza, wanatusaidia kwa sehemu kubwa sana ukiachilia mbali eneo hilo la mradi wa maji vijijini, sehemu nyingine tunaenda vizuri na wametusaidia sana.

Mheshimiwa Spika, niwashukuru kwa zaidi ya shilingi bilioni tano walizotutengea kwa mwaka huu kwa ajili ya kuongeza mtandao. Ni jambo jema, lakini bado naomba *with a serious note,* kwenye hili eneo la Mradi wa Kazilankanda, watusaidie huu mgogoro wa umeme tuondokane nao ili wananchi wa Ukerewe wa-*enjoy* matunda ya kazi inayofanywa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan aliyedhamiria kuondoa shida ya maji kwenye jamii yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa na hayo machache, nashukuru sana kwa nafasi. Mwenyezi Mungu akubariki sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Amandus Julius Chingwile atafuatiwa na Mheshimiwa Boniphace Nyangindu Butondo, na Mheshimiwa Muharami Shabani Mkenge, ajiandae.

**MHE. AMANDUS J. CHINGUILE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi, na kwa hakika siyo tu kwa

kunipa nafasi, wewe umekuwa ni mwalimu na pia umekuwa ni mlezi. Umekuwa ukituongoza vizuri katika Bunge letu, na kwa kweli unaingia sasa kwenye rekodi ya Maspika wa viwango. Nakupongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa zawadi ya uhai. Pili, namshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa kweli Wana-Nachingwea wametufanyia vitu vingi sana, siyo tu kwenye sekta hii ya maji, amegusa karibu maeneo yote. Kwa hiyo, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, kipekee kwenye jambo hili la maji, wakati nikiwa mwanzoni wa Ubunge wangu, nililalamika sana hapa kuhusu suala la maji na hasa kwenye Vijiji vya Mchangani na Namanga. Leo nasimama nikiwa na furaha kwamba vijiji hivi; Kijiji cha Mchangani sasa maji yanamwagika. Hii ni kazi nzuri ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kwenye Kijiji cha Namanga, kwenye huo mradi wa Namanga ambao una zaidi ya Shilingi milioni 700, muda wowote kuanzia sasa mkandarasi yuko *site,* anaendelea kufunga *pump.* Kwa hiyo, maji yanaenda kutoka sasa, muda siyo mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siyo hivyo tu, kwenye ukurasa wa 35, Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, Serikali inakwenda kutekeleza mradi mkubwa wa maji ambao utanufaisha Wilaya ya Ruangwa na Nachingwea pamoja na Wilaya ya Lindi.

Mheshimiwa Spika, naishukuru sana Serikali kwa mradi huu, kwani unaenda kuwatua ndoo wamama wa Nachingwea, Ruangwa pamoja na Lindi. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri na timu yake. Ombi langu kwenye eneo hili, Mheshimiwa

Waziri aende kuhakikisha mradi huu unakamilika kwa wakati. Watu wana matumaini makubwa sana na mradi huu ambao unakwenda kunufaisha vijiji 56. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri alimwagiza Mheshimiwa Naibu Waziri kuja kwenye Jimbo langu la Nachingwea, na kwa kweli alijionea kwa macho namna ambavyo watu wanahainga kwenye suala la maji kwenye Vijiji vya Ngunichile. Alikwenda Namikango, na pia viko vijiji vingine; kuna Mbondo, Kilimarondo na Matekwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye eneo hili la Ngunichile, hakuna chanzo cha uhakika, na tuliomba visima virefu. Kwenye bajeti hii ambayo imepita, tuliomba visima tisa, lakini vilivyoidhinishwa ni vitano. Mheshimiwa Waziri nakuomba sana, tumalizie tu hivyo vinne, peleka fedha kwenye Jimbo langu la Nachingwea ili wananchi wale waendelee kufaidi matunda ya kazi nzuri ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uko mradi wa Mbwinji ambao unanufaisha Wilaya ya Masasi na Nachingwea. Kwa sasa wataalam wetu wanakamilisha usanifu wa mradi mpya, mradi pacha kwenye mradi huu wa Mwbinji. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri, andiko hili litakapokuwa linafika kwenye Wizara, ajitahidi kuhimiza hizo fedha kufika kwa wakati kwa sababu tunakwenda kunufaisha vijiji zaidi ya 18 kwenye Jimbo la Nachingwea na vijiji sita kwenye Wilaya ya Ruangwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, iko changamoto ya wenzetu wa *RUWASA,* wanafanya kazi nzuri sana, na hasa viongozi wa Mkoa wa Lindi pamoja na timu yake, pia *Engineer* wa Nachingwea, *Engineer* Sultan pamoja na timu yake wanafanya kazi nzuri sana. Hata hivyo, wanafanya kazi kwenye mazingira yasiyo rafiki sana, hawana usafiri wa uhakika. Gari waliyonayo ni ya tangu 2010, imechoka.

*Engineer* anaweza kwenda mahali kushuhudia au kufuatilia miradi ya maji, anakwama huko. Pia halina uhakika tena kwa sababu linagharimu matengenezo makubwa ya mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, atuletee gari jipya Nachingwea ili vijana wale walio tayari kufanya kazi hii ya kizalendo waendelee kusimamia miradi hii ambayo Mhehsimiwa Rais anatupatia kwenye jimbo letu. Siyo hivyo tu, kwenye eneo hili, hata watumishi ni wachache. Tunao wahandisi wawili, tunaye dereva mmoja, *secretary* mmoja, pamoja na mwenyewe *Engineer. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hali hii, hawa wanafanya kazi kwa muda mwingi kuliko ilivyo kawaida. Kwenye hili sasa, naomba sana, vijana hawa wanaofanya kazi ya kizalendo, Mheshimiwa Waziri apate nafasi ya kututembelea ili tumwonyeshe kwa macho kazi nzuri na kubwa ambazo wanazifanya ili waone namna ya kuwatumia kwa ukubwa wake zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo yote, ni vizuri tuhakikisha hawa wakandarasi ambao wanapewa miradi, wanakamilisha kwa wakati. Huu mradi ambao nimepongeza na kuusifia wa Namanga, ulitakiwa ukamilike kwa muda mrefu uliopita, mwaka 2022 mwezi wa Kumi na Mbili. Baadaye wakasema kwamba kuna ununuzi wa pamoja wa mabomba na kadhalika. Kwa hiyo, akaongezewa tena muda, akasema mwezi wa Nne. Bado ikaendelea kurushwa hiyo, mpaka sasa hivi ambapo wamefikia hatma ya mradi huu.

Mheshimiwa Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, kwenye mipango yetu wakati tunaenda kutekeleza hii miradi, tuhakikishe tunakwenda kutekeleza kwa wakati, na hii itakwenda kuimarisha, hata namna ambavyo wananchi wanaona hii miradi inakwenda. Kuna maeneo mengine

ukifika ukawaeleza, kwa sababu tayari wameshashuhudia miradi, wakati wa mwanzo wanaambiwa mradi huu utachukua miezi sita, au miezi 18, baadaye inaongezwa tena. Halafu ile ya kuongezwa kimya kimya, inaleta sintofahamu, na wakati mwingine sisi wawakilishi tunaonekana hatuko sawasawa.

Mheshimiwa Spika, kwa kazi nzuri inayofanywa na Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake pamoja na wataalam wake, mimi kama Mbunge wa Nachingwea, naridhika sana. Ninaamini hata haya niliyoyasema kwa uchache yanakwenda kufanyiwa kazi. Mheshimiwa Waziri ukipata nafasi tembelea Nachingwea. Sisi hatuna zawadi kubwa kule, hatufugi ng'ombe, ila tutakushikia kuku. Hizo ndiyo mila za watu wa Kusini, na hiyo ndiyo itakuwa zawadi kubwa kabisa kuliko yote.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, na ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Boniphace Nyangindu Butondo, atafuatiwa na Mheshimiwa Muharami Shabani Mkenge, na Mheshimiwa Francis Isack Mtinga, ajiandae.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Nami naanza kuungana na wenzangu kwanza kukupongeza wewe Spika wetu wa viwango kabisa kwa namna ambavyo Bunge letu hili tukufu ambavyo umekuwa ukiliendesha kwa umahiri na busara ya hali ya juu sana. Hongera sana Mheshimiwa Spika, Dkt. Tulia Ackson. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo Rais huyu ameendelea kukonga nyoyo za Watanzania na hasa kwa kuhakikisha kwamba anaendelea kuwatua ndoo

akina mama ambao wamehangaika kwa muda mrefu sana na tatizo kubwa la maji. Kwa kweli sisi Watanzania tunamtakia kila la heri na afya njema Rais wetu aendelee kutuletea maendeleo katika Taifa letu hili la Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Aweso pamoja na Mheshimiwa Mahundi, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na *DG* wa *RUWASA* kwa namna ambavyo kwa kweli wamekuwa wakitusimamia vizuri sana katika eneo hili la sekta ya maji. Watanzania wote wanaiona kasi yenu, utendaji wenu na kwa kweli sisi kama Wabunge, tunaridhishwa sana kwa namna ambavyo mmekuwa mkishirikiana na watendaji wa ngazi za chini, na pia kwa namna ambavyo mnashirikiana nasi Wabunge katika maeneo yetu mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kumpongeza *Engineer* wetu wa Mkoa wa Shinyanga, Dada Juliet Kayovela, na pia nimshukuru sana *Engineer* wangu Dickson Mazima, huyu ni Meneja wa *TARURA* wa Wilaya ya Kishapu. Hawa wote kwa kweli wamekuwa na ushirikiano mkubwa nasi Wabunge na hasa mimi mwenyewe katika eneo la jimbo langu na watendaji wa Halmashauri na viongozi wengine katika Wilaya yangu ya Kishapu.

Mheshimiwa Spika, na hiyo unaweza kuona kwamba miradi katika Wilaya ya Kishapu imekuwa ikienda vizuri sana, lakini kwa sababu ya ushirikiano mkubwa wa *RM* pamoja na *DM* katika eneo langu hili la Kishapu.

Mheshimiwa Spika, nataka tu niseme kwamba mpaka sasa Kishapu tangu mwaka 2020 mpaka hii 2023, hali halisi ya upatikanaji wa maji ilikuwa ni asilimia 39 katika kipindi cha mwaka 2020, lakini kwa sasa tuko asilimia 76. Ni hatua kubwa sana. Hili ni jambo ambalo wengi wa wanaKishapu wanaona ni ndoto, ni jambo ambalo hawaliamini katika macho yao. Pongezi zote tunaomba tumrudishie Mheshimiwa Rais wa

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuwa kweli Mama anaona umuhimu wa kuweza kuwasaidia na kuwashusha ndoo akina mama wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa tuna miji kama Maganzo inapata maji ya Ziwa Victoria, kuna Mbiu, Kata ya Mwadui Lohumbo, kuna Uchunga, kuna Wela, Ukenyenge na Mji wetu ambao ni Makao Makuu ya Wilaya ya Kishapu, haya maeneo tunapata maji ya Ziwa Victoria, lakini haitoshi. Ipo miradi ambayo sasa hivi inaendelea kutekelezwa. Naomba tu nitaje baadhi ya miradi. Upo mradi wa Nyenze – Mwang'oro hadi Kabila; na Idukilo - Igumandobo ambayo ina thamani ya Shilingi bilioni 2.5. Mradi huu unaendelea mpaka sasa, na huu ni mradi wa maji ya Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Spika, upo Mradi wa Ipeje – Itilima - Ikonopyelo, Ikoma na Ipeja. Huu ni mradi mkubwa wa thamani kubwa ya Shilingi bilioni 3.1, ni mradi ambao sasa hivi unaendelea pia kutekelezwa. Upo mradi wa Mwashohohela, huu ni uchimbaji wa visima; na Dulisi. Hii ni miradi ambayo inatekelezwa kwa sasa, japokuwa kuna changamoto ya upatikanaji wa maji, lakini naamini kwamba tutawasiliana na Mheshimiwa Aweso ili katika usanifu utakaokuwa unaendelea, tuone namna ambayo tunaweza kuwaokoa hawa watu wa Kata ya Sekebugoro, na ikiwezekana tuongezewe bomba pengine kutoka *Old Shinyanga,* ilimradi tuongezewe uwezo wa kuweza kusambaza maji katika maeneo hayo, kwa sababu maeneo hayo yako karibu sana na *Old Shinyanga*.

Mheshimiwa Spika, vile vile upo Mradi wa Wela, Wila, Mataga na Mwanulu, ni mradi ambao unaendelea mpaka sasa hivi, na huu ni mradi mpya. Hii ni miradi ambayo inakwenda. Upo Mradi mkubwa wa Igaga - Mwamashele unakwenda Mwamanota unakwenda Lagana, ni mradi mkubwa wa shilingi bilioni 6.5. Kampuni ya Emirates mpaka

sasa ninavyozungumza iko site inaendelea na kazi. Ni mradi mkubwa wa maji ya Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Spika, uko mradi wa Ndoleleji wa Malasa, Mwakipoya wa bilioni 1.6 mradi wa maji, usambazaji wa maji katika Mji wa Maganzo milioni 250 unaendelea. Lakini mradi wa usambazaji wa maji Mwamalasa, Mwamashimba mradi 101, pia kuna mradi wa Ngundangali – Seseko, mradi wa Mangu, Kiloleli, Ng'oloshinong'ela na Bulekela milioni 156 hizi tumeomba fedha za usanifu. Mheshimiwa Aweso tunaomba utupatie hizi fedha ili mradi tuone namna ambavyo tunaweza tukaamua ni mradi gani tutapeleka maeneo hayo. Kwa sababu uchimbaji wa visima virefu inaonekana kama unashindikana, ikiwezekana tutaomba tuchimbiwe mabwawa katika maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, kuna mradi wa Momolasa, Somagedi, Mwagalankulu ambao huu na wenyewe nimeuzungumzia lakini mradi wa Nobora, Jijongo milioni 510 unaendelea. Mradi wa kutoka Mhunze kwenye Mwabusiga na wenyewe unaendelea. Kwa sababu muda hautoshi naomba nizizungumzie baadhi ya changamoto, miradi wa Maji ambayo inafadhiliwa na Mfuko wa Maji wa Taifa imekuwa na changamoto kubwa, fedha zimekuwa hazifiki kwa wakati na hii imesababisha kuchelewesha miradi mingi ambayo iko chini ya mfuko wa fedha hizi. Mheshimiwa Waziri nakuomba sana hili jambo waone umuhimu wa kuweza kufatilia ili mradi mfuko huu utoe fedha kwa wakati na miradi iweze kutekelezeka kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo kubwa, kuna changamoto pia ya gari juzi nimepewa na *Eng.* Julieth gari moja kukuu nina gari moja lililochoka sana. Kwa hiyo, hili ni tatizo kubwa. Ninakuomba Mheshimiwa Waziri kwa Wilaya ya Kishapu tupatie gari jipya ili mradi kazi ziweze kutembea sawasawa.

Mheshimiwa Spika, kuna suala zima la *certificate* zinapokuwa zimekuwa–*raised* na ziko tayari tatizo kutokutoa, kutokulipa fedha kwa wakati. Kwa fedha ya miradi yote hili limekuwa ni tatizo sugu nakuomba Mheshimiwa Waziri hili lisimamie hili *certificate* zinapokuwa *raised* na zilipwe kwa wakati ili mradi miradi iweze kutekelezeka kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, jambo jingine ni maeneo ambayo…

**SPIKA:** Mheshimiwa Kengele ya pili imeishagonga, dakika moja malizia.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Maeneo mengine ambayo nilikuwa nataka kuzungumzia ni maeneo ambayo hasa ya miradi ambayo ni ya zaidi ya bilioni moja. Kumekuwepo na tatizo kubwa sana kwenye msamaha wa kodi *VAT exemption.* Ninaomba Mheshimiwa Waziri miradi mingi sana imekuwa ikichelewa kutekelezwa kwa sababu ya ucheleweshwaji wa upitishaji wa hii *VAT exemption*. Ninaomba sana hili lizangatiwe na hii itasaidia sana miradi kukamilika kwa wakati lakini hata wakandarasi hawa tuwahurumie wakati mwingine tunaingiza katika mufilisi pasipo kuwepo na sababu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo baada ya kuzungumza hayo ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Muharami Shabani Mkenge atafuatiwa na Mheshimiwa Francis Isack Mtinga na Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya ajiandae.

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kupata nafasi hii leo ya kuchangia Hotuba ya Wizara hii ya Maji. Kwanza kabisa ningependa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uzima wa kuwa hapa siku ya

leo na pili ningependa kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya na hasa katika sekta hii ya maji.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais, ana azma kubwa ya kumtua ndoo mama kichwani, katika kuhakikisha kwamba Tanzania inakuwa na miradi mingi ya maji. Lakini Mheshimiwa Rais si kumtua ndoo mama kichwani peke yake hata sisi wababa wanatutua mizigo ya mawazo vichwani kwa sababu wake zetu walikuwa wanatumia muda mwingi sana kwenda kufuatilia maji ambayo shughuli nyingine zenye maendeleo nyumbani zilikuwa zinasinyaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri ndugu yangu Mheshimiwa Jumaa Aweso kwa kazi kubwa anayoifanya. Mheshimiwa Aweso pamoja na Naibu Waziri wake, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Viongozi wengine wa wizara hiyo wanaitendea haki wizara yao kwa kuhakikisha kwamba miradi ya maji inafanikiwa katika nchi nchi hii.

Mheshimiwa Spika, waswahili wanasema mnyonge mnyongeni haki yake mpeni lakini Mheshimiwa Aweso hatonyongwa atapewa haki yake akiwa mzima na bajeti yake leo itapitishwa hapa ili aweze kwenda kutuhudumia watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia napenda niwapongeze wenzangu katika Jimbo la Bagamoyo na hasa viongozi, ma–*engineer* wanaotoa huduma katika maji ningependa nichukue nafasi hii kumpongeza *engineer* James Kionaomela ambaye yeye huwa mara nyingi sana anatupatia taarifa au Mbunge wake ananipatia taarifa katika miradi ya maji ambayo inayoendelea katika Jimbo la Bagamoyo. Pia ningependa kumpongeza *manager* wa *DAWASA* wa Mapinga ndugu yangu Abrahamu Mwenyemaki ambaye

naye pia amekuwa msaada mkubwa kwangu kunipatia taarifa mbalimbali kuhusu masuala ya maji katika Jimbo langu la Bagamoyo.

Mheshimiwa Spika, tarehe 16 Machi, 2023 Mheshimiwa Waziri Mkuu alizindua mradi kubwa kabisa wa uhifadhi wa maji, alizindua tenki la maji la lita milioni tano pale maeneo ya Kibaha. Mradi huo wa maji umesaidia sana au unaendelea kusaidia sana Mikoa ya Dar es salaam na Pwani. Kwa sababu mradi huu utahudumia watu zaidi ya 37,000 katika Miji wa Dar es Salaam na Mji wa Bagamoyo.

Mheshimiwa Spika, ningependa kabisa nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwamba mradi huo wa maji ambao uko pale uliyozinduliwa wa lita milioni tano unasaidia katika kata zangu za Mapinga na hasa katika vitongoji vya Kibosha pamoja na Kimele, na vilevile unasaidia katika Kata ya Kerege katika vitongoji vya Kitanga, pamoja na Nyakahamba kwa kweli juhudi kubwa imefanyika na Serikali katika kuifanya hili zaidi ya dola milioni 86 zimetumika katika mradi huu.

Mheshimiwa Spika, kuna mradi mwingine wa upanuzi wa mradi wa maji wa Kidomole ambao umetumia shilingi milioni 334, zaidi ya milioni 334 mradi huu kwa kwakweli utakuwa mkombozi mkubwa sana kwa wananchi wangu wa kata ya Fukayosi hasa maeneo ya Kidomole katika Vitongoji vya Relini, kitongoji cha Mwanasenga, kitongoji cha Kinyamvuu pamoja na kitongoji cha Vihagata. Huu mradi utakapokamilika wananchi hawa nafikiri wataishukuru sana Serikali kwa kiwango kikubwa sana, kwa sababu miaka mingi sana hawana maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile kuna mradi wa shilingi milioni 583 wa kupeleka maji katika Kijiji cha Kitame. Mradi huu wa maji wa milioni 385 unaendeshwa na mkandarasi mmoja anaitwa Amkami Mheshimiwa Waziri. Naomba nikwambie

mradi huu ushafikia asilimia 35 lakini mpaka leo mkandarasi bado hajalipwa, ametumia pesa zake mwenyewe kwa uzalendo wake. Kwa hiyo, tunaomba muongeze juhudi katika kuwalipa wakandarasi ili miradi hii ya maji iweze kwenda mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna mradi mwingine wa maji ambao unaitwa Mradi wa SE Kitongoji cha Segwa pamoja na Magofi wa milioni 155. Mradi huu unaendelea vizuri na wananchi muda si mrefu wata-*enjoy* kupata maji.

Mheshimiwa Spika, katika Kata ya Makurunge na Kata ya Fukayosi bado tuna changamoto kubwa sana ya upatikanaji wa maji. Watu wa Fukayosi na Makurunge wanapata maji kutoka katika Mradi wa Wami, lakini sijui mpaka sasa hivi Mheshimiwa Waziri nini kinaendelea? Watu wa Makurunge, watu wa Fukayosi wanakaa mpaka miezi mitatu bila ya kupata maji.

Mheshimiwa Spika juzijuzi hapa watu walinipia simu ilifikia hatua mpaka walimu wakataka kufunga Shule Msingi pale Mkenge kwa sababu wanafunzi hawana maji ya kutumia. Nikamuomba Meneja wa *DAWASA* wa Chalinze Fumbuka ilibidi atume doza la kupeleka maji pale shuleni wananchi ili waweze kunusurika. Kwa kweli Waheshimiwa Waziri hali ya pale mbaya sana.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri nimeona katika hotuba yako nimeona pesa ambazo umezitenga kwa kipindi cha bajeti ya Mwaka 2023/2024 kuna miradi ambayo nitanufaika nayo. Mradi wa Kifuda Razaba, Mradi wa Wami Fukayosi, Makurunge, Mkenge Fukayosi, Kalimeni yote imeingizwa katika programu ya kupatiwa pesa kwa kipindi hiki kijacho hili miradi hii iweze kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala moja ambalo nataka nimwambie Mheshimiwa Waziri. Suala la Misamaha ya Kodi

kwa Vyombo au Vifaa vya Miradi ya Maji. Mheshimiwa Waziri hakuna kitu kinachokuchelewesha sana katika miradi yako kama jambo hili hebu jaribu kufanya kila njia utakayoiweza. Kaa na mamlaka zinazohusika pale wakandarasi ambapo wameishapata *tender* kuhakikisha wanapatiwa hii misamaha ya kodi haraka iwezekanavyo ili miradi iweze kuendelea.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu leo hii utakuta mkataba wa mradi unasainiwa lakini bado mradi unaweza ukakaa zaidi ya miezi minne, mitano mpaka sita au mwaka mmoja ukiulizwa mradi huu kwanini hauendelei utaambiwa kwamba bado hatujapata msamaha wa kodi. Kwa hiyo, niombe Wizara yako nikuombe Mheshimiwa Waziri, uwe karibu na viongozi hawa ambao wanatoa hii misamaha ya kodi kwa ajili ya hii miradi ya maji kukufanyia haraka na wepesi zaidi ili…

**SPIKA:** Mheshimiwa, Kengele imeishagonga.

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE:** …ili uweze kuhakikisha kwamba Miradi hii inafanyika kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache nashukuru sana, Ahsante naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Francis Isack Mtinga, atafuatiwa na Mheshimiwa Aida Khenani na Mheshimiwa Cecil David Mwambe ajiandae.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi niweze kuchangia katika Wizara hii ambayo ni uhai wa Watanzania, kwa sababu wote tunajua kwamba maji ni uhai. Naomba nianze kwa kumshukuru sana Waziri kwa jinsi ambavyo amekuwa akifanya kazi vizuri yeye na timu yake kazi ya kuwasikiliza Watanzania na kuwapelekea maji kama ambavyo Rais wetu amemuagiza.

Mheshimiwa Spika, nimshukuru pia watendaji wake katika ngazi ya Mkoa. Namshukuru sana Meneja wa *RUWASA* wa Mkoa wa Singida ni mtu rahimu sana, anasikiliza watu na hivyo wananchi wa Mkoa wa Singida wanampenda sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha nimpe tena salamu Mheshimiwa Waziri kutoka Wananchi wa Mkalama uliwahamishia Meneja wao *Engineer* Mchunguzi. Wamenituma mimi ndiyo msemaji wao wanamuhitaji meneja wao arudi kwa sababu wana jambo lao. Kwa sababu anawasikiliza vizuri wangekuwa tayari sana kama angekuwa amepandishwa cheo wangemuacha aende lakini kwa sababu ameamishwa anaendelea kuwa Meneja kama alivyokuwa Mkalama na mimi kwa sababu ni msemaji Madiwani, Chama cha Mapinduzi na wananchi walimwambia mpaka Katibu Mkuu wa Chama kwamba wanamtaka Menejaager Mchunguzi arudi. Kwa hiyo, nimefikisha hili nijivue kwamba wanamuhitaji meneja wao *Engineer* Mchunguzi kwa sababu walimuelewa anafanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi hatuna shaka hatujui aliyekuja lakini wenyewe wanamtaka wakwao waendelee nae. Kwa hiyo, nimeona hilo nikwambie ulijue na najua *DG* wa *RUWASA* yupo nilimpigia simu akanihaidi lakini mpaka sasa haijatekelezwa kwa hiyo nimeona niifikishe.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri nikushukuru kwamba umeendelea kutupatia pesa, umetupatia milioni 165 kumalizia mradi wa maji pale Nkalakala tunakushukuru sana, umetupatia milioni 240 kumalizia mradi wa maji pale Maraja tunakushukuru sana. Vilevile nikushukuru nimekusumbua sana ukanipatia milioni 208 kuanza mradi pale Mbigigi wakati naingia Ubunge nilikuta umefanyika upembuzi wa kina na yalipoanza kujengwa maji kule kwenye kijiji nilikozaliwa wakadhani nimehamisha hela za Mbigigi. Kwa hiyo,

nakushukuru sana umezileta milioni 208 na sasa mkandarasi anakwenda kukabidhiwa kazi kwa ajili ya mradi ule nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika bajeti hii umetupitishia shilingi milioni 208 bajeti hii itakapopita kwa ajili ya kwenda kupeleka maji katika kijiji cha Matongo na Isene watu hao wamepata shida sana ya maji kwa kutumia chanzo cha Isene sasa tutajenga mradi wa *tank* pale umetushia milioni 208 na itahudumia vijiji viwili nikushukuru sana kwa ajili ya hilo.

Mheshimiwa Spika vilevile umetupitishia milioni 300 kwenda kujenda miundombinu na umaliziaji katika jiji cha msingi kata ya Msingi nakushukuru sana wewe ni mtu rahimu sana. Vilevile umetupitishia milioni 378 kwa ajili ya kupanua mradi wa maji wa Tumuli ambao umeishajengwa sasa kwenda kuongeza vituo na ile kata nzima iweze kupata maji safi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, haikutosha Mheshimiwa Waziri wewe ni mtu wa Mungu sana umetupitishia milioni 396 kwa ajili ya kwenda kuchimba visima kwenye vijiji vya Domoniki, Nkinto, Ilunda, Kitundili, Kisulwiga, Mwangeza, Kibii, Gumanga, Asanja na Lugongo yote hii umetupitishia katika bajeti hii na hakika bajeti hii itapita nikuombe Mheshimiwa Waziri mara tu baada ya kumaliza Bunge na tukapitisha *finance bill* hela hizi zianze kumwagika wananchi wa maeneo haya wameyasuburi maji haya kwa muda mrefu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimkumbushe Mheshimiwa Waziri tu kidogo mradi ambao umeishafanyiwa upembuzi wa kina wa kutoa maji Ziwa Victoria na kuleta Dodoma. Mradi huu utapita kwenye Jimbo langu na ukishafika kijiji cha Kisana pale Mheshimiwa Dkt. Mwigulu mradi ule unakuja kwa *gravity* mpaka Dodoma kwa hiyo, ni *economical* sana. Kwa hiyo, nikuombe huu mradi msiuweke kapuni, mradi huu uendelee

najua kwa sababu utapiata kwenye jimbo langu hakika sisi wa Mkalama tutaogelea maji cha ajili ya mradi huu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naupigia debe na kukumbusha kwa sababu upembuzi umeishafanyika na ni *economical* unatembea kwa *gravity* kuanzia Singida mpaka hapa hebu mradi hii uangalie ili tupate chanzo cha uhakika cha maji ambacho na hakika sasa wananchi wa Tanzania kama mama ambavyo anaendelea kututua ndoo tunakwenda kula matunda ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa jinsi ambavyo alihaidi kumtua mama ndoo na anaendelea kumtua mimi nimuombee tu Rais wangu maisha marefu mpaka ifike hiyo 2030 na hakika nchi hii sasa itakuwa iko katika hali ambayo inategemewa kuwa kwa jinsi ambavyo tuna neema nzuri katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi watu wa Singada na wananchi wa Tanzania tunacho muombea hicho kura zitamwagika, kwa sababu hatuna shaka ndiyo maana tunaongelea mpaka 2030 kwa sababu ndiyo mama yetu ambaye anatulea na Mungu ametubariki kupata viongozi wa namna hii ni bahati siyo wengi kama ambavyo wanapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia muda nikushukuru sana siyo kwamba sio muhimu lakini umekuwa Spika wa viwango mpenda haki, Spika ambaye tukiwa humu ndani tunajisikia tuko sawa *form one, form two,* na hata waliyo *form three* wote tunajiona tuna haki. Kwa sababu ya uongozi wako na weledi wako mzuri Mungu akubariki akutie nguvu ili tuendelee ku–*enjoy* katika Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MBUNGE FULANI:** Unga hoja.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, atafuatiwa na Mheshimiwa Cecil David Mwambe na Mheshimiwa Abeid Ingondo Ramadhani ajiandae.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema aliye nijalia afya niweze kusimama tena kwenye Bunge lako tukufu. Niungane na Wabunge wenzangu kukushukuru sana kwa namna ambavyo unatuongoza sisi Wabunge wenzio. Binafsi kama Mbunge mwanamke najivunia sana napoona kazi unayoifanya hatutapata kazi ngumu sana sasa juu ya kutambua nafasi ya mwanamke kwenye uongozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kusema uongozi ni pamoja na kuwasikiliza wenzio. Mheshimiwa Waziri wa Maji umekuwa unatuonyesha mfano kila siku, umekuwa ni mtu ambaye unasikiliza na unaamini kila mtu katika ushauri wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na usikivu huo kuna salamu kutoka kwa wana Nkasi Kaskazini, wanatambua ulipokuja ukiwa Naibu Waziri wa maji tukakueleza changamoto ya Maji ukatuambia ni namna gani utaanza kutekeleza mradi wa Kirando ukakamilika, wakakwambia kwa sababu umekamilika utaenda kuwa Waziri baada ya wiki mbili ulivyokuja ukawa Waziri. Siyo kwa sababu wanajua kuomba ni kwa sababu maneno ya kusema ubarikiwe huwa yanatoa baraka kwa watu wengi na jambo lako linafanikiwa. Tunatumaini kwamba kama umekaa muda wote huu ujabadilika huwezi kubadilika tunakushukuru kwa namna ambavyo unafikaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nianze na suala la Ziwa Tanganyika, leo nazungumza hapa nafikili ni zaidi ya mara tisa sasa. Kwa nini tunasema maji yatoke Ziwa Tanganyika? Natambua jitihada za Serikali kwenye jimbo langu juu ya kutatua changamoto ya maji. Mpaka sasa kwenye miradi inayoendelea, iliyopo kwenye matazamio na iliyokamilika kwa miaka mitano tu ni zaidi ya bilioni 18 lakini kata tano peke yake za pale mjini ambazo ndiyo sura ya Wilaya yetu ya Nkasi. Ukitaja hizo asilimia za upatikanaji wa maji vijijini watu wa Nkasi hawapendi hata kusikia hizo asilimia. Kwa sababu mpaka jana nawauliza watalamu wangu, mahitaji ya tano peke yake kati ya kata 17 ni lita 2,900,000 kwa siku yanayopatika ni lita 194 sawa na asilimia saba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nini tunasema maji yatoke Ziwa Tanganyika? Serikali imesha onyesha jitihida ya kutatua changamoto ya maji lakini fedha nyingi zinatumika kwenye kutafuta vyanzo vya maji na vyanzo vyenyewe kwa kuwa siyo vya uhakika kwa fedha zinaonekana hazijafikia yale ambayo watanzania tunategemea, wana Nkasi tunarajia kupata maji.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana Mheshimiwa Waziri alikuja kule, alivyokuja kuna mradi ulikuwa umekwama wa Bwawa la Mufindi, nikamwambia na mkandarasi amesimama kwa sababu hajalipwa. Siku hiyo hiyo Mheshimiwa Waziri aliagiza yule mtu amaliziwe fedha zake. Ule mradi baada ya kumaliziwa umefanya kazi miezi mitatu tu, maji hakuna Bwawa limekauka. Kwa sababu lengo letu ni kushauri kutoka Kilando kuja Namanyele, Kilando ndiko kwenye ziwa Tanganyika, kuja Namanyele ni kilomita 64 kuleta maji pale. Tunahitaji muujiza gani? Nchi yetu haina shida ya vyanzo kilichobaki ni uthubutu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Tano iliweza kuthubutu kutoa maji ziwa Victoria kufikisha mpaka Tabora ni umbali mrefu sana. Nini kinashindikana leo? Kilomita 64 tu wananchi waendelee kulia?

Mheshimiwa Spika, pamoja na yote anayoendelea kuyafanya Mheshimiwa Waziri, naomba nitoe mifano michache tu, kwamba kwenye hizi kata tano, Kata ya Namanyele peke yake hakuna kisima cha uhakika hata kimoja. Kijiji cha Mkangale wanatamani wapate majibu yao leo, kwamba na wao ni Watanzania hivyo wanahitaji kupata maji. Hakuna mbadala wa maji, huwezi kutumia *soda* badala ya maji, haiwezekani.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba hiyo dhamira inaonekana; najua kwamba Serikali ina mpango wa muda mrefu na mpango wa muda mfupi; mpango wa muda mfupi, wameomba fedha bilioni tano kwa ajili ya bwawa jingine; tunaomba kwenye hilo usisite. Lakini walichoniagiza leo wanaamini suluhisho la wilaya ya Nkasi Mkoa wa Rukwa, Mkoa wa Katavi na Mkoa wa Kigoma ni kutoa maji Ziwa Tanganyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kata ya Kipundu Kijiji cha Kakomwa hawana mbadala. Yaani sasa hivi unaona hii *pressure* imepungua ya mimi kukusumbua ni kwa sababu mvua bado inanyesha, ikikata tu *pressure* inarudi pale pale. Mheshimiwa Waziri tunakuomba, kwa sababu umeshaonesha nia tangu mwanzo, tunaomba tuione dhamira kwa kuwasaidia wanawake, kwa kuwasaidia watu wa Nkasi.

Mheshimiwa Spika, aliyeanzisha kauli hii ya kumtua mwanamke ndoo kichwani ni Rais wetu akiwa Makamu wa Rais. Leo aliyeanzisha ile kauli ndiye Rais mwenyewe, mwanamke. Mbunge wa Jimbo mwanamke, Spika wa Bunge ambako nasema leo mwanamke, Katibu Mkuu Wizara yako mwanamke; sasa tunategemea hayo mambo yatafanyika vizuri ili neno hilo tuliishi kwa vitendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, fedha zinazotumika kutafuta vyanzo vya maji ni nyingi sana, na hakuna sababu ya kufanya hivyo. Pamoja na kwamba kuna fedha ambazo zinatumika kwenye

kuchimba visima; naomba nitoe mfano mdogo tu, mwaka wa fedha mwaka 2021/2022 *DUWASA* walidhamiria kuchimba visima 250. Katika visima 250, kwa sababu tunahangaika na vyanzo vya muda mfupi, asilimia 23 visima hivyo vilikuwa havina tija, kutokana na ripoti ya *CAG,* asilimia 18 havikufanyiwa majaribio, asilimia 16 havikuchimbwa kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mazingira haya tumepoteza shilingi milioni 354.9 kwa ajili ya kuwalipa wakandarasi kwa kazi ambazo hazikufanyika. Wakati huo watu wanalipwa kuna maeneo ambayo upatikanaji wa maji ni asilimia saba. Jambo hili halifurahishi hata kidogo. Kama shida ni usimamizi kuna haja ya kuabdilisha ya *approach* ya usimamizi. Lakini kwa nini tuendelee kuchimba visima wakati vyanzo vipo vya uhakika? Kwa nini, tyuendelee kupoteza feha wakati vyanzo vya uhakika vipo?

Mheshimiwa Spika, Wizara walijiwekea malengo, pamoja na kwamba kiwango cha upotevu wa maji kipo katika kiwango kinachokubalika kwa asilimia 20, Wizara wamejiwekea malengo kufika 2022 angalau upotevu wa maji uwe asilimia 28. Kupitia ripoti ya *CAG* ya Machi, 2023 katika mamlaka za maji nane zilizokaguliwa ni mamlaka moja tu ambayo ilikuwa imefikia kiwango cha upotevu wa maji asilimia 20; Mamlaka ya Moshi. Hizi mamlaka saba zote bado tunarudi kulekule. Hii ni 2023, kwa hiyo hata Wizara malengo yenu bado hamjayafikia kwenye suala la upotevu wa maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni nini kinapelekea tufike huko? Kwenye upotevu kwa miaka miwili tu, hizo mamlaka nane ambazo zilikaguliwa tumepoteza kiasi cha shilingi bilioni 118.13. Hizo fedha kama ingekuwa si kupoteza kwenye kutafuta vyanzo zingesaidia maeneo mengine ikiwepo Nkasi ambao tuna uhitaji mkubwa wa maji.

Mheshimiwa Spika, kwa nini tumefikia huko? Aidha tunabahatisha au watalamu wetu wanashindwa kutimiza wajibu wao. Ninarudia tena, kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi mmesema mtatumia vyanzo vya uhakika kumaliza changamoto ya maji. Kama ndivyo tunasubiri nini kwenye hili jambo? Tutazungumza mpaka lini? Hivi kwa hali ya kawaida mtu akaja anasikia mimi nazungumza zaidi ya mara tisa kuhusu kutoa maji Ziwa Tanganyika, kilometa 64, tunahitaji muujiza gani kwenye hili jambo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, fedha ya dharura milioni 200 imekwenda mwezi wa tisa mwaka jana, hakuna hata kisima kimoja kinatoa maji nazungumza hapa. Tufanye nini? Haya mambo hayakubaliki, tunaomba ni bora fedha zikatengwa za kutosha tuanze kufikiria suala la maji miaka 100 ijayo kuhusu kufikiria hili jambo ambalo tunazungumza kila siku kwenye hili Bunge. Jana, leo, kesho na kesho kutwa changamoto ya maji. Vyanzo vipo tunaomba Wizara uthubutu ndio unaohitajika. Nakushukuru sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Cecil David Mwambe, atafuatiwa na Mheshimiwa Abeid Ramadhani Ighondo, Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso ajiandae.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, na mimi nishukuru kwa kupata nafasi hii jioni ya leo. Nikupongeze wewe binafsi kama ambavyo Wabunge wenzangu wamekupongeza, lakini pia nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anazozifanya pamoja na kusimamia Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Nimpongeze pia Mheshimiwa Waziri, Naibu wake, Katibu Mkuu Wizara hii na Katibu Mkuu aliyeondoka, lakini na watendaji wote wa Wizara ya Maji wakiwemo injinia wetu wa mkoa pamoja na injinia wa Wilaya Ndugu Juma. *(Makofi)*.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia *tone* ya Waheshimiwa Wabunge, mimi nimepata nafasi ya kuchangia mwishoni

kabisa, tunaelekea mwisho sasa. Ukiangalia *tone* ya Waheshimiwa Wabunge wote humu ndani sioni kama kuna mashaka kwa Mheshimiwa Waziri kupitishiwa Bajeti yake, tena naamini kwa kishindo kikubwa sana. Kwa sababu ukiangalia *tone* ya leo na miaka mitatu, minne, mitano iliyopita nyuma Waheshimiwa Wabunge wengi sana wameridhika, na nimeona kila mkoa kuna mradi mkubwa wa maji unaotekelezwa, ikiwemo pamoja na Mkoa wetu wa Mtwara.

Mheshimiwa Spika, Mzee Mkuchika angepata nafasi ya kusema hapa Bungeni kama wangekuwa wanatoa ruhusa mawaziri kuchangia nafikiri angedondosha machozi kwa furaha. Kwa sababu katika kipindi chake chote cha uongozi alipokuwa anafanya mikutano Newala, huyu Mzee wetu sikumbuki vizuri lakini walikuwa wanamuita kwa kimakonde Nangudyamedi kitu kama hicho, yaani wakiwa na maana kwamba wakati wa mkutano wananchi wasilmuulize swali linalohusiana na mambo ya maji kwa sababu hataweza kulijibu sababu Newala ilikuwa haipatikani maji kabisa. Ndiyo maana Mheshimiwa Hokororo jana hapa alisema kuwa Newala ndiko ambako wananchi walikuwa wanapika chakula kwa kutumia maji ya matiki maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kwa mradi huu mkubwa unaokwenda kutekelezwa sasa hivi wa Makonde utakaohudumia Wilaya zile nne, ninaamini ni ukombozi mkubwa sana kwa sisi watu wa Mtwara.

Mheshimiwa Spika, nimuombe pia Mheshimiwa Waziri, kwamba mradi huu wa Makonde ni mkubwa sana, utekelezwe kwa wakati, fedha ziende kwa wakati lakini tuangalie na mipango ya muda mrefu. Pamoja na sisi watu wa Ndanda na Masasi, Ruangwa, Nachingwea na wengine wote waliosema, tunajivunia maji ya Mbwinji lakini mradi wa Makonde ungeweza kuleta pia maji maeneo haya, kwa sababu Mto Ruvuma maji yake yamekuwa ya kuhama hama. Pamoja na kwamba mradi unakwenda kutekelezwa

lakini chanzo cha maji cha Makonde ni cha uhakika zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna miradi inayotekelezwa Jimbo la Ndanda; kuna mradi wa Chija Chiwata, Chija Mbemba, Ndanda hadi Nangoo, Mradi wa Nanganga Momburu, mradi wa Nambawala ambako mafundi wako wanachimba mitaro sasa hivi, pamoja na mradi wa Namalembo. Niombe sana pesa ziende sasa kwa wakati, kwa maana ya kwamba uangalie *cash flow* miradi hii itekelezwe ili wananchi waweze kupata maji. Lakini pia tuna maombi. Kuna visima ambavyo vilishachimbwa tayari kwenye vijiji vya Mpanyani, Chilolo, Masiku, Namichi Pamoja Sululu ya leo. Mruhusu Meneja wa Mkoa na Meneja wa Wilaya waweke pale *solar pans* ili wananchi waweze kuanza kupata maji wakati michakato hiyo ya kutaka miradi hii iwe mikubwa ya kuhudumia eneo kubwa iweze kukamilika.

Mheshimiwa Spika, tuna mradi pia wa Mwena Lihoya, umekuwa unasua sua, lakini tunaziona hatua za kuboresha mradi huu. Mheshimiwa naomba ukafanye marejeo kwenye mradi ule, ili wapelekewe fedha mradi huu ukamilike ili uweze kutoa maji ya uhakika kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, kuna miradi inayoendelea Jimbo la Tandahimba na Mheshimiwa Katani hujamuona unakumbuka, nafikiri unaamini *tone* yake ile ya mwaka jana lakini anasema anajipanga kwenye Wizara ya Miundombinu kwa sababu ya barabara zetu kule, mpaka sasa hatuna jibu la uhakika. Wizara ya maji ameamua apumzike kwanza kwa sababu miradi ya maji jimboni kwake inaenda vizuri sana. Vilevile tunangalie *cash flow* tuweze kuwapelekea maji watu hawa na fedha kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, Pamoja na mazuri yote unayoyafanya, mimi binafsi niombe tumsaidie Meneja wetu wa Wilaya kutekeleza majukumu yake vizuri *Eng*. Juma kwa

kumpatia gari litakalofaa. Tunapokwenda kufanya ziara kwenye Wilaya ya Masasi yenye miradi mikubwa zaidi ya kumi, yenye zaidi ya fedha bilioni 15 ndugu yetu huyu kuna wakati anafika kwenye ziara akiwa kwenye pikipiki kwa sababu gari lake ni bovu, halitengenezeki na liko *beyond repair*. Tunaomba apatiwe gari jingine ili aweze kusimamia majukumu yake sawasawa na tufanye nae ziara kwa uhakika.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka siku moja nimeenda kwenye mkutano wa hadhara na kulikuwa kuna masuala yanayohusiana na masuala yanayohusiana na mambo ya maji Chibya. Tuko katikati ya mkutano namuona Injinia wangu anakuja na pikipiki, bodaboda. maana gari lake imeharibika kwenye milima huko chini, ameshindwa kufika kwenye mkutano kwa wakati, kwa hiyo nikuombe umsaidie.

Mheshimiwa Spika, bado tuna mahitaji makubwa sana ya visima, unafahamu jiografia ya Jimbo la Ndanda kuna eneo la upande wa Magharibi wa jimbo kunashida sana ya maji. Pamoja na mafanikio mazuri hivyo visima alivyovitaja vipo maeneo hayo lakini bado tuna mahitaji ya visima kwenye Vijiji vya Migombani, Pangani, Pachani, Miwale Namatutwe, Natepo, Mihima, Makulani ya Leo pamoja na Chimbo. Niombe sana kwenye Bajeti hii ijayo, tuone watu hawa wanakwenda kupata maji, na kwa kutekeleza miradi hiyo kwa kuchimba visima virefu kwenye maeneo haya, tafsiri yake itakuwa tumemaliza kabisa tatizo la maji kwenye ukanda wa Magharibi wa Jimbo la Ndanda.

Mheshimiwa Spika, na Mheshimiwa Waziri ni msikivu sana. Mara nyingi sisi kama Wabunge wa Mtwara tukwenda kwake tukiwa tuna malalamiko, lakini nadhani safri hii mpaka tunakuja hapa ndani hatuna tena malalamiko yale na wala hatujakaa kikao maalumu na yeye ili aweze kutusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunachoomba sasa miradi hii ikatekelezwe kwa wakati. Kama unavyofahamu, mwakani kuna uchaguzi mkuu, maeneo haya yamepata shida kwa kipindi kurefu sana, tangu wakati wa uhuru. Newala hawajawahi kuwa na maji ya kutosha, Nanyamba hawajawahi kuwa na maji ya kutosha na Tandahimba hawajawahi kuwa na maji ya kutosha. Ndiyo maana maeneo haya kulikuwa kuna *dominance* kidogo ya watu wa *opposition.* Tunakwenda kwenye uchaguzi wa ndani, kwa maana ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa, lakini pia tunakwenda kwenye uchaguzi mkuu. Tunaomba miradi hii ikamilike kwa wakati ili wananchi wapate maji wasije wakatulaumu, tusije tukapoteza maeneo yetu kwa sababu ya kiu kuu inayotamalaki katika maeneo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nilisema tangu mwanzo, nimesimama hapa, na Waheshimiwa Wabunge wengi wameongea kwa kipindi kirefu wakimpongeza Mheshimiwa Waziri. Nimsisitize tu, kwamba akamilishe miradi hii ili tukae hapa ndani kwa amani kiabisa. Ninaamini mpaka tutakaporudi kwenye bajeti ijayo Mungu akimjalia kuwa hai na sisi kuwa hai basi mambo yatakuwa mazuri. Miradi itakuwa imetekelezwa kwenye Jimbo letu na Ilani ya chama chetu chama tukufu, Chama cha Mapinduzi tutasimama kifua mbele tukikitetea kwa sababu tayari tutakuwa tumepunguza baadhi ya kero kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo na mimi niungane na wabunge wote waliopita kuunga mkono bajeti hii kwa asilimia 100. Ahsante sana kwa kunisikiliza.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Abeid Ramadhani Ighondo, atafuatiwa na Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kuchauka ajiandae.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa fursa hii muhimu sana kwa ajili ya

kutoa mchango wangu katika sekta hii muhimu sana ambayo ndiyo chanzo cha uhai wa mwanadamu.

Mheshimiwa Spika, na mimi naomba nianze kwa kutoa pongezi nyingi sana kwa Mheshimiwa Waziri kwa utendaji wake mzuri, pamoja na Naibu wake na watendaji wake Wizarani, mikoani na mpaka wilayani.

Mheshimiwa Spika, sisi kule mkoani Singida katika maeneo ambayo tunajivunia kwamba kweli yana watendaji makini ambao kusema kweli wanatupa ushirikiano wa kutosha ni Meneja wa *RUWASA* wa Mkoa pamoja na kwangu wilayani. Kwa kweli nadhani ni labda wametengeneza hivyo wamekuwa *trained* kwa sababu MheshimiwaWaziri yuko hivyo basi hata kule chini pia tunapata hivi vionjo. Ninamuomba Mheshimiwa Waziri pamoja na watendaji hawa wasibadilike, waimarike, waendelee kuwa *humble*, waendelee kuwa imara katika utendaji na sisi tuko tayari kushirikiana nao.

Mheshimiwa Spika, mimi naomba kwanza nitoe shukrani nyingi sana pia kwa Mheshimiwa Rais, kwa ile mitambo aliyotuletea katika mikoa yetu ya kuchimba maji. Katika maeneo ambayo tunaona jambo hili ni la muhimu na kweli limetufaa ni Mkoa wa Singida hasa Jimbo la Singida Kaskazini.

Mheshimiwa Spika, katika kumbukumbu zangu hotuba yangu ya kwanza kwenye Wizara hii nilisema hapa wazi kabisa hapa kwamba, sisi Singida tunakunywa maji na fisi kwa sababu ya shida kubwa ya maji tuliyokuwa tunapata. Wananchi walikuwa wanakesha, usiku wa wa mane akina mama walikuwa hawalali, ndoa zilikuwa zinayumba kwa sababu mama ule muda anaotakiwa kuhudumia ndoa usiku yeye anaenda kusubiri maji kwenye mito. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini leo hii, kwa kupitia ule mtambo wa mama ule alilotuletea mkoani Singida, na kwa wilayani

kwangu kwa Jimbo la Singida Kaskazini umeshatuchimbia visima vinavyopata vitano mpaka hivi sasa. Nimechimba maji katika Kijiji cha Nduhila ambapo huo mradi utakwenda kufanyiwa usambazaji wa zaidi ya Kijiji cha Nduhila. Kupitia mtambo huu tumepata katika Vijiji vya Makuro, Mkenge, Matumbo na bado kazi inaendelea kwenye maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, kwa mazingira kama haya siwezi kuacha kumshukuru na kumpongeza Rais wetu kwa kazi hii kubwa, kwa sababu sisi katika Imani tunasema ukichimba kisima unakuwa umetoa sadaka inayoendelea hata kama ukifa. Kwa hiyo hapa Mheshimiwa Rais ametenda wema na ametoa sadaka ambayo itaishi milele, haitamfuata hata kesho atakapokuwa hatupo hapa duniani.

Mheshimiwa Spika niishukuru sana pia kwa miradi 15 ya maji ambayo tutapata katika Jimbo langu la Singida Kaskazini, ambapo kupitia gari hili alilotuletea Rais wetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan ninaamini tutapata visima katika Vijiji vya Ntondo, Nkwaye, Sekouture, Kinyamwenda, Msikii, Mwalala, Nongwa Mpoku, Igauli, Mwakiti, Itamka, Mkende kama nilivyoisema, Makuro, Nyisinko, Isimihi na Kijiji cha Mahandi.

Mheshimiwa Spika, haya ni maeneo ambayo kwa kweli wananchi walikuwa wana kiu ya maji ya muda mrefu lakini sasa watapata maji na hivyo watakata ile kiu. Jambo kubwa ninaloliomba hap ani kwamba, hii miradi itekelezeke kwa wakati ili wananchi nao waionje hii keki ndogo ya Taifa lao, waonje ule utamu wa maji ambao wamekuwa wakiukosa kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, vilevile niombe kuwasilisha changamoto chache zilizopo kwenye Jimbo langu la Singida Kaskazini ili Waziri atusaidie wananchi wetu nao waendelee kufurahia. Jambo la kwanza kuhusu usambazaji wa maji

katika miji midogo; nikianza na mji wa Ilongero ambayo ni Makao Makuu ya Halmashauri. Huu mji hivi sasa ni *populated,* umeshakuwa na idadi kubwa ya watu na bado watu wanahamia. Una huduma muhimu za kijamii, una Hospitali ya Wilaya ambayo inahitaji maji muda wote.

Mheshimiwa Spika, tunacho kisima pale, lakini sio cha kudumu sana, tunahitaji maji kwenye miji midogo kama vile kuna masoko, kuna huduma nyingine. Katika huu mji kuna mradi pale unaitwa Uyanjo lakini umezidiwa. Naomba upanuzi kwenye huu mradi, ili uweze kuwafikia wananchi wengi ambao wanahamia kwenye ule mji, wanaojenga, sasa hivi kuna ujenzi wa hali ya juu unaendelea, kwa hiyo, niombe maji ya kutosha na ya kudumu, hivyo, upanuzi ufanyike, ili wananchi wengi wapate maji.

Mheshimiwa Spika, Mji Mdogo wa Mtinko. Ule mji una mradi wa maji, lakini mji ule maji yanayotoka pale ni ya chumvi. Kwa hiyo, niombe tupate teknolojia ya ku-*purify* yale maji ili yaweze kuwa matamu, kama haiwezekani basi tutoe maji kwenye miradi ya jirani, ili maji yale yawe matamu. Tunaumia, sasa hivi unaona meno yangu pamoja na kwamba, ni mazuri, lakini yanakuwa ya njano, tunakunywa maji ya chumvi, tunaharibiwa meno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama walivyosema wazungumzaji wa kutoka Mkoa wa Arusha, kule watu wanaharibika viungo wanakuwa walemavu kwa sababu ya maji. Sasa shida yetu sisi Singida ni maji ya chumvi, kwa hiyo, niombe sana kuwe na teknolojia ya ku-*purify* maji, ili yaondoe kero hii, lakini hili niunganishe hapa katika Kitongoji cha Gairu kilichopo Kijiji cha Sagara; pale maji yapo, lakini ni ya chumvi mno, yaani ukinywa ni zaidi ya chumvi hiyo unayoifahamu.

Mheshimiwa Spika, niombe sana badala ya kuchimba kisima katika lile eneo, tutoe maji kwenye Kijiji cha Sagara, kipo chanzo cha kudumu, kizuri, kina maji ya kutosha. Tutoe

maji kule juu tuyashushe, ni umbali wa kama kilometa mbili au *almost two kilometers,* nadhani haziwezi kuzidi hapo. Ni rahisi kusambaza maji kutoka kwenye chanzo cha Sagara kuliko kuchimba kisima kipya kwa sababu, tutakapochimba itakuwa ni chumvi tena. Nimeona kwenye bajeti kwamba, tunacho kisima pale, lakini nashauri badala ya kuchimba kisima tupeleke maji kutoka chanzo cha Kijiji cha Sagara ambacho maji yale ni matamu.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nazungumzia miji midogo, ukiwemo Mji wa Ngamu. Mji wa Ngamu una maji, lakini naomba usambazaji ufanyike ili wananchi wengi wapate huduma ile.

Mheshimiwa Spika, kuna eneo lingine na maeneo ambayo tumekuwa tukichimba maji, lakini hayatoki. Mfano Kijiji cha Mangida, alikisema pia Mheshimiwa Aysharose, Kijiji hiki tumechimba maji zaidi ya mara tatu, lakini maji hayatoki, lakini kuna vijiji jirani ambavyo vina maji na ni maji ya kutosha. Mathalani sasa hivi wanapata maji kutoka Mradi wa Kijiji jirani cha Sefunga.

Mheshimiwa Spika, niombe tufanye *extension* kwenye huu mradi, lakini pia hata Kijiji chenyewe cha Mangida kina maji, lakini yako mbali kidogo kama kilometa mbili. Tuyatoe maji pale, kuna mradi ambao ni wa muda mrefu umechakaa, ni wa tangu Nyerere wenyewe wanasema, kuna yale matanki yale wanasema ya Mjerumani, liko tanki kubwa sana pale, tuyavute maji kutika ule mradi, mengine tuyatoe pale Sefunga, wale wananchi waache kuteseka.

Mheshimiwa Spika, hakika wananchi wa Mangida wanateseka mno kwa shida ya maji. Niombe sana hii iwe ni mara yangu ya mwisho kuitaja Mangida kwa suala la maji, niombe sana Mheshimiwa Waziri alichukue hili kama ni *special case* atuletee maji pale kwenye kile Kijiji. Nimeona pia

kuna mradi wa kisima pale, si sawa kuchimba pale maji kwa sababu, tumekuwa tukichimba hayatoki.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho ni Kijiji cha Mwokulu. Mheshimiwa Waziri aliwahi kufika pale wakati ule walivyokuja, akaahidi pale kwamba, atatusaidia kisima pale, niombe sana atuletee kisima pale, ili wale wananchi waweze kunufaika.

Mheshimiwa Spika, la mwisho kabisa ni gari. Halmashauri yangu ya …

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Kengele ilishagonga Mheshimiwa.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naunga mkono hoja, *RUWASA* Wilaya yangu hawana gari naomba wapatiwe gari, usafiri, wanateseka mno wamekuwa kama digidigi. Naomba kuwasilisha, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, atafuatiwa na Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kuchauka na Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya ajiandae.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuwa miongoni mwa wachangiaji kwenye Wizara hii. Niishukuru sana Serikali kupitia Mheshimiwa Rais kwa kutoa fedha za miradi ya maendeleo ya maji. Nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri na wasaidizi wake kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuwatendea kazi Watanzania.

Mheshimiwa Spika, nianze na Mradi wa Maji wa Ziwa Tanganyika. Wananchi wa Mikoa ya Kigoma, Katavi, Rukwa, kilio chao kikubwa ni Mradi wa Maji kuyatoa Ziwa Tanganyika, ili yaje tatatue kero ya maji kwenye maeneo yao.

Mheshimiwa Waziri amekuja Mpanda na kwa uungwana alionao aliwashirikisha Wabunge na alibadilisha mfumo wa ziara yake ambayo alikuwa amepangiwa na watendaji. Tukaenda naye kwenye chanzo cha maji Ziwa Tanganyika na yeye aliona umuhimu kabisa. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri mradi ule ndiyo utakaowasaidia wananchi wa mikoa hiyo, tunaomba akautekeleze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mji wa Mpanda umekua, una mahitaji makubwa sana ya maji na tatizo la maji kwa Mkoa wa Katavi litatatuliwa kwa Mradi wa Maji wa kuyatoa Ziwa Tanganyika. Niombe sana hili alishughulikie Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mradi mwingine ambao napenda kuuzungumzia ni Mradi wa Mishamo. Mheshimiwa Waziri amenipa miradi mingi ya maendeleo kwenye Wilaya ya Tanganyika, tunayo miradi yenye zaidi ya shilingi bilioni nne ambayo ameitoa na inatusaidia japo ni miradi midogo midogo, lakini ikikamilika tutakuwa na asilimia karibu 80 ya upatikanaji wa maji safi na salama, lakini shida ambayo ipo tuna wakandarasi wabovu wanaotuletea.

Mheshimiwa Spika, tuna Mkandarasi wa Mradi wa Mishamo, *HAMWA;* mradi huu una thamani ya shilingi milioni 886, toka alipokuja akasaini huo mradi na akapewa fedha za awali shilingi milioni 100 hajafanya uendelezaji wa aina yoyote. Nimwombe Mheshimiwa Waziri wamsimamie huyu mkandarasi ili aweze kukamilisha huu mradi ambao utahudumia Vijiji vya Mishamo, eneo la Ifumbula, Kapemba na Kijiji cha Isenga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mradi mwingine ambao Mheshimiwa Waziri tunaomba akasimamie ni Madi wa Kata ya Katuma. Mradi huu ni mradi wa muda mrefu na Naibu Waziri aliambatana na Makamu wa Rais pale Katuma na Makamu wa Rais alitoa maelekezo ya kuhakikisha Mkandarasi

*HERMATEC* anakamilisha ule mradi kwa muda uliokuwa umepangwa. Mpaka sasa tunavyoongea, bado huo mradi haujakamilika na inashangaza Makamu wa Rais anatoa amri, lakini mtekelezaji mpaka muda huu hajafanya hivyo. Sasa sijui atamsikiliza nani? Kama Makamu wa Rais anatoa maagizo na hayatekelezwi?

Mheshimiwa Spika, nimwombe Mheshimiwa Waziri, najua kazi anayoifanya na jitihada anazofanya ni kubwa. Sisi Wabunge asilimia kubwa tunamwamini anachapa kazi nzuri, wakamsimamie ili akamilishe huo mradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni tatizo la vitendeakazi. Halmashauri yangu ya Wilaya ya Tanganyika Mheshimiwa Waziri anaijua, ametembea, tumeenda kule ukanda wa ziwa na ametembea hadi kwenye eneo tunalopakana na Mkoa wa Kigoma. Hakuna magari ambayo yanaweza yakawasaidia kufanya shughuli za maendeleo na wakati huu tuna miradi mingi ambayo inasimamiwa na hao watendaji wa *MURUWASA*. Nimwombe Mheshimiwa Waziri kwenye bajeti hii tunahitaji atoe msukumo ili tupate gari ambalo litasaidia utekelezaji wa miradi ambayo inaenda kwenye maeneo ya kwetu. Mheshimiwa Waziri, akiyafanya haya yatatusaidia sana katika utekelezaji wa miradi ile ambayo anaisukuma ili iweze kuwafanyia kazi wananchi.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo napenda nitoe ushauri, ni kuunganishwa kwa Jumuiya za Watumiaji Maji. Ni wazo zuri ambalo wanakuja kuunganisha mfumo wa kuunganisha jumuiya zile za watumiaji maji, lakini kuna kasoro ambazo zinajitokeza. Unaunganisha eneo ambalo wengine wanataka kupewa huduma na wengine ndio wanaotoa gharama za maji. Sasa nimwombe Mheshimiwa Waziri, tusije tukawalazimisha mahali ambapo mifuko inaweza ikajitegemea, tuwaache wafanye hivyo kwa ajili ya ustawi wa miradi endelevu. Kuna maeneo mengine mifuko hiyo imekufa na huduma inakuwa ya shida kwa sababu tunawalazimisha

kuwaunganisha ili waweze kubebana wakati wapi wengine uwezo wa kubebana haupo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, niendelee kumshukuru Mheshimiwa Waziri na watendaji. Naamini yale ambayo ni ya msingi kwetu sisi Mkoa wa Katavi tunahitaji Mradi wa Maji wa Ziwa Tanganyika ambao naamini atatusaidia katika utekelezaji. Mradi ule ukikamilika kuna nafasi ya kuwa zaidi ya asilimia 100 tutakuwa na upatikanaji wa maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Zuberi Mohammed Kuchauka, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya na Mheshimiwa Livingstone Joseph Lusinde ajiandae.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, nami nikushukuru kwa jioni hii kunipa nafasi nichangie hoja iliyo mbele yetu. Nianze kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa namna anavyokwenda na kauli yake ya kumtua ndoo mama kichwani. Pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, lakini Mheshimiwa Waziri na Naibu wake wana sifa ya ziada, wanapokea simu za Wabunge na wanafikika, hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimesimama hapa niombe, Mheshimiwa Waziri, tuna Mradi wa Maji kwa ajili ya Mji wa Liwale. Sisi Mji wa Liwale hatuna mitaa, tuna vijiji; tuna Kijiji cha Kuchocholokana, Kulia, Kongowele, Nganyaga, Msufini, Kilipwike, Kitamamui, Tepetepe, Msufini, Mbonde, Kinguruila na Laluleo, zaidi ya vijiji 12 havina maji Liwale Mjini. Chanzo pekee tunachokitumia ni cha Mto Liwale. Mto ule masika tu

ndio unatumika, kiangazi mto ule hautiririshi maji unakauka. Tunapata shida sana Mji wa Liwale.

Mheshimiwa Spika, tunamshukuru Waziri na tunamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kutupa fedha na tayari tumeshachimba visima vitatu pale Turuki na vina maji ya kutosha. Kinachosubiriwa ni kutupatia fedha na mradi ule nafikiri gharama yake kama sio bilioni moja ni kama bilioni mbili, lakini nimeongea na Mhandisi anasema akipata hata milioni 500 ule mradi unakwenda kuanza. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, hili ndio jambo ambalo limenisimamisha kwenye Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, nimpe taarifa Mheshimiwa Waziri, tunapokwenda kufikiria kuyatoa maji Mto Rufiji kuyaleta Dar-es-Salaam, afikirie kuyatoa maji hayo hayo kuyapeleka mikoa ya Lindi na Mtwara. Isije ikatokea huko nyuma watu wa Mtwara na Lindi wakaanza kulalamika kama leo tunavyoilalamikia Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwamba, Mkoa wa Lindi na Mtwara ulisahaulika. Basi, Wizara hii isiwemo kwenye *list* ya Mkoa wa Lindi na Mtwara kusahauliwa kwenye miradi hii ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri. Wilaya ya Liwale yenye vijiji 76, leo unasimama hapa havifiki vijiji 20 ambavyo havina maji. Asilimia zaidi ya 70 kama sio 80 vina miradi ya maji. Nimpongeze sana na hii nampongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutimiza kauli yake hii. Tunavyo vijiji vinane tayari wakandarasi wako *site* na tuna vijiji zaidi ya vinne tayari miradi imeshakamilika. Kwenye bajeti hii nimeona vijiji zaidi ya vinne vinakwenda kupata miradi mipya ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ombi langu, miradi hii iende ikakamilike kwa wakati. Kuna mradi wa Makata, mradi huu umesuasua kwa muda mrefu sana. Kuna Mradi wa Kiangara

na Mradi wa Nangano, miradi hii ni ya muda mrefu inakwenda kwa kusuasua sana. Nimwombe sana Waziri, miradi hii iende kukamilika ili azma ya Mama ya kumtua mama ndoo kichwani iweze kukamilika.

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ambacho nataka niseme kwamba, katika Wizara hii sio tu Mheshimiwa Waziri mwenyewe na Naibu wake na Katibu Mkuu wake wanafanya vizuri, lakini hata safu aliyonayo kuanzia ngazi ya Taifa mpaka Halmashauri. Ndiyo maana kila Mbunge akisimama hapa anasema Mhandisi aliyenaye kule kwenye Halmashauri yake asihamishwe anafanya vizuri na wanafanya vizuri. Kama kuna *rehabilitation* imefanywa kwenye Wizara hii, Wizara ya Maji wanafanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niliomba dakika tano nisema haya machache niliyosema, hivyo, naunga mkono hoja, lakini nahitaji maji kwenye Mji wa Liwale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, atafuatiwa na Mheshimiwa Livingstone Joseph Lusinde na Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga ajiandae.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Spika, kipekee nikushukuru kwa kunipa hii nafasi ili nichangie kwenye Wizara ya Maji. Pia nichukue nafasi hii kipekee vilevile nimshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi nyingi ambazo anazifanya. Katika Jimbo langu la Manyoni Mashariki tulikuwa na miradi mingi ya maji kichefuchefu, lakini nikwambie sasa hivi miradi mingi ya maji katika Jimbo la Manyoni Mashariki inaenda vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Aweso, ndugu yangu, lakini na Naibu Waziri, Mheshimiwa *Engineer* Mary. Wengi wamesema hapa hawa vijana wetu, ndugu zetu wanafanya kazi nzuri sana. Kwangu Mheshimiwa Aweso nadhani anaenda kuweka historia kubwa sana ya kutatua kero ya maji Manyoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna Mradi wa Kintinku - Lusilile na siku hizi unaniita mzee wa Kintinku - Lusilile. Huu mradi una miaka 15 ulishindikana kukamilika wa bilioni 12, lakini hapa ninapovyoongea mwezi uliopita mkandarasi alipewa bilioni mbili kwa ajili ya kwenda kukamilisha Mradi wa Kintinku - Lusilile. Nimwombe Mheshimiwa Waziri, huu mradi wa bilioni 12 ni mradi mkubwa sana, ukikamilika amwombe Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia aje auzindue huu mradi kwa sababu atakuwa ameweka historia kubwa, lakini ameweka heshima kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimshukuru Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, *Engineer* wetu, lakini nimshukuru sana Mkurugenzi wa *RUWASA*. Kwa kweli, huyu Mkurugenzi ni msikivu sana, anatusaidia sana na Mheshimiwa Waziri kwa kweli, ana Mkurugenzi ambaye anamfanyia kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina mambo mawili ambayo ningependa kuchangia leo. La kwanza, nimeshaeleza kuhusu hii miradi yangu ya maji, tuna huu Mradi wa Kintinku - Lusilile; huu mradi ulikaa miaka 15 ulikuwa umeshindikana kukamilika, mradi wa vijiji 11, lakini nimesema tumepewa bilioni mbili na mkandarasi yupo *site* ameshaanza kufanya ile kazi ya kumalizia. Amesaini mkataba wa kumaliza huu mradi ifikapo Oktoba mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikuombe sasa tuisimamie Serikali, lakini nimwombe Waziri amsimamie mkandarasi. Nimshukuru yule mkandarasi aliyenipa ni msikivu sana, anafanya kazi nzuri

sana. Kazi ilikuwa ngumu, lakini ameweza kuusukuma ule mradi.

Mheshimiwa Spika, tuna Mradi pia wa Miji 28 ambao na wenyewe tulipata pale Mamlaka ya Mji Mdogo wa Manyoni. Wakandarasi walishakuja, lakini nimwombe Mheshimiwa Waziri awasukume wale wakandarasi kwa kuwa wananchi wamesubiri sana huu mradi kwa muda mrefu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna vijiji ambavyo tumechimba visima vya maji kwa muda mrefu tumekosa. Kuna Kijiji cha Mpapa, Kijiji cha Igwamadete, Kijiji cha Mazwichii, Kijiji cha Kitalalo, Kijiji cha Magasai, kwa kweli, hivi vijiji tumefanya *survey* ya maji muda mrefu na kwa bahati mbaya hatujapata maji. Nimwombe Waziri sasa watafute namna ya kuhakikisha kwamba, hawa wananchi ambao wamesubiri muda mrefu kupata maji, tuje na ubunifu wa kuweza kuwasaidia waweze kupata maji.

Mheshimiwa Spika, suala la pili na la mwisho ni kuhusu Mfuko wetu wa Maji wa Taifa *(National Water Fund)*. Wabunge wengi wanaposimama hapa kuchangia wanatamani kuona tunakwenda kutatua tatizo la maji kwenye Majimbo yao, ili tuweze kutatua tatizo la maji kwenye Majimbo yao tunahitaji kuwa na *financing system* ambayo iko *very stable and sustainable. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunahitaji kumsaidia Mheshimiwa Waziri. Sheria ya kuanzisha Mfuko wa Maji ya 2019 inasema kwamba tutapata kutoka kwenye *fuel levy* angalau shilingi 50 kwa kila lita. Mimi naona tuna tatizo. Mfuko wa Maji wa Taifa ndiyo Mfuko ambao unatakiwa uwe *very sustainable* kwa ajili ya kusimamia miradi ya maji Tanzania. Ukiacha kwamba tunapata fedha kutoka kwa wafadhili, lakini hiki ni chanzo ambacho sisi kama Watanzania tunahitaji kukisimamia. Nadhani kuna jambo la kufanya kwenye huu Mfuko wa Maji.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni nini; kwanza tuna Jumuiya za Watumia Maji. Kwa mfano, kwa Manyoni nina Jumuiya moja ya Watumia Maji inaitwa Mkombozi, sasa hivi wana milioni 140 kwenye akaunti yao. Nina Jumuiya moja ya Watumia Maji kutoka Kijiji cha London, wana milioni 125 kwenye akaunti yao, nina jumuiya moja kutoka Sorya wana milioni 60 kwenye akaunti yao. *Idea* yangu ni nini kama tunataka kusaidia Mfuko wa Maji ku-*expand* ile *financing mechanism* yao tunahitaji vilevile ku-*diversify,* kutafuta vyanzo mbalimbali vya maji. Nashauri nini, zile fedha ambazo tunazikusanya kwa kupitia Jumuiya za Watumia Maji zinakuwa *idle,* kwa nini tusitengeneze mfumo zile jumuiya za maji vilevile zichangie kwenye Mfuko wa Taifa wa Maji? Ninashauri kwa kupitia hili tunaweza tukakusanya fedha nyingi ambazo hizohizo zitasaidia kwa ajili ya kuchimba visima kulekule na kwa ajili ya *expand* hata utoaji wa huduma ya maji vilevile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kwenye Sheria ya Kuanzisha Mfuko wa Maji, imetoa *provision* kwamba zaidi ya asilimia 88 ya fedha itakayokusanywa iende kwenye miradi ya maji, *of which* mimi naona ni kitu kizuri, kwamba tunaweza tukafanya mambo makubwa sana kwenye suala la kupeleka miradi ya maji. Kwa kupitia hili nina uhakika sasa kilio hiki cha Wabunge wengi kwamba miradi haikamiliki na kadhalika, nadhani tunaweza tukatatua. Mbali ya kutegemea fedha za wahisani tu, lakini tutakuwa na uhakika wa kutegemea fedha ambazo zinatokana na miradi yetu ileile ya kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, mimi nirudie tena kumshukuru Waziri. Kwa kweli kwa sisi watu wa Kintinku – Lusilile kwenye ule mradi wako mkubwa wa bilioni 12 umetutendea haki sana. Ninakuombea wewe na Naibu Waziri wako muendelee kutusaidia, ule mradi wa maji ikifika Oktoba mwaka huu tukaweke historia na Mheshimiwa Rais aje auzindue ule mradi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Livingstone Joseph Lusinde, atafuatiwa na Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete ajiandae.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara ya Maji. Ninaomba nikupongeze sana kwa namna ambavyo, unajua watu wengi wanafikiri tunakupongeza kwa kuendesha Bunge, kwa namna unavyotuongoza sisi Wabunge ndani ya Bunge na nje ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wengi wameshazungumza, tumetoa pongezi na ahsante nyingi kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa namna ambavyo anamwaga pesa kwenye miradi mbalimbali, hususan kwenye miradi ya maji.

Mheshimiwa Spika, ukitazama hata namna ambavyo Mheshimiwa Rais anaipanga kiuongozi Wizara ya Maji unaona nia ya Rais ni kuongeza *speed* ya utendaji katika Wizara hiyo. Tumeona juzi hapa Mheshimiwa Rais amemteua *Eng.* Luhemeja kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji. Tunaona nia nzuri ya Rais ya kuifanya Wizara iwe imara katika utendaji. Waziri amekaa sawasawa, Naibu yuko sawa, sasa mnaongezewa nguvu, Katibu Mkuu amekuja ili mtoke pale alipoishia *Eng.* Sanga kwenda mbele kwa spidi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wabunge wamepiga kelele sana kuhusu maji kwa sababu maji hayana mbadala. Hata wale ambao hawakupata nafasi ya kuzungumza bado ungewasimamisha wote wangetaka maji kwenye Majimbo yao. Kwa hiyo, tunamuomba sana Mheshimiwa Waziri kuigawanya rasilimali maji.

Mheshimiwa Spika, unajua tumemaliza sensa juzi. Sensa itupeleke kuona wingi wa watu na namna ya kujenga matenki makubwa, tuondoke tena kwenye yale matenki madogo ya lita 50,000, lita 60,000. Tuanze sasa kujenga lita 200,000 na kuendelea ili yaweze kusaidia kusukuma maji kwa wingi katika vijiji.

Mheshimiwa Spika, leo kuna miji imekua. Ukiangalia sasa hivi kwa mujibu wa sensa iliyopita Kijiji kama cha Mkwayungu katika Jimbo langu, kina watu 19,000, Mvumi *Mission* kuna watu 19,000, ukienda Mlowa kuna watu 18,000. Hapa huwezi kutengeneza tena tenki la lita 50,000 likatosha.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo rai yangu kwa Wizara, ikiwezekana tubadili sasa ujenzi wa matenki tuende tujenge matenki makubwa kwenye vijiji vyote ambayo mengine yatabaki kama *reserve*. Kama kijiji kina watu wachache, watakapoongezeka tenki tusijenge tena kwa sababu lipo la kutosheleza kusukuma maji kwa ajili ya kijiji hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa Dodoma tunapongeza sana uongozi wa maji wa Mkoa wa Dodoma, wanajitahidi sana. Nanyi Wabunge ni mashahidi na wengi muda mrefu tuko hapa. Lakini tunaona bado maji hayatutoshi. Kulikuwa kuna mpango wa kuyachukua maji kutoka Mtera kuyaleta hapa Dodoma Mjini. Nataka kupata majibu ya Mheshimiwa Waziri mmefikia wapi? Kwa sababu maji yale yakichukuliwa kwenye Bwawa la Mtera kuyaleta hapa Dodoma yatanufaisha vijiji vyangu vingi kule njiani yatakakopita. Kwanza tutambue kwamba kuna vijiji kuanzia kwenye Jimbo la Kibakwe kwa Mheshimiwa Simbachawene, ukanda ule wote, vijiji vile vina maji ya chumvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ukitupitishia maji kutoka Bwawa la Mtera maana yake Vijiji kuanzia Fufu, Isima kwa Mheshimiwa Simbachawene, Chipogoro kwa Mheshimiwa Simbachawene, ukija kwangu Manzase, ukija Mlodaa,

Mlowa, Ng'wenda, wote watapata maji safi na salama. Kwa hiyo, naomba majibu utakaposimama Mheshimiwa Waziri utusaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna vijiji tumefanya utafiti na kuchimba maji hayapatikani. Kijiji kama Chinoje tumechimba zaidi ya mara tatu maji yako mbali. Tumechimba maji kwenye Kijiji cha Ng'wenda, zaidi ya mara tano, maji hayapatikani. Ni nia yangu kuiomba Wizara tutoe maji kwenye vijiji jirani kupeleka huduma ya maji. Kumbe wale wananchi wahame wote, waende wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka kuiomba Wizara ni ukamilishaji wa miradi mikubwa ambayo imeanza kujengwa mingi imesimama kwa sababu ya kukosa pesa. Pale *Mvumi Mission* tunao mradi wa milioni 988. Mkandarasi ameshajenga, ame-*raise certificate* Wizarani ya milioni 522 mpaka sasa hivi hamjampatia, matokeo yake mradi umesimama.

Mheshimiwa Spika, vilevile ukienda Handali kuna tatizo pale. Mkandarasi yule pale tangu mmempa ile kazi ameweka mabomba halafu ameingia mitini. Mtusaidie, hii miradi kadri inavyochelewa inaongeza gharama ya utendaji. Ukienda Mlowa Bwawani pale tulikuwa tunatengeneza tenki, mifuko 200 ya simenti imekauka. Kwa hiy,o tunapata gharama inakuwa kubwa inazidi ile ya mwanzo ambayo mlikuwa mmeikisia kwa ajili ya kujenga mradi.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Chamwino ndiyo Wilaya yenye Ikulu. Nikuombe sana Mheshimiwa Waziri utupatie gari, meneja wetu pale hana gari. Na ile Wilaya ndiyo Wilaya ya kimkakati wewe unajua na Mama anakaa pale. Mimi sitaki kuwasemea kwa Mama, hebu tupatieni gari jipya ili yule Meneja aweze kukimbia kwenye Majimbo yote mawili kwa wakati muafaka na aweze kutupatia maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu bei ya maji. Wakati mwingine wanakurupuka tu watu wanajipangia bei ya maji. Maji siyo biashara, maji ni huduma. Kwa hiyo tumuombe Mheshimiwa Waziri, hebu elekeza mameneja wako hawa bei ya uhakika ya maji ni ipi, kwa sababu maji ni huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukienda huku *unit* ni shilingi 2,000, kwingine *unit* ni shilingi 2,500, kwingine *unit* ni shilingi 3,000, haiwezekani! Tuwe na bei moja maana maji ni ibada, maji ni uhai. Yakiwepo maji ya kutosha, safi na salama, yatapunguza hata bajeti ya baadhi ya Wizara, magonjwa ya maji haya kama *typhoid* yote yatatoweka tukiwa na maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia akina mama ukiwapunguzia muda wanaopotoza wa kutafuta maji, nikuhakikishie kwamba uchumi wa nchi yetu utakua kwa sababu akina mama ni jeshi kubwa, likishiriki kwenye maendeleo na kuacha kupoteza muda kwenye maji, mambo yetu yatakwenda kwa *speed* sana kwenye kuiendeleza nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba sana Mheshimiwa Waziri wataalam wakuletee idadi ya visima vya maji vya zamani ambavyo mitambo yake ni chakavu ili muweze kutu-*boost* kama mlivyofanya kwenye elimu. Umesema kwenye hotuba yako kwamba tunataka tutengeneze utaratibu wa kuvuna maji. Hebu tuanze na Serikali, kwanza hapa Bungeni tunavuna maji kutoka wapi kuja hapa? Bunge hili linavuna maji kutoka wapi?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo miundombinu ianzie Serikalini, majengo yote ya shule yawe na namna ya kuvuna maji. Kwenye Wizara zenu tukija tukute mifumo ya kuvuna maji, halafu wananchi ndiyo wataiga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini mkituambia tu sisi tutengeneze *structures* za kuvuna maji wakati tukienda kwenye Wizara

zenu, kwa Mheshimiwa Jenista pale, hakuna mfumo wa kuvuna maji, ndiyo wanaanza kuweka juzi hapa. Tukienda kwa Mheshimiwa Doto pale, hakuna mfumo wa kuvuna maji, kwa Mheshimiwa Simbachawene hakuna, sasa tunajifunza wapi? Tuanzie kwenu, ninyi muanze kuonesha njia ili sisi tufuate. Majengo yote ya Serikali yatengenezewe mfumo wa kuvuna maji halafu sisi wananchi tutaiga. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, naunga mkono hoja, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete, Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde ajiandae.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Spika, nami nakushukuru kwa kuniona na kunipa nafasi niweze kuungana na Wabunge wenzangu kuchangia katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, Wabunge wote hapa waliapata muda wa kuchangia wamezungumzia kwanza, kila aliyeanza anampongeza Rais. Kwa nini tunampongeza Rais? Tunampongeza Rais kwa sababu ana nia njema ya kuhakikisha anamtua mama ndoo kichwani. Ndiyo maana kwenye Wizara hii ameongeza fedha kutoka shilingi bilioni 708 za mwaka jana, mwaka huu ameongeza shilingi bilioni 756. Hizi tunazungumzia siyo milioni, haya ni ma-'bi' na ma-'bi' na ma-'b'. Ndiyo maana tunampongeza Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, vilevile tunampongeza aliyekabidhiwa hii Wizara, Amekabidhiwa kijana wetu, Waziri huyu anaitendea haki Wizara. Anaisimamia vizuri pamoja na Naibu Waziri wake. Vilevile wako watendaji wake, yupo Katibu Mkuu wa Wizara na Naibu Katibu Mkuu na Watendaji

wote walioko Mikoani na Wilayani akiwemo wa Mkoani kwangu Njombe na Wilayani kwangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Aweso kweli wewe umekabidhiwa dhima hii ya kuhakikisha unamtua mama ndoo kichwani. Ombi langu Waziri, ma 'B' haya uliyokabidhiwa yanayokwenda huko kwenye Majimbo yetu yasimamie vizuri yasiliwe. Kazi hiyo unaiweza kwa sababu umedhamiria, tunakuona una nia njema, tunakupongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika miradi ile ya miji 28 na Mji wa Makambako umo. Katika Mji wa Makambako tumepewa katika miradi wa miji hiyo 28 ma 'B' 42. Sasa utakaposimama hapa Wanamakambako wana hamu kukusikia, miradi hii inaanza lini? Useme. Utakaposema waambie Wanamakambako kwamba sasa, maana mradi huu mkubwa wa Makambako unahudumia Kata Tisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri, ombi langu utakaposema katika Kata tisa, Kata moja ya Mlowa imo katika hizi Kata Tisa. Katika fedha za kujenga tenki kubwa la kuhudumia, tenki moja linatakiwa liwe kule Mlowa ambalo litahudumia katika kiwanda cha dawa kilichojengwa Makambako, litahudumia katika Hospitali ya Halmashauri yetu iliyojengwa katika Kata hii ya Mlowa na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, tuliomba fedha zaidi ya bilioni tatu na milioni mia tatu kwa ajili ya bajeti ya mwaka huu ili waanze kujenga tenki hilo kubwa la zaidi ya lita 300,000 ili wananchi wa Mlowa kule, Mkolango, Igumila, Idofi pamoja na kiwanda hiki cha dawa waweze kupata maji.

Mheshimiwa Spika, vilevile nikubaliane na ushauri wa Kamati ya Maji na Mazingira. Kamati hii imetoa mapendekezo yafuatayo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza imeomba mradi wa Bwawa la Mtera uanze ili uweze kuhudumia Dodoma, tatizo la maji Dodoma ni kubwa, kama alivyosema Mheshimiwa Lusinde pale, utakapokuwa unaleta maji Dodoma utahudumia na vijiji vilivyoko njiani. Vilevile Kamati ilishauri pia Dodoma, kwa sababu bado tatizo ni kubwa, vichimbwe visima vya kutosha ili wananchi wa Jiji la Dodoma na kwa sababu linakua kwa haraka waweze kupata maji. *(Maji)*

Mheshimiwa Spika, vilevile Kamati ilishauri uvunaji wa maji. Kamati imeshauri tuhakikishe kuna uvunaji wa maji. Lakini mwenzangu amezungumzia pale sasa elimu hii tuanzie kwenu, tuanzie kwenye majumba ya Serikali. Kamati imeshauri sana juu ya jambo hili. Tunampongeza Mwenyekiti wetu wa Kamati, Mheshimiwa Kiswaga na Wajumbe ambao wametoa ushauri mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, hili halihusiani na Kamati, linahusiana na watu wa Nishati, Naibu Waziri yuko hapa. Kwangu kumekuwa na tatizo kubwa la umeme wa upepo Makambako. Wananchi hawa zaidi ya miaka 14 wamechukuliwa maeneo yao, hawawezi kuendeleza kufanya jambo lolote. Serikali ilisimamisha kwa sababu walipata wawekezaji ambao watawekeza umeme wa upepo Makambako ni jambo jema, lakini mpaka sasa hakuna majibu.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri, leo nimemuunganisha ameongea na wananchi wangu Makambako. Naomba yale uliyowaambia Naibu Waziri yatekelezwe wapate majibu yale uliyowaambia ili kama imeshindikana basi waweze kuruhusiwa kuendelea na mipango yao.

Mheshimiwa Spika, tunapopongeza wote hawa ni lazima tugeuke tukuangalie Spika unayeongoza Bunge hili, tunakupongeza sana kwa kazi nzuri unayoisimamia Bunge,

unavyoisimamia Serikali ukishirikana na Wabunge wenzako, tuko pamoja na wewe tutahakikisha shughuli za Bunge hili zinakwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, hili namrudia Mheshimiwa Aweso. Unajua Mheshimiwa Aweso - Waziri pamoja na Naibu Waziri na timu nzima ya Wataalam, unapofanya kazi nzuri zipo changamoto, lakini katika chagamoto simamia, songa mbele, nyingine zitakuwa humu, songa mbele unapatia, kazi inakwenda vizuri. Huo ndiyo ukweli kijana. Kimbia hakikisha Majimbo yetu tunamtua Mama ndoo kichwani kama Rais alivyokukabidhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema maneno haya, nakushukuru sana, ahsante sana. Wananchi wa Jimbo la Makambako baadhi ya maeneo maji tunapata tunaendelea vizuri, sitaki nitaje maeneo hayo, maji tulishapata. Ombi langu tu mradi mkubwa huu utakapokuwa unahitimisha uwaambie wananchi wa Makambako mradi huu utaanza lini kwenye Jimbo langu. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete, atafuatiwa na Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde, Mheshimiwa Abdallah Hamis Ulega ajiandae.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kutoa mchango wangu.

Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru Mungu, hatimaye nitoe shukrani na pongezi kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kazi kubwa na nzuri ambayo anaifanya kwa Taifa letu hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amedhamiria kuwatua akina mama au wanawake

ndoo kichwani, dhamira hii inadhihirishwa na bajeti baina ya 2022/2023 na 2023/2024. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bajeti ya mwaka 2023/2024 ni shilingi bilioni 756.205 wakati bajeti iliyopita ni shilingi bilioni 709.326, na ndiyo maana hii inadhihirisha hilo. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, anahitaji dunia iendelee kuwepo. Bila kuwa na maji hakuna viumbe. Kama hakuna viumbe, nani ataishi katika hiyo dunia? Hakuna kitu. Kwa muktadha huo, ndiyo maana ya kutaka Watanzania na ulimwengu kwa ujumla uendelee kuwepo; kuna ile Sheria ambayo tumeipitisha hapa katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mita sitini kutoka vyanzo vya maji, wasilime na wasifanye shughuli zozote za kibinadamu sehemu hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa baada ya kuyasema hayo, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Aweso pamoja na Naibu wake, Katibu Mkuu na watendaji wote katika Wizara hii. Hapa naungana na Wabunge wote, kila Mbunge aliyesimama, hakuna ambaye hajampongeza Mheshimiwa Rais, hakuna ambaye hajampongeza Mheshimiwa Waziri. Hawa ni viongozi wazuri ambao waliishika; aliyeishika *Quran*, aliyeishika Biblia, anatekeleza yale ambayo aliyaapa katika kiapo chake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nikushukuru tena, Jimbo langu la Mchinga, limetengewa pesa takribani ya zaidi ya shilingi bilioni mbili kwenye maeneo yafuatayo: Mputwa, shilingi milioni 492; Mlangala A na B, shilingi milioni 340; Milola, shilingi milioni 496; Matimba, shilingi miloni 250; Nangaru, shilingi 58,322,000,000; Mkwajuni, halikadharika kama nilivyotaja pale Nangaru; na Mipingo shilingi milioni 400. Watu wa Mchinga wanakusubiri, wanasema, huyu kijana; maana wanakuita kijana, mtoto; tunamhitaji aje kwetu, hatuna cha kumpa. Hivi hapa tafuta muda ili twende, wale watakushukuru. Hata mimi Mbunge wao hawajaniambia

wanachotaka kukufanyia pamoja na Naibu Waziri wake. Tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na miradi hii mipya ambayo umetupatia, kuna ule mradi ambao unatokea kule Myapa unakuja mpaka Mitaro hatimaye unaenda kwenye Jimbo la Mchinga. Kazi iliyofanyika ni kubwa na kazi iliyofanyika ni nzuri, na Mkandarasi anafanya kazi nzuri. Mimi hapo sitasema, mnyonge mnyongeni, haki yake mpeni. Ukishamnyonga, haki utampa saa ngapi? Hutaweza kumpa hiyo haki. Tumwombee aendelee kufanya hizi kazi ambazo wana-Mchinga wamemtuma na Watanzania wamemtuma. Kufanikiwa kwa Mchinga ni kufanikiwa kwa Tanzania yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, tulipewa shilingi bilioni 12. Mpaka sasa tumepokea takribani shilingi bilioni 7.7, bado shilingi bilioni 4.7. Mradi ilibidi uishe mwezi Mei, bado haujaisha. Tunachoshauri, hizi pesa ambazo zimebaki, zipelekwe haraka. Wana-Mchinga wana imani sana na Mheshimiwa Waziri, na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa sababu wakati wanachimba ile mitaro kuweka yale mabomba, hakuna aliyeamini, kwa sababu miaka mingi imepita Mchinga bila kuona ile koki ya kufungulia maji. Sasa hapo wameona kumesimama simama, tunaomba Mheshimiwa Waziri ajitahidi kadri inavyowezekana tumalize hizi shilingi bilioni 4.3. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, huu mradi ulikuwa wa awamu mbili. Awamu ya kwanza ni shilingi bilioni 12.4 na awamu ya pili ni shilingi bilioni 22.9. Wakati tunamaliza huu, tuangalie ile awamu ya pili. Kwa nini tunazungumzia awamu ya mbili? Ndani ya awamu ya pili, mradi huu utanufaisha maeneo mengi kama yafuatayo; kuna Kijiweni, Mnang'ole, Mvuleni A na B, Bimba, Kilolambwani, na Maluu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu mradi huu unapita mjini, kwenye mji kutokea Lindi kuelekea Dar es Salaam, njiani mle kuna vijiji navyo vitanufaika na mradi huu. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri ni msikivu, Serikali yetu ni sikivu, naomba hili liwekwe kwenye ajenda kwa maana ya kwamba liwekwe kwenye utaratibu, wakati tunamalizia *phase* ya kwanza, tutaingia *phase* ya pili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo nilikuwa nataka niseme hayo, nimshukuru Mheshimiwa Waziri, nimpongeze, na hizi pongezi anazopewa ni za haki na anastahili kupewa pongezi hizo. Msione vinaelea, mjue vimefanya nini? Vimeundwa, na waumbaji ni nani? Sisi Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Bila kuyapitisha haya, hayo mengine hayawezi kufanyika. Bila Mheshimiwa Rais kutafuta hizo pesa, mengine hayawezi kufanyika. Yatafanyikaje? Anayesimamia, Mwenyekiti pale ni nani? Ni Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, anafanya kazi kubwa na nzuri. Tunakutakia kila la kheri na Afya njema, Mwenyezi Mungu akubariki sana, akisaidiwa na Msimamizi anayesimamia Bunge, ambaye sio mwingine bali ni Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuwapongeza Wizara kwa kazi nzuri lakini kubwa kwa ushirikishwaji wa sisi Wabunge kuanzia ngazi ya Wizara mpaka Mameneja wa *RUWASA* Mikoa na Wilaya na pia kwa Wakurugenzi wa Mamlaka za Maji. Tunaona *team work* na kwa mwendo huu sekta hii itaendelea kuimarika, tuendelee ushirikishaji wa sisi Wabunge, lakini pia katika ngazi za Wilaya

kwa maAna ya Halmashauri, Madiwani na Ofisi za ma-*DC* wote wawe wanaelewa katika maeneo yao kuna miradi gani, itatekelezwa kwa namna gani na kwa muda gani. Hii itatusaidia kuwa wamoja. Na kwa kuwa tunatekeleza Ilani ya CCM basi ni muhimu sana viongozi wa chama katika maeneo ambako mradi unatekelezwa kuwa na ufahamu kwa maana ya *ownership,* vivyo hivyo viongozi wa ngazi za chini kwa maana ya Wenyeviti wa Mitaa na Vijiji. Nasema hivi kwa sababu kazi kubwa inafanyika, kwa hiyo, tusipokuwa na muunganiko wa taarifa hakika watu wengi na hasa wapotoshaji watazungumza tofauti.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mradi wa Miji 28 Mafinga; tunashukuru sana kazi imeanza japo wananchi wanatamani sana kuona *physical works* kama uchimbwaji wa mitaro na kadhalika. Tunawaelimisha kuwa mradi huu ni miezi 20 na kwamba ni *design and construction,* tunawafafanulia.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, matarajio ya wananchi ni kwamba mradi huu ni mkombozi wa kero ya maji, lakini kwa upande mwingine, *scope* ya utekelezaji kwa maana ya *distribution* ni kilometa 20 tu. Kwa ukuaji wa Mji wa Mafinga kutokana na viwanda vya mazao ya misitu, nashauri Serikali ianze kufikiria awamu ya pili ya mradi ambayo itajielekeza katika ujenzi wa matanki na usambazaji, nawapongeza timu yangu ya *MAUWASA* wanajituma sana hasa katika kuwasiliana na Wizara kuhusu fursa mbalimbali zinazojitokeza. Mradi huu wa miji 28 ni mkubwa sana, haitaleta picha nzuri ikiwa baada ya kukamilika maeneo mengi ya mji yafikiwe na huduma, sote tunatambua ambavyo *signing ceremony* sio tu ilihudhuriwa na Mheshimiwa Rais, lakini pia wananchi walishuhudia *live,* na hivyo wamejenga matumaini makubwa sana, lakini wanaposikia kuwa kuna maeneo mradi hautafika inawakatisha tamaa, ndio maana nashauri mapema, tuanze kuona kwa namna gani tutapata *phase two* kama mwendelezo wa mradi huu.

Mheshimiwa Spika, nafahamu kuimarisha chanzo ndio jambo kubwa, *distribution* na matanki sio kazi kubwa sana, tukitengewa *around* shilingi bilioni 10 yaani bilioni kumi kuanzia mwaka ujao wa fedha, tutaweza kufikisha maji eneo kubwa la mji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *RUWASA*; nawapongeza kwa maeneo ya vijijini, hata hivyo kilio kikubwa ni kukamilisha Mradi wa Matanana na Itimbo ambao ni wa visima, lakini kilio zaidi ni Kijiji cha Kisada, nilitaraji kuwa kitakuwepo katika mpango wa mwaka wa fedha ujao, lakini sijaona Kisada kwa hiyo naomba iwepo, lakini la pili pamoja na kuwa *RUWASA* ipo kiwilaya. Nashauri miradi kati ya Halmashauri mbili isichaganywe, kwa mfano kuweka vijiji vya *Mafinga TC* katika orodha ya vijiji vya *Mufindi DC* inaleta mkanganyiko, na hili lilishajitokeza mwaka jana, mradi wangu wa Kitelwasi Ugute ukaachwa kwa kile kilichotajwa kama *oversight,* hivyo ushauri wangu tupange mipango kwa kuzingatia kijiji kipo Halmashauri gani.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Spika, kwanza nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa juhudi na hatua mbalimbali anazochukua kuhakikisha wananchi wanapata maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri na watendaji wake wote kwa kuhakikisha wanatekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuishauri Serikali; kwanza Wizara iendelee na jitihada za kudhibiti upotevu wa maji; pili, kulinda na kuhifadhi vyanzo vya maji; na tatu, kuongeza matumizi ya mita za LUKU *(prepaid meter)* kwa matumizi ya majumbani ili kuepusha mtumiaji wa maji kuchelewa kulipa

bili za maji pia kumsaidia mwanachi kulimbikiziwa madeni ya maji.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ahsante.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, kwanza niwapongeze kwa kazi kubwa inayofanywa na Wizara ya Maji chini ya Waziri Aweso, kipekee sana kwa heshima na taadhima wananchi wa Iringa tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa unayofanya ya kuliongoza Taifa letu, na kusimamia maendeleo ya Taifa letu, na hususani katika Manispaa yetu ya Iringa. Tunashukuru kwa kuwa maji ndani ya Jimbo la Iringa imekidhi utekelezaji wa Ilani.

Mheshimiwa Spika, maombi; kwanza, tunaomba maji yafikishwe kwenye maeneo ya vijijini ndani ya Jimbo la Iringa ambayo ni eneo la Ugele, Kata ya Mkimbizi na Mosi Kata ya Kitwiru. Pia ninaomba kisima katika eneo letu la Uwanja wa Samora pale tulipofanyia mkutano ulipotuahidi kutuletea visima, siku ya ziara ya Rais, pamoja na zile shule tulizoomba kuchimbiwa visima.

Mheshimiwa Spika, Mkurugenzi wako *IRUWASA* amesema maji yapo kwenye shule hizo, na wamefungiwa *prepaid,* lakini hawatumii kwa kuwa *bills* hawawezi kulipia.

Pili, ninatoa ushauri kuwa katika *bill* ya maji muongeze hata shilingi 10 au tano kwa *unit* ili fedha hizi zichangie huduma za maji mashuleni, kwenye zahanati na vituo vya afya. Shule hizi zinawekewa miundombinu ya kisasa sana inayohitaji matumizi ya maji. Sasa kutegemea *capitation* pekee yake itakuwa vigumu sana.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mawaziri na viongozi wote wa Wizara ya Maji, kwa uongozi wao na utendaji uliotukuka.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na uongozi wote wa Bunge kwa uongozi wenu mahiri na wenye ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza mhimili wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri wa Maji, kwa hotuba nzuri iliyojaa ubunifu mkubwa na imedhihirisha utayari wa Serikali katika utekelezaji wa ustawi wa jamii na maendelo endelevu, na hii ni mojawapo ya nguzo kuu katika utayari wetu wa ushindani wa kimataifa *(national competitiveness)*. Bajeti hii inaenda sambamba na Dhima ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026 ambayo ni Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miezi kumi ya bajeti ya 2022/2023, Serikali kupitia Wizara ya Maji imetekeleza miradi mingi ya maji. Katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya inatekeleza kwa ufanisi mkubwa miradi ya vijiji vya Simambwe, Usoha Njiapanda, tembela, Iyawaya, Izyira, Ruanda, Ilembo, Inyala, Igoma, Iwalanje, Galijembe, Tembela, Pashungu, Shigamba, Santilya, Inyala Ilembo, Mshewe, Muvwa, Njelenje, Mapogoro, Mjele, Chang'ombe, Ipwizi, Ikukwa, Simboya, Itimba, Utengule, Ihombe, Idugumbi, Iwala, Ilota, Ikhoho na pia mradi mkubwa katika Mji wa Mbalizi. Miradi yote hiyo imetekelezwa kwa ufanisi mkubwa, ingawa kunahitajika uboreshaji wa miundombinu ya mabomba hasa katika mradi wa Mbalizi kuna upotevu

mkubwa wa maji kutokana na uchakavu wa mabomba yaliyokuwepo awali.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo makubwa, katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya bado kuna changamoto kubwa ya maji salama kwa wananchi katika maeneo mengi ya vijijini. Pamoja na kuwepo kwa vyanzo vingi vya mseleleko *(gravity),* asilimia kubwa ya vijiji havina maji salama. Nashukuru kwa kuwepo bajeti ya mradi mkubwa wa Mto Kiwira ambao utakuwa mkombozi wa maeneo mengi ya Mkoa wa Mbeya na hata Mkoa wa Songwe. Napendekeza Serikali iendelee kutekeleza miradi ya maji ikiwa ni pamoja na kuweka mkakati wa kuhakikisha upatikanaji wa maji unakuwa endelevu na mafanikio ya kupunguza gharama za miradi na pia utekezaji uwe wa haki na haraka na kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, napendekeza Serikali iweke msukumo mkubwa wa kuharakisha utekelezaji wa miradi iliyomo kwenye Mradi wa Bonde la Mto Songwe *(Songwe River Basin Development Programme - SRBDP),* wenye ofisi zake Kyela, Tanzania. Mradi huu unaotekelezwa kwa pamoja na Serikali za Tanzania na Malawi, ni muhimu sana kwa sasa kutokana hasa na ujenzi wa mabwawa ambayo pamoja na manufaa mengine, yatasaidia kupunguza mafuriko ya Bonde la Kyela. Mabwawa haya yamelenga kuzalisha umeme, kilimo cha umwagiliaji, shughuli za uvuvi na hata utalii ambao unahitajika sana katika Wilaya ya Mbeya na ukanda wote wa Nyanda za Juu Kusini.

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto za tabianchi, kumekuwepo na uharibifu mkubwa wa mazingira na ongezeko la upungufu wa vyanzo vya maji. Uharibifu unaotokana na shughuli za kibinadamu umepelekea misitu mingi kuharibiwa na uchomaji moto, ukataji misitu kwa matumizi ya mkaa, na hata kilimo kwenye vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Spika, napendekeza Serikali iongeze msukumo wa Wizara za Maji, Kilimo, Maliasili, na Mazingira kufanya kazi kama timu moja ili kukabiliana na janga hili kubwa ikiwemo ujenzi wa mabwawa makubwa katika maeneo yanayokumbwa na mafuriko. Kama ilivyo kwa athari za mafuriko ya Kyela, hata Ziwa Rukwa linaathirika sana na kujaa mchanga na udongo unaosombwa na mito kutokana na mmomonyoko wa udongo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mahitaji ya maji kwenye kilimo, mifugo na hata mahitaji ya mabwawa kwa ajili ya kuzuia mafuriko ikiwemo kwenye miundombinu yetu ya reli na barabara, kuna haja na kuwepo kwa taasisi moja kuratibu na kusimamia mipango ya matumizi ya maji. Nchi yetu ina neema kubwa ya maji na hii ni fursa ya kipekee kutumia haya maji kama mojawapo ya nguzo kuu kukuza uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya ufinyu wa muda sikuweza kumaliza mambo machache ambayo nilitaka kuyasema hususan mahitaji ya visima virefu, kwa hiyo, kwa ridhaa yako naomba maandishi haya yawe sehemu ya mchango wangu.

Mheshimiwa Spika, tuna uhitaji mkubwa wa visima virefu katika vijiji vfuatavyo; Kijiji cha Oldonyongiro ambako pia kuna kituo kipya cha afya cha Mareu Kata ya Kingori; Kijiji cha Ngyani Kata ya Nkoaranga; Kijiji cha Nkoaranga; Kijiji cha Kilinga; na Kijiji cha Poli.

Mheshimiwa Spika, miundombinu ya kuwapatia maji wananchi walioko katika vijiji ambavyo bomba kubwa la mradi mkubwa wa shilingi bilioni 520 Mradi wa *AUWSA* linapita Makiba, Mbuguni, Msitu wa Mbogo, Karangai Maweni, Kikwe na Nambala.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. MUNIRA MUSTAFA KHATIBU:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote namshukuru Mungu kwa kunijalia afya njema. Aidha, nampogeza Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa juhudi zake katika kushughulikia tatizo la maji nchini.

Mheshimiwa Spika, juhudi za Mheshimiwa Rais zinaonesha wazi dhamira yake ya kutua ndoo kichwani wanawake ambao ni waathirika wakubwa wa tatizo la maji. Hatua hizi za Mheshimiwa Rais zinaonekana kupitia namna alivyotoa fedha za miradi ya maendeleo ya maji.

Mheshimiwa Spika, miradi ya maendeleo; katika mwaka 2022/2023 Wizara ya Maji - Fungu 49 ilitengewa shilingi 657,899,338,000; kiasi hicho kinajumuisha shilingi 407,064,860,000 fedha za ndani na shilingi 250,834,478,000 fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, hadi mwezi Aprili, 2023 Wizara imepokea jumla ya shilingi 623,753,326,424.64 sawa na asilimia 94.81 ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka 2022/2023; kati ya fedha zilizopokelewa shilingi 374,794,312,195.31 sawa na asilimia 92.07 ni fedha za ndani na fedha za nje ni shilingi 248,959,014,229.33 sawa na asilimia 99.25.

Mheshimiwa Spika, kwa namna fedha zilivyotolewa na Mheshimiwa Rais ni wazi kuwa amelenga kuondoa changamoto ya maji nchini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kutoa fedha za kutosha katika Wizara hii, bado kuna changamoto kadhaa ambazo zinaathiri malengo yaliyokusudiwa. Changamoto hizo ni kama ifuatavyo; upatikanaji wa maji katika Jiji la Dodoma.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi za Serikali, tatizo la maji Dodoma limeendelea kuumiza wananchi kutokana na uhitaji wa maji. Mahitaji hayo yanatokana na ongezeko la wananchi waliohamia Dodoma na kuanzisha makazi. Hali ilivyo sasa maji yanatolewa kwa mgao wa mara tatu kwa wiki hali ambayo inarudisha nyuma maendeleo hasa kwa wale wananchi wanaojishughulisha na biashara ya maji na sekta ya maji.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi za Serikali za kuondoa changamoto hizo kwa kuanza mpango wa kuleta maji kutoka Bwawa la Mtera na kujenga bwawa jipya la Farkwa, hatua hiyo haijaonesha dhamira ya muda mfupi ya kuondoa tatizo hilo. Nashauri Wizara kuharakisha mchakato wa kukamilisha hatua za ujenzi wa miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu changamoto ya wakandarasi kuchelewa kulipwa; kumekuwepo na changamoto ya wakandarasi kutekeleza miradi bila kulipwa fedha zao kwa wakati hali ambayo imesabisha miradi kuchelewa kukamilika na nyingine kukwama na kuongeza gharama za utekelezaji wa miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kulipa madeni ya wakandarasi kwa wakati ili miradi ya maji iweze kukamilika kwa wakati.

Kuhusu changamoto ya wakandarasi kupewa mradi zaidi ya mmoja; taarifa zinaonesha kuwa moja ya changamoto kubwa ya kutokukamilika kwa miradi ya maji nchini ni pamoja na mkandarasi mmoja kupewa mradi zaidi ya mmoja. Hali hiyo imesababisha wakandarasi wengi kushindwa kukamilisha miradi hiyo kwa wakati kwa kuwa wamekuwa wakihamisha mashine na nguvu kazi kutoka mradi mmoja kwenda mradi mwingine.

Mheshimiwa Spika, tatizo hili linasababisha hasara kubwa kwa Serikali kutokana na miradi kuchelewa kukamilika na kusababisha ongezeko la gharama za vifaa. Hivyo ni rai yangu kuwa Wizara itaangalia suala hili kwa kina katika mipango ijayo ya miradi ya maji nchini.

Mheshimiwa Spika, mwisho nampongeza Waziri wa Maji Mheshimiwa Jumaa Aweso na Naibu wake Mheshimiwa Maryprisca Mahundi kwa kazi nzuri wanayoendelea kufanya katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika,naunga mkono hoja.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, naungana na Watanzania wenzangu wote kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujalia baraka zake katika nyanja mbalimbali za ustawi wa kijamii, amani, upendo, mshikamano wakati wote tangu kuanzishwa kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, naungana na wananchi wote wa jimbo langu la Mbulu Mjini kumpongeza sana Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, viongozi na watendaji wote Serikalini kwa jinsi walivyotatua changamoto mbalimbali na utekelezaji wa Ilani ya CCM 2022-2025, tunawaombea kwa Mwenyezi Mungu awajalie mafanikio na baraka.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kukupongeza wewe Mheshimiwa Spika kwa jinsi unavyoliongoza Bunge letu toka ulivyopokea majukumu yako, nawe Mwenyezi Mungu akujalie baraka na mafanikio pamoja na wananchi wa jimbo la Mbeya Mjini.

Mheshimiwa Spika, kwa moyo wa dhati nampongeza Mheshimiwa Jumaa Aweso – Waziri wetu; Mheshimiwa Maryprisca Mahundi - Naibu Waziri; Katibu Mkuu *Engineer* Nadhifa Kemikimba; Naibu Katibu Mkuu na watendaji wetu

wote wa Wizara kwa ngazi zote. Kwa kweli jitihada zinaonekana japo kuna changamoto.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kutoa mchango wangu kupitia mapendekezo ya bajeti ya Wizara hii muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa letu; kwanza, Serikali iongeze jitihada za kutafuta fedha za kujenga miundombinu ya visima vyote vilivyotayari kuchimbwa katika maeneo mbalimbali kwani tayari tumemaliza uchimbaji wa visima saba katika jimbo langu la Mbulu Mjini yapata mwaka sasa, lakini hatujaweza kujenga matanki na kuweka mtandao wa mabomba kwenye vijiji, hali hii inawafanya wananchi kusubiri huduma ya maji kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, Serikali itazame upya suala la mchakato wa uteuzi wa bodi mpya ya maji kwenye mamlaka za maji za *RUWASA* Wilaya na Miji kwani maeneo mengi bodi humaliza muda wake, lakini ngazi hizo hazichukui hatua za mchakato wa uteuzi wa bodi mpya haraka.

Mheshimiwa Spika, Serikali iwe na ratiba ya ukaguzi wa tathimini ya kiufanisi wa utendaji, mapato na matumizi pamoja kuangalia mwongozo wa uendeshaji wa mamlaka za maji kama unakidhi haja na kutoa fursa ya maoni kama upande wa wapokea huduma wanaridhika.

Mheshimiwa Spika, Serikali iangalie suala la upotevu wa maji kwenye mitandao ya mabomba kwa kulinganisha uzalishaji wa maji kutoka vyanzo mpaka ankara za malipo kwa watumiaji, kwenye suala la madeni mpango wa kuunganisha mfumo wa kulipa *bill* ya maji kwa kununua kwanza ili kufanikisha upunguzaji wa madeni.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa maeneo mengi ya mji yanapokea wimbi kubwa la wananchi wengi wanahamia, Serikali iangalie upatikanaji wa vyanzo vikubwa vya maji

badala ya kuchimba visima vingi kwenye eneo moja ilhali upatikanaji wa maji hauendani na wingi wa watu.

Mheshimiwa Spika, Serikali ijitahidi kutoa fedha zote zinazoombwa kwenye bajeti ya Wizara hii kwani kuna maeneo mengi miradi mingi imekwama kwa ajili ya upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, Serikali itafute fedha za ujenzi wa majengo ya Ofisi za Mamlaka ya Maji *RUWASA* kwa ngazi ya Wilaya na mijini ili kupunguza gharama za uendeshaji isiyolingana na mapato halisi ya mamlaka mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na naomba kuwasilisha.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa kazi nzuri mnayoifanya. Wizara ina viongozi wasikivu katika kusikiliza hoja za Wabunge kuanzia ngazi ya Wizara, Mikoa na Wilaya.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utajikita katika maeneo mawili; kwanza ni kuhusu Mradi wa Makonde. Tunaipongeza Wizara ya Maji kwa kuanza kutekeleza mradi huu ambao unanufaisha wakazi wa Halmashauri za Nanyamba; Newala na Tandahimba. Mradi huu kwa usanifu wa sasa unaonekana inaishia kwenye baadhi ya maeneo tu na kusema kuwa sehemu zingine itakuwa *Phase II.* Tunaomba kazi hiyo ifanywe kwenye *Phase I* ukizingatia kuwa Wilaya nufaika na mradi huu upatikanaji wa maji upo chini ya asilimia 50.

Pili ni kuhusu mradi wa kutoa maji Mto Ruvuma na kupeleka Mtwara Manispaa, mradi huu ni wa muda mrefu na bado haujaanza kutekelezwa. Mradi huu utanufaisha Halmashauri ya Nanyamba, Mtwara na Manispaa ya

Mtwara, mradi huu sasa utengewe fedha ili uanze kutekelezwa.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa uamuzi wake wa busara wa kuendelea kutenga fedha za ujenzi wa Bwawa la Kidunda, bwawa ambalo ni faraja kubwa kwa wakazi wa Mkoa Dar es Salaam na Pwani kupata maji kwa wakati wote.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Makatibu Wakuu na watendaji wote wa Serikali kwa kazi nzuri kuhakikisha kuwa Mkoa wa Dar es Salaam tunapata maji safi na salama isipokuwa changamoto yetu kubwa ni kupungua kwa maji na mabomba kupasuka na kupoteza maji mengi sana; naiomba Serikali iendelee kupambana na changamoto hizo.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali ikamilishe miradi ya maji ya Dar es Salaam pamoja na Mradi wa Visima vya Maji vya Kimbiji na Mpera sasa ukamilike na maji yasambazwe kwenye Wilaya ya Kigamboni yote na Temeke, Mbagala pia Jimbo la Ukonga.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu Serikali ikafanye utafiti wa maji tuweze kuchimba visima virefu maeneo ya Mvuti Dondwe nao wananchi wa Ilala wapate chanzo kipya cha maji. Ni matumaini yangu chanzo hicho kitawasaidia sana.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja naipongeza sana Serikali kwa utekelezaji na juhudi zake, endeleeni hivyo Mungu atasimama nasi.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, nyongeza yangu ya mchango wa bajeti Wizara ya Maji ni kuwa naomba pia kuikumbusha Wizara juu ya gari kwa ajili ya *RUWASA* Wilaya ya Nyasa kama ambavyo nilijibiwa kupitia swali langu la msingi Bungeni. Je, katika magari zaidi ya

hamsini mliyogawa Nyasa imo? Jimbo la Nyasa ni kubwa ni vema wawezeshwe katika suala la usafiri.

Mheshimiwa Spika, Mkandarasi wa Puulu, Songambele na Ngeye anaanza lini mradi? Ana zaidi ya miezi saba sasa.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nimpongeze sana Waziri Jumaa Aweso na Naibu wake *Engineer* Maryprisca Mahundi, Katibu Mkuu *Engineer* Kemikimba pamoja na wataalam wa Wizara ya Maji kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Spika, Waziri na timu yake wamekuwa mfano wa kuigwa kwenye kutatua changamoto za maji na kuwatua akinamama ndoo kichwani, kwani maji ni haki ya msingi kwa binadamu wote.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla inatia faraja kuona upatikanaji wa maji vijijini unaongezeka kama alivyoonesha kwa kina katika hotuba yake ya bajeti ya mwaka huu wa 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, katika jimbo langu la Moshi Vijijini kuna changamoto ya upatikanaji wa maji ya bomba katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, Kata ya Mabogini ina wakazi wengi wapatao 57,231 na kuna changamoto kubwa ya maji ya kunywa. Katika Kata ya Mabogini kuna changamoto ya maji katika vijiji vya Mabogini, Muungano, Chekereni, Maendeleo, Mtakuja na Mserekia. Ninaomba Wizara ipeleke maji katika vitongojj ambavyo havijapata maji katika vijiji vilivyotajwa

Mheshimiwa Spika, pili, Kata ya Kimochi ina zaidi ya wakazi 16,046. Kata hii ina vijiji vya Mowo, Sango, Shia, Miami, Lyakombila na Kisaseni. Eneo lote linahudumiwa na *MUWSA*.

Tunaishukuru Serikali kwa jitihada za awali kuwafikishia wakazi wa eneo hili maji, ila bado kuna changamoto kubwa sana ya upatikanaji maji katika maeneo mengi hasa Kijiji cha Sango, Shia na Kisaseni. Ninaiomba Serikali itutengee pesa za kutosha ili maji yafike maeneo yote ya kata hii vikiwepo vijiji vya maeneo ya tambarare.

Mheshimiwa Spika, katika Kata ya Uru Kusini yenye vijiji saba vya Okaseni, Kimanganuni, Rua, Kariwa, Longuo A, Kitandu na Shinga ina takribani wakazi 31,557 na ina miradi mitatu ya Mang'ana, Kisimeni na Mbora. Changamoto ya miradi hii ni maji kidogo katika mifumo ambayo hayatoshelezi. Naiomba Serikali isaidie, kwani mbali na hivyo vijiji kuna taasisi ya Chuo Kikuu cha Kikatoliki Mwenge. Kuna shida kubwa sana ya maji hapo chuoni. Ninaiomba Wizara iangalie namna ya kusaidia.

Mheshimiwa Spika, nne, Kata ya Arusha Chini yenye wakazi 13,977 kuna shida ya maji katika Vijiji vya Mikocheni na Chemchem. Sasa hivi ni watu wa Kirua Kahe wanatoa huduma ya maji ya kuuza katika maeneo haya. Maji huuzwa kwa bei ya juu na si salama kwa matumizi ya binadamu. Kata hii inahudumiwa na *RUWASA*. Ninaiomba Wizara ijenge mradi kwa kutumia maji ya kutoka Mto Ronga na Kikuletwa.

Mheshimiwa Spika, tano, katika Kata ya Uru Kaskazini yenye wakazi 10,817 *MUWSA* haijatekeleza ahadi ya kuunganisha vijiji vya Msuni na Njari. Kuna chanzo cha maji Uru Kaskazini ambacho hupeleka maji Kata ya Uru Kusini na Kata ya Pasua ya Manispaa ya Moshi Mjini. Wananchi wananyanyasika sana kwani maji ya eneo lao hayawasaidii. Ninaiomba Wizara iunganishe Vijiji vya Msuni na Njari ili wananchi wapate maji.

Mheshimiwa Spika, katika Kata ya Old Moshi Magharibi, kuna wakazi 8,431 na kuna mradi wa maji wa Tela Mande ambao umekamilika. Mradi huu una maji mengi sana

na ya ziada ambayo kwa sasa yanahudumia wananchi wa ukanda wa milimani.

Mheshimiwa Spika, vijiji na vitongoji vya kata hii vilivyopo ukanda wa tambarare kama kile cha Mandaka Mnono na Saningo havina maji ya bomba. Ninaiomba Wizara iwapelekee maji wananchi hawa walioko ukanda wa tambarare.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu hapo juu, naunga mkono hoja.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru wewe na Mheshimiwa Rais kwa kutoa shilingi bilioni 100 kwa Mradi wa Maji Geita Mjini, mkandarasi yupo, tatizo kwa mwaka mzima sasa hakuna kazi ya kuonekana imeanza kufanyika.

Mheshimiwa Spika, zipo taarifa za kuchelewa kuanza kwa mradi sababu ya fidia ndogo sana ya vibanda vya wavuvi nane na nyumba moja, naomba Wizara ilifanyie kazi.

Mheshimiwa Spika, naomba kumkumbusha Mheshimiwa Waziri ahadi yake ya ukarabati wa Bwawa la Kasamwa, aliahidi ndani ya Bunge na wananchi wa Kasamwa wanategemea utekelezaji wa ahadi yako.

Mheshimiwa Spika, umekuwepo mradi wa maji katika Kata ya Bulela ambao awali uliwekwa kwenye bajeti ya maji, Wizara kupitia *RUWASA* shilingi milioni 510; fedha hizi kwa miaka mitatu sasa bado haujatekelezwa, kata hii ina kituo cha afya, shule ya wasichana ya bweni na josho.

Mheshimiwa Spika, Kata za Nyanguku na Ihanamilo visima vinakauka kiangazi kwa kuwa ni vifupi. Naomba Mheshimiwa Waziri maeneo haya yafanyiwe kazi.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze mchango wangu kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri inayofanyika kwenye sekta ya maji. Kwenye Wilaya ya Hanang inategemewa miradi mikubwa ambayo inaenda kutatua kero kubwa ya maji kwa wana-Hanang.

Mheshimiwa Spika, miradi ya maji Hanang; Wilaya ya Hanang ina Mradi wa Mogitu - Gehandu, Gawlolo, Mureru, Ziwa Bassotu, Bwawa la Bassotughang, Basodesh, Gijetamhog, Mamlaka ya Mji Mdogo wa Katesh na vijiji vingine ambavyo jumla zimechimbwa visima 24 na utaratibu unafanyika wa kuchimba visima vingine 16 ili jumla tutakuwa na visima 40 ndani ya miaka mitatu. Wana-Hanang wanaendelea kusubiri kwa hamu kukamilika kwa miradi hii ili maji yawafikee wananchi.

Mheshimiwa Spika, maombi mahsusi; Bwawa la Gidahababiye ambalo usanifu wake umekamilika muda mrefu tupate fedha ya kuujenga, imekuwa ni ahadi ya muda mrefu sana, pia mnaweza kushirikiana na Wizara ya Kilimo ili litumike kwa ajili ya umwagiliaji.

Kuhusu miradi inayoendelea ikamilike kwa wakati hasa Mamlaka ya Mji wa Katesh ambayo ili mradi ukamilike inahitajika tu 570,000,000 ukizingatia mpaka sasa tumeshatumia zaidi shilingi bilioni tano kwenye mradi huu.

Mheshimiwa Spika, kasi ya ujenzi wa mradi wa Ziwa Bassotu ni ndogo sana ikilinganishwa na mahitaji, tuendelee kutenga fedha za kutosha ili uweze kukamilika; na tupate gari ili kurahisisha utendaji kazi kwa *RUWASA* ndani ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema, aidha, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa Rais mwenye maono na anayewapenda na kuwajali watu wake. Kazi nzuri iliyofanyika katika kuondoa kero ya maji sehemu mbalimbali ni jambo la kujivunia kama Watanzania tukizingatia kuwa maji na uhai.

Mheshimiwa Spika, mbali na sekta ya maji Mheshimiwa Rais amefanya maajabu katika sekta zote za miundombinu, elimu, afya, ardhi, kilimo na kadhalika. Mwenyezi Mungu amjalie afya njema na aendelee kulitumikia Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, ninampongeza sana Waziri wa Maji yeye binafsi, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na timu nzima ya Wizara kwa kazi nzuri ya kumtua mama ndoo, mwenyezi Mungu awajalie afya njema muendelee kulitumikia Taifa letu.

Pili, ninakushukuru sana kwa kuweka katika bajeti Mradi wa Kabangaja wa chanzo kipya cha maji utaondoa adha ya maji Manispaa ya Ilemela.

Mheshimiwa Spika, ombi langu, wakati tunasubiri kukamilika kwa mradi mkubwa wa chanzo cha maji cha Butimba, naomba sana kupatiwa visima virefu angalau kumi tu kwa kata zilizoko pembezoni *(peri urban)* mwa mji ambazo hazina maji ya bomba kabisa wanatumia visima visivyo rasmi, itapendeza nao wakapata maji ya visima. Maeneo husika ni eneo la Kata za Nsumba, Kiseke; Lutongo, Kayenze; Lugeye, Sangabuye; Ilekako, Bugogwa; Isanzu, Bugogwa; Bulyanghulu, Shibula; Ibaya, Shibula; Wiluhya, Kahama; Magaka, Kahama; na Nkoronto, Bugugwa.

Mheshimiwa Spika, naomba sana Wizara ione namna ya kuwasaidia wananchi wa Ilemela ambao ziwa liko hatua chache kutoka makazi yao lakini hawana maji.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde, atafuatiwa na Mheshimiwa Abdallah Hamis Ulega, na Mheshimiwa Mhandisi Maryprisca Winfred Mahundi, ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO**: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi. Kipekee kabisa nichukue fursa hii kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uwekezaji mkubwa alioufanya kwenye sekta hii ya maji, ambao unakwenda kuleta mapinduzi makubwa.

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote katika Wizara ya Maji kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya katika kuhakikisha kwamba wanatatua changamoto za maji kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Juma Aweso ni kijana ambaye pia anatoa somo kwa vijana wengine wanaopewa dhamana namna ya kutekeleza majukumu yao. Anajitahidi sana kufanya kazi vizuri na tunamwombea kila la kheri kwa Mwenyezi Mungu akamilishe kazi hii kubwa ambayo anaendelea kuifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi Wizara ya Kilimo tunafanya kazi kwa ukaribu sana na Wizara ya Maji. Tumeshuhudia hivi karibuni mapinduzi makubwa kabisa kwenye sekta hii ya maji juu ya uingizaji wa mitambo zaidi ya 25 ambayo itasaidia katika uchimbaji wa visima na mabwawa. Mabwawa haya yatakwenda kuongeza vyanzo vya maji ambayo yatatumika pia kwa ajili ya matumizi ya binadamu, na katika maeneo mengine pia wanufaika watakuwa wakulima wadogo wadogo katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, kazi inayofanywa na Wizara ya Maji inakwenda sambamba na ile inayofanywa na Wizara ya Kilimo ya uchimbaji wa mabwawa 100 katika bajeti kama tulivyoyasema ambayo yatagusa maeneo mbalimbali katika nchi yetu ya Tanzania. Hii inatupa uhakika katika ku-*address* changamoto za mabadiliko ya tabianchi ambapo moja kati ya jambo kubwa ambalo limekuwa na athari kubwa ni la ukame. Sasa tutapata nafasi ya kuweza kuyavuna maji na pia kuyatumia kwa ajili ya shughuli mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, tunaingia katika historia katika kipindi hiki cha bajeti hizi mbili; ya kilimo na ya maji, zikitekelezwa ipasavyo, maana yake tutakuwa na uhakika wa vyanzo vingi sana vya maji kupitia mabwawa haya na visima ambavyo vitachimbwa.

Mheshimiwa Spika, sisi Wizara ya Kilimo pamoja na TAMISEMI*,* Wizara ya Maliasili na Wizara ya Mifugo, mbele ya Mheshimiwa Makamu wa Rais tuliweka makubaliano ya kuhakikisha kwamba tunatunza vyanzo vya maji ili tuwe tuna uhakika wa vyanzo vyetu vya maji na kuhifadhi mazingira katika vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Spika, katika miradi ambayo tutaitekeleza katika Wizara ya Kilimo hivi sasa, tutahakikisha mifereji tutakayoijenga katika miradi yote ya umwagiliaji, ambayo itakuwa inatumia vyanzo vya maji ya mito na maziwa, tutahakikisha kwamba, maji yale yakishatumika kwenye kilimo yawe na uwezo wa kurudi katika mito na yatumike katika shughuli nyingine. Hivyo, sisi pamoja na wenzetu wa Wizara ya Maji katika eneo hilo, tutahakikisha kwamba mifereji ambayo tutaijenga safari hii kwenye miradi mikubwa hii ambayo inaendelea, itakuwa ni ile ambayo haitakuwa na upotevu mkubwa wa maji tofauti na ilivyo hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, mifereji mingi ya hivi sasa inapoteza maji zaidi ya asilimia 40 kwa sababu ya kukosa ile

miundombinu rafiki ya kuweza kurudisha maji katika chanzo chake cha awali. Kwa hiyo, sisi kwa pamoja tutaifanya kazi hiyo. Sambamba na hilo, tutahakikisha tunatumia mabomba katika baadhi ya maeneo ili maji yatumike katika ufasaha wake mzuri pasipo kuleta changamoto yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja kubwa hapa ni kuzuia upotevu mkubwa wa maji, na bahati nzuri sana tunao wakulima wetu ambao wanafanya kilimo pembezoni mwa vyanzo vya maji, tumeshakaa pamoja na Wizara kwa ajili ya kutoa elimu juu ya matumizi sahihi ya maji lakini na kilimo cha kisasa ambacho hakitaharibu mazingira. Hiyo ndiyo kazi kubwa ambayo tutaifanya kwa pamoja na wenzetu wa Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Spika, katika mikakati ambayo ukiiangalia katika Wizara ya Maji wamezungumza jambo zuri sana la namna pia ya kuondoa changamoto kubwa ya huduma ya usafi wa mazingira katika maeneo mengi. Kwa sababu mimi pia nipo katika eneo hili, nataka nitoe ushuhuda wa kazi nzuri inayofanywa na Wizara ya Maji katika eneo letu la hapa hapa Dodoma ambapo tumeshuhudia juzi tu Mheshimiwa Waziri Aweso amesimamia uingiaji wa mikataba mkubwa kabisa wa zaidi ya Shilingi bilioni 164 ambayo inakwenda kutatua changamoto kubwa ya usafi wa mazingira katika jiji la Dodoma na hasa katika kuhakikisha kwamba sehemu zenye changamoto ya huduma ya majitaka, hivi sasa zinakwenda kuwekewa mfumo mzuri ili kutatua changamoto hii.

Mheshimiwa Spika, katika eneo hili, umefanya katika maeneo mengi nchi nzima, lakini nataka nitoe ushuhuda kwamba, katika eneo hili la Dodoma, ambapo pia Wabunge wengi sana mnaishi na mmesema katika sehemu ya hoja zenu, kwamba Serikali inakwenda kuweka mradi mkubwa ambao utagusa kata 14 na bomba refu la kilometa 117 kwa ajili ya kuondoa majitaka katika maeneo mbalimbali ambayo imekuwa ni changamoto kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hoja ambazo zimesemwa hapa ambazo nataka nizitolee ushuhuda kuonesha kazi nzuri inayofanywa na Mheshimiwa Waziri na timu yake nzima ni suala la maji katika eneo letu la hapa Dodoma Jiji, na nikiwa kama sehemu ya Serikali na vile vile kama kiongozi katika eneo hili, nataka nipongeze kazi nzuri ambayo Mheshimiwa Waziri ameifanya, juu ya changamoto mbalimbali ya maji kwa kutumia mfumo wa uchimbaji wa visima. Tumeona katika maeneo mengi hivi sasa huduma ya maji imeanza kupatikana hasa baada ya Mheshimiwa Waziri kuweka nguvu kubwa ya uchimbaji wa visima vya pembezoni. Tumeshuhudia mradi mkubwa wa Nzuguni ambao unakwenda kutatua changamoto kubwa katika maeneo ya Ilazo, Swaswa, Mlimwa C, pamoja na Kisasa. Vile vile na uchimbaji wa visima vingine virefu katika maeneo ya Makulu, Nala, Zuzu, Iyumbu na Chang'ombe. Haya maeneo yote yanakwenda kutatua changamoto kwa kiwango kikubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii ilikuwa ni kutoa tu ushuhuda wa kazi kubwa na nzuri ambayo anaifanya Mheshimiwa Waziri katika eneo letu la hapa Dodoma, lakini kikubwa na katika kumalizia hoja yangu, nataka tu nimhakikishie kwamba sisi Wizara ya Maji pamoja na Wizara ya Kilimo tutafanya kazi kwa pamoja kuhakikisha tunatatua changamoto za msingi na hasa katika kilimo ambacho hakitaharibu mazingira ili kwa pamoja basi, wakulima wanufaike na vyanzo vya maji, lakini na vile vile tuweze kuyatunza maji kwa ajili ya mazingira.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Nakushukuru sana kwa nafasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa ahsante sana. Mheshimiwa Abdallah Hamis Ulega, atafuatiwa na Mheshimiwa Mhandisi Maryprisca Mahundi, na Mheshimiwa Mtoa hoja, ajiandae.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, nami naomba nichukue fursa hii kukushukuru kwa kunipa fursa ya kusema kwenye bajeti hii ya Wizara ya Maji. Nimesimama kuunga mkono hoja, na pili, nimesimama kuchangia kidogo kwenye bajeti hii ya Wizara ya Maji inayoongozwa na Mheshimiwa Aweso.

Mheshimiwa Spika, nami nimshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, maana mwaka 2022 tulipata mitambo kwa ajili ya uchimbaji wa visima na mabwawa katika mikoa yetu. Kwa kuwa maji haya ni kwa ajili ya wanadamu, lakini pia maji haya ni kwa ajili ya mifugo na huduma nyingine ikiwemo kilimo, nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge baadhi ya waliochangia hapa leo, wakisisitiza kwamba, katika maeneo yenye mifugo na ikiwa kama uko mradi wa maji kwenye eneo lile, basi ni vizuri sana ule mradi wa maji uzingatie kutoa huduma kwa mifugo pia.

Mheshimiwa Spika, katika hili namshukuru sana mtu muungwana, mtu mzuri, mweledi, mchapakazi, Waziri Aweso na timu yake yote, kwa hakika tumekubaliana kwamba katika kila *designing* ya mradi wa maji pale unapopita kwenye eneo la mifugo, basi uzingatie sana kupatikana kwa namna ambayo utasaidia mifugo yetu kuhudumiwa na maji yale.

Mheshimwa Spika, nimemsikia hapa Mbunge wa Ngorongoro, Mheshimiwa Shangai, vilevile nimemsikia Mheshimiwa Shangazi, wamesisitiza sana. Mimi ninafahamu, kwa wadau wa mifugo, sisi wafugaji ni bora wakati mwingine tukose maji sisi wenyewe lakini mifugo yetu iweze kupata maji. Ndiyo maana ninamshukuru sana ndugu yangu, Comred Jumaa Aweso, kwa kuwa tumekubaliana kimsingi ya kwamba tunakwenda kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, nawaomba Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwenye kusisitiza juu ya jambo hili, ikiwa

mtaona kama kuna wasiwasi juu ya ile *designing,* siyo tu kumfuata kaka yangu, Mheshimiwa Aweso, hata nami nishirikisheni ili kusudi niweze kusukuma kwa pamoja; mimi, yeye na timu zetu, ili wafugaji wetu waweze kupata maji. Maana sote tunafahamu ya kwamba mifugo ni utajiri, na ili iweze kukaa vizuri, ipate malisho na maji.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mhandisi Maryprisca Mahundi, Naibu Waziri wa Maji, na mtoa hoja ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi na nipende kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu wingi wa Rehema, ambae ameweza kutufanikisha kuweza kujadiliana na kutimiza majukumu yetu kwa siku mbili.

Mheshimiwa Spika, pia nipende kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa wema wake na hekima alizojaliwa na Mwenyezi Mungu na akaona kwamba aweze kututumikia watanzania, aweze kuokoa jamii ya watanzania kwa kuwa na dhamira safi ya kuhakikisha maji safi na salama yanapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, dhamira hii ililenga kumtua mama ndoo kichwani lakini kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wameweza kuongea. Pia, si tu kumtua ndoo mama kichwani bali kuokoa familia kwa sababu ndoa zinakwenda kuimarika. Wakinamama wanaacha kwenda kutembea umbali mrefu na kutumia muda mwingi kutafuta maji, sasa wanakwenda kufanya majukumu yao kama mama kama Mke ndani ya familia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais, dhamira yake hii ameweza kuitekeleza na mara kadhaa akiwa katika misafara

anapotembelea miradi na kuzindua, amewahi kuongea "anachukizwa anapokutana na wakinamama huko kwenye vijiji wamebeba ndoo kichwani" na dhamira hii imeendelea kuonekana. Vilevile, alishasema yeye mwenyewe ni Mama maji, atahakikisha Tanzania inakwenda kupata maji safi na salama. Hili ameweza kulithibitisha kwa mwaka huu wa fedha tunaokwenda kuumaliza 2022/2023, kupata fedha asilimia 96. Hii inaonesha mama amekuwa akisema na kutenda na tunamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile, naomba nimshukuru Mheshimiwa Makamu wa Rais, Dkt. Philip Isdor Mpango, nae hajawa nyuma katika hili wakati akiyatetea mazingira. Tunafahamu vyanzo vya maji vinahitaji mazingira lakini tunamshukuru pia Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa na yeye pia vita hii ya kuhakikisha tunamtua ndoo mama kichwani hajawa nyuma. Hata katika hotuba yake tumeweza kumsikiliza na tumeona kabisa *commitment* ya Serikali katika kuhakikisha tunapata fedha zitakazohakikisha miradi inabuniwa lakini vilevile inatekelezwa na kukamilishwa kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nikupongeze wewe mwenyewe, wewe ni Spika wa viwango kama walivyosema wengine, umekuwa ukitupa ushauri mara kadhaa sisi Serikali na ushauri wako mara zote umekuwa na tija kubwa sana kwa sisi kuweza kutimiza majukumu yetu. Ninakuombea kwa Mwenyezi Mungu, wananchi wa Mbeya Mjini waendelee kukuelewa kama wanavyokuelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawapongeza wananchi wa Mbeya Mjini kwa kuweza kuongozwa na wewe kwani hata kwenye jimbo lako tunajifunza kwa matendo. Kazi nyingi unazozifanya na sisi tunakuiga kwa sababu wewe ni kiongozi wa mfano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze pia Naibu Spika kwa kazi nzuri pia anayoifanya na ushirikiano mkubwa ambao ametupatia sisi Wizara ya Maji, ushauri wake tutaendelea kuzingatia na kuhakikisha tunatimiza majukumu yetu vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze na kuishukuru Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira. Mheshimiwa Mwenyekiti, Jackson Kiswaga, pamoja na Makamu wake Mheshimiwa Anna Lupembe pamoja na Kamati nzima, mmekuwa washauri wazuri katika kuona tunatimiza wajibu wetu na tunahakikisha tunamtua ndoo mama kichwani kwa umoja wetu. Tunawashukuruni sana Kamati tuko tayari kuendelea kushauriwa ili tuweze kufanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru Wabunge wote, mmeongea vizuri sana tunawashukuru kwa pongezi, tunawashukuru kwa ushirikiano. Pale mnapoweza kuwasemea watendaji wetu kama ya mameneja wa wilaya waweze kuthibitishwa inaonesha dhahiri mna mashirikiano nao mazuri. Kwenye hilo tunawashukuruni sana na hayo ni maelekezo ya Mheshimiwa Waziri, Jumaa Hamidu Aweso, nyakati zote za vikao kwamba, watendaji wawe na mahusiano mazuri na Serikali, wabunge, pamoja na Chama Tawala ambacho ilani yake tunaitekeleza. Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge, hoja zote, ushauri ambao mmetupatia, sisi kama wasaidizi wa Mheshimiwa Waziri, tumesikia, tumepokea tutatekeleza kwa msaada wa Mwenyezi Mungu. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hoja ambazo Waheshimiwa Wabunge wameweza kuziongea humu ndani, naomba nitaziongea chache na nyingi ataziongea Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na suala la uvunaji wa maji ya mvua. Sisi kama Wizara tumejipanga vizuri na kuhakikisha

suala la uvunaji wa maji ya mvua tunakwenda kulifanyia kazi kwa umakini mkubwa. Pamoja na kutumia majengo makubwa ya Serikali, pamoja na kutumia majengo ambayo pia tunashauri wananchi waweze kuvuna kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge mmeweza kushauri, tutazingatia na kufanya hayo yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile, kumshukuru Mheshimiwa Samia Samia Suluhu Hassan, ni pamoja na kutendea kazi vifaa alivyotupatia. Mvua kwetu kama Wizara huwa tunahesabu ni baraka na mvua hii ambayo Tanzania tunaipata kwa wingi hatutaki iendelee kuonekana ni laana. Tuna vifaa vya kuchimbia mabwawa, tutavitumia vifaa hivi ambavyo Mheshimiwa Rais, alitoa fedha nyingi tumeweza kuvinunua na tayari tumeshavipokea hapa nchini na tayari vimekwishaanza kazi. Maeneo mbalimbali ambayo yanakuwa na mafuriko tutahalkikisha tunakwenda kuchimba mabwawa madogo, makubwa na ya kati ili tuweze kuvuna maji haya yaweze kutumika kwa mifugo, kilimo vilevile kwa mahitaji ya majumbani na viwandani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile tutaendelea kuhakikisha miradi mikubwa ambayo tunaijenga nchi nzima, tunakwenda kutumia vizuri rasilimali fedha ambayo Mheshimiwa Rais anakesha kuitafuta na kutupatia sisi Wizara kwa uaminifu mkubwa, kuona maeneo ya vijijini ambayo miradi hii mikubwa inapita basi na wao wakabaki kuwa wanufaika. Hatutapitisha mabomba makubwa na kuwacha vijiji hivi ambavyo vinapitiwa na miradi mikubwa bila kupewa huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile, tuna Chuo chetu cha Maji. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, ameendelea kutoa fedha nyingi kwenye Chuo cha Maji, sasa hivi Chuo cha Maji kina sura nzuri, tunaamini elimu nzuri inapatikana kwenye mazingira mazuri. Mazingira ya Chuo cha Maji yameboreshwa kwa sehemu kubwa na yanaendelea

kuboreshwa. Tutahakikisha wale wahitimu tunaendelea kuwatumia kwenye miradi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri, anapenda kusema tunajenga hospitali anapelekwa daktari na *nurse*. Sasa Wizara ya Maji tumesema si tu kukabidhi zile jumuiya za watumia maji, tutatumia wataalam wetu ambao tunawazalisha kwenye chuo chetu ili waeze kusimamia hii miradi vizuri kwa weledi mkubwa ili kuongeza tija zaidi. Tayari tumekwisha anza kuwatumia wataalamu hawa na tutaendelea kuwatumia zaidi na zaidi.

Mheshimiwa Spika, suala la vifaa vya kazi, sisi kama Wizara tayari tumelifanyia kazi. kwa mwaka huu wa fedha tunaomaliza 2022/2023 tumeweza kuagiza magari 21 kupitia *RUWASA,* vilevile kwa mwaka ujao wa fedha 2023/2024 tuna magari 25 ambayo tumeagiza na wizara kama wizara imeagiza magari matatu, jumla magari 49. Vifaa hivi vya kazi tutahakikisha vinapatikana na kuongeza kila wakati kadri tunavyoendelea kupata fedha.

Mheshimiwa Spika, suala la kuwathibitisha watendaji wa *RUWASA*. Wabunge wengi wamewasemea mameneja wa wilaya. Tayari sisi kama wizara tumelichukulia hatua na tayari tumelifanyia kazi mpaka sasa watumishi 44 wameshathibitishwa na tayari watumishi 117 wapo kwenye *vetting* wanafanyiwa kazi ili na wao waweze kuthibitishwa. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, tumepokea ushauri na tutahakikisha hawa wote ambao watakidhi vigezo wataweza kupatiwa nafasi ambazo wanazifanyia kazi sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa nafasi na niseme tena Waheshimiwa Wabunge tunawashukuru kwa ushirikiano mkubwa tuendelee kushirikiana. Baada ya Bunge kama kawaida tutaendelea kufika kwenye majimbo kuhakikisha kazi zinafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Nimwite sasa Mheshimiwa Waziri wa Maji, Mheshimiwa Jumaa Hamidu Aweso, mtoa hoja aje ahitimishe hoja yake. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote kwanza nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema pamoja na ninyi sote na kuweza kuchangia bajeti ya Wizara yetu ya Maji. Waheshimiwa Wabunge, Mwenyezi Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu limeweza kujadili bajeti yetu ya Wizara ya Maji ya Mwaka 2023/2024 niliyoiwasilisha hapa Bungeni tarehe 10 Mei, 2023.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwako wewe binafasi kwa kazi kubwa na usimamizi mzuri katika Bunge lako hili Tukufu lakini kama kiongozi kijana yako mengi ambayo nimejifunza kutoka kwa Spika wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo moja ambalo nimejifunza kutoka kwako, kwamba hata uwe kiongozi na cheo kikubwa namna gani usisahau ulipotoka. Hata uwe na nyadhifa kubwa namna gani usiwasahau unaowaongoza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimepata dhamana ya kuwa Waziri wa Maji, niliwahi kufika pale Mbeya, pamoja na kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hujaacha hata siku moja kuwasemea wananchi wako katika Jiji la Mbeya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nikutie moyo, upo msemo unaosema” ukipigana vita ugenini nyumbani lazima kuwe na amani” pamoja na bajeti hii ambayo tunayopitisha, tunajua

ombi ambalo ulilotupa kwetu sisi kama wizara, tunatekelea mradi wa bilioni 117 pale Mbeya na *Advance payment* tumekwishaitoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kumpongeza Naibu Spika, pamoja na wenyeviti wote wa Kamati, kwa namna walivyoweza kusimamia bajeti yetu ya Wizara yetu ya Maji. Lakini kwa namna ya kipeke usione vyaelea ujue vimeundwa. Leo tunapongezwa Wizara yetu ya maji sio jambo jepesi sana. Mageuzi haya ambayo sisi kama viongozi wa Wizara ya Maji ambao tumeshirikiana na wenzangu haikuwa Rais. Kwa sababu tulipoyaleta katika Bunge lako Tukufu tulipata baraka zote. Hatuna cha kuwalipa Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo kabla sijaja kuhitimisha bajeti yetu, hivi mchana nilikuwa nimekaa na watendaji wetu wa wizara tulikuwa tunaangalia na kuweza kutoa *commitment* ya utekelezaji wa zile hoja ambazo zimetolewa na Waheshimia Wabunge. Moja wa mtendaji wetu alisimama na akasema Mheshimiwa Waziri, naomba utufikishie salamu kwa waheshimiwa wabunge. Pamoja na ukurugenzi wangu nimefanya kazi katika Wizara ya Maji leo inafika miaka 20. Wizara yetu hii ya Maji ilikuwa wizara ya kero na lawama tu. Kila tukija Bungeni hali ilikua ni tete sana. Leo Waheshimiwa Wabunge wanatupongeza, Waheshimiwa Wabunge, Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, funzo ambalo mmetupatia sisi kama viongozi na watendaji wa Wizara ya Maji, huna sababu ya kujitutumua wewe fanya kazi watu wanaona. Mmetutia moyo, mmetutupia nguvu kubwa sana. *Commitment* ambayo nimepewa na watendaji wetu wa Wizara ya Maji, kusema katika Bunge hili Tukufu na kumwambia Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, wanasema kama betri ambalo lilikuwa linachajiwa sasa liko *full charge* watafia *site*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wametoa *slogan* katika kikao ambacho kilichokaliwa leo, wamesema *slogan* ya sasa ya Wizara ya Maji, itakuwa *Die empty.* Watatumia maarifa yao, watatumia nguvu zao kuhakikisha azma ya Rais wetu Mama Dkt. Samia Suluhu Hassan, kuhakikisha maelekezo na *target* za Chama cha Mapinduzi kwamba itakapofika mwaka 2025, asilimia 85 ya upatikanaji wa maji vijijini na asilimia 95 ya upatikanaji wa maji Mjini tunakwenda kuitekeleza kwa dhati kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wamenituma niwaeleze waheshimiwa wabunge, pongezi ambazo mmezitoa wanadeni kubwa sana. Wanasema kwamba ukicheza ngoma lazima uangalie na jua. Maji ni pamoja na uhai, maji ni pamoja na huduma muhimu lakini maji ni siasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, michango yenu ambayo mmeieleza katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, utekelezaji wake maana yake ni kuhakikisha kwamba mnarudi. Kwa hiyo, sisi watendaji wa Wizara ya Maji, pamoja na kazi ya kupeleka maji lakini tuna kazi ya kulinda majimbo ya Waheshimiwa Wabunge katika kuhakikisha mnarudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara yetu ya Maji kama nilivyoeleza hakuna hata mmoja asiyejua. Mheshimiwa Rais, aliwahi kuhutubia katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano tarehe 22 Aprili, alinisimamisha pale akatoa maelezo mahususi kwamba, yeye ni mama na hataki kusikia, hataki kuona wamama wa Taifa hili wanahangaika juu ya adha ya maji. Pia, akaenda mbali zaidi akaniambia, Waziri wa Maji, wewe unawaambia watendaji wako ukinizingua nitakuzingua.

Mheshimiwa Spika, hakuna siku ngumu katika maisha yangu kama siku ile. Niliweza kukaa na watendaji wangu kwa kina nikawauliza swali moja, je, hii kazi tunaiweza au

hatuiwezi? Wameniambia hii kazi tunaiweza. Nataka niwambie pongezi hizi ambazo waheshimiwa mmezitoa, nataka nizirudishe kwa watendaji wote wa Wizara ya Maji. Waheshimiwa Wabunge, pongezi hizi zote ambazo mmezitoa naomba nizirudishe kwa Rais wangu Mpendwa, Samia Suluhu Hassan, ambae ameasisi kauli ya kumtua Mama ndoo kichwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, moja ya chanagamoto kubwa ya Wizara yetu ya Maji juu ya utekelezaji wa maji ni ufinyu wa bajeti. Ipo miradi ambayo sisi tumeikuta ambapo hata mimi sijawahi hata kumaliza chuo au sekondari. Kwa Mfano, ukienda Serengeti kulikuwa kuna mradi unaitwa Mugumu na kweli mgumu kweli kweli. Zimepita awamu zote mradi ule haujakamilika. Waziri ukija hapa kimbembe chake si mchezo. Mradi ule Mugumu umemalizwa na Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna miradi ilikuwa ya kichefuchefu ambapo imejengwa unaweza ukawa kiongozi ukafika pale ukauzindua mradi, maji yanatoka leo ukiondoka unaondoka na maji yako. Wananchi wanateseka pesa zimetolewa, Mwakitolyo, Nyantukuza kule Nyang'wale lakini Mheshimiwa Rais alitupa maelekezo miradi ile ambayo ilikuwa ikiitwa kichefuchefiu ambayo tuliianisha 177, Waheshimiwa Wabunge mlipitisha mageuzi ya kuanzisha wakala wa maji vijijini *RUWASA* kwa ajili ya kwenda kutatua matatizo ya maji. Miradi 157 yote tumeikwamua watu wanapata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara yetu ya Maji, ilikuwa inafanya sasa mageuzi. Nini? kwa maana ya *designing manual,* ipo miradi ilikuwa inajengwa kwa gharama kubwa sana. Kwa mfano, ukienda kwa Kaka yangu Festo, kuna miradi ambayo ilitakiwa kutekelezwa zaidi ya billioni sita, sisi tukasema hapana. Matamba - Kinyika, tulifika pale tukasema miradi hii haiwezi kutekelezwa hivi. Wewe unapokuwa Mhandisi wa Maji wewe umesomea maji. Badala ya kumpa mkandarasi

hebu tuone uwezo wako, mradi ule umejengwa kwa bilioni mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukienda Shinyanga Vijijini mradi ambao unaitwa *Muze Group* ambao ulitaka kutekelezwa kwa zaidi ya bilioni tano tukasema hapana. Tunaposema mhandisi wa maji wewe umesomea maji unaweza kufanya hiyo kazi. Tumewapa ile kazi wameweza kutekeleza hata bilioni haijakamilika mradi umekwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ukienda zako Babati mradi ambao unaitwa Singu Sibino, na Kamati ilifika imejionea, ulitakiwa kujengwa na mkandarasi kwa zaidi ya bilioni 20, tukasema hapana wataalamu mtafanya hii kazi. Wameifanya, na leo hata bilioni 12 haijakamilika na ule mradi unaenda kukamilika na watu wanapata maji.

Mheshimiwa Spika, nini maana yangu; niwashukuru sana viongozi wetu wakuu. Mheshimiwa Rais, Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuja kutufungulia, nakumbuka pale Chuo Kikuu cha Mipango; *Design Manual* kwamba kila mhandisi wa maji katika Wizara ya Maji anapotaka ku-*design* lazima afuate *design manual.*

Mheshimiwa Spika, hatuweze kutekeleza miradi ya maji hapa Dodoma eneo moja lakini kila tenki saizi moja lakini gharama tofauti, haiwezekani. Tumeanzisha Chuo cha Maji kwa minajili ya kuwatumia wataalamu wasaidie sekta ya maji, mageuzi haya leo tunawapongeza ni kazi kubwa ambazo mmezifanya Waheshimiwa Wabunge, Mwenyezi Mungu atawabariki sana na mtakumbukwa katika historia ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukitaka kufika haraka nenda zako mwenyewe, lakini ukitaka kufika mbali nenda na wenzako. Nitumie nafasi hii kumshukuru sana Naibu Waziri Maryprisca Mahundi, nitumie nafasi hii kumshukuru sana Katibu Mkuu

wangu wa Wizara ya Maji *Engineer* Nadhifa Kemikimba - *STK,* mama wa sheria, taratibu na kanuni. Pia nitumie nafasi hii kumshukuru Naibu Katibu Mkuu wetu wa Wizara yetu ya Maji *Engineer* Cyprian Luhemeja, kwa muda mfupi na Menejimenti ya Wizara ya Maji na watendaji wote wa Wizara ya Maji Mwenyezi Mungu ndiye atakayewalipa; tutafanya kazi. Hii ni Wizara ya Maji si wizara ya ukame, tutafanya kila linalowezekana kuhakikisha Watanzania waishio mijini na vijijini wanapata huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, ukimuona kobe juu ya mti amepandishwa, mara kwa mara nasema. Niishukuru Kamati yako kwa maoni, ushauri, maelekezo na maagizo mbalimbali. Leo tunaona faida yake jamii ipo tu, ukiishirikisha utafanikiwa, usipoishirikisha utakwama. Sisi kama Wizara ya Maji hatutakuwa kikwazo kwa kamati yetu, sisi Wizara ya Maji hatutakuwa kikwazo kwa Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote katika kuhakikisha tunatekeleza miradi yetu ya maji na iwe na matokeo chanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja yangu leo imechangiwa na jumla ya Waheshimiwa Wabunge 75, lakini Wabunge watatu akiwemo Mheshimiwa Mtaturu wamechangia kwa maandishi. Kwa muda mfupi ambao nimepewa haitakuwa rahisi kujibu kwa kina hoja zote zilizotolewa. Ningependa kuahidi mbele ya Bunge hili tukufu, kwamba hoja zote za Waheshimiwa Wabunge tutazijibu kwa maandishi na kuziwasilisha kuingizwa kwenye kumbukumbu za Bunge. Hivyo ninaomba nitumie muda huu mfupi niliopewa kutoa ufafanuzi wa baadhi ya hoja zilizotolewa kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, moja, hoja ya Kamati za Kudumu za Maji na Mazingira, kukamulisha malipo ya wakandarasi, *National Plan, National Water Grid, Non-Revenue water*, mapitio ya Sera ya Taifa, Mradi wa Maji wa Tunduma, Mradi wa kukabiliana na mabaliko ya tabianchi Simiyu, vipi kuhusu utekelezaji wa mradi wa maji wa Ziwa Tanganyika, kwa

maana ya Kigoma, Rukwa na Katavi, bili za maji na maunganisho ya gharama za maji.

Mheshimiwa Spika, labda nianze juu ya maji katika Jiji letu hili la Dodoma. Kabla Serikali haijahamia Dodoma mahitaji ya maji katika Jiji la Dodoma ilikuwa lita milioni 44, lakini kupitia mamlaka yetu ya maji *DUWASA* ilikuwa na uwezo wa kuzalisha lita milioni 66. Tulikuwa na maji mengi kuliko mahitaji.

Mheshimiwa Spika, lakini baada ya Serikali kuhamia hapa Dodoma ongezeko kubwa la watu na mahitaji yameendana sambamba. Leo ukienda Dar es salaam maeneo mbalimbali unaona namna ujenzi unavyofanyika. Leo ukenda maeneo ya Singida maeneo ya Nara ujenzi unafanyika. Kwa hiyo baada ya kuongezeka kwa idadi ya watu tumefanya tathmini na tumeona mahitaji katika Jiji la Dodoma ni lita milioni 133 lakini uwezo wa mamlaka yetu kuzalisha ni lita milioni 68. Hapa kuna haja ya kufanya kila linalowezekana ili kuhakikisha Jiji hili la Dodoma linapata maji.

Mheshimiwa Spika, tuna mipango ya muda mfupi lakini tuna mipango ya muda mrefu. Mipango ya muda mfupi tumetumia wataalamu wetu wa rasilimali za maji. Tunatambua maji yaliyo chini ya ardhi ni mita za ujazo bilioni 21, tumewaambia wafanye kila linalowezeka watuoneshe wapi kuna mengi katika Jiji hili la Dodoma, kwa sababu chanzo cha maji tunachokitegemea peke yake ni cha Mzava.

Mheshimiwa Spika, niwapongeze sana wataalam wetu wa rasilimali za maji wamepata maji mengi Nzuguni na tumechimba visima vitano vyenye uwezo wa kuzalisha lita zaidi ya lita milioni saba, tunaziingiza kwenye mfumo ambapo zitaweza kuongeza maji kwa asilimia 11. Maji haya ambayo mradi wake tunauanzisha pale Nzuguni utaweza kuwanufaisha wananchi zaidi ya 75,000. Nini maana yake?

maeneo korofi ambayo yalikuwa na kero kubwa sana ya maji, Nzuguni yenyewe na maeneo ya Ilazo, Kisasa na Swaswa yatapata huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Kunti amezungumza Mheshimiwa Mavunde anazungumzia Jiji la Dodoma, nataka niwambie mradi huu tunakwenda kuukamilisha mwezi wa nane ili kuweza kupunguza adha katika Jiji hili la Dodoma.

Mheshimiwa Spika, zipo jitihada kubwa ambazo tunazozifanya. Tunajua leo mvua badala ya kuwa fursa wakati mwingine imekuwa ikileta maafa. Tumeona mvua inanyeesha inapotea baharini, tunaona mvua inanyesha nyingine inapotelea kwenye mito lakini wananchi hawana maji. Mwelekeo wa Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ni juu ya uvunaji wa maji, kwamba maji badala ya kuwa maafa sasa yawe fursa. Tumejielekeza juu ya ujenzi wa mabwawa, na huo ndio mwelekeo wa Kamati yetu. Kwamba kuwa na ujenzi wa mabwawa madogo makubwa na ya kimkakati ili kuhakikisha kwamba meneo haya kame ambayo hata ukichimba kisima hupati maji tunakwenda kuchimba mabwawa. Nataka niwahakikishie, Mheshimiwa Mbunge wa Kiteto, Mbunge wa Meatu na Mbunge wa Ngorongoro, kwamba tunakwenda kuchimba mabwawa. Mheshimiwa Rais ameshatupatia mitambo kwa ajili ya kuchimbia mabwawa.

Mheshimiwa Spika, yapo mabwawa ambayo yalikuwa yakisomeka tu kwenye *documents,* Bwawa la Kidunda na Bwawa la Farkwa; lakini dhamira njema na uthubutu wa Rais wetu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan leo tunakwenda kuyatekeleza mabwawa haya, haijawahi kutokea Waheshimiwa Wabunge. Mlikuwa mkizungumza kwenye Bunge hili mnashauri kila mara mbona utekelezaji hautokei?

Mheshimiwa Spika, leo miradi mingi ambayo tulikuwa tukiitekeleza midogomidogo leo pale Dar es salaam tume-*experience water crisis;* baada ya pale tulijenga mradi wa bilioni zaidi ya 23 kwa fedha za ndani, ametoa Rais na mradi tumekamilisha. Amesema adha ile hataki aione tena. Mradi wa zaidi ya bilioni mia tatu naa ambao tulikuwa tukisubiri wafadhiri Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan anasema tunaenda kuutekeleza kwa fedha za ndani. Amekwishatoa bilioni 49 na mkadaarasi yupo *site,* Mungu atupe nini ndugu zangu?

Mheshimiwa Spika, Bwawa la Farkwa ambalo tulikuwa tukilizungumza kila kukicha; leo nataka niwaambie tumezungumza na wenzangu hapa katika *commitment* ambazo tunazozifanya, kwamba kabla ya tarehe 30 mhandisi mshauri apatikatene kazi ya kuanza hilo bwawa ianze na mkandarasi apatikane ili mradi huu wa Bwawa la Farkwa uweze kutekelezwa kwa sababu fedha tumekwishapata na Mheshimiwa Rais ametupa, hatuna kisingizio

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, dhamira njema Rais wetu ya kumtua mwana mama ndoo kichwani hapa Dodoma inatamia.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wamezungumza, Kaka yangu Moni amezungumza, na Mheshimiwa Kunti, kwamba mradi huu wa Bwawa la Farkwa maji yanaelekezwa Dodoma vipi kuhusu Chemba? Nataka niwaambie, ukikaa na waridi lazima unukie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lengo la bwawa hili, pamoja na kuyapeleka maji Dodoma lakini wanufaika wa kwanza watakuwa Wana-Chemba. Mpango wetu ni kuhakikisha hadi Bahi tunayapeleka maji ili wananchi wa Bahi wapate maji. Pamoja na hilo Mheshimiwa Rais anatuelekeza kwamba tuna rasilimali toshelevu hivyo lazima tutumie Ziwa Victoria kuhakikisha kwamba tunaleta maji hapa ambapo pia

atawasaidia wananchi wa Singida. Itoshe kusema kwamba Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan ni suluhu ya matatizo ya Watanzania. Tumpigie makofi mengi sana Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, limezungumzwa hapa suala la pamoja na haya mageuzi ambayo tunayafanya, na mimi kuna baadhi ya mambo lazima nikubali. Yapo maeneo ambayo tunafanya vizuri lakini pia yapo maeneo ambayo hatufanyi vizuri. Msema kweli ni mpenzi wa Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Spika, tunasema kwamba vijijini tuna asilimia 77 lakini ukweli kuna baadhi ya maeneo ukienda, hata mimi Waziri wa Maji wakati mwingine napata unyonge. Ukienda Kilindi hali siyo nzuri, ukienda Ushetu kwa kaka yangu Chereheni hali siyo nzuri, ukienda Meatu hali siyo nzuri. Lakini nataka niwaambie, kwa muda mfupi ambao tumefanya, mpaka sasa tuna vijiji Tanzania takribani 12,318. Pamoja na jitihada zilifanywa na fedha zilizotolewa tumeweza kufikia vijiji zaidi ya 9,000 kwa muda mfupi. Sasa hivi tuna deni la vijiji zaidi ya 3,000.

Mheshimiwa Spika, nini maana yetu? Tunatambua tuna rasilimali za maji juu ardhi mita za ujazo bilioni 105 na pia tuna maji chini ya ardhi mita za ujazo bilioni 21. Nataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge, sehemu ambapo tukichimba kisima tutapata maji tunakwenda kuchimba kisima kwa sababu magari tunayo. sehemu ambapo tunaona kabisa ukichimba kisima haupati maji tunakwenda kuchimba mabwawa kwa sababu vifaa tumekwishapewa. Nataka niwatie moyo Waheshimiwa Wabunge, ukiona giza nene ujue kumekucha, baada ya dhiki siyo dhiki bali baada ya dhiki ni faraja na faraja yetu ni Mheshimiwa Rais Samia Suluhu hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii kazi tunaiweza, tunaiweza sana na tutafanya kila linalowezekana kuhakikisha adhma ya Mheshimiwa Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan ya kumtua mwana mama ndoo kichwani inatimia. Kwa hiyo

Mheshimiwa wa Ushetu umezungumza hili suala, tumetuma wataalamu wanafanya tathmini. Acha wamalize kazi, tutahakikisha hatuwezi kufikisha maji maeneo mengine ilhali Ushetu wasipate maji. Tutaweka historia katika Jimbo la Ushetu.

Mheshimiwa Spika, amezungumza dada yangu hapa, Mheshimiwa Rehema wa Bulyanhulu na mama yangu Mama Sitta kuhusu Urambo, Kaliua na Sikonge. Ni kweli maeneo haya yana changamoto, na ndiyo maana nasema yapo baadhi ya maeneo hatukufanya vizuri. Sisi Waheshimiwa Wabunge tulikuwa na mradi hapa unaitwa miji 28. Mradi huu ni wa muda mrefu, ulikuwa ukizungumzwa tu Bungeni. Mheshimiwa Rais alipoingia muda mfupi ameweza ku-*unlock* mradi ule na tumeweza kusaini na makandarasi.

Mheshimiwa Spika, tukawa na changamoto ya msamaha wa kodi; na hapa nitumie dhati ya moyo nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha pamoja na Naibu Waziri wa Fedha, Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha pamoja na Naibu Makatibu Wakuu wote na kamishna wa bajeti; wametutendea haki sisi Wizara ya Maji. Nataka niwaambie Mheshimiwa Rehema, Mheshimiwa Kakunda na Mheshimiwa Mama Sitta unyonge basi. *(Makaofi)*

Mheshimiwa Spika, msamahawa kodi kwa wakandasi wale ambao ni kwa ajili ya miji 28 umetoka na *advance payment* imekwishatolewa, kwa hiyo, hawana kisingizio, kazi yao ni kwenda kutekeleza mradi kwa sababu mradi ule fedha zake zote zipo. Na ninataka niweke *commitment,* nipo tayari kufanya ziara rasmi ili tukafanye mikutano Kaliua, Sikonge na Urambo ili kwenda kuwakabidhi wakandarasi kwa sababu *advance payment* wamekwishapewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge, tumezungumzia fedha zilizotolewa, na hata angalieni bajeti yetu ilivyonono kitabu kizima. Fedha hizi

zinahitaji usimamizi na ufuatiliaji. Ndiyo maana nilizungumza kwamba ukiona hapa tunasema mradi umefanya vizuri ni kwa sababu umesimamiwa vizuri. Hii kazi peke yangu Waheshimiwa Wabunge sitaiweza, lazima tukubali kushirikiana. Ndiyo maana nilizungumza, ukisoma Ezra inasema; "Inuka hii shughuli inakuhusu na ukaitende kwa moyo mkuu." Sisi wasaidizi wa Mheshimiwa Rais tupo pamoja na ninyi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, miradi yetu hii tukienda kuisimamia vizuri matokeo yataonekana, na matokeo yakionekana nini maana yake, ukisoma Isaya 12:3 inasema; "Kwa shangwe mtachota maji katika visima vya wokovu." Kwa hiyo niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge twende tukasimamie hili jambo ili liende vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, imezungumzwa kwamba tuna rasilimali toshelevu, kwa mfano maeneo ya Kigoma, Katavi na Rukwa. Mimi mwenyewe nimefika, nilipangiwa ziara na watendaji wangu, nilighairisha, nikasema hebu tusikie mawazo ya Waheshimiwa Wabunge. Kwa kweli nimeamini, wakati mwingine tutoe nafasi kwa Waheshimiwa Wabunge, ninyi ni *consultancy* wa ukweli, mnatoa mawazo kwa maslahi ya Watanzania na kwa ajili ya kumsaidia Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, nitawapa mfano mmoja; *study* za Wizara ya Maji zilikuwa zinasema maji Liwale hakuna, zinasema hivyo; mimi nikasema haiwezekani, tukaja kwa Mheshimiwa Mbunge. Kweli, *study* zinasema, lakini hebu ngoja twende. Tukaenda tena, leo tumechimba visima maji ni bwerere. Nataka nikuhakikishie Mheshimiwa Liwale, tutaweka historia ambayo ilikuwa imekata tamaa kwa muda mrefu. Hii ni kazi kubwa na nzuri ya Rais wetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wa Kigoma Katavi na Rukwa wamezungumzia suala la Ziwa Tanganyika,

na mimi mwenyewe nimekwenda kujiridhisha na Katibu Mkuu amekwenda kujiridhisha. Nimefika mpaka kwenye chanzo pale Kalema. Nikiri na kusema kwa dhati kabisa dada yangu Aida umezungumza na Waheshimiwa Wabunge wote mmezungumza, kwamba Ziwa Tanganyika ndilo suluhu ya changamoto ya maji katika mikoa ile. Niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge twendeni tukaweke historia ya pamoja. Leo hapa ninavyozungumza naisikia sauti ya Rais wangu juu ya moja ya maelekezo ambayo ametupatia akiwemo na kiongozi wetu katika Bunge, Mheshimiwa Waziri Mkuu, ni kwamba, mawaziri chukueni hatua; tunakwenda kuchukua hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatua tunayokwenda kuchukua ni kumwajiri mhandisi mshauri ili aweze kwenda kufanya usanifu juu ya ujenzi wa mradi huu. Suala la fedha tutakaa na Mheshimiwa Rais, kama maeneo mengine tulivyotekeleza Mheshimiwa Rais wetu atakwenda kutekeleza mradi huu na wananchi hawa waweze kupata huduma ya maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, imezungumzwa hapa, pamoja na mageuzi haya tunayoyafanya lakini sasa hivi tunakwenda kwenye mabadiliko ya tabia ya nchi, vipi kuhusu Sera ya Maji? Sera ya maji imeanzishwa 2002 leo 2023.

Mheshimiwa Spika, ni kweli Sera yetu imepitwa na wakati, na ndiyo maana hata katika vipaumbele ya Wizara tumesema lazima twende tukafanye mapitio ya Sera yetu. Kamati pia imelizungumzia hilo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Kihenzile amezungumza, nadhani hili wala halihitaji mjadala. Maelekezo ya Mheshimiwa Spika wa Bunge pamoja na Bunge lako ni kuhakikisha kwamba twende tukaipitie hii Sera ili ije kuendana na mazingira ya sasa na kasi ambayo anaifanya Mheshimiwa

Rais wetu ili kuhakikisha kwamba tunafanya mageuzi na kuleta matumaini makubwa kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni kuhusu suala la gridi ya maji ya taifa. Mwenyezi Mungu ameijalia nchi yetu. Ukienda Kanda ya Ziwa kuna Ziwa Victoria, ukienda mkoa wa Ruvuma kuna mto Ruvuma, ukienda Kigoma, Rukwa na Katavi kuna Ziwa Tanganyika. Pia ukienda Mbeya kuna Mto Kiwila, ukienda kila eneo; leo ukienda zako Mtwara, ukienda kusini kuna Mto Rufiji.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais ametupa maelekezo, kwamba twende tukahakikishe; hii i ndiyo ajenda yake, na Waheshimiwa Wabunge hii kazi tumeshaianza. Leo hii ukienda zako Ziwa Victoria tunayachukua maji ya Ziwa Victoria tunakwenda kupeleka maji katika Jimbo la Rorya, tunayapeleka Tarime Mjini hadi Tarime Vijijini.

Mheshimiwa Spika, ukienda pale Musoma upo mradi wa bilioni 134, mradi mkubwa, tumejenga hadi tenki kubwa la Bahima. Ukienda Mgango Kiabakali na Butiama tuna mradi wa zaidi ya bilioni 70 kwa ajili ya kutumia Ziwa Victoria. Ukienda Mwanza, leo tumeona mahitaji katika Jiji la Mwanza ni lita milioni 154, mamlaka yetu ya maji ina uwezo wa kuzalisha lita milioni 90.

Mheshimiwa Spika, tuna mradi wa bilioni 69 wa Butimba sikulisaidia tu Jiji la Mwanza, maji yale yanakwenda mpaka Magu na yanakwenda mpaka Jimbo la Misungwi.

Mheshimiwa Spika, achana na hilo, leo hii tunazungumza mradi ambao tulikwishautekeleza ya kuyatoa maji kuyaleta Shinyanga, tumeyapeleka Tabora, tumeyapeleka Igunga, tumeyapeleka Nzega. Mheshimiwa Rais anatueleza kwamba sasa hivi tanayapeleka Igalula, lakini tunayapeleka Kaliua, tunayapeleka Sikonge na

tunayapeleka mpaka Urambo kwa Mama Sitta, tumpigie makofi mengi sana Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, achana na hilo, leo imekuja hoja hapa ya Ziwa Tanganyika, hii ndio Gridi ya Taifa ambayo tunatakiwa kwenda kuifanya, tunakwenda kuweka historia hii. Nilizungumza hata Baba wa Taifa alivyokuwa anakwenda kupigana vita vya Idd Amini, alisema maneno machache tu kwamba, uwezo tunao, nia tunayo na sababu pia tunayo. Sababu ya kwenda kujenga mradi huu wa Ziwa Tanganyika kwa maeneo haya tunayo na Mheshimiwa Rais kazi hii alishaianza. Ukienda Kigoma Jimbo ambalo lina kata 19, amejenga mradi wa bilioni 42, zaidi ya kata 19 zimepata maji. Mradi ule tumeshaufanyia *extension,* tumepeleka mpaka Mwandiga, nini sasa kilichobaki? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mradi ule uongezewe kufanyiwa *extension* na huyu Mhandisi Mshauri aliyepatikana maeneo ya Rukwa na Katavi waende kupata huduma ya maji safi na salama. Leo tunakwenda kutumia Mradi wa Maji wa Mto Ruvuma, *target* yetu katika miji hii 28 tunaendea kuanza. Mkandarasi yuko *site*, tunayatoa maji ya Mto Ruvuma tunayapeleka katika Jimbo la Nanyumbu ambalo lilikuwa na shida kubwa sana ya maji, lakini maji yanayofika Nanyumbu tutayashusha mpaka Masasi ili kuhakikisha Jimbo la Masasi wanapata huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, ukienda kwa Mheshimiwa Mkuchika, tuna mradi mkubwa wa Makonde. Mradi una umri mkubwa umekuwa chakavu kuliko mimi Waziri wa Maji, leo Rais ameshatupatia bilioni 84. Tunayatoa maji pale kwa Mheshimiwa Mkuchika Newala tunayapeleka Tandahimba kwa Mheshimiwa Katani, yanafika mpaka kwa Mheshimiwa Chikota. Huo ndio uelekeo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mradi ambao ulikuwa umekwama wa Same - Mwanga, ambao mradi wenye uwezo mkubwa

wa uzalishaji mkubwa si kuwasaidia Wanamwanga na Same, mradi ule unafika hadi Tanga. Achana na hilo, tuna mradi wa zaidi ya bilioni 170, ambapo tunakwenda kuyachukua maji ya Mto Pangani. Mkandarasi yupo *site* maji yale yanaenda Korogwe, Muhenza mpaka Kilindi huko, lakini mpaka katika Jimbo la Pangani. Kwa hiyo, huo ndio uelekeo.

Mheshimiwa Spika, hata ukienda zako Mbeya, ulizungumza katika Bunge lililopita, pale tuna Mto Kiwira tukichukua Mto Kiwira, nitapeleka katika Jiji la Mbeya lakini katika maeneo mengine. Umeona kazi tuliyoifanya, safari moja huanzisha nyingine, safari tumeianza acha tuiendeleze.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wasisahau miradi hii mikubwa inahitaji fedha nyingi, lakini Rais wetu ameonyesha uthubutu. Nilivyokuwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kulikuwa somo likuwa linaitwa haya mambo ya *civics, civics, development studies*. Tuliambiwa *development is the progressive change from low level to higher level*. Maendeleo ni mchakato na Rais wetu amekwishayaanza na maendeleo yanaonekana na namna Wabunge wanavyompongeza. Kikubwa tumpe ushirikiano, yale mambo ambayo tulikuwa tunaamini hayawezi kufanyika, leo yanafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Maendeleo katika Sekta ya Maji na Tanzania yanaanza na mimi. Maendeleo ya Taifa letu yanaanza na wewe, maendeleo ya Taifa letu yanaanza na sisi sote kwa kushikamana.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine lilizungumzwa na Mheshimiwa Shonza, Mheshimiwa Hasunga na Mheshimiwa Stella juu ya utekelezaji wa mradi katika Jimbo la Tunduma la kuyaleta maji Vwawa, Mloo. Tumeshakubaliana kabla ya Mwezi wa Saba mkandarasi atakuwa amepatikana, tunakwenda kuanza utekelezaji wa mradi wa maji katika kuhakikisha tunapeleka maji katika Eneo la Tunduma.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo tumelizungumza, hatuwezi tukawa na Wizara ambayo haina *National Water Master Plan*, haya ni maoni ya Kamati, haya ni maoni ya Waheshimiwa Wabunge, lakini pia sisi katika vipaumbele vyetu vya Wizara tumeliona hili. Tunalipokea acha twende tukalifanyie kazi juu ya utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Simiyu, huu ni mradi mmoja wa miradi ambayo utekelezaji wake ulikua mgumu. Tulikuwa na miradi mitatu, Mradi wa Same - Mwanga, Mradi wa Miji 28 pamoja na Mradi huu wa Simiyu. Tuliwaita wafadhili *KfW,* tulikaa nao ofisini. Huu ni mradi wa muda mrefu sana na Serikali pale imeahidi, tutapoteza imani ya Serikali yetu, tunaomba twende juu ya utekelezaji. Waheshimiwa Wabunge wali mtamu sana kwa maini, lakini ukikaa sana unakuwa kiporo na kiporo kikaa sana kina chacha na mwisho wake kinaumiza tumbo. Wafadhili wale wametuelewa… *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri dakika mbili, malizia.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, wafadhili wale wametuelewa na nataka niwaambie Wabunge wa Mkoa wa Simiyu, naomba wa-*note* tarehe hii hapa, kwamba tarehe hii 30 Mei tunakwenda kusaini mradi ule ili kuhakikisha Wanasimiyu kwa maana ya Bariadi, Itilima wanaenda kupata huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee niendelee kukushukuru na niendelee kumshukuru Mheshimiwa Rais pamoja na Bunge lako tukufu pamoja na Kamati yote na Watendaji wote wa Wizara ya Maji, Wenyeviti wa Kamati bila kusahau familia yangu. Ninachotaka kusema sisi tutafanya kazi usiku na mchana kuhakikisha Watanzania wanapata huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Tutaendelea na utaratibu wetu. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. MONICA MWANGA – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaanza na kitabu cha pili Fungu 49 - Wizara ya Maji kwenye kitabu ni ukurasa wa 446, na kwenye kishkwambi ni ukurasa wa 445.

**MWENYEKITI:** Tuendelee.

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

**Fungu 49 - Wizara ya Maji**

Kifungu 1001- *Administration and Human Resources Management*……………………..Sh. 4,029,857,458

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge kifungu hiki kina Mshahara wa Waziri na nina majina hapa ya Wabunge wanaotaka ufafanuzi. Sasa nilikuwa nawaza yale makofi na zile pongezi, sijui ufafanuzi ni wa kitu gani hapa? Haya, Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi. Nikiri nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa ufafanuzi wake mzuri ambao amesema, lakini inawezekana sisi wengine ambao tunatoka majimbo ya vijijini, Mheshimiwa Waziri kweli amefafanua vizuri kabisa, lakini wananchi wetu wameendelea kupata mashaka huko. Maneno mazuri ambayo Mheshimiwa Waziri haya anayaongea, wanatamani na wenyewe kwenye vijiji mbalimbali waweze kusikia na majimbo mengine labda ambayo hayakutajwa mahali hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe tu Mheshimiwa Waziri niombe *commitment* yake, kwa sababu sisi baadhi ya majimbo ambayo tunatoka vijijini ambao tuko chini ya asilimia 78 ambazo zilisemwa na Serikali na asilimia 77 za kwake. Atupe neno la matumaini tulio chini ya asilimia 50, mfano Jimbo la Momba asilimia 30 na majimbo mengine ambayo yalikuwa yametajwa, atupe faraja ili wananchi walioko vijijini huko wasikie angalau ni lini na sisi tutasogea tufifike angalau hata asilimia 70. Mheshimiwa Waziri kama ambavyo Waziri anasemea…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa …

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:**…anayelala na mgonjwa ndiye anayejua mihemo yake, sisi pia tunaotoka vijijini ndio tunajua. Tunajua namna ambavyo tunateseka, tunaumia, kuna wakati tunashindwa kusema mbele ya wananchi wetu tutasema nini, Mheshimiwa Waziri aseme neno na nafsi yangu ipoe. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri ufafanuzi.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niliweka wazi na nilisema kwamba msema ukweli ni mpenzi wa Mwenyezi Mungu. Tumefika asilimia 77 lakini katika hizi asilimia 77 yako maeneo ambayo tumefanya vizuri. Kwa mfano, ukienda Mbalizi, kulikuwa na changamoto akisimama Mbunge atasema kwa sababu watu wamepata maji. Nikiri kama Waziri wa Maji, Eneo la Momba kuna changamoto na ndio maana sisi kama Viongozi wa Wizara tulivyopata magari haya 25, moja tu katika Mkoa wa Songwe tulipeleka katika Jimbo lake Mheshimiwa Mbunge. La pili tulimtuma Katibu Mkuu wa Wizara yetu ya Maji, aende akatizame chanzo ili kuhakikisha tunamsaidia kwa kupeleka maji Tunduma, lakini kabla ya Tunduma tuone tunamsaidiaje Mheshimiwa Condester. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katibu Mkuu amekwenda ametazama vyanzo ameona chanzo cha Mto Momba ni toshelevu. Kwa hiyo chanzo hiki tume-*propose* kwamba tutawasaidia maji Momba, lakini maji yataenda Tunduma, yatakwenda Vwawa mpaka Mlo na tumetoa *commitment* tunatoka katika Bunge hili tunakwenda kutangaza hii tenda. Kabla ya Mwezi wa Saba mkarandasi atapatikana, nataka nimwalike siku ya kwenda kumkabidhi mkandarasi ili faraja wananchi waone namna alivyopigania jimbo lake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru maadam wana Momba wamesikia na watu wengine huko vijijini. Namshukuru Mheshimiwa Waziri.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge katika ngazi hii ukiwa umeridhika unakaa, husimami tena,

ukisimama maana yake bado unahitaji kushika shilingi. Mheshimiwa Rehema Juma Mgilla.

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru. Nimemsikiliza kaka yangu Mheshimiwa Juma Aweso katika ufafanuzi wake, amejipambanua vizuri sana kwa kuitaja Ulyankulu na Kaliua kwa ujumla. Tunapoitaja Kaliua ina majimbo mawili, sasa nataka *commitment* na wananchi wa Ulyankulu. Huu Mradi wa Maji kutoka Ziwa Victoria ambao anasema anaupeleka Kaliua. Je, utakwenda kuanzia Ulyankulu au wapi na hao wananchi watapata maji?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rehema Migilla tafuta vifungu huku mbele vya kusimama kwa ajili ya jimbo lako. Kwa sababu hapa kwenye Mshahara wa Waziri unaongea jambo mahsusi la kisera, si la jimbo. Kwa hiyo unaweza kutafuta kifungu huku mbele ambapo unaweza kusimama ili Mheshimiwa Waziri alisemee hilo mahsusi la jimbo lako.

Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kutokana na maelezo ya Mheshimiwa Waziri amenipa imani. Kwa hiyo nimepata matumaini, kusudio langu la kushika mshahara wake nimeliahirisha, namrudishia shilingi yake tukafanye kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ester Amos Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika hoja yangu nilizungumzia suala la Serikali kutolipa bili ya maji kwenye taasisi zake na wewe ni shahidi hili jambo ni la muda mrefu sana. Hizi mamlaka zetu za maji

zinashindwa kufanya hata ukarabati mdogo mdogo kwa sababu Taasisi za Serikali hazilipi bili ya maji. Nahitaji *commitment* ya Serikali ili huyu Mheshiiwa Aweso leo tunayempigia makofi Waheshimiwa Wabunge, hizi mamlaka zetu za maji ziweze kufanya hata vitu vidogo vidogo huko. Sasa pesa zote zipo mikononi mwa Serikali na nikatolea tu mfano *DAWASA* bilioni tisa, Tanga bilioni moja na kitu, Mtwara bilioni moja na kitu, Sumbawanga milioni 120 na kitu. Hizi pesa karibu mamlaka mbalimbali zote wanatoa huduma. Hivi kweli, kweli hizi mamlaka zetu tanataka zifanye kazi gani? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya Mheshimiwa…

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nahitaji *commitment* ya Serikali na kama sijapata lini wanaanza kulipa haya madeni, nitatoa shilingi na Wabunge wenzangu waniunge mkono.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester Bulaya, kabla hata sijamnyanyua Mheshimiwa Waziri, katika zile taasisi ulizotaja zinazodaiwa, Wizara ya Maji inadaiwa pia?

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Aliongea bila kutumia kipaza sauti.

**MWENYEKITI:** Ngoja kwanza, Wizara ya Maji inadaiwa pia?

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Maji ndio inadai.

**MWENYEKITI:** Kama inadai, sasa itawekaje kwenye bajeti yake na wewe unataka jambo hapa lilifafanuliwe lile ambalo yeye litakuwa kwenye bajeti yake. Maana yake ni nini, zile taasisi ambazo zinadaiwa na hoja ya Mheshimiwa Mdee ni hoja ya msingi ya kuisaidia Wizara hii, lakini kwa sababu sio

Wizara hii inayodaiwa haiwezi kuwa imetenga fedha kwenye mafungu yake. Kwa hiyo, Wizara zile zinazokuja ambazo zinadaiwa atakaposimama Mheshimiwa Ester Bulaya mjipange, lakini kwenye hii hawezi kutoa *commitment* Waziri wa Maji kwa sababu yeye Wizara yake haidaiwi.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, …

**MWENYEKITI:** Nakusikiliza.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni mkakati wa Serikali nzima, tunahitaji *commitment* na ndio maana Waziri wa Fedha alisimama…

**MWENYEKITI:** Ngoja, ngoja, umesimama kwenye Kifungu chenye Mshahara wa Waziri yupi?

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Wa Maji.

**MWENYEKITI:** Wa maji? Ahsante sana.

Haya Waheshimiwa tuendelee.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitisha na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1002 - *Finance and Accounts Unit*.......Sh. 1,959,830,420

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitisha na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1003 - *Policy and Planning Unit*............Sh. 1,195,706,200

**MWENYEKITI:** Soma upya.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

Kifungu 1003 - *Policy and Planning Unit*..........Sh. 1,195,706,200
Kifungu 1004 - *Government Comm. Unit*.............Sh. 567,764,000
Kifungu 1005 - *Legal Services Unit*.........................Sh. 593,673,000
Kifungu 1006 - *Procurement Mngnt Unit*..............Sh. 960,953,000
Kifungu 1007 - *Management Information System Unit*....................................Sh. 558,855,000
Kifungu 1008 - *Internal Audit Unit*..........................Sh. 683,727,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge. muda uliobaki tunapitisha mafungu.

Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

**Fungu 49 – Wizara ya Maji**

Kifungu 1001- *Administration and Human Resources Management*...............................Sh. 4,029,857,458
Kifungu 1002 - *Finance and Accounts Unit*.......Sh. 1,959,830,420
Kifungu 1003 - *Policy and Planning Unit*............Sh. 1,195,706,200
Kifungu 1004 - *Government Communication Unit*...................................................Sh. 567,764,000
Kifungu 1005 - *Legal Services Unit*.........................Sh. 593,673,000
Kifungu 1006 - *Procurement Management Unit*..................................................Sh. 960,953,000
Kifungu 1007 - *Management Information System Unit*..................................................Sh. 558,855,000
Kifungu 1008 - *Internal Audit Unit*..........................Sh. 683,727,000
Kifungu 1009 - *Project Preparation, Coordination and Delivery Unit*............................Sh. 760,704,000
Kifungu 2001 - *Water Resources*........................Sh. 6,741,346,750
Kifungu 2003 - *Water Laboratory*.......................Sh. 3,242,636,400

Kifungu 3001 - *Water Supply and Sanitation Division*....................................Sh.35, 034,719,922
Kifungu 5001 - *Water Development and Management Institute*..............Sh. 4,045,700,850
Kifungu 6001 - *Drilling and Dam Construction Agency*.......Sh. 0

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:** Matumizi ya Maendeleo, ukurasa 129.

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 49 – Wizara ya Maji**

Kifungu 1001- *Administration and Human Resources Management*..............................Sh. 1,800,000,000
Kifungu 1003 - *Policy and Planning Unit*..........Sh. 12,467,050,000
Kifungu 2001 - *Water Resources*.......................Sh. 41,500,000,000
Kifungu 2003 - *Water Laboratory*.......................Sh. 1,950,000,000
Kifungu 3001 - *Water Supply and Sanitation Division*…….........……………Sh. 638,112,582,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Matumizi imemaliza kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae. Mtoa Hoja taarifa.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kuwa Bunge lako limekaa kama Kamati ya Matumizi, imekamilisha kazi zake. Naomba taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge lako.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA HABARI NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Ahsante sana. Hoja imeunga mkono na sasa niwahoji Waheshimiwa Wabunge kuhusiana na hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Maji kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024. Wote wameafiki. *(Makofi)*

Ahsante sana Waheshimiwa.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 Yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nitumie fursa hii kutangaza rasmi kwamba Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Maji kwa mwaka wa fedha 2023/2024 yamepitishwa rasmi na Bunge.

Nitumie pia fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Watendaji wote chini ya Wizara hii kwa kupitishiwa bajeti yenu na Bunge. Nawapongeza sana, lakini pia tunawatakia kila la kheri katika utekelezaji wa ahadi ambazo mmezitoa,

zingine ziko kwenye kitabu hiki cha bajeti, lakini zingine mmezitoa hapa kwa Waheshimiwa Wabunge. Niwatakie kila la kheri kwenye utekelezaji wa hayo yote.

Pia nitumie fursa hii kuishukuru sana Kamati yetu ya Maji na Mazingira, Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati kwa kazi nzuri mnayoifanya ya kuisimamia Wizara hii, tunawashukuru sana na tunawapongeza sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mmechangia wengi sana kwenye Wizara hii na mmetoa mawazo yenu namna ya kupata ufumbuzi wa changamoto ambao kwenye majimbo yenu bado kuna changamoto ambao kwenye majimbo yenu bado kuna changamoto mmetoa mawazo yenu na Waziri amesema hapa wanayachukua na wanaenda kuyafanya kazi. Kwa hiyo na ninyi nawapongeza kwa kuwasemea wananchi ambao mnawawakilisha. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ni dhahiri Wabunge wengi wangependa kuchangia lakini hawajapata nafasi lakini kama mlivyotoa pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wao wote milango yao iko wazi kama mtu hakupata fursa ya kuchangia anaweza akawaona akawaeleza na atasikilizwa.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo ambayo nimeyasema, nitumie sasa fursa hii kutoa mwongozo mmojawapo kati ya miongozo mingi ambayo bado inasubiriwa, lakini leo tutatoa mwongozo mmoja ambao uliombwa na Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava kuhusu maneno yaliyotumika na Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara siku ya tarehe 5 Mei, 2023.

Waheshimiwa Wabunge, mnamo tarehe 9 Mei wakati wa kipindi cha jioni katika Kikao cha Ishirini na Mbili cha Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge, Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava alisimama na kuomba mwongozo wa Spika

chini ya Kanuni ya 76 ya Kanuni za Kudumu za Bunge kuhusu maneno yaliyotolewa na Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara wakati akihitimisha hoja ya Bajeti ya Wizara hiyo siku ya Ijumaa tarehe 5 Mei, 2023.

Waheshimiwa Wabunge, katika maombi ya mwongozo pamoja na mambo mengine, Mheshimiwa Mnzava alieleza kuwa Mheshimiwa Waziri, nanukuu, "Nawashukuru Wabunge ambao wengine wameniambia na wengine wamenionesha picha za watu waliokuwa wakizunguka kuwaomba Wabunge wawaunge mkono kulipinga jambo hili ndani ya Bunge hili. Waheshimiwa Wabunge, ninaomba tusitumike." Mwisho wa kunukuu.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Mnzava aliendelea kueleza kuwa anaona maneno hayo yanagusa moja kwa moja heshima, uhuru na majadiliano na mijadala ndani ya Bunge. Hivyo aliomba mwongozo wa Spika kama maneno hayo ni maneno sahihi kutumika ndani ya Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya Mheshimiwa Mnzava kuomba mwongozo huo nilitoa ufafanuzi wa masharti ya Kanuni ya 76 yanayosimamia mambo ya mwongozo. Kwa mujibu wa kanuni hii Mbunge anapaswa kuomba mwongozo kwa jambo linalokuwa limetokea mapema siku hiyo ambayo mwongozo unakuwa umeombwa. Aidha nililieleza Bunge kuwa jambo ambalo Mheshimiwa Mnzava aliliombea mwongozo halikuwa limetokea siku hiyo ila kwa sababu Mheshimiwa Mnzava alieleza kwamba maneno yaliyotumiwa na Mheshimiwa Waziri yanagusa moja kwa moja heshima, uhuru wa majadiliano na mjadala ndani ya Bunge niliahidi kulitazama jambo hilo.

Waheshimiwa Wabunge, niliahidi kufuatilia Taarifa Rasmi za Bunge pamoja na maelezo ya Mheshimiwa Mnzava ili kujiridhisha iwapo maneno yaliyotumiwa na Mheshimiwa

Waziri yalikuwa sahihi kutumiwa ndani ya Bunge, halafu nitatoa pengine siyo mwongozo lakini maelezo kuhusu jambo hilo.

Waheshimiwa Wabunge, nilirejea Taarifa Rasmi za Bunge za tarehe 5 Mei, 2023 na kubaini kwamba Mheshimiwa Waziri alieleza kuhusu mapungufu ya usajili na upatikanaji wa taarifa za Kampuni ya *Chalinze Cement.* Aidha, alifafanua kwamba Wizara imekuwa ikifanyia kazi changamoto hizo. Pamoja na maelezo mengine ya ufafanuzi kuhusu hoja yake, Mheshimiwa Waziri alitumia maneno yafuatayo, nanukuu: "Mheshimiwa Spika, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wenye dhamira njema ya kulinda jitihada za Dkt. Samia Suluhu Hassan za kuita wawekezaji kutoka nje na kuwalinda wawekezaji wa ndani ambao tayari walishawekeza, nawashukuru sana. Wapo walioniambia na wengine wamenionyesha mpaka picha ya watu hao wakizunguka kwa Wabunge kuwaeleza msaidie kupinga jambo hili." Mwisho wa kunukuu.

Waheshimiwa Wabunge, aidha Mheshimiwa Waziri aliendelea na kueleza kuwa, nanukuu; "Waheshimiwa Wabunge, naomba tuchukue tahadhari ya hali ya juu na watu wasiolitakia mema Taifa letu. Mheshimiwa Rais amefanya kazi kubwa sana ya kui-brand Tanzania, wawekezaji wengi wanakuja, nimesema kwa mwaka mmoja tuna wawekezaji 240 hawakuwahi kutokea katika historia ya miaka 60 ya Taifa letu, imetokea sasa tusitumike." Mwisho wa kunukuu.

Waheshimiwa Wabunge, itakumbukwa kuwa wakati wa uchangiaji wa bajeti ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara Wabunge waligawanyika kuhusu suala la Kampuni ya *Twiga Cement* na *Tanga Cement* kuungana. Katika majadiliano hayo baadhi ya Wabunge walitoa maoni yanayounga mkono mchakato wa kuunganishwa kwa kampuni hizo. Wengine walikuwa na maoni kwamba

kampuni hizo zisiungane na wengine walipendekeza kampuni hizo ziungane kwa masharti mahususi waliyoyapendekeza.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kupitia *hansard* na kulinganisha na maombi ya mwongozo wa Mheshimiwa Mnzava, nimejiridhisha kuwa ni kweli kwamba Mheshimiwa Waziri alitamka maneno hayo yaliyolalamikiwa na Mheshimiwa Mnzava. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Ibara ya 100(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatoa haki na uhuru kwa Wabunge kujadili jambo lolote ndani ya Bunge na kwamba haitakuwa haki kwa majadiliano hayo kujadiliwa au kuhojiwa. Ibara hiyo inaeleza kama ifuatavyo, nanukuu; "Kutakuwa na uhuru wa mawazo, majadiliano na utaratibu katika Bunge na uhuru huo hautavunjwa wala kuhojiwa na chombo chochote katika Jamhuri ya Muungano au katika Mahakama au mahali penginepo nje ya Bunge." Mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, maneno yaliyotumiwa na Mheshimiwa Waziri yanakinzana na masharti ya Ibara ya 100(1) ya Katiba, kwa sababu yanagusa moja kwa moja heshima, uhuru wa majadiliano na mijadala ndani ya Bunge. Iwapo maneno hayo yataachwa kwenye *hansard* yatakuwa yanaashiria kwamba wapo Wabunge wanaounga mkono na wapo Wabunge wengine wasiounga mkono shughuli za maendeleo nchini ambazo zinafanywa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, vile vile *hansard* zitaonyesha kwamba wapo Wabunge ambao wanatumiwa na kushawishiwa na watu wenye nia mbaya na maendeleo ya nchi yetu wakati wa kujadili hoja Bungeni. Kwa hivyo, si maneno yanayofaa kutumiwa ndani ya Bunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kutokana na kasoro hiyo, maneno hayafai kuendelea kuwepo kwenye Kumbukumbu

za Bunge hivyo maneno hayo yanafutwa kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo hoja iliyokuwa imeletwa na Mheshimiwa Mnzava inamalizika kwa hatua hii.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka saa tatu kamili asubuhi kesho.

*(Saa 1.48 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa, Tarehe 12 Mei, 2023 Saa Tatu Asubuhi)*